

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Kumi na Mbili - Tarehe 25 Mei, 2015

(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

MHE. MAUA ABEID DAFTARI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2014/15 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

MHE. MOSES J. MACHALI (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO):

Taarifa ya Msemaji wa Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

MHE. AGNESS E. HOKORORO (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

MHE. CECILIA D. PARESSO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA KAZI NA AJIRA:

Taarifa ya Msemaji wa Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu, amemteua Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu Kukaimu nafasi ya Uwaziri Mkuu. Kwa hiyo, sasa ndiyo atachukua nafasi ya Kiongozi Mkuu wa Serikali Bungeni. Mambo yanaanza polepole. *(Kicheko)*

Katibu, hatua inayofuata.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 78

Uhuishwaji wa Daftari la Wapiga Kura

MHE. JOSEPH R. SELASINI aliuliza:-

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeweka muda maalum wa kuhuisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, zoezi ambalo litaendelea wakati walimu na wanafunzi wako vyuoni:-

(a) Je, ni kwa nini Tume isiandae utaratibu utakaowezesha Walimu na Wanafunzi kujiandikisha katika maeneo watakayopigia kura?

(b) Je, kama Tume haitafanya hivyo haioni kuwa ni sawa na kuwanyima wananchi hao haki ya kuchagua Viongozi wanaowataka?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (K.n.y. WAZIRI MKUU)
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kifungu cha 15 cha Sheria ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina wajibu wa kuandikisha wapiga kura katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Uandikishaji unajumuisha kuhuisha Daftari ili kuwapa nafasi wale waliotimiza sifa za kuandikishwa na kuwaondoa wale waliokosa sifa au kubadili taarifa zao. Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekuwa ikihuisha Daftari la Kudumu la Mpigakura kama sheria inavyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria za Uchaguzi zinamtaka mpiga kura kujitokeza mwenyewe kituoni kujiandikisha au kurekebisha taarifa zake kila inapotokea mahitaji ya kufanya hivyo. Wakati wa kupiga kura, kila mpiga kura anatakiwa aende kupiga kura katika kituo alichojiandikisha. Hata hivyo, vifungu 17 na 19 vya Sheria ya Uchaguzi, vinatoa fursa na utaratibu kwa wapiga kura kuhamishia taarifa zao katika maeneo watakayoweza kupiga kura. Kwa utekelezaji wa vifungu hivi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina utaratibu wa kutoa kipindi maalum kabla tarehe ya kupiga kura ili wale wanaotaka kuhamisha taarifa wafanye hivyo. Kwa mfano, katika Uchaguzi Mkuu wa 2010, Tume ilitoa muda wa siku 30 kabla ya uchaguzi ili wapiga kura waliohitaji kuhamisha taarifa zao kufanya hivyo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi nilioueleza katika sehemu (a), walimu, wanafunzi walioko vyuoni na wananchi wengine wenye mahitaji kama hayo, watajiandikisha katika vituo walivyopo sasa na endapo wakati wa kupiga kura watapenda kupiga kura katika vituo tofauti na vile walikojiandikisha, utaratibu uliowekwa na Tume wa kuhamisha taarifa zao utatumika ili kuwapa haki ya Kikatiba wananchi hao kushiriki katika uchaguzi. *(Makofi)*

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya hili swali yanachekesha na niseme kwa mara ya kwanza yanaudhi. Kwa sababu mimi sikuulizia wapigakura kwa ujumla wake, nimeuliza wanafunzi wa vyuo vikuu, wanafunzi wa colleges na wanafunzi wa sekondari, ambao hivi sasa zoezi hili likiendelea wapo mashuleni na wakati uchaguzi utakapokuwa unafanyika watakuwa majumbani.

(i) Je, hizo siku 30 zinazosemwa vyuo vyote vitafungwa ili hawa wanafunzi waende wakarekebishe hizo taarifa? *(Makofi)*

(ii) Zoezi hili linaendelea kwa teknolojia ambayo tunaamini ni ya kisasa; ni kwa sababu gani wanafunzi hawa wanapoandikishwa huko vyuoni wasieleze vilevile maeneo wanapotoka ili taarifa zao zikahamishwa kwa mtandao kupelekwa kwenye maeneo ambayo wanategemea kupiga kura au hili linafanywa kwa makusudi mazima ili kuwanyima wanafunzi haki yao ya kupiga kura? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la msingi Mheshimiwa ameuliza wanafunzi, lakini pia na sisi tumeleza kwamba, katika muda mwafaka na tukaeleza na mifano iliyotumika huko nyuma kwamba, Tume kawaida kabla ya kwenda kwenye uchaguzi, inatoa siku 30 za mwisho, wawe wanafunzi wa vyuo vikuu, wawe watumishi wa vyuo vikuu, wawe Watanzania wengine wote wa kawaida, wanapewa fursa ya kubadilisha na kueleza nia yao kwamba ni wapi wangependa wapigie kura zao. Hili liko bayana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimweleze Mheshimiwa Selasini kuwa, Serikali inajua kabisa kwamba, vyuo vyetu kwa sasa vina wanafunzi wengi na ambao kwa vyovyote vile, hawawezi kunyimwa fursa ya kwenda kupiga kura katika maeneo ambayo wangependa kwenda kupiga kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, hili tumeliweka bayana kabisa.

Swali la pili anasema kwamba, nini wasieleze maeneo ambayo watapigia kura. Haya mambo mengine ni masuala ya kuzungumza, ninaamini Tume wanasikia na sisi kama Serikali tumeendelea kuzungumza na Tume. Kwa kuwa Tume wa utaratibu wao, tumesema wakati mwingi siyo vizuri tukaingilia sana

utendaji wa kazi wa Tume, maana itaonekana na sisi kama Bunge tunaingilia pia utendaji wa kazi wa vyombo vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi tulilolisema ni kwamba, tutahakikisha wale wote wanapiga kura katika vituo ambavyo wangependa kupiga kura, pamoja na kwamba wanaweza wakajiandikisha katika kituo chochote. Kama Serikali tutahakikisha wanapiga kura bila kukosa na wala hakutakuwa na kisingizio chochote.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, hebu subiri hapo hapo, kwa namna ya kuliweka sawa katika jibu lako la msingi la Serikali, hebu soma tena majibu yako ya msingi sehemu (b) ili Bunge lielewe msimamo mzuri wa Serikali.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuelewa. Tumejibu kwa msingi kwamba, swali (b) linasema kama Tume haitafanya hivyo, haioni kuwa ni sawa na kuwanyima wananchi hao haki ya kuchagua Viongozi wao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwenye majibu ya msingi ...

MWENYEKITI: *No, no, no*, mimi ninataka nikusaidie wewe, katika jibu lako la msingi, jibu la Serikali soma kipengele cha (b) ili Mbunge aelewe Serikali imesema nini. Umenielewa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa sawa. (b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi nilioueleza katika sehemu (a), walimu, wanafunzi walioko vyuoni na wananchi wengine wenye mahitaji kama hayo, watajiandikisha katika vituo walivyopo sasa na endapo wakati wa kupiga kura watapenda kupiga kura katika vituo tofauti na vile walivyojiandikisha, utaratibu uliowekwa na Tume wa kuhamisha taarifa zao utatumika ili kuwapa haki ya Kikatiba wananchi hao kushiriki katika uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye amesema wanafunzi, wanachuo, tumeshaeleza hayo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, umeshajieleza. Mheshimiwa Paresso!

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Utaratibu wa kuandikisha mpiga kura kwa kutumia Mfumo wa BVR unahitaji mwananchi aweke alama za vidole na maeneo mbalimbali wananchi

wamekuwa wakilalamika zile mashine zinakuwa hazichukui alama za vidole kwa maana ya *finger print*. Kuna akina mama wanaenda mara mbili mpaka mara saba alama hiyo ya vidole haiwezi kuchukuliwa:-

Je, watu hawa ambao wanaathirika kwa namna moja ama nyingine watakosa haki yao ya kupiga kura na kujiandikisha; nini kauli ya Serikali?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli lazima tukubali kwamba, hii ni teknolojia ya kisasa ambayo inatumika katika uandikishaji. Mashine zile kwa kawaida kama vidole vile, sote tunajua vidole gumba vina alama fulani kama kontua. Sasa zinapokuwa zimepotea, kwa vyovyote vile mashine zile hazirekodi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema, wataalam wetu wanaendelea na kuhakikisha kwamba, hakuna mtu kwa sababu hiyo atakayeshindwa kujiandikisha. Wameendelea kurudia na wengine wamefanikiwa. Mpaka sasa hata maeneo ambayo yameandikishwa, hatujasikia kuna mtu au mpiga kura yeyote au mwandikishaji yeyote ambaye ameshindwa kujiandikisha kwa sababu hiyo. Baada ya marekebisho waliyofanya kufanyika na wakarudia wengine, tuseme wote hakuna ambaye ameshindwa na wote kimsingi amejiandikisha na tutahakikisha kwamba wote wanaendelea kujiandikisha.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kwa kuwa zoezi hili la uandikishaji hivi sasa linafanyika katika Mkoa wa Katavi pia katika Jimbo la Mpanda Mjini; na kwa kuwa mashine zilizopelekwa hazitoshelezi; na kwa kuwa kumekuwa na msongamano mkubwa na tabu kwa wananchi inabidi walale kwenye vituo kwa sababu ya kuandikishwa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha ndani ya muda huu mdogo wa wiki moja uliowekwa wananchi wote wanaandikishwa na kuwaondolea hiyo bugudha?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunaeleza hapa Bungeni kwamba, ni kweli mashine zile zilianza kuja kwa awamu. Ninataka nimhakikishie kaka yangu Mheshimiwa Said Arfi kwamba, mashine hizi zinaendelea kuja na mwisho wa mwezi huu tunapokea hizi BVR 1550. Katika maeneo yote ambayo yanaonekana yana upungufu, tutahakikisha vifaa hivi vinaongezwa.

Kubwa zaidi ambalo ningependa nimhakikishie Mheshimiwa Arfi ni kwamba, hakuna mwananchi yeyote kwa muda tuliouweka ambaye atashindwa kujiandikisha kwa sababu tu inawezekana vifaa hivi vitakuwa vichache. Hilo ninataka niwahakikishie Wabunge wote na Watanzania wote

kwamba, Tume itahakikisha kwa muda uliowekwa wananchi wote ambao wana sifa za kujiandikisha, basi wanajiandikisha katika Daftari la Mpiga Kura.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwa kuwa moja ya kujiandikisha moja ya takwa la kisheria la Kikatiba ni kuwa Mtanzania na mtu mwenye umri wa miaka 18; na kwa kuwa katika Jimbo langu la Iringa Mjini kwa sababu ya uelewa mdogo watu wengine wamekuwa wakizuiwa kuandikishwa wakitumia Sheria ile ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kuwalazimisha wananchi wajiandikishe wale tu wanaotoka katika ule mtaa, kitu ambacho ni kinyume cha sheria:-

Je, Serikali itakuwa tayari kuwatangazia Watanzania kwamba wale wote wenye umri wa miaka 18 na ambao ni Watanzania wana haki ya kujiandikisha mahali pale wanapotaka?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena naomba niwahakikishie Watanzania wote kwamba, wote watajiandikisha katika Daftari la Kudumu la Mpiga Kura. Kwa Watanzania wote mwenye sifa, kwa maana ya kuanzia miaka 18 pamoja na sifa nyingine.

Hili la kwamba wajiandikishe mahali popote, tumeweka utaratibu kwamba ni lazima watu hawa watambuliwe na vyama vyote. Huwezi ukampeleka mpiga kura yeyote katika kila eneo hata pale ambapo wenyeji wa eneo hilo hawamtambui. Inawezekana Chama kimoja kikasema kinamtambua, lakini wengine wa eneo lile, kuna Viongozi wetu tuliowachagua kwenye mitaa, kwenye vitongoji, hao wanatusaidia sisi. Tukisema kila mtu aende hata pale ambapo anashindwa kutambuliwa akajiandikishe, tunaweza tukavuruga zoezi zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba, watu wote watajiandikisha na kutambuliwa na Viongozi katika maeneo hayo. Tukiruhusu vinginevyo, tutakuwa tunaleta fujo na vurugu katika maeneo ya uandikishaji. *(Makofi)*

Na. 79

Mahakama ya Wilaya au ya Mwanzo

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE aliuliza:-

(a) Je, katika Wilaya zote za Tanzania, zile za zamani na hizi mpya, ni Wilaya zipi kati ya hizo hazina Mahakama hata moja ya Wilaya au ya Mwanzo inayofanya kazi?

(b) Haki isipotolewa kwa wakati kisheria ni sawa na haki iliyopuuzwa; je, Serikali inachukua hatua gani za kimkakati za kuhakikisha Mahakama za Mwanzo za Matai, Kasanga na Mwimbi zinaanza kufanya kazi?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wilaya mpya 19 na za zamani 11, ambazo hazina majengo ya Mahakama. Hata hivyo, Wilaya hizo zinapata huduma ya Mahakama ya Wilaya kwa kutembelewa na Mahakimu wa Mahakama za Wilaya ambao wamepewa mamlaka chini ya Kifungu cha 4(5) cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11. Pamoja na hayo, Serikali ina mpango wa kujenga majengo ya Mahakama yenye hadhi katika Wilaya zote mpya nchini na zile zisizo na majengo ya Mahakama.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mahakama ya Mwanzo Matai, inafanya kazi na kwa sasa wapo Mahakimu Waakazi wawili katika Kituo hicho. Mahakama ya Mwanzo Mwimbi inatembelewa na Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya Laela. Kwa upande wake, Mahakama ya Mwanzo Kasanga haifanyi kazi kutokana na uchakavu wa jengo lililopo. Hata hivyo, Mahakama hii imepatiwa jengo la Kata kwa ajili ya kuendesha shughuli zake. Mchakato wa kununua samani na kupeleka watumishi unaendelea.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Serikali imekiri kwamba, Mahakama ya Mwanzo Kasanga haifanyi kazi kwa sababu jengo limechakaa. Kwa kutambua juu ya uhitaji wa uwepo wa Mahakama ndiyo maana Kata imetoa jingo litumike kama Mahakama ya Mwanzo. Ningependa kujua ni lini utaratibu wa kununua samani utakamilika ili wananchi waweze kupata haki yao ya Kisheria?

(ii) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba, Mahakama ya Mwanzo iliyopo Mwimbi inapata huduma kutoka Mahakama ya Mwanzo iliyopo Laela, ambayo ni Wilaya tofauti kabisa. Je, Serikali haioni kwamba, iko haja ya kumpeleka Hakimu kwa sababu tayari jengo lipo; kinachokosekana ni uwepo wa Hakimu ili kuweza kutoa haki kwa wakati?

WAZIRI KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Kandege, kwa sababu amekuwa akifuatilia masuala haya ya Mahakama katika Jimbo lake kwa karibu sana. Kuhusu utaratibu wa samani, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, hivi sasa katika Miradi yetu ya Ujenzi na Ukarabati wa Mahakama za Tanzania, tunaangalia pia suala la samani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, sasa hivi inatumika Ofisi ya Kata, lakini sisi bado tunaendelea na mpango wetu wa kuhakikisha tunajenga Majengo ya Mahakama. Kwa upande wa samani, kwa kuwa Mahakama hii ipo katika Kata, basi napenda kumuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika utaratibu wetu mzima wa ukarabati tutaangalia pia na suala hilo la samani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu kumpeleka Hakimu; ni kweli sasa hivi Mahakama ile inatembelewa na Hakimu wa Laela. Katika mpango wetu wa 2015/2016 tunaongeza idadi ya Mahakimu, kibali tulikwishapata toka 2014/2015. Tumetangaza nafasi, maombi tumepokea na kwa mwaka huu tutaendelea kuongeza idadi. Hilo litakapofanyika, tutapeleka Hakimu katika Mahakama hiyo.

MHE. MARYAM S. MSABAHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba na mimi nimwulize Mheshimiwa Waziri swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa wale Wazee wa Mahakama wanawasaidia saa nyingine Watanzania ambao hata zile shughuli za Mahakama hawazijui. Je, Serikali ina mipango gani kuboresha masilahi ya Wazee wa Mahakama?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maryam Msabaha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana nae kwamba, Wazee wa Mahakama wana masaada mkubwa, lakini siyo tu kwa wananchi kama watakuwa wametaka ushauri kutoka kwao, lakini Wazee wa Mahakama ni Taasisi ambayo inaambatana na haki katika Mahakama za Mwanzo. Kwa hiyo, wanafanya kazi kubwa na kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masilahi; masilahi yao yamekuwa yakipanda mwaka hadi mwaka na hivi sasa tunajua kwamba, kuna wale ambao bado hawajalipwa. Tuko katika utaratibu wa kuhakiki madai yao na kwa mwaka huu wa fedha, tutapiga hatua zaidi katika kuhakikisha kwamba, wanayapata kwa wakati. Kwa hiyo, napenda kumhakikishia Mbunge kwamba, tunatoa umuhimu mkubwa sana kwa Wazee wa Mahakama, kama sehemu ya utoaji haki katika nchi yetu.

MHE. RACHEL R. MASHISHANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mahakama ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga kuna jengo zuri sana na tayari lilishafunguliwa na Jaji Mkuu wa Serikali. Nataka kujua ni lini sasa jengo hilo litaanza kufanya kazi? Ahsante.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rachel Mashishanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Shinyanga ni mojawapo ya majengo ambayo yanatufanya sisi kama Wizara, tuone fahari sana kwamba, tumeweza kupanua huduma zetu. Tunawashukuru Wananchi wa Shinyanga, kwa ushirikiano walioutoa mpaka kukamilisha ujenzi. Jengo hilo litaanza kufanya kazi hivi karibuni tutakapokuwa tumekamilisha yale yote yanayohitajika kwa ajili ya kulifanya litoe mazingira mazuri ya utoaji haki; lakini hilo ni suala ambalo hata hivi juzi tu Viongozi wa Mahakama walitembelea kuhakikisha kwamba, linaanza kazi kwa wakati.

Na. 80

Taa za Kuruhusu Ndege Kutua Katika Kiwanja cha Ndege cha Songwe

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (K.n.y. MHE. CYNTHIA H. NGOYE) aliuliza:-

Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe umekamilika na kuanza kutumika tangu mwaka 2013 lakini wa usiku ndege haziwezi kuruka na kutua kwa sababu hakuna taa za kuruhusu ndege kuondoka na kutua:-

Je, ni lini Uwanja huo utawekewa taa hizo za kuongoza ndege kutua na kuruka nyakati za usiku?

WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu kwa swali la Mheshimiwa Hilda Cynthia Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya, ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha ndege kutua kwa usalama majira yote katika Uwanja wa Ndege wa Songwe, Serikali iko katika hatua za mwisho za uteuzi wa mkandarasi atakayesimika taa za kuongoza ndege kutua na kuruka, kitaalamu inaitwa *Precision Approach Path Indicator*, ambazo ni sehemu ya mfumo mzima wa taa za kuongozea ndege. Aidha, kazi ya kusimika taa hizo za kuongozea ndege kutua na kuruka katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Songwe imepangwa kuanza mwezi ujao wa Juni 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa usalama wa ndege na abiria, Serikali ina mpango pia wa kusimika mfumo wa kikamilifu zaidi uitwao *Aeronautical Ground Lighting* na mitambo ya kuongozea ndege katika kiwanja hicho cha ndege cha Songwe, kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza:-

(i) Uwanja wa Songwe pamoja na kuwa na matatizo ya taa za kuongozea ndege pia jengo la kupokelea abiria ukamilishaji wake unasuasua sana. Je, Serikali itakamilisha lini jengo hilo la kupokelea abiria?

(ii) Kwa kuwa uwanja wa ndege wa zamani wa Mbeya, siyo wa Songwe, uwanja wa ndege wa zamani, sasa hivi hautumiki kwa ndege za abiria na sehemu hiyo ni kubwa sana. Je, Serikali iko tayari sasa kuwahamasisha wawekezaji katika uwanja wa ndege wa zamani wa Songwe ziweze kujengwa hoteli za kimataifa na magodauni makubwa kwa ajili ya kuhifadhi mazao ya kusafirisha nje ya nchi?

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kuhusu jengo la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe, maelezo kamili nitayatoa katika Hotuba yangu ya Bajeti, Jumamosi ijayo, tarehe 30. Itosheleze tu kumwambia, Mheshimiwa Mwambalaswa pamoja na Wadau wote wa Mkoa wa Mbeya kwamba, fedha zimetengwa na kazi hiyo inatazamiwa kufanywa kwa kipindi cha mwaka mmoja, ili kufika mwaka 2016, Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Songwe kitumike kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwanja wa ndege wa zamani uliopo katikati ya Mji wa Mbeya, Serikali itasubiri tu maoni ya Mipango Miji Mbeya, watueleze jambo gani wanataka lifanyike hapo. Bila shaka kupitia TAMISEMI, hayo watakatayoyapendekeza tutayapokea, kuyatathmini na kuchukua uamuzi kama tujenge hoteli, tujenge viwanda au tujenge miundombinu ipi kuweza kupatumia vizuri hapo ambapo kiwanja cha ndege kimekwishafungwa. Ahsante.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuelewa; katika Uwanja wa

Tabora kwanza tunashukuru umetengenezwa vizuri sana sasa. Je, Waziri atatuhakikishia lini wataweka taa ndege ziweze kutua na usiku?

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuweka taa za kuongozea ndege katika Uwanja wa Tabora linaenda sambamba na mpango mzima wa kujenga jengo la abiria na pia kuongezea ile nia ya kutua ndege, ambayo kwa Tabora ni njia mbili, moja imewekwa lami, nyingine inasubiri kuwekwa lami. Mpango mzima huu ambao una gharama kubwa kidogo, kwa bahati njema tumeshapata wafadhili na nitaeleza katika Hotuba yangu ya Bajeti, Siku ya Jumamosi. Kiwanja cha Tabora kitakaa vizuri tu na hakuna haja ya Wananchi wa Tabora kuwa na wasiwasi juu ya kiwanja hicho, Ninakifahamu, ninakitumia sana, kwa hiyo, mimi mwenyewe nitahakikisha kwamba, kinafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pia salamu kwa Kilimanjaro. Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro nao tunatumaini kuweka Jiwe la Msingi, KIA, ili uwe wa kisasa zaidi. Uweze kupokea ndege kubwa nyakati zote na tuweke ushindani kidogo na *Kenyatta International Airport* ya Nairobi, ambayo hivi sasa wanatuletea maneno yasiyofaa na sisi ni Taifa kubwa, hatuwezi kuwa hatuna uwanja ambao tunapokea watalii moja kwa moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Nami ningependa kumwuliza swali la nyongeza Mheshimiwa Waziri.

Miaka saba sasa imepita tangu katika eneo la Nkenge, maeneo ya Umkajunguti, Serikali iliahidi hasa wakati Rais wetu alipokuwa ametutembelea 2010 kwamba, tutajengewa uwanja wa ndege wa kimataifa kwa ajili ya kibiashara zaidi. Wananchi walisimamishwa kuendeleza kazi yoyote na ni sehemu ya kulima miwa, miti na vitu vingine.

Naomba kauli yako; hilo suala bado lipo; na kama lipo ni lini mtawafidia au waruhusuni waendeleo ili waweze kuzalisha na kupata mahitaji yao ya kila siku?

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijibu swali la Mheshimiwa Mshama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kinachotafutwa pale ni fidia na uwezo wa kulipa fidia sasa tunao. Kwa bahati njema, kama tulivyotoa taarifa katika Kamati yetu ya Miundombinu, Serikali imeruhusu Mamlaka ya Viwanja vya

Ndege (TAA), iweze kubaki na 100% retention. Asilimia ya retention ya TAA ni shilingi bilioni 60. Kwa hiyo, suala hili lililokuwa likitukwamisha tumelipangia katika mwaka huu wa fedha kuweza kulipa fidia katika eneo alilolitaja Mheshimiwa Mbunge, ili sasa tuweze kujenga kiwanja kipyua chenye hadhi pale Bukoba. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, isisahaulike kwamba, sasa hivi tumekwishamaliza uwekaji lami wa Kiwanja cha Ndege Bukoba, kile kilichopo na jengo jipya kabisa zuri, ili katika miaka ambayo tunasubiri kukamilisha ujenzi wa kiwanja kipyua, basi kiwanja hiki ambacho tunakizowea, tunachokitumia, kipo katika hali nzuri sana. Nami ningetegemea Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote wa Kagera, wangetoa mwaliko ili Waziri niende kule! Kama nilivyojibu mapema katika mambo mengine haya, huu ni wakati wa kuzungukazunguka huu; kwa hiyo, nikialikwa Bukoba, nikaalikwa Mbeya, nikaalikwa Chake-Chake Pemba, ni mambo mazuri tu nayatarajia. (Kicheko/Makofi)

Na. 81

Bei ya Nyumba za NHC

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA aliuliza:-

Shirika la Nyumba linajenga nyumba kwa ajili ya kuuza au kuwakopesha wafanyakazi na watu wengine na nyumba hizo nyingi ni ghorofa kwa matumizi mazuri ya ardhi:-

Je, flat/apartment moja yenye vyumba viwili inauzwa kwa bei gani na apartment moja ya vyumba vitatu inauzwa kwa bei gani?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Jimbo la Mji Mkongwe, kama ifutavayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na Mpango Mkakati wa Shirika la Nyumba la Taifa kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 hadi mwaka 2014/2015, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), linajenga nyumba kwa ajili ya kuuza kwa wananchi wa aina zote za vipato; yaani wale wa vipato vya chini, vya kati na juu. Ujenzi wa nyumba za ghorofa huwalenga wananchi wa vipato vya kati na vipato vya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya nyumba kwenye majengo ya ghorofa yanayojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa kwa ajili ya kuuzwa, hutofautiana

kulingana na gharama za ujenzi, thamani ya ardhi ya eneo husika, ukubwa wa nyumba, gharama za miundombinu, huduma zinazowekwa katika jengo, pamoja na gharama za mikopo endapo Shirika linakuwa limekopa kwa ajili ya ujenzi wa mradi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei za nyumba za vyumba viwili kwenye majengo ya ghorofa (*Apartments*) ni kati ya shilingi milioni 80.2 na shilingi milioni 96.9. Kadhalika, bei ya nyumba za vyumba vitatu kwenye majengo ya ghorofa au 3 *bedrooms apartments* ni kati ya shilingi milioni 186.8 na shilingi milioni 321. Bei hizi zinajumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

(i) Mheshimiwa Waziri, ukiangalia hali halisi ya Mtanzania na kipato alichonacho na nyumba hizi za kipato cha watu wa kati na juu ni bei kubwa sana na hailingani kabisa na maisha ya Mtanzania na wala Mtanzania wa kawaida hataweza kumiliki nyumba kulipa kwa bei hii. Je, hatuoni iko haja ya Serikali kutia mkono wake, yaani ku-*subsidy* ili wananchi wake wafaidike na majengo haya badala ya kuwatwika mzigo ambao hadi atakufa na kurithiwa hataweza kulipa deni la milioni 186 au 321?

(ii) Serikali ina mpango gani basi wa kufidia ili yapatikane yale maisha bora ya Mtanzania angalau kwa 50% kwa kipindi cha miaka 10 inayokuja ili watu waweze kuishi maisha bora katika nyumba hizo?

(iii) Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba, kuna nchi ambazo huwa zinatoa nyumba namna hii na hazizidi Dola elfu 28, yaani kama shilingi milioni 56 mpaka dola 30,000, yaani shilingi milioni 60. Nchi hizo zimepika hatua nzuri ya kuwapatia wananchi wake maendeleo ya kuwapatia nyumba za kisasa zilizo nzuri na bora na wao kuishi vizuri. Hamwoni kwamba, kuna haja ya kwenda kujifunza katika nchi hizo; mojawapo ni Moroko ili kusaidia wananchi wetu kupata nyumba za bei rahisi kuliko nyumba hizi ambazo ni kitendawili na zitakaliwa na watu wanaofanya kazi *TRA* peke yake?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, ameeleza namna ambavyo nyumba hizi ni ghali. Vilevile alitaka kufahamu Serikali ina mkakati gani wa kuweza labda kuipa ruzuku *National Housing* au kuiongezea fedha ili waweze kujenga nyumba nyingi zaidi za gharama nafuu.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimweleze kuwa, hivi sasa *National Housing* inachukua mikopo mbalimbali. Vilevile tunayo Sheria ya *Mortgage Financing*, ambayo kupitia Sheria hiyo, tumeanzisha *Tanzania Mortgage Financing Company* na imekuwa ikisaidia mabanki mbalimbali ambayo yanaweza kutoa mikopo kwa ajili ya benki zingine ili kuweza kupunguza gharama za mikopo ya nyumba. Sambamba na hiyo, sisi kama Serikali kwa kutambua hili, ukiangalia mzigo mkubwa pia uko katika VAT, Serikali imeanza kuchukua hatua na hivi sasa tuko katika mashauriano na vyombo mbalimbali Serikalini ili kuona ni kwa namna gani kwa hatua ya haraka tuweze kuondoa Kodi hii ya Ongezeko la Thamani au VAT ambayo ni asilimia 18. Tunaamini endapo itafanikiwa, hiyo ni hatua ya kwanza ya kupunguza gharama hizi za nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muuliza swali, swali lake lilikuwa kwenye nyumba za maghorofa, tunazo nyumba za chini, nitoe mfano Katavi, zipo nyumba za shilingi milioni 36 na tukiondoa VAT nyumba hizi ni shilingi milioni 30. Tukichukua kwa upande wa nyumba za Longido, tumeziua kwa shilingi milioni 51 bila VAT. Tukichukua nyumba za Kibada, bila VAT ingekuwa shilingi milioni 39, lakini tulipoziua kwa VAT ilikuwa shilingi milioni 46. Kwa hiyo, niseme tu kwamba, siyo nyumba zote ni za gharama juu, kama nilivyoeleza, hizi za maghorofani au *apartments* nyingi ni za watu wa kipato cha kati na cha juu.

Lengo letu, *National Housing* kama ilivyo Sera ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000 na kama ilivyo dhamira tangu mwaka 1962 Shirika hili lilipoanzishwa ni kwamba, tuhakikishe kwa kadiri inavyowezekana, tunahudumia watu wasio na kipato. Sisi kama Wizara, tumewapa maelekezo *National Housing*, kuangalia wanaweka jitihada gani kuhakikisha gharama hizi zinapungua kwa kadiri inavyowezekana. Kwa hiyo, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge, tutakapokuwa tukisoma bajeti yetu, huenda tutatangaza hatua zaidi ni nini tunachoweza kukifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la pili, ametolea mfano wa nchi ya Morocco. Napenda tu kumwambia, hatujaenda huko, lakini sisi tumeenda Uturuki, Malaysia na nchi zingine. Ukiangalia kwa nchi zingine hatua wanayoifanya, ukiangalia kwa hivi sasa kuna *mortgage*, huwezi ukalipa siku hiyo hiyo milioni 50; endapo utachukua mkopo wa nyumba wa milioni 10 mpaka milioni 20 na hivi sasa tuna benki takribani 40 zinazotoa mkopo wa nyumba, gharama kwa kweli itaweza kulipika, haitakuwa ambavyo unaiona hivi sasa milioni 40 kutoa mfukoni.

Ukiangalia kwa mkopo wa milioni 20 au 25 mfano wa *FNB*, kwa takribani riba ya asilimia 16, kama mtu analipa hivi sasa kodi ya nyumba kwa 400,000 au 500,000, angeweza kwenda kulipa mkopo wa nyumba benki kwa shilingi 200,000 mpaka 300,000 na bado nyumba ikawa yake. Bado sisi kama Serikali

tunajitahidi kuhakikisha kadiri inavyowezekana, tunashusha bei za nyumba hizi na ndiyo maana tumepanga kuanzisha taasisi au mamlaka itakayodhibiti bei mbalimbali za nyumba au *Real Estate Regulatory Authority* na tayari taratibu za kumpata mshauri mwelekezi zimekwishaanza, kwa hiyo, tunaamini hili litawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru.

MHE. ABAS Z. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mwaka 2007 kwenye Bunge hili tuli azimia nyumba za vipato vya chini kama Keko, Ubungo, Chang'ombe na pale kwa Mama Mfuko wauziwe wananchi wale. Cha kusikitisha hadi leo utekelezaji haujafanyika halafu yako mambo ya ujanja ya kutaka kuwaondoa wananchi wale. Sasa

Je, ni lini wananchi wale watakabidhiwa nyumba zile kama mnavyoendelea sasa hivi kujenga na kukabidhi nyumba kwa watu wengine?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mvemvu, Mbunge wa Temeke, ambaye ametaka kujua ni lini wananchi wanaoishi katika nyumba za *National Housing* zilizoko Keko, Ubungo na Chang'ombe na vilevile ameongezea kwa Mama Mfuko ni lini watakabidhiwa nyumba hizi.

Nipende kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba, huko nyuma ulikuwepo utaratibu wa *tenant purchase scheme*. Watu ambao walikuwa wakiishi kwa muda mrefu walikuwa wakizingatiwa katika kukabidhiwa nyumba hizo. Nipende tu kumwambia kwamba, tayari Mheshimiwa Waziri ametoa maelekezo suala hili liweze kuangaliwa. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge avute subira mpaka tutakapokamilisha suala hili, lakini tunalifahamu tunalizingatia na Mheshimiwa Waziri amelitolea maelekezo.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwanza, nawapongeza sana *National Housing* kwa kujenga nyumba Longido. Nyumba zilizojengwa kwa gharama ya sasa wananchi wa kipato cha chini hawawezi kununua kwa shilingi milioni 51.

Je, ni lini Serikali itapunguza VAT ili wananchi waweze kununua kwa sababu wanahitaji lakini wameshindwa kununua na nyumba zimemalizika na hakuna wananchi walioweza kumudu kufikia bei hiyo? Ni lini Serikali itapunguza

hiyo VAT iende milioni 31 ili wananchi wa kawaida waweze kuzinunua hizo nyumba? Nashukuru.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, nimpongeze Mheshimiwa Laizer, kwa namna anavyofuatilia maendeleo ya jimbo lake hususan suala zima la maendeleo ya makazi. Kama nilivyotangulia kusema wakati nikimjibu Mheshimiwa Sanya, Serikali tayari imeanza kulifanyia kazi suala zima la kuondoa VAT kuhusiana na nyumba mbalimbali za gharama nafuu. Kwa hiyo, wakati wa bajeti yetu tarehe 4 huenda tuja na majibu, lakini siwezi kusema tutakuja na majibu gani kwa sasa, lakini kama Serikali kupitia Kamati ya Huduma ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na kupitia Bunge hili Tukufu, imekuwa ikitoa maelekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tunalishughulikia na Serikali inayo nia na dhamira ya dhati kabisa katika suala hili. Ukiangalia mfano katika nyumba za Longido, takribani shilingi 9,180,000 ilikuwa inaenda kuwa VAT, kwa hiyo, endapo itaweza kupunguzwa kwa kweli itampa nafuu sana mnunuzi wa nyumba hizi.

Vilevile kwa kumwongezea Mheshimiwa Lekule Laizer na Waheshimiwa Wabunge, niwaambie tu kwamba, pamoja na jitihada zingine, tumewaelekeza pia *National Housing* kuhakikisha sasa kwa nyumba zinavyowezekana ziwe milioni 25 mpaka 30 ili kuweza kuwawezesha wananchi wengi kumiliki nyumba.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Bajeti yetu inalenga tujitegemee asilimia mia moja bila misaada kutoka nje. Hili la kusamehe VAT baadhi ya miji, baadhi ya majengo, italeti hasara kwa nchi yetu. Je, Waziri anahakikishaje kwamba anaweza kuwasaidia Watanzania nchi nzima vifaa vya ujenzi kuliko kuwabagua baadhi ya Watanzania ili wanufaike wachache na kule vijijini wasinufaike na majengo yao?

Utaihakikishiaje nchi hii kwamba tutajitegemea asilimia mia moja wakati mnasamehe VAT baadhi ya majengo na kusababisha iwe ni mtiririko wa kuiba hela za Serikali?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Keissy, kama ifuatavyo:-

Kwanza, haiwezi kuwa ni wizi, inategemea na dhamira yenyewe na naamini Mheshimiwa Mbunge ataelewa na atakubaliana na hilo. Kunapokuwa na madhumuni mahususi, kwa sababu kama hapa endapo tutasamehe,

tunakuwa hatujasamehe kiholela. Tumesamehe tukijua kila Mtanzania anastahili kuwa na makazi salama, makazi endelevu, ambayo tunaamini kwa makazi yale, anaweza akayatumia kama nyumba yake ya kuishi ikamhifadhi yeye na familia yake kwa usalama na ustahmilivu. Vilevile nyumba ile anaweza akaitumia kama dhamana na kuweza kupata mtaji na kwa kufanya hivyo, tunaamini kiuchumi tutaweza pia kuongeza uchumi na Pato la Taifa letu.

Kuhusiana na suala zima la vifaa, bado tunarudi pale pale, tutakapoweza kupunguza bei za vifaa, bado tunarudi kwenye suala hilo hilo zima la kodi. Kwa hiyo, nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge, aweze kutuunga mkono kwamba, Serikali inayo nia ya dhati katika kuhakikisha tunapunguza gharama mbalimbali za nyumba na vilevile kuweka mikakati ya makusudi au *tax measures* mbalimbali, kuhakikisha Watanzania wengi wanaweza kumiliki nyumba. Suala hili la vifaa pia nalo tumeanza kuliangalia, lakini siwezi kusema kwa sasa tutatumia utaratibu gani.

Na. 82

Umiliki wa Shamba la Mifugo la Razaba Makurunge Bagamoyo

MHE. JAKU HASHIM AYOUB aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha Shamba la Mifugo ya Ng'ombe huko Makurunge – Bagamoyo baada ya kupata ridhaa ya Serikali ya Muungano na kupatiwa Shamba la Razaba mnamo mwaka 1976:-

- (a) Je, Shamba hilo ni mali ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar?
- (b) Je, Serikali inaweza kuonyesha Hati Miliki ya Shamba hilo ambalo kwa muda mrefu halijulikani ukweli wake pamoja na vikao vingi kufanyika bila mafanikio?
- (c) Je, kuna ugumu gani wa kutoa hati ya umiliki wa Shamba hilo kwa kuwa tangu mwaka 1976 hati ya kumiliki ardhi ya Shamba hilo haijatolewa?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, lenye sehemu (a), (b) na (c), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shamba linalojulikana kwa jina la Ranchi ya Zanzibar Bagamoyo au Razaba, lilitolewa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa barua, yaani *Government Allocation Letter*, yenye Kumbu. Na. LD 14429/135/VB ya tarehe 21 Februari 1977. Shamba hili limetolewa kwa ajili ya

matumizi ya ufugaji wa ng'ombe na kilimo kwa Wananchi wa Zanzibar. Mwaka 2008 Shamba hilo liligawanywa baada ya makubaliano ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa na kupima mashamba mawili ambayo ni Shamba 3565 Makurunge, lenye ukubwa wa ekari 20,373 kwa ajili ya uwekezaji lililotolewa kwa Bagamoyo Eco-Energy na Shamba Namba 3564 lenye ukubwa wa ekari 6217 lilibaki chini ya umiliki wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2004 Mji wa Bagamoyo ulitangazwa kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Bagamoyo, kupitia Tangazo la Serikali Na. 353 na kujumuisha sehemu ya Shamba la RAZABA lililopo katika Kata ya Magomeni, Kitongoji cha Makurunge katika eneo la mji. Kufuatia eneo hilo kuwa ndani ya eneo la mpango, yaani *planning area*, uendelezaji wake unapaswa kuzingatia mpango kabambe kwa mujibu wa Kifungu cha 8 – 12 cha Sheria ya Mipangomiji ya Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rasimu ya Mpango Kabambe ya Mji wa Bagamoyo, yaani *Master Plan*, imeshaandaliwa na iko katika hatua ya kutolewa maoni na wadau wakiwemo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa vile hatua hiyo ina mchakato mrefu, kwa sasa Wizara yangu imeshatoa maelekezo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, kuanza taratibu wa umilikishaji wa Shamba hilo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Chuo cha Kilimo Kizimbani cha Zanzibar kulingana na matumizi yaliyoko sasa. Aidha, baada ya Mpango Kabambe au *Master Plan* utakaoongoza ukuuaji wa Mji wa Bagamoyo kukamilika, matumizi hayo yatahuishwa ili yanaendane na mpango huo.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kutojibu swali la msingi kama nilivyoliuliza na ya kuvunja moyo na hayaridhishi kabisa ukizingatia kuwa yeye aliwahi kuwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu haya ni ya kuvunja moyo. Naomba kuuliza maswali mawili tu madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa jambo hili linahusu Serikali ya Zanzibar na Muungano, ugumu umetoka wapi kutopatikana hati hii kwa kipindi chote hiki karibu nusu karne kutoka 1976 hadi leo; hiyo hati inaandikwa elfu moja, moja (a), (b), (c) haijakamilika mpaka leo? (Kicheko)

(ii) Kwa kuwa Zanzibar imeungana na Tanganyika, upatikanaji wa hati hii ya Zanzibar kuendelea kupoteza eneo kutoka ekari 20,373 mpaka kubaki ekari 6,271 kunaleta sura gani katika kuendeleza misingi yetu ya utawala kati ya Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar? Ni lini hati hii itapatikana? Kwa muda mrefu hati hii imedaiwa na Viongozi wetu Wakuu wakifuatilia suala hili bila mafanikio yoyote. Hii ni *try*, mchezo ni tarehe 4 kama ulivyosema wakati wa bajeti. (Kicheko)

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini hati imechelewa na kwamba muda mrefu tangu mwaka 1977 SMZ haijapewa hati; kwanza, nimweleze tu kwa mujibu wa Sheria zetu za Ardhi, huwa Serikali imekuwa haipeani au Taasisi za Serikali zimekuwa hazipewi hati. Kwa hiyo, si kwa makusudi hata kidogo na ndiyo maana kama ulisikia vizuri, nilieleza kwamba Februari 1977, SMZ ilipewa *Government Allocation Letter* au barua ya toleo la ardhi kwa Serikali. Imekuwa ikiitumia ardhi hiyo na haijabadhiwa kwa wakati wowote mpaka ilipofikia 2008, tulipotangaza kupitia Tangazo la Serikali kuweka mipango ya uwekezaji.

Kama nilivyoieleza katika jibu la msingi, Viongozi wetu wa Kitaifa wa Serikali mbili walikubaliana. Kwa hiyo, ukisema kama ni ujanja ujanja, kwa kweli sidhani kama unatenda haki. Kweli nilikuwa Naibu Waziri wa Katiba na ninaamini swali hili nimelijibu kikamilifu kama inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuweka uzito kwa suala hili, tumefanya vikao mara kwa mara hata na watangulizi wetu waliokuwa Waziri wa Ardhi Mheshimiwa Tibaijuka, lakini vilevile Mheshimiwa Ramadhani na Viongozi wengine wa Zanzibar, kujadili suala hili. Siyo kwamba tunaliwekea mchezo suala hili, tunalipa mkazo kuhakikisha kweli Chuo hiki cha Kilimo cha Kizimbani kinapata hati.

Ukiangalia huko nyuma, ilikuwa ni SMZ. Shamba hili likawa limeatelekezwa mwaka 1990, lakini bado Serikali bado inayo dhamira ya dhati; pamoja na kwamba Mji Mdogo wa Bagamoyo linaundwa na eneo hili limegeuzwa kuwa ni eneo la *beach hotel* na *recreational areas*, tayari tumewapa fursa SMZ kueleza hati yao apewe nani. Wameleta mapendekezo tarehe 9 Aprili 2014 kwamba, wapewe Chuo cha Kilimo cha Kizimbani na wameleta Mpango wa Matumizi ya Ardhi na tayari *detail land use plan* imekuwa ikifanyika kwa Serikali zote hizo mbili.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hati hii itatolewa haraka iwezekanavyo ifikapo tarehe 30 Juni. Naomba ushirikiano wa SMZ, lakini vilevile naielekeza Halmashauri ya Bagamoyo kulipa mkazo suala hili. Nakushukuru. *(Makofi)*

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kuuliza swali lifuatalo:-

Kwa mujibu wa maelezo ya Naibu Waziri, Shamba hili lilikuwa na urefu au ukubwa wa hekta 32,000, ambalo ndilo walilokabidhiwa Serikali ya Zanzibar. Hata kama imeonekana panatakiwa kufanywa Mradi; kwa nini wakapokonywa Serikali ya Zanzibar kwa ajili ya kufanyiwa huo Mradi?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, narudia kusema na nadhani mtu akisoma kwenye maelezo yangu mistari, *you can read between the lines* na unatambua Mheshimiwa Kombo hayo unayoyasema siyo sahihi. Kama nilivyoieleza, Shamba halikuwa la ekari 32,000, lilikuwa la ekari 28,000. Tayari nimeeleza Eco-Energy kupitia Shamba Na. 3565 wameshapewa hati na nimeeleza sababu kwa nini kwa SMZ ilikuwa hawajapewa hati.

Cha msingi ni dhamira tuliyonayo, katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano na SMZ, kushirikiana na kutambua kwamba SMZ nayo inaongozwa na Watanzania na ni Watanzania na wana haki ya kutumia ardhi hii kama Watanzania. Nipende kumhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge, hawakupokonywa, yalikuwa ni makubaliano baina ya Serikali hizi mbili kwa manufaa ya Taifa letu.

MHE. HAMAD ALI HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na nina swali moja.

Mheshimiwa Waziri katika jibu lako la msingi umesema Viongozi wa Kitaifa walishirikishwa katika makubaliano hayo. Je, katika ekari hizi 20,373 alizopewa mwekezaji Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshirikishwaje na wamepata faida kiasi gani tangu wakati huo? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri kwa kifupi!

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, alitaka kujua ni kwa namna gani SMZ imeshirikishwa katika kutoa shamba hili kwa Bagamoyo Eco-Energy. Kwanza, nimwambie kwamba, Bagamoyo Eco-Energy walipanga kuzalisha miwa kwa ajili ya kuzalisha sukari na umeme, lakini vilevile kwa ajili ya kupata *Bio-fuel* au mafuta ya kuendeshea magari. Serikali sasa ya SMZ itanufaikaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo Serikali ya Jamhuri ya Muungano, tumeingia Mpango wa *Land for Equity*, tunawekeza kwa pamoja baina ya Bagamoyo Eco-Energy pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Hivi sasa tayari mipango imeshafanywa kupitia Bagamoyo Eco-energy, ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano inamiliki asilimia 25 na *obviously interest* za SMZ katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano nazo ziko humo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba na SMZ inanufaika. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea, Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mbunge anayetegemewa Kibaha!

WABUNGE FULANI: *Super Star!*

Na. 83

**Ujenzi wa Barabara Sita Kutoka Dar es Salaam
hadi Mlandizi**

MHE. HAMOUD A. JUMAA aliuliza:-

Katika bajeti ya mwaka 2013/2014, Serikali ilikuja na mpango wa ujenzi wa barabara sita kutoka Dar es Salaam hadi Mlandizi, lakini katika bajeti ya mwaka 2014/2015 suala hilo halijazungumziwa kabisa:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani kuhusu mradi huo?
- (b) Je, ni lini mradi huo utanza utekelezaji wake?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kweli kuwa Barabara ya Dar es Salaam – Mlandizi haijazungumzwa kabisa katika Bajeti ya mwaka 2014/2015. Ikumbukwe kuwa, katika Kitabu cha Hotuba yangu ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2014/15, ukurasa wa 108 na 109, Mradi huo wa Barabara umetajwa kama *Dar es Salaam – Chalinze - Morogoro Expressway* na utajengwa kwa njia sita kati ya Dar es salaam – Mlandizi - Chalinze. Hivyo, sehemu ya Dar es Salaam – Mlandizi ipo ndani ya Mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali ni kujenga Barabara ya Dar es Salaam – Mlandizi – Chalinze, kilometa 100 kwa kiwango cha expressway na utekelezaji wake umekwishanza. Maandalizi ya Mradi huu utakaotekelezwa kwa ubia baina ya Serikali na Kampuni Binafsi (PPP), yameanza na yanaendelea vizuri. Mshauri Mwelekezi, Kampuni ya *Cheil Engineering Company* kutoka Korea Kusini anaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu pamoja na utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya kuingia mkataba na mwekezaji mbia. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2015.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwanza kukubaliana na Waziri na kumpongeza kwa jitihada kubwa hizo ambazo amezifanya mpaka sasa.

(i) Nataka kujua kwa sababu mwezi Juni uko karibu sana; sasa atuhakikishie lini Barabara ya Dar es Salaam mpaka Mlandizi Chalinze itaanza kutengenezwa?

(ii) Wakati unakuwa na mipango ya kutengeneza barabara kubwa lazima uwe na mipango ya muda mrefu na mipango ya muda mfupi. Sasa nilitaka kujua kipande cha kutoka Mlandizi Juu mpaka Ruvu Darajani na sisi Wabunge sote ni mashahidi, kipande kile kina tatizo kubwa na kinasababisha ajali nyingi sana kwa wananchi. Kwa hiyo, nilitaka kujua ni lini wanaweza kufanya maarifa na kushughulikia hicho kipande ambacho kinasumbua? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, napokea pongezi zake. Niseme tu kwamba, huyu *transaction advisor* ambaye ndiyo anatushauri katika Mradi huu, kwanza, ameshawasilisha ripoti ya awali ambayo inaonyesha njia ipi itapita hiyo *express way*. Katika Miradi hii ambayo itabidi watu walipie lazima uwe na *option* ambayo watu wengine wasiotaka kulipia watakuwa na barabara ya kutumia na ndiyo maana tumetumia muda mrefu. Katika hotuba yetu itakayosomwa Jumatano, tutaelezea kwa kirefu zaidi kuhusu Mradi huu.

Swali lake la pili kuhusu kipande cha Mlandizi - Chalinze ambacho kimeharibika, Serikali tumeweka fedha katika mwaka huu pia tuweze kuanza kufanya ukarabati mkubwa wa sehemu ambazo zimeharibika. Mwaka unaokuja pia tunategemea kuongeza fedha zaidi tuweze kukamilisha tatizo hilo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Idd Azzan, ajiandae Mheshimiwa Nchambi!

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maneno mchakato, usanifu, usanii, yanachosha sana kuyasikia. Kulikuwa na mpango wa kujenga *flyover* Dar es

Salaam katika kuondoa msongamano katika Jiji la Dar es Salaam, sambamba na hiyo barabara ya *highway* ya Chalinze, lakini hadi leo maneno ni hayo hayo; usanifu, usanii na mambo mbalimbali.

Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza Miradi hii kuliko kuendelea kuwadanganya Wananchi wa Dar es Salaam kama kana kwamba ni watoto wa kuku ambao wanaambiwa watanyonya kesho au keshokutwa? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Magufuli, Waziri wa Ujenzi!

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la rafiki yangu Mheshimiwa Azzan, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ujenzi wa barabara yoyote au daraja lolote au *flyover* yoyote, kitu cha kwanza ni lazima ufanye *feasibility study*, ambayo nayo ina-*involve* hela, lazima ufanye *detail design* ambayo nayo inahitaji hela, halafu ndipo unakuja kwenye *construction*. Kuhusu Barabara ya Dar es Salaam - Chalinze ambayo ina jumla kilometa 100, *transaction advisor* Kampuni ya *Cheil Engineering Company* kutoka South Korea na Makampuni mengine 11, mkataba umeshasainiwa kwa shilingi bilioni 7.72, *transaction advisor* yuko kwenye *site* na ile barabara itakuwa na *flyover* tano, nyingine itakuwa Charambe, nyingine itakuwa Mlandizi, nyingine itakuwa Chalinze na haya yote tutayafafanua katika bajeti yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *flyover* za Dar es Salaam, *fly over* ya TAZARA, *tender* zimeshatangazwa zitafunguliwa tarehe 29 Mei 2015 kule Japani. Mkataba utasainiwa tarehe 3 Juni kule Japani na Kandarasi ataanza kufanya kazi na gharama ya *flyover* ile itakuwa shilingi 93 bilioni. Kuhusu *interchange* ya Ubungo, ambayo nayo *feasibility study* na *detail design* zimeshafanyika chini ya ufadhili wa *World Bank*, *consultant* ameshateuliwa imeshatangazwa na *tender* zake za kumpata kandarasi kwa ajili ya kufanya kazi zile ziko kwenye *process*.

Kwa hiyo, nataka kuwathibitisha Waheshimiwa Wabunge wa Dar es Salaam na wananchi kwa ujumla kwamba, haya siyo maneno tu ya danganya toto, bali tunafanya juhudi kubwa za kuhakikisha Jiji la Dar es Salaam ambalo linachangia kiasi kikubwa katika Pato la Taifa, linatengenezwa barabara zake, *flyover*, *interchange* na kadhalika ili siku moja liwe Jiji ambalo halina msongamano. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nchambi!

MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, wabeja sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo shapu la Kishapu, kwanza kabisa, napenda nimpongeze Mheshimiwa Magufuli, Naibu na Wizara kwa ujumla, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Wizara ya Ujenzi ni miongoni mwa Wizara tatu ninazozijua mimi zinazofanya kazi ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa umakini.

(i) Kwa kuwa Kishapu ni miongoni mwa Majimbo ambayo yamefanikiwa Miradi mikubwa sana ya Maendeleo katika kipindi hiki cha Ubunge wangu. Miradi hiyo ni Miradi ya Maji ya Ziwa Victoria, Miradi ya Hospitali ya Kisasa ya Wilaya, Miradi mbalimbali ambayo imefanikiwa na Mawaziri wote ambao wamefanikisha Miradi hiyo tayari wamekwishafika Kishapu na wamepewa shukrani na Wananchi wa Jimbo la Kishapu kwa kutekeleza Miradi mikubwa.

(ii) Kwa kuwa unanza utekelezaji wa Mradi Kambambe wa Barabara ya Lami ya kutoka Mwingumbi kuelekea Maswa Bariadi na Lamadi. Uko tayari kabla ya Bunge hili kuvunjwa ufike katika Kijiji cha Mwingumbi, Kata ya Mondo, Tarafa ya Mondo, Jimbo la Kishapu, Wilaya ya Kishapu, yenye wananchi Shapu, waje wakupe shukrani za dhati kutoka katika mioyo yao kwa ajili ya kuwatekeleza Mradi Kambambe wa Barabara ya Lami? *Wabeja sana. (Makofi)*

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali na ombi la Mheshimiwa Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Miradi yote inayofanyika katika nchi hii ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, ambayo msimamizi mkubwa ni Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. *(Makofi)*

Kwa vile *tender* za barabara ya kutoka Mwingumbi hadi Maswa zimeshatangazwa na Kandarasi ameanza kufanya *mobilization* ili barabara ile ikaunganishwe na Barabara ya Lamadi kuja Bariadi, yenye jumla ya Kilometa 71.8; nataka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge ambaye ni mchapakazi sana kwamba, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, atakuja kuweka Jiwe la Msingi katika barabara hiyo ya Mwingumbi kwenda Maswa na sisi vibarua wake tutakuwepo tukiwa tunamsindikiza. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Dkt. Grace Puja kwa niaba ya Mheshimiwa Ritta Kabati!

**Watoto Wanaotelekezwa na Kuishi Katika
Mazingira Hatarishi**

MHE. RITTA E. KABATI (K.n.y. MHE. DKT. GRACE K. PUJA) aliuliza:-

Hapa nchini kuna idadi kubwa ya watoto wa mitaani ambao wanaishi katika mazingira hatarishi kutokana na kutelekezwa na familia zao:-

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu wanaume wanaozaa watoto nje ya ndoa na kisha kuwatelekeza?

(b) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wanawake wanaotelekeza watoto kwa lengo la kuanzisha maisha mapya na wanaume wengine huku watoto wao wakilelewa na babu na bibi zao?

(c) Je, Serikali haioni kuwa kwa kutolipa kipaumbele suala hili inachangia kujenga tabaka la watu waliotelekezwa ambao wanaweza kutishia amani na usalama wa nchi?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya ... *Jesus! (Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa mwacheni. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sana kwa usumbufu uliojitokeza, kwa sababu wamebadilisha maswali lilikuwa liwe la...

MWENYEKITI: Ni kweli Waheshimiwa Wabunge, tatizo ni langu mimi na siyo la Mawaziri.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Grace Khwaya Puja, Mbunge wa Kuteuliwa, lenye vipengele (a), (b) na (c), kuhusu watoto wanaotelekezwa na kuishi katika mazingira hatarishi kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakemea vikali tabia ya wanaume na wanawake wanaozaa watoto nje ya ndoa na kisha kuwatelekeza. Tabia hii ni kinyume cha haki na ustawi wa mtoto kama ilivyo katika Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Mwaka 2009, Kifungu Namba 9, kinachoelekeza wajibu wa wazazi kumpatia mtoto haki zake za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu atakayehusika na makosa ya kumnyima kwa makusudi mtoto haki hizi kwa kumuumiza au kumpunguzia hadhi yake, Sheria itaendelea kuchukua mkondo wake kama ilivyoelekezwa katika kifungu namba 14 cha Sheria hii kuwa, atatozwa faini isiyopungua shilingi laki tano, kifungo cha miezi sita au vyote pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatoa wito kwa wananchi kuhakikisha kuwa, haki za mtoto zinazingatiwa kwa kutoa taarifa kwa mamlaka husika, pale inapotokea mzazi au mlezi amemtelekeza mtoto kama Kifungu Namba 95 cha Sheria ya Mtoto kinavyoelekeza kuwa ni wajibu wa kila mwanajamii kutoa taarifa pale anapona haki za mtoto hazizingatiwi na mzazi au mlezi. Aidha, Serikali za Mitaa zina wajibu wa kufuatilia na kuwarejesha watoto na kuwachukulia hatua wazazi wanaowatelekeza watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inalipa kipaumbele kikubwa suala la malezi na makuzi ya watoto na ndiyo maana imetunga Sera, Sheria na kuweka Mikakati na Mipango mbalimbali ya kuimarisha mifumo ya malezi, matunzo na ulinzi wa mtoto katika ngazi ya Taifa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo ya Watoto. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi Jamii, TAMISEMI na Wadau wengine, tunatekeleza Mpango Kazi wa Jamii wa Kudhibiti Tatizo la Watoto Wanaoishi au Kufanya Kazi Mitaa ni wa 2014 - 2017 na ule wa Huduma za Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi wa mwaka 2013 - 2017. Mipango ambayo imejikita katika kuimarisha mifumo ya utoaji huduma, mkazo ukiwa kuwajengea uwezo wa kiuchumi familia na kaya maskini ili ziweze kujitegemea na kutoa huduma bora na endelevu kwa watoto wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kuwa, kupitia utekelezaji thabiti wa mikakati hii, tutakuwa na kizazi kilichoengeka kimaadili na kuwa na Taifa Bora. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kabati!

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba kuuliza maswali madogo mawili tu.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili.

(i) Kwa kuwa kuna baadhi ya wazazi na walezi wamekuwa wakiwatumia watoto wao kwenye biashara ya kuombaomba. Ukichukua mfano wa Dar es Salaam, nafikiri wewe mwenyewe unajua kwenye Wilaya yako, unakuta watoto wadogo kabisa ambao wanaweza kwenda kusoma kwenye shule za

chekechea mpaka shule za sekondari bado wanatumia na wale wazazi kuombaomba. Wale wazazi wamekaa kandokando ya barabara wakiwasubiri wale watoto labda walete riziki jioni. Je, Serikali inalitambua hilo; kwa sababu hawa wazazi wapo na wengine wamezaliwa humo humo kwenye maeneo ambayo hao ombaomba wanakaa? Hatua gani imechukuliwa na Serikali kuhakikisha hawa wazazi hawarudii tena tabia hiyo mbaya ili iwe fundisho kwa wazazi wengine au walezi wengine?

(ii) Ukitembelea katika miji mikubwa unakuta watoto wengi sana sasa hivi wamesambaa, wametoka vijijini wanaenda kuomba kwenye miji mikubwa, kwa mfano, Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, hata hapa Dodoma, jioni unakuta vijana wanaombaomba. Je, chanzo ni nini na hatua gani inachukuliwa ili tatizo lisiendelee tena kwa watoto kwenda kuombaomba badala ya kwenda kusoma?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi!

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Ritta Kabati, kwa kujali haki za watoto. Kimsingi ni kweli kwamba, kuna watoto wanatumika kuombaomba barabarani.

Namba moja, Serikali imehakikisha kwamba, umri wa watoto lazima wawe mashuleni, ndiyo maana Serikali imefuta ada za shule za msingi. Kwa hiyo, ni ajabu sana tunapona wazazi wanawatumia wale watoto kwenda kuombaomba wakati ambapo watoto wale wanapaswa kuwa katika shule zetu za msingi, ambapo hakuna ada kabisa. Hivyo, kupitia swali hili naomba nsieme kwamba, tuna Kamati za Ulinzi wa Mtoto, Halmashauri zetu zinapaswa kufanya jitihada za kutosha kuhakikisha watoto wale wanaondoka katika mitaa yetu, katika vitongoji vyetu na vijiji na wawepo katika shule zetu madarasani.

Sababu zinazopelekea watoto wa mitaani ni nyingi. Utafiti umeonyesha kwamba, asilimia 40 ya sababu zinazopelekea ni ukatili. Sasa hivi kwenye nyumba zetu kuna ukatili wa kila aina; vipigo, kunyimwa chakula na sababu mbalimbali. Sababu nyingine ni kuparaganyika kwa ndoa, hiyo pia imeonyesha wazazi wanapokuwa mbalimbali, mtoto anaenda kwa mzazi baba, anaenda kwa mzazi mama, wakati mwingine kunakuwa na miparaganyiko.

Hali ya maisha pia ni sababu nyingine. Baadhi ya maeneo imeonekana hali ya uduni wa maisha ni baadhi ya changamoto. Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuboresha hayo yote ikiwa ni pamoja na Miradi

mbalimbali; kwa mfano, kuna Miradi ya TASAF kusaidia kaya maskini waweze kuwa na vipato na masuala kama hayo.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Nishati na Madini; Mheshimiwa Njwayo kwa niaba ya Mheshimiwa Mkapa!

Na. 84

**Miundombinu ya Kusambaza Gesi Mikoa
ya Lindi na Mtwara**

MHE. DUNSTAN D. MKAPA (K.n.y. MHE. JUMA A. NJWAYO) aliuliza:-

Ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam umekaribia kukamilika:-

Je, ni lini miundombinu ya uhakika ya kusambaza gesi hiyo Mkoani Mtwara na Lindi itaanza kujengwa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kusambaza Gesi Asilia katika Mji wa Lindi na Mtwara ni Mradi wa kipaumbele kwa Serikali. Upembuzi yakinifu umekwishakamilika na umefanywa na Mshauri Mwelekezi Kampuni ya Kitanzania iitwayo *Fabcast Technologies Co. Ltd.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016, Serikali imeomba kutengewa kiasi cha shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kufanya usanifu wa kihandisi na kimazingira (*Environmental and Social Impact Assessment*) ili kuanza utekelezaji wa Mradi huu.

MHE. DUNSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize maswali mawili kama ifuatavyo:-

(i) Bomba hili la gesi linapita katika baadhi ya vijiji ndani ya Mkoa wa Mtwara na Lindi. Je, wanavijiji hawa watanufaika vipi na Mradi huu?

(ii) Wizara ya Nishati na Madini iliniandikia barua ikiorodhesha vijiji ambavyo vitapatiwa umeme katika Mpango Kabambe wa REA Namba Mbili, lakini mpaka sasa huu ni mwezi wa tano na walisema mwisho mwezi wa sita, sijaona kitu chochote kinafanyika ndani ya wilaya yangu. Sijui Wizara inasemaje kuhusu hili?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI YA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE):
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Mkapa, kama ifuatavyo:-

Bomba la gesi kutoka *Mnazi Bay*, mpaka Dar es Salaam litakuwa na matoleo ambayo yataweza kugawa gesi kwa vijiji au maeneo ya kiuchumi kama kuendesha viwanda, lakini vijiji vyote *along the pipeline*, wataweza kupata huduma za maji na huduma za umeme.

Vijiji ambavyo tulikuandikia barua, pamoja na wananchi wote wa Lindi na Mtwara hususan njia ya bomba, Serikali imetenga kiasi maalumu cha fedha na Mheshimiwa Waziri wangu, alikwenda Mtwara akawaambia kwamba, vijiji vyote 100 vitapata umeme na ndiyo kazi ambazo zinatuzungusha nchi nzima, tunahakikisha umeme vijiji 100 vya Lindi na Mtwara vyote unapatikana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha. Sasa nitawatambua wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; Wageni wa Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kutoka Wizarani kwake wakiongozwa na Bi. Anna Maembe - Katibu Mkuu, Bi. Nuru Milalo - Naibu Katibu Mkuu, Bi. Rukia Masasi - Mwenyekiti wa Taifa NGOs, Bi. Marry Luwilo - Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya NGOs, Ndugu Ismail Suleiman - Katibu Baraza la Taifa la NGOs, Bi. Fortunata Temu - Mwakilishi wa UN Women, Bi. Magreth Chacha - Mkurugenzi wa Benki ya Wanawake, Ndugu Anatory Bunduki - Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Wakurugenzi Wakuu wa Vitengo na Wataalam mbalimbali wa Wizara na Maafisa 30 kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni familia yake; Ndugu Adinani Saku Kondo, mtoto wake, Ndugu Giji Kondo, mtoto wake, Bi. Joyce Simba, mdogo wake, Bwana Abdulaziz Mwinjuma, mtoto wake na wageni wanane ambao ni ndugu na marafiki wa Mheshimiwa Waziri, Wanakwaya 26 kutoka *Haleluya Gospel Choir*, Tabata Dar es Salaam.

Wageni wa Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Waziri wa Kazi na Ajira, wakiongozwa na Ndugu Erick Shitindi - Katibu Mkuu, Dkt. Akwilina Kayumba -

Mtendaji Mkuu OSHA, Ndugu Cosmas Msigwa - Mkurugenzi CMA, Ndugu Irene Isaka - Mkurugenzi Mkuu SSRA, Ndugu Juma Muhimbi - Mwenyekiti wa Bodi ya SSRA, Ndugu Abubakar Rajab - Mwenyekiti wa Bodi ya NSSF, Dkt. Ramadhan Dau - Mkurugenzi Mkuu NSSF, Ndugu Nicholas Mgaya - Katibu Mkuu, Ndugu Idrisa Mavura - Mwenyekiti Tume ya Usuluhishi na Uamuzi CMA, Ndugu Samwel Nyatahe - Mwenyekiti RESCO, Ndugu Masha Mshomba - Mkurugenzi Mkuu Mfuko wa Fidia, Ndugu Erigon Moshi - Kaimu Mkurugenzi ILO na Wakurugenzi, Makamishna Wakuu wa Vitengo na Taasisi zilizo chini ya Wizara. (Makofi)

Wageni wa Mheshimiwa John Mnyika kutoka Kijiji cha Hombolo Makulu, Kata ya Hombolo Dodoma, ambao ni Ndugu Pascal Maziku, Ndugu Melania Dalali kutoka Dar es Salaam, Ndugu Emmanuel Mahumbule, Ndugu Martha Emmanuel, Ndugu Michael Nyagulu, Ndugu Sabina Nyagulu, Ndugu Emmanuel Nyagulu, Ndugu Anna Nyagulu na Alex Soya. (Makofi)

Wageni wa Mheshimiwa Abbas Mtemvu ni Bi. Mariam Mtemvu, mke wake, Ndugu Sitti Mtemvu, mtoto wake, Ndugu Tamia Mtemvu, mtoto wake na Ndugu Matukio, Mratibu wa *Sitti Foundation*. (Makofi)

Wageni waliopo kwa ajili ya mafunzo Bungeni; wanafuzi 60 na walimu 10 kutoka Shule ya Sekondari Makole Dodoma; karibuni Dodoma.

Wapo wanafunzi 23 kutoka Chuo Kikuu cha Iringa Tumaini; karibuni Dodoma.

Yupo Ndugu Elias Nawela, Mwanasheria kutoka Dar es Salaam, Jimbo la Kawe.

Matangazo ya kazi; Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa, kutakuwa na kikao leo saa nane katika Ukumbi wa Msekwa B, Jengo la Pius Msekwa.

Katibu wa Wabunge wa CUF, Mheshimiwa Rukia Kassim, anaomba kuwatangazia Wabunge wote wa CUF kuwa, leo saa nane katika ukumbi huo huo wa Pius Msekwa, mara tu baada ya kikao cha asubuhi.

MWONGOZO

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Mwenyekiti, -ahsante. Kanuni ya 68(7) ndiyo iliyonisimamisha hapa. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, alipokuwa akijibu swali nililoliuliza, alisema tarehe 30 Juni hati hii itapatikana, lakini hakusema kama ni Juni mwakani au mwaka huu. Katika kukabidhi hati hiyo, napigia kelele suala hili, ikiwa mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo kwa

upande wa Zanzibar. Lini ataikabidhi na mimi nikawe shahidi katika makabidhiano hayo? (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jaku, mwongozo wako majbu yake tutalifuatilia na utapewa jibu leo hii na Waziri.

Katibu, hatua inayofuata!

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2015/2016 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

na

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2015/2016 Wizara ya Kazi na Ajira

MWENYEKITI: Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, dakika 40!
Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka 2015/2016 kama yalivyowasilishwa Bungeni

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia Taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, iliyoichambua bajeti ya Wizara yangu, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka 2015/16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na Utukufu, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu nikiwa na afya njema na hivyo kuweza kushiriki Mkutano huu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii, kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta Mohammed Gharib Bilal - Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda - Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wao mahiri na maelekezo yao ambayo yamewezesha kushamiri kwa usawa wa jinsia na uzingatiaji wa haki za mtoto katika jamii ya Watanzania. Mwenyezi Mungu, awajalie afya njema ili waendeleo kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa uendeshaji mahiri wa shughuli za Bunge. Namwomba Mwenyezi Mungu, awajalie afya njema ili muweze kusimamia na kuratibu shughuli za Bunge kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, ikiongozwa na Mwenyekiti mahiri, Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, kwa kuchambua na kujadili bajeti ya Wizara yangu. Ushauri na maelekezo ya Kamati hiyo, yamewezeshwa Wizara yangu kuandaa bajeti kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Wabunge waliochaguliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivi karibuni, ambao ni Mheshimiwa Dkt. Grace Khwaya Puja na Mheshimiwa Innocent Rwabushaija Sebba. Aidha, napenda pia kuishukuru familia yangu wakiwemo watoto wangu na wadogo zangu, kwa kunitia moyo wa kuendelea kutekeleza majukumu yangu, wakiwemo na marafiki zangu pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kutoa salamu za pole kwako na Bunge lako Tukufu, Familia na Wananchi wa Jimbo la Mbinga Magharibi, kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge wao na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Kapteni Mstaafu John Damiani Komba. Bunge hili na Taifa kwa ujumla litamkumbuka daima kwa michango yake. Aidha, kwa masikitiko makubwa natumia fursa hii kuwapa pole wale wote waliopatwa na majanga ya ajali na mafuriko pamoja na kufiwa na ndugu, jamaa na wapendwa wao katika matukio mbalimbali yaliyotokea hapa nchini. Nitangulize dua zangu kwa Mwenyezi Mungu, awapokee na kuwalaza mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imetekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2015. Maeneo makuu manne yaliyotekelezwa yanahusu: Ajira na Uwezeshaji wa Wananchi; Elimu ya Juu, Uendelezaji wa Makundi Mbalimbali; na Demokrasia na Madaraka ya Umma. Katika kipindi husika, utekelezaji wa maeneo hayo umekuwa wa mafanikio kama inavyoelezwa kwa kirefu kwenye Kitabu cha Hotuba yangu, ukurasa wa 4 hadi 9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuelezea kwa kifupi hali halisi ya Sekta ya Maendeleo ya Jamii katika maeneo ya ushiriki wa wananchi katika maendeleo ya kiuchumi, maendeleo ya kijinsia, maendeleo ya watoto na mchango wa mashirika yasiyo ya kiserikali katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii ni muhimu katika kuhamasisha na kuwezesha ushiriki wa wananchi katika kujitea maendeleo yao na Taifa kwa ujumla. Dhana ya maendeleo ya Jamii inatumia mbinu shirikishi inayojenga na kuimarisha misingi ya watu katika jamii kujitambua, kutumia uwezo walionao, kubaini matatizo yao, fursa na rasilimali walizonazo, kupanga na kutoa maamuzi ya kazi au miradi ya kutekeleza ili kutatua kero na matatizo yao.

Umuhimu wa Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii umeendelea kutambuliwa na wadau mbalimbali kutokana na mchango wao katika maendeleo ya Taifa letu katika kuhamasisha, kuraghabisha, kushauri, kushawishi na kuelimisha wananchi na viongozi wao kwa kuwapatia elimu, maarifa na taarifa mbalimbali ili kuwaongezea uelewa, uwezo wa kufikiri na kufanya maamuzi sahihi ya utekelezaji wa dhana hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii, Sekta hii bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo vitendea kazi na kutokuwepo kwa wataalamu wa kutosha katika ngazi mbalimbali kama Sera ya Maendeleo ya jamii inavyoelekeza; kwa mfano, katika ngazi ya Kata kuna upungufu wa Wataalamu 2,029.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara inaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma juu ya uwezekano wa kuwaajiri Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii moja kwa moja kutoka vyuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya Taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Astashahada katika Vyuo vyake vya Buhare, Rungemba, Missungwi, Monduli, Uyole, Ruaha, Mlale na Mabughai. Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kilipandishwa hadhi na kuwa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru kupitia Azimio la Bunge Na.1 la Mwaka 2014. Aidha, udahili wa wanafunzi katika Taasisi ya Tengeru na vyuo vingine vinane vya Maendeleo ya Jamii umeendelea ukiongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi katika wilaya mbalimbali nchini. Vyuo hivi vinatoa mafunzo na stadi kwa wananchi sanjali na mafunzo ya ufundi stadi kwa kushirikiana na VETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vinakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo; mahitaji makubwa ya rasilimali fedha na upungufu wa watumishi hususan wakufunzi, ubovu na uchakavu wa majengo na miundombinu, ukosefu wa

vifaa vya kufundishia na kujifunzia, vyombo vya usafiri na maeneo ya vyuo kuvamiwa na wananchi kwa shughuli za kilimo na ujenzi wa makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya usawa wa kijinsia katika nyanja mbalimbali hapa nchini imeendelea kuimarika katika maeneo ya ushiriki wa wanawake katika siasa na ngazi za maamuzi, uwezeshaji wanawake kiuchumi, elimu, mafunzo, ajira na upatikanaji wa haki za wanawake kisheria. Takwimu zilizopatikana kupitia Taarifa ya Hali ya Jinsia Nchini (*Tanzania Country Gender Profile*) ya 2015, zinathibitisha uimarishaji huo ingawa bado kuna changamoto mbalimbali zinazotokana na mila na desturi kandamizi.

Wizara inachukua hatua mbalimbali kupambana na changamoto hizi kwa kushirikiana na wadau hasa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Aidha, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kuzuia na Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake, Watoto na Albino wa 2001 - 2015, kwa kuijengea uwezo Kamati hii ili iweze kushughulikia masuala ya ukatili, kuratibu Kampeni za Utokomezaji Vitendo vya Ukatili Dhidi ya Wanawake ili kuongeza uelewa wa madhara ya vitendo vya ukatili katika jamii na kuandaa Mwongozo wa Kuzuia na Kudhibiti Ukatili wa Kijinsia kwa Kamati za Vijiji, Mitaa, Kata na Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwezesha wanawake kiuchumi, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kutoa mikopo kwa wanawake wengi kupitia Benki ya Wanawake, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, kutoa mafunzo ya ujasiriamali na uwekaji wa akiba na kushiriki katika maonesho mbalimbali. Aidha, changamoto katika eneo hili ni mahitaji makubwa ya mikopo, mafunzo ya ujasiriamali yanayotolewa kwa wakopaji kutotosheleza kujenga uwezo unaohitajika, marejesho hafifu ya mikopo, mahitaji makubwa ya huduma za Benki ya Wanawake Tanzania hususan kwa wanawake wajasiriamali, idadi ndogo ya wanawake katika nafasi za uongozi na maamuzi hasa vijijini, ndoa na mimba za utotoni na mila na desturi zenye madhara kwa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na baadhi ya changamoto, Wizara imefanya tathmini ya uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ili kuuboresha utendaji wake na kufungua vituo zaidi vya kutolea mikopo vya Benki ya Wanawake Tanzania katika Wilaya zote za Mikoa ya Mwanza, Dar es Salaam na Dodoma na kuendelea kutoa elimu juu ya madhara yatokanayo na mila potofu ili jamii iachane nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sensa ya Idadi ya Watu na Makazi Nchini ya Mwaka 2012 ilibainisha kuwa, Tanzania inakadiriwa kuwa na watoto 24,377,052 walio chini ya umri wa miaka 18. Kati yao 12,201,122 ni wasichana na 12,175,930 ni wavulana, sawa na asilimia 50.1 ya Watanzania. Kundi hili linahitaji mipango madhubuti ya kuhakikisha kuwa wanapata haki zao zote za msingi, ambazo ni

kuishi, kuendelezwa, kulindwa, kushiriki na kutobaguliwa ili watakapokua waweze kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba, watoto nchini wanapata haki hizo za msingi, Wizara yangu imefanya mapitio ya Sera ya Mtoto ya Mwaka 2008 kwa kuingiza masuala ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto na kutoa ufafanuzi wa mahitaji ya mtoto kiumri na wajibu wa wazazi au walezi, jamii na Taifa. Aidha, tumeendelea kuratibu shughuli za Kikosi Kazi cha Taifa cha Kuzuia na Kupambana na Ukatili Dhidi ya Watoto ambacho hutoa taarifa za utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Mwitikio na Kuzuia Ukatili Dhidi ya Watoto kuanzia mwaka 2013 hadi 2016 kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Pia tumeandaa kijitabu (zana) cha mawasiliano cha kuzuia ukatili dhidi ya watoto Tanzania. Kijitabu hiki kitatumika katika kutoa elimu ya malezi katika ngazi za familia na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuwa watoto wanashirikishwa katika kuamua mambo yanayowahusu, Wizara yangu imeendelea kuratibu uanzishwaji wa Mabaraza ya Watoto katika ngazi mbalimbali na kusimamia shughuli za Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Idadi ya Mabaraza ya Watoto katika ngazi ya Mikoa yameongezeka kutoka 12 mwaka 2005 hadi kufikia Mabaraza 22 mwaka 2014 na Wilaya kutoka Mabaraza 57 mwaka 2005 hadi kufikia Mabaraza 93 mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utekelezaji wa mipango na mikakati iliyopo na mafanikio yaliyopatikana, bado kuna changamoto mbalimbali katika kusimamia na kuratibu utoaji wa haki za watoto hapa nchini. Changamoto hizo ni pamoja na kuendelea kwa mila potofu kama vile ukeketaji, ndoa na mimba za utotoni, kufanyishwa kazi zisizolingana na umri wao na katika mazingira hatarishi katika mashamba, migodi, viwanda, uvuvi na majumbani. Aidha, idadi ya watoto wanaoishi mitaani imeongezeka kwa kasi hapa nchini hasa katika majiji, miji mikubwa na mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa zinazochangia matatizo haya ni pamoja na umaskini, uelewa mdogo wa jamii kuhusu haki za mtoto, mamlaka mbalimbali kushindwa kuchukua hatua stahiki ili kukabiliana na matatizo hayo pamoja na mila na desturi zenye madhara kwa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Mwaka 2001 na Sheria ya NGOs Na. 24 ya Mwaka 2002 kama ilivyorekebisha mwaka 2005, zimechangia kuimarisha utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kutoa huduma kwa jamii katika masuala mbalimbali umeendelea kuimarika.

Mchango huo unaonekana zaidi katika Sekta ya Maendeleo ya Elimu, Afya, Maji, Maendeleo ya Jinsia, Maendeleo Shirikishi, Mazingira, Ustawi wa Jamii, Kilimo, Utawala Bora, Haki za Binadamu, Huduma za Sheria na Ujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yameendelea kukuza fursa ya ajira kwa kuhimiza na kutekeleza vyema dhana ya kujitolea. Taarifa ya mwaka 2012 ya Wizara kuhusu mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maeneo inaonesha kuwa, mashirika haya yaliajiri jumla ya watu 60,700 ambapo kati yao, watu 27,312 wanafanya kazi kwa kujitolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uwepo wa michango mingi na mizuri ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, bado kuna changamoto mbalimbali zikiwemo mashirika mengi Yasiyo ya Kiserikali kujikita zaidi mijini badala ya vijijini, kuendelea kutegemea ufadhili wa nje katika kutekeleza shughuli na ukiukwaji wa Sheria ya NGOs.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutatua changamoto hizo, hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa NGOs kuhusu umuhimu wa taasisi hizi kuwafikia wadau wengi zaidi nchini hususan vijijini. Kuendelea kuyahimiza Mashirika haya kutumia fursa ya marekebisho ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2005 kwa kuanzisha miradi ya kujipatia kipato kinachoweza kuepukana na utegemezi uliokithiri kwa wafadhili wa nje katika kuwahudumia walengwa wao na kufuta NGOs zinazofanya kazi kinyume na malengo ya kuanzishwa kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu NGOs, mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizopo, yapo kwenye Ukurasa wa 23 hadi 27 wa Kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Wizara yangu iliendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu yake kulingana na malengo na shabaha zilizopangwa. Katika bajeti ya mwaka 2014/15, Wizara ilikisia kukusanya jumla ya Shilingi bilioni moja milioni mia nane arobaini na tano laki tatu na sitini kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi Machi 2015, makusanyo yalifikia Shilingi bilioni moja milioni mia nane kumi na tano laki moja arobaini na tano na mia sita, sawa na asilimia 98.4 ya lengo. Aidha, Wizara iliidhinishiwa jumla ya Shilingi bilioni ishirini na tisa milioni mia nne hamsini na tatu laki tano na tisini na tisa ambapo kati ya hizo, Matumizi ya Kawaida ni Shilingi bilioni ishirini milioni mia tano ishirini na sita na hamsini na tano elfu, yakijumuisha Shilingi bilioni kumi na mbili milioni mia nane kumi na nane laki nne na thelathini na nne kwa ajili ya mishahara na Shilingi bilioni saba milioni mia saba na saba laki sita na ishirini na moja kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Bajeti ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishwa ni Shilingi bilioni nane milioni mia tisa ishirini na saba laki tano arobaini na nne.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili 2015, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi bilioni nane milioni mia sita thelathini na tisa laki mbili thelathini na moja na mia tisa na tatu, sawa na asilimia 67 ya Bajeti ya Mishahara iliyoidhinishwa na matumizi yakiwa bilioni nane milioni mia tatu thelathini na tisa laki mbili thelathini na moja mia tisa na tatu sawa na asilimia 100 ya fedha za Mishahara zilizotolewa. Matumizi Mengineyo Shilingi bilioni tatu milioni mia mbili sitini laki nane ishirini na tano na sitini, sawa na asilimia 42 ya fedha za matumizi mengineyo zilizopokelewa na kutumika Shilingi bilioni tatu milioni mia mbili sitini laki nane na ishirini na tano, sawa na asilimia 100 ya fedha zilizotolewa na kutumika. Aidha, fedha za ndani za maendeleo Shilingi bilioni moja milioni mia saba zilitolewa, sawa na asilimia 25 ya fedha za ndani zilizoidhinishwa na Shilingi milioni mia tatu thelathini na nane laki sita thelathini na nne fedha za nje, sawa na asilimia 17 ya fedha za nje zilitolewa na kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha utekelezaji wa Mwaka 2014/15 na malengo ya mwaka 2015/16 kwa kuzingatia maeneo yafuatayo:-

Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya Taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Astashahada ambapo jumla ya wanachuo 1,885 walidahiliwa katika mwaka 2014/15. Kati yao wanaume 758 na wanawake 1,128. Aidha, katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru wanachuo 276 walidahiliwa katika ngazi ya Shahada ambapo wanaume walikuwa 87 na wanawake 189. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kudahili na kutoa mafunzo kuanzia ngazi ya Astashahada hadi Stashahada ya Uzamili na pia kukamilisha jengo la maktaba katika Chuo cha Tengeru, ujenzi wa uzio wa Chuo cha Rungemba na Ruaha, kujenga jengo la utawala na jengo la maktaba, ukumbi wa mikutano, nyumba za watumishi katika Chuo cha Uyole, kukarabati majengo na miundombinu katika Vyuo vya Buhare, Mlale, Ruaha, Mabughai, Missungwi na Monduli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Vyuo vitano vya Maendeleo ya Wananchi vya Sofi, Mputa, Kilwa Masoko, Tarime Mwanhala vilifanyiwa ukarabati wa madarasa, mabweni, majengo ya utawala, ujenzi wa vyoo, mabwalo ya kulia chakula, miundombinu ya umeme, maji safi na maji taka. Aidha, Vyuo vya Nandembo, Sengerema na Chala vilipewa magari ili yatumike kwa usafiri na kutolea mafunzo kwa vitendo. Katika mwaka wa fedha wa 2015/16, Wizara itaendelea kuboresha maeneo ya kutolea mafunzo kwa kujenga madarasa, nyumba za watumishi na majengo ya utawala katika Vyuo vya Ilula na Newala, kuweka mfumo wa umeme katika Vyuo vya Munguri, Ulembwe, Rubondo, Msingi, Malya na Mwanhala na kugharimia upimaji wa upatikanaji wa Hati Miliki wa Vyuo vya Ifakara, Ikwiriri, Msingi, Mwanva, Musoma, Arnautoglu, Chilala, Kilwa Masoko, Chisalu na Kisarawe ili kupunguza migogoro

inayosababishwa na wananchi kuvamia maeneo ya vyuo kwa shughuli za kilimo na ujenzi wa makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kushiriki na kutekeleza Mikataba na Maazimio mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa ambayo nchi imeridhia. Wizara ilishiriki katika mkutano wa *African Regional Conference* uliofanyika tarehe 17 - 19 Novemba 2014 Addis Ababa - Ethiopia. Mkutano huo ulilenga kupitia taarifa ya nchi ya Beijing+20 na kutoa maazimio ya utekelezaji wa maeneo 12 yaliyoainishwa. Taarifa hiyo iliwasilishwa katika Kikao cha 59 cha Kamisheni ya Hali ya Wanawake Duniani kilifanyika nchini Marekani mwezi Machi 2015. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kushiriki katika utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa ikiwa ni pamoja na kutoa michango na uzoefu wake katika kuboresha na kuimarisha usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia lengo la kuwepo kwa usawa wa jinsia, uingizwaji wa masuala ya jinsia katika mipango, mikakati na bajeti, sera na programu mbalimbali, bado unaendelea kutiliwa mkazo. Katika kipindi cha mwaka 2014/15, Wizara iliendesha mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu zilizochambuliwa kijinsia kwa maafisa 50 kutoka Wizara mbalimbali, Taasisi zisizo za Serikali na Taasisi za Elimu. Taarifa hizo zitatumwa na serikali pamoja na wadau mbalimbali katika kufanya maamuzi, ushawishi, utungaji sera na mipango mbalimbali ya maendeleo kwa kuzingatia usawa wa jinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia vikao vya robo mwaka vya kikundi cha uingizaji wa masuala ya kijinsia katika Sera za Kitaifa na Kisekta (*Gender Mainstreaming Working Group for Macro Policies*) imeweza kuandaa Mwongozo wa Uingizaji wa Masuala ya Jinsia katika Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now- BRN*). Lengo ni kuwezesha kuwepo kwa matokeo makubwa kwa kuzingatia mahitaji ya makundi yote ya wanawake na wanaume. Mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kuratibu uingizwaji wa masuala ya jinsia katika Sera za Kitaifapamoja na kujenga uwezo kuhusu uingizwaji wa masuala ya kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake Tanzania ni mali ya umma inayomilikiwa kwa kiasi kikubwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hadi mwaka 2014/15, Benki ina wanahisa wadogowadogo wanaokadiriwa kufikia 160 wanaomiliki hisa zisizozidi asilimia mbili. Katika mwaka, 2014/15, Benki ilitoa mikopo kwa wajasiriamali wapatao 10,847. Kati ya idadi hiyo wanawake ni 8,165 sawa na asilimia 75 ya wateja wote waliopatiwa mikopo. Thamani ya mikopo iliyotolewa ni kiasi cha Shilingi bilioni kumi na mbili milioni mia nne sitini na tisa laki sita na hamsini. Kati ya kiasi hicho, jumla ya Shilingi bilioni nane mia tano sitini na moja laki mbili zilikopeshwa kwa wanawake, sawa na asilimia 69 ya mikopo iliyotolewa.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/16, Benki inatarajia kuendelea kutoa huduma zake katika maeneo mengi zaidi kupitia njia Wakala wa Benki (*Agency Banking*) kwa kufungua ofisi za kutolea huduma za mikopo mikoani. Aidha, katika mwaka wa kibajeti wa 2014, Benki ya Wanawake imetengeneza faida ya shilingi milioni mia moja arobaini na moja kabla ya kodi (*Profit Before Tax*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/15, Mfuko wa Wanawake umetoa jumla ya Shilingi milioni thelathini na moja kwa Halmashauri tatu ambazo ni Bunda, Iringa pamoja Mkalama. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeadhimisha Siku ya Wanawake Duniani iliyofanyika Mkoani Morogoro na kutoa tuzo kwa watu binafsi, asasi na makundi yaliyotoa mchango mkubwa katika kuwawezesha wanawake nchini. Kaulimbiu ya siku hiyo ilikuwa Uwezeshaji Wanawake; Tekeleza Wakati ni Sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Wizara iliandaa Mpango Kazi wa Taifa wa Miaka Mitano wa Ushiriki wa Watoto (2014 - 2019). Lengo la Mpango Kazi huo ni kuongeza ushiriki wa watoto katika masuala mbalimbali yanayowahusu. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kusambaza mpango kazi huu katika Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekamilisha uandaaji wa Rasimu ya Sera ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto pamoja na Mkakati wake wa Utekelezaji. Sera hii ipo katika ngazi za juu za maamuzi kwa ajili ya kupitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kuratibu utoaji wa taarifa zinazohusu vitendo vya ukatili dhidi ya watoto kwa kushirikiana na Asasi isiyokuwa ya Kiserikali ya C-SEMA, ambapo kati ya mwezi Julai 2014 na Machi 2015, jumla ya simu 21,960 zilipigwa kupitia mtandao wa simu namba 116. Taarifa hizo zilishughulikiwa kulingana na aina ya tatizo au suala lililowasilishwa. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kuratibu utoaji wa huduma hii kwa kushirikiana na asasi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Wizara iliratibu maandalizi ya taarifa ya kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Kamati ya Haki za Watoto ya Umoja wa Mataifa kuhusu ripoti ya nchi ya 3, 4 na 5 iliyowasilishwa katika kamati hiyo mnamo mwezi Januari 2012 na kuwasilisha majibu ya hoja kwenye kamati hiyo 2015. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kuyafanyia kazi maoni ya jumla (*Concluding Observation*) yaliyotolewa na Kamati hiyo ya Haki za Watoto ya Umoja wa Mataifa.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014/15, Wizara yangu ilizindua rasmi Zana ya Mawasiliano kwa ajili ya kuzuia ukatili dhidi ya watoto yenye lengo la kuelimisha wazazi, watoto, wanahabari na wanajamii, jinsi ya kujizuia na kutoa taarifa kuhusu matukio mbalimbali ya ukatili dhidi ya mtoto ambapo nakala 1,000 za zana hizo zilisambazwa kwa wadau wa masuala ya ulinzi na haki za watoto hapa nchini. Katika mwaka 2015/16, Wizara itasambaza nakala 2,000 za zana hizo na kuratibu utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Wizara yangu imeratibu Maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani ambayo huadhimishwa kila mwaka tarehe 16 Juni na mwaka huu yameadhimishwa katika ngazi ya Mkoa. Kaulimbiu ya mwaka 2015 ni Usawa wa Kijinsia na Haki za Watoto katika Familia; Wanaume Wawajibike. Aidha, Wizara imeratibu maandalizi ya Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika ambayo kila mwaka tarehe 16 Juni yanaadhimishwa maadhimisho ya mtoto na tarehe 15 Mei ni maadhimisho ya familia. Kaulimbiu ya mwaka huu ilikuwa Tokomeza Mimba na Ndoa za Utotoni; Kwa Pamoja Tunaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Wizara yangu iliendelea kusajili NGOs ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 pamoja na Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 24 ya 2002 iliyorekebisha mwaka 2005. Hadi kufikia mwezi Machi 2015, jumla ya mashirika 7,060 yalipata usajili katika ngazi mbalimbali ili kuyawezesha kutambulika kisheria na kutekeleza malengo yaliyokusudiwa. Katika kipindi cha mwaka 2015/16 Wizara itaendelea na usajili wa Mashirika hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014/15, Wizara yangu ilichukua hatua mbalimbali za kuimarisha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini. Hatua hizi ni pamoja na kuendelea kuliwezesha Baraza la Taifa la NGOs kutekeleza majukumu yake ya kisheria kwa kupitisha Kanuni za Uendeshaji wake na Kanuni za uchaguzi za Baraza hilo za ngazi mbalimbali. Kanuni hizi zitaliwezesha Baraza na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kujiendesha kwa ufanisi zaidi kwa kudhibiti ili kuimarisha taswira na mchango wao katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Wizara yangu iliandaa vipindi vya runinga na redio, matangazo kupitia magazeti, vipeperushi na mabango, mikutano ya waandishi wa habari kwa ajili ya kuelimisha umma kuhusu masuala ya maendeleo ya jamii, jinsia na haki za watoto na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Aidha, kwa kushirikiana na UNICEF, Wizara yangu imeandaa kipindi maalum cha 'WALINDE WATOTO' ambacho kinatangazwa kupitia redio 14 zenye usikivu wa kitaifa na kikanda Tanzania Bara na Zanzibar.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Lengo la kipindi ni kuhamasisha wadau wa maendeleo ya mtoto kushiriki kikamilifu katika jitihada za kuzuia na kutokomeza ukatili dhidi ya watoto. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea na kuhamasisha, kuelimisha na kushawishi umma kuhusu masuala ya maendeleo ya jamii, jinsia, haki za watoto na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/15, Wizara yangu imeandaa Andiko la Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Wananchi lenye awamu mbili za utekelezaji kwa vipindi vya miaka mitano mitano zilizohuishwa na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka Mitano awamu ya pili na ya tatu. Aidha, Programu hiyo ni sehemu ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu na rasimu yake imewasilishwa na kupitishwa katika vikao vya Sekta ya Elimu.

Programu hii inalenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, utoaji wa ujuzi na stadi mbalimbali na elimu ya ujasiriamali zitakazoweza vijana na wananchi kupata fursa ya kuongeza vipato vyao kwa kujijiri au kuajiriwa. Aidha, Wizara inaandaa maandiko ya Programu ya Kuwezesha Wanawake na Wasichana Kiuchumi, Programu ya Kutokomeza Ndoa za Utotoni na Programu ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto kama sehemu ya utekelezaji wa Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063 kwa kuanza kutoa msukumo maalum wa kuwaendeleza wanawake na watoto. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kuratibu utafutaji wa fedha kutoka vyanzo mbalimbali ili kutekeleza programu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kusimamia maendeleo ya sera na *program* ya Sekta ya Maendeleo ya Jamii katika mwaka 2015/2016. Wizara itafanya tathmini kuhusu ufanisi wa Sera ya Taifa ya mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ili kubaini changamoto na mafanikio ili kuweka mazingira wezeshi kwa NGOs na kuziwezesha kushiriki kikamilifu na kuleta maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kuboresha utendaji kazi kwa kuzingatia misingi ya haki, usawa, uadilifu, utawala bora na uwazi. Wizara yangu imeendelea kuweka mkazo katika kudhibiti vitendo vya rushwa na uzembe kazini ili kuwa na watumishi waadilifu na wawajibikaji wenye ari, moyo na msimamo thabiti katika utekelezaji wa majukumu katika utumishi wa Umma. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara itaendelea kutoa huduma za kiutawala na usimamizi wa rasilmali watu kwa kuzingatia misingi ya haki, usawa, uadilifu na utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara yangu imeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kufanya ukarabati na uboreshaji wa baadhi ya maeneo ya Ofisi ya Makao Makuu kama vile ujenzi wa maeneo ya kuegesha magari, ununuzi wa jenereta, uboreshaji wa masjala

pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya umeme, simu na *internet*. Kwa mwaka 2015/2016 Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa kuendelea kufanya ukarabati mdogo mdogo katika jengo la Wizara, Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/2015 Wizara yangu imeajiri watumishi wapya wa kada mbalimbali wapatao 148 na kufanya idadi ya watumishi kufikia 1,122. Nafasi 428 zimeshatangazwa na Sekretarieti ya Ajira hivyo mchakato utakapokamilika watumishi hao pia wataajiriwa. Hata hivyo, Wizara bado inakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi hasa wa kada ya ukufunzi katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Katika kukabiliana na changamoto hizi, Wizara imepeleka maombi Ofisi ya Ofisi Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya kupata kibali cha kuwaajiri watumishi wa kada mbalimbali. Mwaka 2015/2016 Wizara itaendelea kuomba kibali cha kuwaajiri watumishi ili kupunguza pengo lililopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, majukumu ya Wizara yangu ni kuhakikisha jamii na wananchi wanabadilika kifikra na kimtazamo ili kuwa na jamii inayoshiriki kikamilifu katika kujiletea maendeleo yao wenyewe na Taifa kwa ujumla. Majukumu haya ni mtambuka, hivyo basi, utekelezaji wa malengo na mipango ya Wizara kwa mwaka 2015/2016 bado utahitaji ushirikiano mkubwa zaidi wa wadau mbalimbali hasa Mikoa na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana kwa ushirikiano wake mkubwa anaonipa katika kuongoza Wizara hii.

Vilevile, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu, Bibi Anna Tayari Maembe, Naibu Katibu Mkuu Bibi Nuru H. M. Milao, Wakurugenzi Wakuu wa Vitengo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Wanawake Bibi Margareth Chacha, Wakuu wa Vyuo na Wafanyakazi wote wa Wizara yangu wa ngazi zote kwa jitihada zao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ambayo ni pamoja na kuniwezesha mimi kuwasilisha hotuba hii mbele ya Bunge lako Tukufu leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumaliza hotuba yangu kwa kuwashukuru wadau wote tunaofanya nao kazi na kushirikiana kwa namna moja au nyingine. Peke yetu kama Wizara tusingefikia mafanikio tuliyoataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupitia Bunge lako Tukufu kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafuatao:-

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Asasi ya Wanawake na Maendeleo (WAMA), Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wanawake Wote (EOTF), Mtandao wa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Jinsia (TGNP), Chama cha Wanasheria Wanawake (TAWLA), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Shirikisho la Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (FAWETA), Medical Women Association of Tanzania (MEWATA), White Ribbon, Planning International, Save the Children na mashirika mengi mbalimbali yasiyo ya Kiserikali pamoja na wale wanaofanya kazi kwa maslahi ya jamii kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuyashukuru Mashirika kutoka nchi rafiki ambayo yameendelea kutusaidia na kufanya kazi na sisi. Mashirika hayo ni pamoja na GPE, KOIKA na UK Education.

Aidha, nayashukuru Mashirika ya Umoja wa Mataifa ambayo ni UNICEF, UNDP, UNFPA na UN Women kwa misaada yao mbalimbali iliyofanikisha utekelezaji wa majukumu mengi ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara yangu itekeleze majukumu na malengo yake kwa mwaka 2015/2016 sasa naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe matumizi ya Sh. 31,421,641,000/= . Kati ya fedha hizo:-

- (a) Sh. 11,038,075,000/= ni kwa ajili ya mishahara;
- (b) Sh. 9,460,146,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo; na
- (c) Sh. 10,923,420,000/= ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo Sh. 8,000,000,000/= ni fedha za ndani na Sh. 2,923,420,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja. (Makofi)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

MWENYEKITI: Ahsante, hoja imeungwa mkono.

**Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia
na Watoto kwa mwaka 2015/2016**

Kama ilivyowasilishwa Mezani

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA
NA WATOTO MHESHIMIWA SOPHIA M. SIMBA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI
MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA
MWAKA 2015/16**

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii iliyoichambua bajeti ya Wizara yangu, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako tukufu likubali kupokea na kupitisha makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka 2015/16.

2. Mheshimiwa Spika, niruhusu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na utukufu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu nikiwa na afya njema na hivyo kuweza kushiriki mkutano huu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

3. Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mohammed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao mahiri na maelekezo yao ambayo yamewezesha kushamiri kwa usawa wa jinsia na uzingatiaji wa haki za mtoto katika jamii ya Watanzania. Mwenyezi Mungu awajalie afya njema ili waendeleo kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

4. Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza Mhe Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa uendeshaji bora wa shughuli za Bunge. Tunaendelea kumuomba Mwenyezi Mungu awajalie afya njema ili muweze kusimamia na kuratibu shughuli za Bunge kwa ufanisi.

5. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ikiongozwa na Mwenyekiti mahiri Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, kwa kuchambua na kujadili bajeti ya Wizara yangu. Ushauri na maelekezo ya Kamati hiyo yamewezesha Wizara yangu kuandaa bajeti kwa ufanisi.

6. Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza wabunge waliochaguliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni Dkt. Grace Khwaya Puja na Innocent Rwabushaija Sebba kuwa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

7. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa salamu za pole kwako, Bunge lako Tukufu, familia na wananchi wa Jimbo la Mbinga Magharibi kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge wao na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii Mheshimiwa Kapteni Mstaafu John Damiani Komba. Bunge hili litamkumbuka daima kwa michango yake. Aidha, kwa masikitiko makubwa natumia fursa hii kuwapa pole wale wote waliopatwa na majanga ya ajali na mafuriko pamoja na kufiwa na ndugu, jamaa na wapendwa wao katika matukio mbalimbali yaliyotokea hapa nchini. Nitangulize dua zangu kwa Mwenyezi Mungu awapokee na kuwalaza mahali pema peponi. Amina.

B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM KWA KIPINDI CHA MWAKA 2005 HADI 2015

I. Ajira na Uwezeshaji wa Wananchi

Mheshimiwa Spika, Udahili wa washiriki katika Elimu ya Wananchi na ufundi stadi kupitia vyo vyetu vya maendeleo ya wananchi umeongezeka kutoka washiriki 25,486 mwaka 2005 hadi kufikia washiriki 40,692 mwaka 2015 na idadi ya wasichana waliopata mafunzo ya “Mama course” iliongezeka kutoka 60 mwaka 2005 hadi kufikia wasichana 449 mwaka 2014. Wizara yangu ilibuni “mama course” mwaka 2000 kwa lengo la kuwapa wasichana waliopata mimba wakiwa shuleni fursa ya kujiendeleza kielimu kupitia mafunzo ya elimu ya wananchi baada ya kupoteza fursa hiyo katika mifumo rasmi kutokana na kanuni na taratibu za uendeshaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari Tanzania. Aidha, kwa mwaka, jumla ya washiriki 36,838 walihitimu katika Vyo vya Maendeleoya Wananchi, kati yao, 22,939 ni wanaume na 13,899 ni wanawake. Wahitimu 33,319 sawa na asilimia 90.44 ya wahitimu kutoka katika vyo vya Maendeleo ya wananchi wamejajiri na wahitimu 3,047 sawa na asilimia 8.27 ya wahitimu wa Vyo vya Maendeleo ya Wananchi wameajiriwa katika makampuni ya watu binafsi na Taasisi mbalimbali za Serikali.

II. Uendelezaji wa Makundi Mbalimbali

Maendeleo ya Watoto

8. Mheshimiwa Spika, Wizara iliwasilisha taarifa za 3, 4 za 5 ya Nchi yetu kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto. Aidha, Wizara

inaandaa taarifa ya 2 na 3 ya utekelezaji wa Mkataba wa Afrika Kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto ambayo itawasilishwa katika Kamati ya Umoja wa Afrika ya Haki na Ustawi wa Mtoto.

9. Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa na kuanza kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Miaka Mitano wa Ushiriki wa Watoto. Mpango huo utatoa fursa kwa wazazi na walezi kujifunza njia bora za mawasiliano na mahusiano mazuri kati yao na watoto. Aidha, Mpango Kazi huu utabainisha namna ya kuwashirikisha watoto katika majadiliano na hata kunufaika na michango yao kimawazo, kiushauri na katika utekelezaji wa maamuzi mbalimbali ya kutatua matatizo yao.

Maendeleo ya Wanawake

10. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwahamasisha wanawake kujiendeleza kielimu na kujenga uelewa wao katika kuweka nguvu za kutetea haki zao na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kimaendeleo. Aidha, wanawake wamejengewa uwezo wa ujasiriamali, utaalum wa biashara, jinsi ya kupata mitaji zaidi, masoko pamoja na kutoa mikopo mbalimbali

III. Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru

11. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru iliendelea kudahili wanafunzi katika ngazi ya Shahada ya Kwanza kuanzia mwaka 2008/09 katika fani ya uandaaji na usimamizi shirikishi wa miradi, usimamizi wa programu za maendeleo ya jamii, maendeleo ya jinsia na stahhada ya uzamili ya maendeleo ya jamii. Udahili wa wanachuo umeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka, katika mwaka 2012/13, jumla ya wanachuo 139 wakiwemo wanaume 64 na wanawake 75, walidahiliwa. Mwaka 2013/14, jumla ya wanachuo 234 wakiwemo wanaume 88 na wanawake 146 walidahiliwa na katika mwaka 2014/15, jumla ya wanachuo 276, wakiwemo wanawake 189 na wanaume 87 walidahiliwa

12. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2014/15, Serikali ilikipandisha hadhi Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kuwa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru kupitia Azimio Na.1 la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la mwezi wa Aprili, 2014, katika Mkutano wake wa 17 Kikao cha 27 Taasisi hii inatarajiwa kuongeza Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii wa Ngazi ya Shahada ya maendeleo ya jamii ambao ni muhimu sana katika kuimarisha utendaji wa shughuli za Maendeleo ya Jamii. Hasa katika ngazi ya Halmashauri ambapo kuna uhaba mkubwa wa watumishi hawa.

IV. Demokrasia na Mamlaka ya Umma

13. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ilitunga na kupitisha Kanuni za Maadili ya NGOs. Utekelezaji wa Kanuni za Maadili ya NGOs umelenga kukuza uwazi, uwajibikaji na uwezo wa Mashirika haya kujitathimini na kujikagua katika utekelezaji wa shughuli zao kulingana na katiba au miongozo ya kusajiliwa kwao. Kanuni hizi zimeamsha ari ya wadau wa NGOs kujitafiti na kubaini maeneo ambayo wanauwezo mkubwa wa kusaidia jamii na kuyaendeleza maeneo ambayo wako dhaifu kubuni mikakati ya kujijengea uwezo ili kutekeleza kwa ufanisi majukumu yao katika sekta mbalimbali nchini

14. Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ambazo Wizara yangu imechukua ni pamoja na kuanzishwa kwa Tovuti Maalum ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (<http://www.tnnc.go.tz>) ambayo hutumiwa na wadau mbalimbali ikiwemo wanufaika wa miradi ya NGOs kutolea mrejesho kuhusu utendaji wa NGOs katika maeneo yao. Idadi ya wadau ambao wametoa mrejesho kuhusu utendaji wa NGOs hadi kufikia Machi, 2015 ni 30,679. Aidha, Wizara imekuwa ikitembelea na kukagua shughuli/kazi, miradi na program mbalimbali zinazotekelezwa na NGOs nchini kwa lengo la kutathimini utendaji na uendeshaji wa Mashirika hayo, ambapo jumla ya Mashirika 66 yamefikwa hadi kufikia Machi, 2015.

C. HALI HALISI YA SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII NA CHANGAMOTO ZILIZOPO

Hali ya Maendeleo ya Jamii nchini

15. Mheshimiwa spika, utekelezaji wa dhana ya Maendeleo ya Jamii ambayo ni dhana shirikishi unajenga na kuimarisha misingi ya watu katika jamii kujitambua kwa kutambua uwezo walionao wa kubaini matatizo yao, kuweka vipaumbele, kubaini fursa na rasilimali walizonazo, kupanga na kutoa maamuzi ya kazi au miradi ya kutekeleza ili kutatua kero na matatizo yao. Kipimo cha mafanikio ya dhana hii ni ongezeko la watu katika jamii kubadilika kutoka kifikra na kintazamo na kushiriki kikamilifu katika masuala yanayowaletea maendeleo endelevu. Katika kufanikisha haya, Wataalam wa maendeleo ya Jamii ni muhimu katika kuhamasisha, kuraghabisha, kushauri, kushawishi na kuelimisha wananchi na viongozi wao kwa kuwapatia elimu, maarifa na taarifa mbalimbali ili kuwaongezea uelewa, uwezo wa kufikiri na kufanya maamuzi sahihi ya utekelezaji wa dhana hiyo.

16. Mheshimiwa Spika, Pamoja na umuhimu wa Wataalam wa Maendeleo ya Jamii kama ilivyobainishwa katika Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996) inayosisitiza kuwepo kwa Mtaalam wa Maendeleo ya Jamii mmoja kila kata ili

kuchochea ari na mwamko wa wananchi katika kujiletea maendeleo yao, Sekta hii bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazosababisha utekelezaji usioridhisha wa dhana ya maendeleo ya jamii nchini. Hadi sasa Wataalam, waliopo katika Halmashauri za Wilaya na Manispaa ni 2,774, kati ya hao walioko Makao Makuu ya Wilaya ni 1,464, kwenye Kata ni 1,310. Kwa sasa kuna jumla ya kata 3,339 nchini na hivyo kufanya upungufu wa Wataalam wa Maendeleo ya Jamii kuwa 2,029 katika Kata. (Jedwali Na.1).

Aidha, wataalamu hao wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa vitendea kazi na vyombo vya usafiri. Changamoto hizi zimesababisha maeneo mengi hasa vijijini kukosa wahamasishaji na waraghibishi na hivyo kubaki nyuma katika suala zima la kujiletea maendeleo. Aidha, wananchi wameendelea kukosa elimu, ujuzi na taarifa mbalimbali zihusuzo maendeleo. Upungufu huo pia umesababisha ufuatiliaji usioridhisha wa shughuli balimbali za maendeleo katika Jamii.

17. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliwa na changamoto hizo, Wizara inaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma juu ya uwezekano wa kuwaajiri wataalam wa Maendeleo ya jamii moja kwa moja kutoka vyuoni.

Vyuo vya Maendeleo ya Jamii

18. Mheshimiwa Spika, Mwaka 1960 serikali ya kikoloni ilianzisha Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru. Chuo hiki kilianza kwa kutoa mafunzo ya ngazi ya Astashahada. Mwaka 1983 chuo kilianza kutoa mafunzo ya Stashahada ya juu. Hivi sasa Chuo hiki ni Taasisi inyotoa mafunzo ya Shahada za Maendeleo ya Jamii, Jinsia na maendeleo na Mipango na usimamizi shirikishi wa miradi ya maendeleo ya jamii. Halikadhalika, Taasisi inatoa Stashahada ya Uzamili katika masuala ya maendeleo ya jamii. Aidha, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Buhare, Rungemba na Missungwi vinatoa wataalam wengi zaidi wenye viwango tofauti vya taaluma, ili kukidhi mahitaji ya maendeleo ya jamii ngazi ya cheti na diploma. ya wataalamu wa Maendeleo ya Jamii katika Vijiji, Kata na Halmashauri.

19. Mheshimiwa Spika, Vyuo hivi vinakabiliwa na uhaba wa majengo, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, vyombo vya usafiri, na upungufu wa watumishi hasa wakufunzi. Licha ya changamoto hizi, udahili umeongezeka kutoka wanachuo 940 mwaka 2005/06 hadi kufikia 3,634 mwaka 2014/15 kama inavyoonekana katika Hali ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

20. Mheshimiwa Spika, Vyuo hivi vilianzishwa kati ya miaka ya 1970 na 1980 kwa kurithi majengo yaliyokuwa yakitumika na taasisi mbalimbali kama vile Vyuo vya Maendeleo Vijijini (Rural Training Centre's), Shule za Kati (Middle

Schools), Vituo vya Mafunzo ya Ushirika na Vituo vya Mafunzo ya wakulima (Farmers Training Centres). Majengo haya yalijengwa kati ya mwaka 1950 hadi 1963. Kutokana na umri wa majengo haya, kwa sasa ni machakavu na hayaendani na mahitaji ya kutolea mafunzo kwa sasa. Madhumuni ya kuanzishwa kwa vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ni kujenga uwezo wa wananchi wa kujitegemea kwa kuinua hali za maisha yao na ya Taifa kwa ujumla. Tangu kuanzishwa kwake vyuo hivi vimekuwa vikitoa mafunzo ya stadi na maarifa ya kuwawezesha wananchi kuajiriwa, kujajiri na kuajiri wengine. Mafunzo haya huwajengea wananchi uwezo wa kuongeza uzalishaji mali wenye tija na ambao huongeza pato la kaya na hivyo kupunguza umasikini katika familia na Taifa kwa ujumla

21. Mheshimiwa Spika, Hivi sasa kuna jumla ya vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi ambavyo vipo katika wilaya mbalimbali nchini na baadhi ya wilaya zina zaidi ya chuo kimoja. Vyuo hivi vinatoa mafunzo na stadi mbalimbali kwa wananchi kama matumizi bora ya pembejeo, kilimo, uashi na useremala pamoja na stadi nyingine za maisha. Vyuo hivi pia vinatoa mafunzo ya Ufundi Stadi kwa kushirikiana na VETA. Kutokana na uchakavu wa majengo na miundombinu ya vyuo hivi, wizara inaendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia, jitihada mbalimbali zimefanywa na Wizara za kujenga majengo mapya, kufanya ukarabati wa majengo ya zamani na kuboresha mifumo ya maji na umeme

Changamoto na namna ya kuzitatua

22. Mheshimiwa Spika, Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vinakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo: mahitaji makubwa ya rasilimali fedha na watumishi, ubovu na uchakavu wa majengo na miundombinu, ukosefu wa vifaa vya mafunzo, vyombo vya usafiri na maeneo ya vyuo kuvamiwa na wananchi kwa shughuli za kilimo na ujenzi wa makazi

23. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hizi, Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya utoaji mafunzo Vyuoni kwa kuajiri watumishi wa kada mbalimbali kufanya ukarabati wa majengo na miundombinu na kuvipatia vyuo nyenzo na zana za kufanyia kazi kulingana na rasilimali zilizopo.

Hali ya Maendeleo ya Jinsia nchini Uwezeshaji wa wanawake

24. Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa usawa wa jinsia nchini unazingatiwa katika mipango na mikakati ya

utekelezaji katika Nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kupitia programu na mikakati mbalimbali ya kuleta usawa wa jinsia, mafanikio makubwa yamepatikana kwa mfano: Idadi ya Mawaziri wanawake imeongezeka kutoka Mawaziri wanawake 6 kati ya Mawaziri 25 mwaka 2005 hadi kufikia Mawaziri wanawake 10 kati ya Mawaziri 30 mwaka 2015; Wakuu wa Wilaya wanawake wameongezeka kutoka 20 kati ya Wakuu wa Wilaya 104 mwaka 2005 hadi kufikia Wakuu wa Wilaya wanawake 46 kati ya Wakuu wa Wilaya 133 mwaka 2015; Majaji wanawake wameongezeka kutoka Majaji wanawake 8 kati ya Majaji 50 mwaka 2005 hadi kufikia Majaji wanawake 24 kati ya Majaji 67 mwaka 2015; na Wabunge Wanawake wameongezeka kutoka Wabunge wanawake 62 kati ya Wabunge 288 mwaka 2005 hadi kufikia Wabunge wanawake 127 kati Wabunge 357 mwaka 2015.

Aidha, Katika kuhakikisha wanawake wanapata fursa ya elimu, mafunzo na ajira, idadi ya Madirisha ya Taarifa kwa Wanawake yameongezeka kutoka madirisha manne mwaka 2005 hadi kufikia madirisha 12 mwaka 2014. Jumla ya wanawake 14,589 wamefikwa na watoa huduma wa dirisha kupitia huduma ya mmoja mmoja katika ofisi za Madirisha ya Taarifa kwa Wanawake.

25. Mheshimiwa Spika, katika kuwezesha wanawake kiuchumi, Wizara kupitia Benki ya Wanawake Tanzania imetoa mafunzo ya ujasiriamali na mikopo yenye thamani ya Sh.bilioni 24.86. Mikopo hiyo imewezesha wajasiriamali kujijiri katika shughuli mbalimbali za biashara na hivyo kuinua vipato vyao kiuchumi na kijamii. Aidha, Benki ya Wanawake imeongeza vituo vya kutolea huduma za kibenki kutoka vituo 18 mwaka 2012/13 hadi kufikia vituo 81 mwaka 2013/14.

26. Mheshimiwa Spika, Idadi ya wanawake wanaopata mikopo kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Kiasi cha fedha kilichokopeshwa kimeongezeka kutoka Sh. 260,000,000 mwaka 2005 hadi kufikia Sh.bilioni 1,900,000,000 mwaka 2014. Mikopo hiyo imewawezesha wanawake wanawake kufanya shughuli za ujasiriamali ikiwa ni pamoja na: ufugaji; utengenezaji wa mvinyo; usindikaji wa mazao, mbogamboga, matunda na nafaka; kilimo cha bustani za mboga na mazao mbalimbali; biashara ya kuuza na kununua mazao kama mahindi, mpunga, ufuta, karanga, alizeti na mchele; ufumaji; ususi wa mikeka na vikapu. Aidha, mikopo hiyo imewawezesha kuinua vipato vyao na kuweza kugharamia mahitaji mbalimbali ya msingi kama vile; kulipia gharama za matibabu, kusomesha watoto, kujenga na kukarabati nyumba zao. (Jedwali Na. 2).

Ukatili na ubaguzi wa kijinsia

27. Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kuzuia na Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto

(2001-2015) kwa kujengea uwezo Kamati ya Kitaifa ya Kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto ili iweze kushughulikia masuala ya ukatili, kuratibu Kampeni za Kutokomeza Vitendo vya Ukatili Dhidi ya Wanawake ili kuongeza uelewa wa madhara ya vitendo vya ukatili katika jamii na kuandaa Mwongozo wa Kuzuia na Kudhibiti Ukatili wa Kijinsia kwa Kamati a Vijiji, Mitaa, Kata na Wilaya.

Utekelezaji wa mikataba ya kikanda na kimataifa

28. Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza mikataba na maazimio mbalimbali ya kikanda na kimataifa ambayo nchi imeridhia, Wizara imeendelea kushiriki katika mikutano na kutekeleza mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ikiwa ni pamoja na kutoa michango na uzoefu wake katika kuboresha na kuimarisha usawa wa jinsia na uwezesaji wa Wanawake. Mikutano hiyo hutoa fursa kwa washiriki kujadili masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya wanawake na haki za wasichana na kutoa mapendekezo ya kiutekelezaji katika kufikia usawa wa jinsia.

Changamoto za Kuleta Maendeleo ya Jinsia

29. Mheshimiwa Spika, Pamoja na mafanikio yaliyopatikana bado zipo changamoto mbalimbali ambazo ni; Mahitaji makubwa yamikopo ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, mafunzo ya ujasiriamali yanayotolewa kwa wakopaji kutotosheleza kujenga uwezo unaohitajika, marejesho hafifu ya mikopo, mahitaji makubwa ya huduma za Benki ya Wanawake Tanzania hususan kwa wanawake wajasiriamali wa vijijini. Aidha, wanawake wengi kushindwa kushika nafasi za uongozi na maamuzi kutokana na majukumu mengi ya familia. Kuendelea kuwepo kwa mila na desturi ambazo zinahamasisha ndoa za utotoni na hivyo kuendeleza ukandamizaji kwa watoto wa kike na kusababisha mimba za utotoni

30. Mheshimiwa Spika, Katika kukabiliana na changamoto hizo hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kufuatilia na kutathmini matokeo ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake; kutoa mafunzo kwa wanawake wajasiriamali kuhusu utunzaji wa kumbukumbu za biashara, jinsi ya kutumia mikopo na kulipa, kuweka akiba na kukuza biashara; kutafuta vyanzo vingine vya uwezesaji wa wanawake kiuchumi na kufungua vituo vya kutolea mikopo vya Benki ya Wanawake Tanzania katika Wilaya zote za Mikoa ya Mwanza, Dar es Salaam na Dodoma.

Hali ya Maendeleo ya Watoto

31. Mheshimiwa Spika, Takwimu za idadi ya watu na Makazi nchini ya mwaka 2012 inaonyesha kuwa kwa sasa Tanzania inakadiriwa kuwa na watoto

24,377,052 chini ya miaka 18 ambao kati yao 12,201,122 ni wasichana na 12,175,930 ni wavulana sawa na asilimia 50.1 ya Watanzania. Kundi hili linahitaji mipango madhubuti ili kuweza kuwalea na kuwaendeleza katika nyanja za afya, elimu, Lishe bora na ulinzi ili waweze kushiriki katika ujenzi wa Taifa.

32. Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikisha kwamba watoto nchini wanapata haki yao ya ulinzi, Wizara imeendelea kuratibu shughuli za Kikosi Kazi cha Taifa cha Kuzuia na Kupambana na Ukatili Dhidi ya watoto ambacho kinasimamia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Mwitikio na Kuzuia Ukatili Dhidi ya Watoto kuanzia mwaka 2013 hadi 2016 kwa kushirikiana na wadau.

33. Mheshimiwa Spika, haki ya watoto ya kushiriki ni muhimu kwa kuwa inampa fursa ya kujadili na kutoa maoni kwa uhuru kuhusu mambo yanayowahusu na hivyo kumjengea uwezo wa kujiamini na kujieleza. Kwa kutambua hilo, Wizara imeendelea kuratibu shughuli za Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo vikao vyote vya Baraza Kuu na Kamati kuu vilifanyika. Hadi sasa mabaraza ya watoto katika ngazi ya Mikoa yameongezeka kutoka 12 mwaka 2005 hadi kufikia 22 mwaka 2014 na Wilaya kutoka mabaraza 57 mwaka 2005 hadi mabaraza 93 mwaka 2014

34. Mheshimiwa Spika, Pamoja na mafanikio niliyoyataja, Wizara imekabiliwa na changamoto mbalimbali katika kusimamia utoaji wa haki za watoto hapa nchini kama ifuatavyo; kuongezeka kwa vitendo vya ukatili Dhidi ya watoto ambapo kuanzia mwaka 2000 hadi 2014 matukio 150 ya ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi yameripotiwa na kusabaisha vifo 74 ambapo asilimia 45 ni watoto. Kushuka kwa kiwango cha ukeketaji kusikoridhisha kwa asilimia 3 kutoka 18 mwaka 1999 hadi 15 mwaka 2014. kuwepo kwa tatizo kubwa la ndoa na mimba za utotoni ambazo zinasababisha matatizo makubwa katika maendeleo ya kielimu na afya kwa wasichana hapa nchini. Takwimu zinaonyesha kwamba wasichana 2 kati ya 5 wanaolewa kabla hawajafikisha umri wa miaka 15. Mikoa inayoongoza kwa ndoa za utotoni ni Mara (43%), Shinyanga (37%) na Tabora (38%). Aidha, takwimu za mwaka 2014 zinaonyesha kuwa asilimia 43 ya wasichana wanazaa kabla hawajafika umri wa miaka 18.

35. Mheshimiwa Spika, Ajira hatarishi kwa watoto ni tatizo jingine ambalo limeanza kushamiri hapa nchini. Inakadiriwa kwamba asilimia 28 ya watoto hapa nchini wenye umri kati ya miaka 5 hadi 17 wanafanyishwa kazi katika mashamba, migodi, viwanda, uvuvi na majumbani. Watoto hawa wanakosa haki yao ya kupata elimu na baadae wanakuja kuwa wategemezi katika taifa lao. Aidha, Idadi ya watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani imeongezeka kwa kasi hapa nchini hasa katika majiji, miji mikubwa, mipakani na katika mikusanyiko ya watu. Mwaka 2012 (Dogodogo Centre na Ustawi wa Jamii) takwimu zinaonyesha Jiji la Dar es salaam ambalo lina watu zaidi ya million 5 lilikuwa na watoto wanaofanya kazi na kuishi mitaani zaidi ya 5,000.

36. Mheshimiwa Spika, sababu kubwa zinazochangia matatizo haya ni uelewa mdogo wa jamii kuhusu haki za mtoto, mamlaka mbalimbali kushindwa kuchukua hatua zinazostahili kukabiliana na matatizo punde yanapotokea na kuendelezwa kwa mila na desturi zenye madhara katika jamii yetu. Wizara yangu imepanga mambo yafuatayo kukabiliana na changamoto hizi: Kudurusu Sera ya Mtoto ya 2008 kwa kuingiza masuala ya Malezi, makuzi na maendeleo ya Awali ya Mtoto katika kuimarisha misingi ya malezi ya watoto hasa katika umri mdogo; Kuimarisha mikakati ya ulinzi wa mtoto na kuboresha uratibu wa masuala ya watoto. Aidha, jamii utaendelea kuhamasishwa kutoa taarifa za vitendo vya ukatili kwa vyombo vya ulinzi na usalama. Sera hii ikikamilika italetwa uwajibikaji shirikishi kwa sekta na wadau wote katika malezi ya watoto.

Hali ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

37. Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 na Sheria ya NGOs Na. 24 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebisha mwaka 2005 zimechangia kuimarisha hali ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini. Lengo kuu la Sera hii ni kujenga mazingira wezeshi kwa ajili ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kushiriki kikamilifu na kuchagua kwa ufanisi katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Aidha, Sheria ya NGOs ilitungwa ili kuupa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nguvu ya kisheria.

38. Mheshimiwa Spika, kutokana na utekelezaji wa sera na sheria hiyo, idadi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imeongezeka kutoka 3000 iliyokadiriwa kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 hadi kufikia 7,060 mwezi Machi, 2015. Kati ya mashirika hayo, 277 ni ya kimataifa na mashirika 6,783 ni ya ndani ya nchi yanayofanya kazi katika ngazi ya wilaya, mkoa na taifa. Aidha, Wizara ilifuta usajili wa NGOs 24, kati ya hizo, NGOs 10 ziliomba kuondolewa kwenye rejista ya NGOs baada ya kukamilika kwa miradi na programu zao. Utekelezaji huo upo kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambayo inampa Msajili wa NGOs mamlaka ya kuyafutia usajili mashirika ambayo yanakiuka masharti ya usajili wao au pale mashirika husika yanapoomba kuondolewa kwenye rejista ya usajili kutokana na sababu mbalimbali

39. Mheshimiwa Spika, mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kutoa huduma kwa jamii katika masuala mbalimbali umeendelea kuimarika. Mchango huo unaonekana zaidi katika sekta na maeneo ya elimu, afya, maji, maendeleo ya jinsia, maendeleo shirikishi, mazingira, ustawi wa jamii, kilimo, utawala bora, haki za binadamu, huduma za sheria na ujasiriamali. Mfano, Shirika la CCBRT liliwezesha matibabu ya akina mama 868 wenye tatizo la fistula katika Hospitali za Seliani (Arusha), KCMC (Kilimanjaro) na CCBRT (Makao Makuu Dar es Salaam). Aidha, wanawake hao baada ya kupona

walipatiwa ujuzi mbalimbali kupitia mafunzo yatolewayo na Kituo cha Mabinti kilichopo Dar es Salaam ili kuwawezesha wanawake hao kujitegemea kiuchumi.

40. Mheshimiwa Spika, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pia yameendelea kukuza fursa za ajira kwa kuhimiza na kutekeleza vyema dhana ya kujitolea. Taarifa ya mwaka 2012 ya Wizara kuhusu mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo inaonesha kuwa, mashirika haya yaliajiri jumla ya watu 60,700 ambapo kati yao, watu 27,312 wanafanyakazi kwa kujitolea.

41. Mheshimiwa Spika, pamoja na uwepo wa michango mingi na mizuri ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika utekelezaji wa mipango na program mbalimbali za nchi ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), MKUKUTA I na II, bado kuna changamoto mbalimbali zinazohitaji kufanyiwa kazi. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na Mashirika mengi Yasiyo ya Kiserikali kujikita zaidi mijini badala ya vijijini ambapo kuna wananchi wengi wenye kuhitaji huduma zao na kuendelea kutegemea ufadhili wa nje katika kutekeleza shughuli zao ambapo masharti ya ufadhili huo yanapelekea baadhi ya mashirika haya kukiuka mila, desturi, taratibu na sheria mbalimbali za nchi.

42. Mheshimiwa Spika, katika kutatua changamoto hizo, hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kutoa elimukwa NGOs kuhusu umuhimu wa taasisi hizi kuwafikia wadau wengi zaidi nchini hususan vijijini. Jitihada hizi zimefanyika kupitia Ofisi za Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, mikutano kati ya wadau wa mashirika haya na Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini pamoja na Wasajili Wasaidizi wa ngazi ya Wilaya na Mkoa. Aidha, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yameendelea kuhimizwa kutumia fursa ya marekebisho ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2005 kwa kuanzisha miradi ya kujipatia kipato kitakachoyawezesha kuepukana na utegemezi uliokithiri kwa wafadhili wa nje katika kuwahudumia walengwa wao.

D. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA 2014/15 NA MALENGO YA MWAKA 2015/16.

Sekta ya Maendeleo ya Jamii

43. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15, Wizara yangu iliendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu yake kulingana na malengo na shabaha zilizopangwa. Katika bajeti ya mwaka huo, Wizara ilikisia kukusanya jumla ya Sh. 1,845,360,000 kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi Machi 2015, makusanyo yalifikia Sh.1, 815,145,600 sawa na asilimia 98.4 ya lengo. Aidha, Wizara iliidhinishiwa jumla ya Sh. 29,453,599,000 ambapo kati ya hizo, Matumizi ya Kawaida ni Sh. 20,526,055,000 yakijumuisha Sh. 12,818,434,000 kwa ajili ya mishahara na Sh.

7,707,621,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Bajeti ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishwa ni Sh.8,927,544,000

44. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili,2015, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Sh. 8,639,231,903 sawa na 67% ya Bajeti ya Mishahara iliyoidhinishwa na matumizi yakiwa Sh.8,639,231,903 sawa na 100% ya fedha za Mishahara zilizotolewa, fedha za Matumizi Mengineyo Sh. 3,260,825,060 ikiwa ni 42% ya fedha za matumizi mengineyo zilizopokelewa na Sh. 3,260,825,000 sawa na 100% ya fedha zilizotolewa zimetumika. Aidha, fedha za ndani za maendeleo Sh.1,700,000,000 zilitolewa sawa na 25% ya fedha zilizoidhinishwa na Sh.338,634,000 sawa na 17% ya fedha za njezilitolewa ambapo Sh.1,450,000,000 sawa na 85% ya fedha za ndani zilizotolewa na Sh.338,634,000 sawa na 100% ya fedha za nje zilizotolewa zilitumika.

45. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua mchango wa Wataalam wa Maendeleo ya jamii katika kusaidia jamii ili ziweze kujiletea maendeleo. Katika mwaka 2015/16, Wizara yangu itaendelea kuwajengea uwezo Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya Mkoa na Halmashauri za Wilaya kuhusu mbinu shirikishi jamii, utatuzi wa migogoro ya kijamii na mbinu za ujasiriamali ili kuboresha utendaji kazi wa wataalam hawa waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Vyuo vya Maendeleo ya Jamii

46. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya Taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Astashahada ambapo jumla ya wanachuo 1,885 walidahiliwa katika mwaka 2014/15, ambapo kati yao wanaume 758 na wanawake ni 1,128, Stashahada ni 1,430 wakiwemo wanaume 378 na wanawake 1,052 kwa Vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii ambavyo ni Buhare, Rungemba, Missungwi, Monduli, Uyole, Ruaha, Mlale na Mabughai. Aidha, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru wanachuo 276 walidahiliwa katika ngazi ya Shahada ambapo wanaume walikuwa 87 na wanawake 189. Hali kadhalika wanachuo watatu (3) walidahiliwa katika ngazi ya Stashahada ya Uzamili kati yao kulikuwa na mwanume mmoja (1) na wanawake wawili (2).

47. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kudahili na kutoa mafunzo kuanzia ngazi ya Astashahada hadi Stashahada ya Uzamili. Mafunzo haya yanahusu misingi ya maendeleo ya jamii, mipango shirikishi, ubunifu na uandishi wa miradi, mbinu za uongozina utawala, mbinu za kuendesha biashara, uchambuzi na upangaji wa masoko. Lengo la mafunzo hayo ni kutoa elimu, ujuzi na mbinu mbalimbali zitakazowasaidia wataalam wa Maendeleo ya Jamii kutekeleza dhana ya maendeleo ya jamii kwa vitendo katika jamii kwa kuwawezesha watu kutambua uwezo walio nao wa kubaini matatizo na uwezo wao wakutumia raslimali zilizopo ili kuongeza kipato na

kupunguza umaskini. Aidha, Wizara itaendelea kukamilisha jengo la maktaba katika Chuo cha Tengeru, ujenzi wa uzio katika Chuo cha Rungemba na Ruaha, kujenga jengo la utawala, jengo la maktaba, ukumbi wa mikutano, nyumba za watumishi katika Chuo cha Uyole, kukarabati majengo na miundombinu katika Vyuo vya Buhare, Mlale, Ruaha, Mabughai, Missungwi na Monduli ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi

48. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2014/15, Vyuo vitano vya Maendeleo ya Wananchi vya Sofi, Mputa, Kilwa Masoko, Tarime na Mwanhala vilifanyiwa ukarabati mkubwa na mdogo wa madarasa, mabweni, majengo ya utawala, ujenzi wa vyoo, mabwalo ya kulia chakula, miundombinu ya mifumo ya umeme, maji safi na maji taka. Aidha, Vyuo vya Nandembo, Sengerema na Chala vilipewa magari ili yatumike kwa usafiri na kutolea mafunzo kwa vitendo. Katika mwaka wa fedha wa 2015/16, Wizara itaendelea kuboresha maeneo ya kutolea

49. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kushiriki na kutekeleza mikataba na maazimio mbalimbali ya kikanda na kimataifa ambayo nchi imeridhia, Wizara ilishiriki katika mkutano wa'' African Regional Conference'' uliofanyika tarehe 17-19 Novemba, 2014 Addis Ababa - Ethiopia. Mkutano huo ulilenga kupitia taarifa ya nchi ya Beijing+20 na kutoa maazimio ya utekelezaji wa maeneo 12 yaliyoanishwa. Taarifa hiyo iliwasilishwa katika kikao cha 59 cha Kamisheni ya Hali ya Wanawake ambacho kilifanyika nchini Marekani Machi, 2015.

Aidha, mkutano huo ulitoa fursa kwa washiriki kujadili masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya wanawake na haki za wasichana na kutoa mapendekezo ya kiutekelezaji katika kufikia usawa wa kijinsia. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kushiriki katika utekelezaji wa mikataba ya kikanda na kimataifa ikiwa ni pamoja na kutoa michango na uzoefu wake katika kuboresha na kuimarisha usawa wa jinsia na uwezesaji wa wanawake pamoja na kushiriki mikutano mbalimbali.

50. Mheshimiwa Spika, Ili kufikia lengo la kuwepo kwa usawa wa jinsia, uingizwaji wa masuala ya jinsia katika mipango, mikakati, bajeti, sera na programu mbalimbali bado unaendelea kutiliwa mkazo. Katika kipindi cha mwaka 2014/15, Wizara iliendesha mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu zilizochambuliwa kijinsia kwa maafisa 50 kutoka Wizara mbalimbali, Taasisi zisizo za serikali na Taasisi za Elimu. Mafunzo hayo yaliwezesha ukusanyaji wa takwimu zilizochambuliwa kijinsia na hivyo kuweza kukamilisha Taarifa ya Hali ya Jinsia Nchini "Tanzania Country Gender Profile – TCGP". Taarifa hizo zitatumiwa na

serikali pamoja na wadau mbalimbali katika kufanya maamuzi, ushawishi, utungaji sera na mipango mbalimbali ya maendeleo kwa kuzingatia usawa wa jinsia. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa ngazi mbalimbali za uongozi ili kujenga uelewa wa pamoja kuhusu uingizwaji wa masuala ya jinsia, uboreshaji wa Taarifa ya Hali ya Jinsia Nchini pamoja na usambazaji wa taarifa hiyo.

51. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia vikao vya robo mwaka vya kikundi cha uingizaji wa masuala ya kijinsia katika Sera za Kitaifa na Kisekta (Gender Mainstreaming Working Group for Macro Policies) imeweza kuandaa Mwongozo wa Uingizaji wa Masuala ya Jinsia katika Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (Big Results Now - BRN). Lengo ni kuwezesha kuwepo kwa matokeomakubwa kwa kuzingatia mahitaji ya makundi yote ya wanawake na wanaume. Mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kuratibu uingizwaji wa masuala ya jinsia katika Sera za Kitaifa pamoja na kujenga uwezo kuhusu uingizwaji wa masuala ya kijinsia

52. Mheshimiwa Spika, Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) ambayo ni mali ya umma inayomilikiwa kwa kiasi kikubwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kufikia mwaka 2014/15, Benki ina wanahisa wadogowadogo wanaokadiriwa kufikia 160 wanaomiliki hisa zisizozidi asilimia 2. Katika mwaka, 2014/15, Benki ilitoa mikopo kwa wajasiriamali wapatao 10,847.

Kati ya idadi hiyo wanawake ni 8,135 sawa na asilimia 75 ya wateja wote waliopatiwa mikopo. Thamani ya mikopo iliyotolewa ni kiasi cha Sh. 12,469,650,000. Kati ya kiasi hicho, jumla ya Sh. 8,561,200,000 zilikopeshwa kwa wanawake, sawa na asilimia 69 ya mikopo iliyotolewa. Benki imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya mtaji kwa kutafuta fursa mbalimbali za kupata fedha za kujiendesha na kutanua mtaji wake.

53. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2015/16, benki inatarajia kuendelea kutoa huduma zake katika maeneo mengi zaidi kupitia njia ya wakala wa benki (Agency Banking) na kufungua ofisi za kutolea huduma za mikopo mikoani.

Aidha, katika mwaka wa kibenki wa 2014, Benki ya Wanawake imetengeneza faida ya shilingi milioni 141 kabla ya kodi (Profit Before Tax). Menejimenti na Bodi ya Wakurugenzi wa benki wanaona mwaka 2015 ni kipindi mwafaka cha kuanza mchakato rasmi wa kuuza hisa ili kukuza mtaji wa benki na kuiwezesha Benki kujiendesha na kupanua wigo wa huduma pasipo kutegemea mtaji kutoka Serikalini.

54. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2014/15, Mfuko wa Wanawake umetoa jumla ya Sh. 31,000,000 kwa Halmashauri tatu ambazo ni Bunda, Iringa pamoja Mkalama. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeadhimisha Siku ya Wanawake Duniani iliyofanyika Mkoani Morogoro katika Uwanja wa Jamuhuri na Mgeni Rasmi alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Kaulimbiu ya siku hiyo ilikuwa 'Uwezeshaji Wanawake; Tekeleza Wakati ni Sasa'. Aidha, siku ya Maadhimisho shughuli mbalimbali zilifanyika ikiwemo maonyesho ya biashara kutoka Wizara

Maendeleo ya Watoto

55. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2014/15, Wizara iliandaa Mpango Kazi wa Taifa wa Miaka Mitano wa Ushiriki wa Watoto (2014-2019). Lengo la Mpango Kazi huo likiwa ni kuongeza ushiriki wa watoto katika masuala mbalimbali yanayowahusu. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kusambaza mpango kazi huu katika Halmashauri za Wilaya.

56. Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha uandaaji wa rasimu ya Sera ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto pamoja na Mkakati wake wa Utekelezaji. Sera hii ipo katika ngazi za juu za maamuzi kwa ajili ya kupitishwa. Sera imeandaliwa mahsusi ili kuhakikisha uwepo wa mfumo fungamanishi na shirikishi wa utoaji huduma za Malezi Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto.

Katika mwaka 2015/16, Wizara inataraji kukamilisha mchakato na kutoa nakala 3,000 za sera hiyo pamoja na mkakati wake wautekelezaji na kusambaza kwa wadau kwa ajili ya utekelezaji

57. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuratibu utoaji wa taarifa zinazohusu vitendo vya ukatili dhidi ya watoto kwa kushirikiana na Asasi isiyokuwa ya Kiserkali ya C-SEMA ambapo kati ya mwezi Julai, 2014 na Machi, 2015 jumla ya simu 21,960 zilipigwa kupitia mtandao wa simu namba 116. Taarifa hizo zilishughulikiwa kulingana na aina ya tatizo/ suala lililowasilishwa. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kuratibu utoaji wa huduma hii kwa kushirikiana na asasi husika.

58. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2014/15, Wizara iliratibu maandalizi ya taarifa ya kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Kamati ya Haki za Watoto ya Umoja wa Mataifa kuhusu ripoti ya nchi ya 3, 4 na 5 iliyowasilishwa katika kamati hiyo mnamo mwezi Januari, 2012 na kuwasilisha majibu ya hoja kwenye kamati hiyo mwaka 2015. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kuyafanyia kazi maoni yajumla 'Concluding Observation' yaliyotolewa na Kamati hiyo ya Haki za Watoto ya Umoja wa Mataifa.

59. Mheshimiwa Spika, Mwaka 2014/15, Wizara yangu ilizindua rasmi Zana za Mawasiliano kwa ajili ya kuzuia ukatili dhidi ya watoto yenye lengo la kuelimisha wazazi, watoto, wanahabari na wanajamii jinsi ya kujizuia na kutoa taarifa kuhusu matukio mbalimbali ya ukatili dhidi ya mtoto ambapo nakala 1,000 za zana hizo zilisambazwa kwa wadau wa masuala ya ulinzi na haki za watoto hapa nchini. Katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara itasambaza nakala 2,000 za zana hizo na kuratibu utekelezaji wake.

60. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2014/15, Wizara yangu imeratibu Maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani ambayo huadhimishwa kila mwaka tarehe 15 Mei na mwaka huu yameadhimishwa katika ngazi ya Mkoa. Kaulimbiu ya mwaka 2015 ni:

“Usawa wa Kijinsia na Haki za Watoto katika Familia: Wanaume Wawajibike”

Kaulimbiu hii inaelekeza umuhimu wa wanaume katika kutambua na kuheshimu usawa wa kijinsia katika jamii zetu. Kuachana na mfumo dume ndani ya jamii kutompa fursa mwanamke/msichana kupata maendeleo ya kiuchumi, kisiasa, kielimu, afya na kiutamaduni.

Aidha, Wizara imeratibu maandalizi ya Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika ambayo kila mwaka yanaadhimishwa tarehe 16 Juni. Kaulimbiu ya mwaka 2015 ni:

“Tokomeza Mimba na Ndoa za Utotoni: Kwa Pamoja Tunaweza”.

Kaulimbiu hii inatukumbusha sisi wadau wa maendeleo ya watoto pamoja na wananchi jukumu letu katika kuwalinda watoto dhidi ya ndoa na mimba za utotoni, ambazo zina athari kubwa katika maendeleo ya elimu na afya ya mtoto. Aidha, kuachana na kupiga vita mila na desturi zenye athari katika jamii zetu ndio silaha pekee katika kukabiliana na tatizo la mimba na ndoa za utotoni.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

61. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15, Wizara yangu iliendelea kusajili NGOs ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 pamoja na Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na.24/2002 iliyorekebishwa mwaka 2005. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2015 jumla ya mashirika 7,060 yalipatiwa sajili katika ngazi mbalimbali ili kuyawezesha kutambulika kisheria na kutekeleza malengo yaliyokusudiwa. (Jedwali Na.3). Katika ipindi cha mwaka 2015/16, Wizara itaendelea na usajili wa Mashirika hayo.

62. Mheshimiwa Spika, mwaka 2014/15, Wizara yangu ilichukua hatua mbalimbali za kuimarisha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini. Hatua hizi ni pamoja na: kuendelea kuliwezesha Baraza la Taifa la NGOs kutekeleza majukumu yake ya kisheria kwa kupitisha Kanuni za Uendeshaji wake na Kanuni za Chaguzi za Baraza hilo za ngazi mbalimbali. Kanuni hizi zitaliwezesha Baraza na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa ujumla kujiendesha kwa ufanisi zaidi kwa kujidhibiti ili kuimarisha taswira na mchango wao katika jamii.

63. Mheshimiwa Spika, hatua nyingine iliyochukuliwa katika uratibu wa NGOs ni kukuza ubia baina ya Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuingia makubaliano ya kufanya kazi kwa pamoja na NGOs 20 zinazojihusisha na maendeleo ya wanawake na watoto.

Aidha, Wizara iliendelea kuhamasisha ubia baina ya mashirika haya na Taasisi nyingine za Serikali zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa. Pia, Wizara yangu iliiboresha Benki ya Taarifa na Takwimu za NGOs kwa kuingiza masuala ya jinsia. Taarifa na takwimu hizi zinatumiwa na wadau katika kufikia maamuzi mbalimbali ya kimaendeleo. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kuratibu na kufuatilia shughuli za NGOs kwa lengo la kuendelea kujenga mazingira wezeshi ya NGOs katika kushiriki na kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla.

Uhamasishaji, Uelimishaji na Ushawishi

64. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15, Wizara yangu iliandaa vipindi vya luinga na redio, matangazo kupitia magazeti, vipeperushi na mabango, mikutano ya waandishi wa habari kwa ajili ya kuelimisha umma kuhusu masuala ya maendeleo ya jamii, jinsia, wanawake, familia, haki za watoto na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Aidha, kwa kushirikiana na UNICEF, Wizara yangu imeandaa kipindi maalum cha 'WALINDE WATOTO' ambacho kinatangazwa kupitia redio 14 zenye usikivu wa kitaifa na kikanda Tanzania Bara na Zanzibar. Lengo la kipindi ni kuhamasisha wadau wa maendeleo ya mtoto kushiriki kikamilifu katikajitihada za kuzuia na kutokomeza ukatili dhidi ya watoto nchini. Katika mwaka 2015/16 Wizara itaendelea kuhamasisha, kuelimisha na kushawishi umma kuhusu masuala ya maendeleo ya jamii, jinsia, wanawake, familia, haki za watoto na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Uratibu wa Sera, Programu na Mipango ya Wizara.

65. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2014/15, Wizara yangu imeandaa Andiko la Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Wananchi lenye awamu mbili za utekelezaji kwa vipindi vya miaka mitano mitano zilizohuishwa na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano awamu ya pili na ya tatu. Aidha, programu hiyo ni sehemu ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu na

rasimu yake imewasilishwa na kupitishwa katika vikao vya sekta ya Elimu. Programu inalenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, utoaji wa ujuzi na stadi mbalimbali na elimu ya ujasiriamali zitakazoweza vijana na wananchi kupata fursa za kuongeza vipato vyao kwa kujiajiri au kuajiriwa na hivyokuchangia katika kutekeleza malengo ya Dira ya Taifa 2025. Kwa mfano, kuzalisha mafundi mchundo watakaotumika katika fursa iliyopo ya uchumi wa gesi na mafuta katika jamii.

Aidha, Wizara inaandaa maandiko ya Programu ya Kuwezesha Wanawake na Wasichana Kiuchumi, Programu ya Kutokomeza Ndoa za Utotoni na Programu ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kama sehemu ya kutekeleza **Agenda ya Maendeleo ya Afrika 2063** kwa kuanza kutoa msukumo maalum wa kuwaendeleza wanawake na watoto. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kuratibu utafutaji wa fedha kutoka vyanzo mbalimbali ili kutekeleza programu hizo.

66. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliandaa Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini utakaotumika kufuatilia utekelezaji wa sera, mikakati, mipango na mikataba ya kikanda na kimataifa iliyoridhiwa. Katika mwaka 2015/16, Wizara itawezesha upatikanaji wa taarifa za msingi kulingana na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ulioandaliwa. Aidha, itawajengea uwezo Maafisa 25 wa Maendeleo ya Jamii wa Mikoa kuhusu ukusanyaji, uchakataji, uchambuzi na uandaaji wa taarifa za utekelezaji wa sera za Wizara.

67. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia maendeleo ya Sera na Programu za Sekta ya Maendeleo ya Jamii. Katika mwaka 2015/16, Wizara itafanya tathmini kuhusu ufanisi wa Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kubaini changamoto na mafanikio yaliyopatikana. Aidha, matokeo ya tathmini yatatumika kurekebisha sera iliyopo ili kuweka mazingira wezeshi kwa NGOs na kuziwezesha kushiriki kikamilifu katika kuleta maendeleo kwa wananchi.

Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu

68. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kutoa huduma za Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu kwa madhumuni ya kuboresha utendaji kazi kwa kuzingatia misingi ya haki, usawa, uadilifu, utawala bora na uwazi kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi katika kazi. Wizara imeendelea kuwekamkazo katika kudhibiti vitendo vya rushwa na uzembe kazini ili kuwa na watumishi waadilifu na wawajibikaji, wenye ari, moyo na msimamo thabiti katika utekelezaji wa majukumu katika utumishi wa Umma. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2015/16, Wizara itaendelea kutoa huduma za kiutawala na usimamizi wa rasilimaliwatu kwa kuzingatia misingi ya haki, usawa, uadilifu na utawala bora.

69. Mheshimiwa Spika, Ili kuwawezesha watumishi kutekelezajukumu yao kwa ufanisi, Wizara imewawezesha watumishi kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ndani na nje ya nchi. Kwa mwaka 2014/15, watumishi 64 wamewezeshwa kupata mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwapatia mafunzo ya kuongeza weledi na ufanisi wa kazi za utumishi wa umma.

70. Mheshimiwa Spika, Mwaka 2014/15, Wizara imeendelea kutoa motisha kwa watumishi kwa kuwapandisha vyeo jumla ya watumishi 156, kuwabadilisha kada watumishi 2 na kuwathibitisha kazini watumishi 38 wa kada mbalimbali. Katika mwaka 2015/16, Wizara inatarajia kuwabadilisha kada watumishi 15, kuwapandisha vyeo watumishi 355 na kati yao watumishi 105 ni wa kada ya ualimu

71. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2014/15, Wizara yangu imeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kufanya ukarabati na uboreshaji wa baadhi ya maeneo ya ofisi (Makao Makuu) kama vile ujenzi wa eneo la kuegesha magari, ununuzi wa jenereta, uboreshaji wa masijala pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya umeme, simu na *Internet*. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa kuendelea kufanya ukarabati mdogomdogo katika jengo la Wizara Makao makuu.

72. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka 2014/15, Wizara imeajiri watumishi wapya wa kada mbalimbali wapatao 148 na kufanya Wizara kuwa na watumishi 1,122. Nafasi 428 zimekwisha tangazwa na Sekretarieti ya Ajira, hivyo mchakato utakapo kamilika watumishi hao pia wataajiriwa. Hata hivyo, Wizara bado inakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi hasa wa kada ya ukufunzi katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na vya Maendeleo ya Jamii. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imepeleka maombi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya kupata kibali cha kuajiri watumishi wa kada mbalimbali. Kwa mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kuomba kibali cha kuajiri watumishi ili kupunguza pengo lililopo.

73. Mheshimiwa Spika, katika kupambana na janga la UKIMWI na magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile kisukari na magonjwa ya moyo, mwaka 2014/15 Wizara imewawezesha watumishi 154 kupata mafunzo, ushauri nasaha pamoja na huduma ya upimaji afya kwa hiari. Wizara imeendelea kuhamasisha watumishi kupima afya zao kwa kutumia utaratibu wa kuwaleta wataalamu wa huduma za afya kwa ajili ya ushauri nasaha, upimaji wa hiari na kuwapatia watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI huduma ya lishe.

Kwa kutambua umuhimu wa michezo katika kuimarisha afya za watumishi, kwa mwaka 2014/15, Wizara iliwawezesha watumishi kushiriki katika mashindano ya SHIMIWI. Kwa mwaka wa fedha 2015/16, Wizara itaendelea kuhamasisha upimaji wa afya ikiwa ni pamoja na kutoa huduma stahiki na kuendelea kuhamasisha watumishi kushiriki katika michezo.

74. Mheshimiwa Spika, Kutokana na umuhimu wa kushirikisha watumishi kuboresha utendaji kazi, utekelezaji wa majukumu ya Wizara na kukabiliana na changamoto mbalimbali za kiutendaji, Wizara imeweza kufanya Mkutano mmoja wa Baraza la Wafanyakazi kwa mwaka 2014/15. Kwa mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kuhakikisha Mikutano ya Baraza la Wafanyakazi inafanyika.

E. HITIMISHO

75. Mheshimiwa Spika, Majukumu ya Wizara yangu ni kuhakikisha jamii na wananchi wanabadilika kifikra na kimtizamo ili kuwa na jamii inayoshiriki kikamilifu katika kujitea maendeleo yao wenyewe na Taifa kwa ujumla Majukumu haya ni mtambuka, hivyo basi utekelezaji wa Malengo na Mipango ya Wizara kwa mwaka 2015/16, bado utahitaji ushirikiano mkubwa zaidi wa wadau mbalimbali hasa Mikoa na Halmashauri.

F. SHUKRANI

76. Mheshimiwa Spika, Napenda sasa kumshukuru sana Naibu Waziri, Mhe. Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb.), kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kuongoza Wizara hii. Vilevile, napenda kutoa shukrani za dhati kwa: Katibu Mkuu, Bibi Anna Tayari Maembe, Naibu Katibu Mkuu, Bibi Nuru H. M. Millao; Wakurugenzi; Wakuu wa Vitengo; Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Wanawake Tanzania - Bibi Magreth Chacha; Wakuu wa Vyuo; na Wafanyakazi wote wa Wizara yangu wa ngazi zote, kwa jitihada zao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ambayo ni pamoja na kuniwezesha mimi kuwasilisha hotuba hii mbele ya Bunge lako tukufu.

77. Mheshimiwa Spika, Napenda kumalizia hotuba yangu kwa kuwashukuru wadau wote tunaofanya nao kazi na kushirikiana kwa namna moja au nyingine. Peke yetu kama Wizara tusingefikia mafanikio niliyoyataja.

Naomba kupitia Bunge lako tukufu, kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafuatao: Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Asasi ya Wanawake na Maendeleo (WAMA); Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (EOTF); Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP); Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA); Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA); Shirikisho la Vyama vya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (FAWETA); *Medical Women Association of Tanzania (MEWATA); White Ribon; Plan International; Save the*

Children na Mashirika mengine mbalimbali Yasiyo ya Kiserikali pamoja na wale wanaofanya kazi kwa maslahi ya jamii kwa namna moja au nyingine.

78. Mheshimiwa Spika, Napenda pia kuyashukuru Mashirika kutoka nchi rafiki ambayo yameendelea kutusaidia na kufanya kazi na sisi. Mashirika hayo ni pamoja na: GPE; KOICA na UK Education. Aidha, nayashukuru Mashirika ya Umoja wa Mataifa ambayo ni: UNICEF; UNDP; UNFPA na UN WOMEN kwa misaada yao mbalimbali iliyofanikisha utekelezaji wa majukumu mengi ya Wizara yangu.

G. MAKADIRIO YA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2015/16

79. Mheshimiwa Spika, Ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa mwaka 2015/16, sasa naliomba Bunge lako tukufu liidhinishe matumizi ya shilingi 31,421,641,000. Kati ya fedha hizo,

- a. Shilingi 11,038,075,000 ni kwa ajili ya Mishahara
- b. Shilingi 9,460,146,000 ni kwa ajili ya Matumizi
Mengineyo
- c. Shilingi 10,923,420,000 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambapo Shilingi 8,000,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 2,923,420,000 ni fedha za nje.

80. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Waziri wa Kazi!

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii iliyochambua bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira (Fungu 65) na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (Fungu 15), naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio na Mapato ya Wizara ya Kazi na Ajira na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hai na kuniwezesha kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu leo. Vile vile sina budi kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mkubwa walionipa ndani na nje ya Bunge katika kipindi chote cha Bunge hili, katika kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiki ni kikao cha mwisho cha uhai wa Bunge hili Tukufu la Ishirini kabla halijavunjwa, niruhusu nichukue nafasi hii

kutoa shukrani zangu za dhata kwanza kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa imani kubwa aliyoonyesha kwangu kipindi chote cha uongozi wake kwa kuendelea kunitiua kuwa mmoja wa washauri wake; kwanza kama Naibu Waziri na kwa miaka mitano hii ya mwisho kama Waziri wa Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi chote hiki nimejifunza mengi sana kutoka kwake na nimefaidika na vipaji vingi alivyonavyo ikiwemo ustahimilivu, uvumilivu, umahiri na upendo kwa wenzake na anaowaongoza. Nategemea kuwa nami nimetoa mchango wangu katika kumsaidia ili kutimiza majukumu yake kama Kiongozi Mkuu wa nchi yetu na pia katika kutimiza malengo tuliyojiwekea katika Ilani yetu ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Namshukuru sana na namwombea afya njema na maisha marefu hapa duniani.

Pia napenda nimshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Gharib Bilal ambaye katika kipindi hiki cha miaka mitano, amekuwa pia mfano mkubwa kwangu hasa kwa umahiri katika uongozi.

Aidha, nachukua nafasi hii kumshukuru Waziri Mkuu Mheshimiwa Kayanza Mizengo Peter Pinda kwa umakini mkubwa katika uongozi wake na maelekezo yake mahiri katika utendaji wangu wa kazi wa siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu ambao tumeshirikiana vema na maafisa wa Serikali wote ambao tumeshirikiana nao vema katika kipindi chote. Wengi wao wamenipa ushauri na ushirikiano mkubwa ulioniwezesha nitekeleze majukumu yangu kama Waziri wa Kazi na Ajira. Wote nawashukuru sana na nawaombea Mungu awabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga, Mbunge wa Segerea, Naibu Waziri wa Kazi na Ajira kwa ushirikiano mkubwa alionipatia na kuifanya Wizara yetu ifanye kazi kwa umoja na upendo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Katibu Mkuu wa Wizara yangu, Ndugu Eric Shitindi ambaye alikuwa kiungo kikubwa kati ya ofisi yetu, Wizara yangu, nami binafsi na Watendaji wengine wa Wizara yetu na hata Wizara nyingine. Nawashukuru Wakurugenzi, Maafisa wa Wizara pamoja na Wakuu na Watendaji wote wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ambao nimefanya nao kazi kwa karibu na kwa ushirikiano mkubwa sana na leo hii tumeifikisha Sekta ya Kazi na Ajira hapa tulipofikia.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi hii ya pekee naomba kuishukuru sana familia yangu ambayo imekuwa nguzo kubwa katika maisha yangu ya kisiasa, kijamii na kiroho. Namshukuru kwa dhati binti yangu Patricia Robi Kabaka na wajukuu zangu wapendwa Christina, Michael-Angelo na somo wangu Gaudentia kwa upendo na urafiki mkubwa walio nao kwangu. Mungu ndiye ajuaye na ndiye Mpaji wa yote.

Mwisho ingawa siyo kwa umuhimu, nawashukuru wanawake wapendwa wa Mkoa wa Mara walioniwezesha kuwa Mbunge. Sina cha kuwapa ila kuwaombea baraka za Mwenyezi Mungu. Wananchi wa Mkoa wangu wa Mara wamenipatia ushirikiano na upendo mkubwa sana nawashukuruni sana nyote na kuwasihii tuendeleo kuwa wamoja katika kuleta maendeleo ya Mkoa wetu wa Mara kwani Mara ni imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuungana na Wabunge wenzangu kuwapongeza Viongozi wetu wa Chama na Serikali kwa kazi nzuri waliyoifanya tangu wateuliwe kushika nyadhifa mbalimbali. Ni matumaini yangu kwamba bado wananchi wana imani na Chama cha Mapinduzi na Wabunge wake na hivyo nina imani kubwa kwamba wataendelea kuwapigia kura ili waendeleo kuwawakilisha katika kipindi kijacho cha miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza na kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Said Mtanda, Mbunge wa Mchinga (Lindi) na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Albert Obama, kwa ushauri, maoni na ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wote wa uhai wa Kamati hii na hususan wakati wa maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Kamati kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina Taarifa ya Utekelezaji ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2014/2015 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2015/2016 katika kikao chake kilichofanyika Dar es Salaam tarehe 6 na 7 Mei, 2015. Kadhalika ninaishukuru Kamati hii kwa kutembelea Taasisi na miradi mbalimbali inayotekelezwa na Tasisi zilizo chini ya Wizara yangu ikiwemo mradi unaotekelezwa na NSSF wa daraja la Kigamboni na ujenzi wa nyumba za kisasa zinazojengwa na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF). Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hiyo yamezingatiwa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa napenda nichukue fursa hii kuungana na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii ambayo inasimamia Wizara yangu kwa kuomboleza kifo cha ghafla cha aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu, Marehemu

Capt. John Damiano Komba aliyekuwa Mbunge wa Mbinga Magharibi. Kifo hicho kimekuwa ni pigo kwa Kamati yetu kwa kuwa Marehemu alikuwa nguzo imara katika Kamati hiyo. Nichukue fursa hii kuwapa pole familia, ndugu, jamaa na marafiki wa Marehemu. Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ailaze Roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amina!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kutekeleza shughuli zake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Malengo ya Milenia, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Awamu ya Pili, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano, Mikataba mbalimbali ya Kimataifa inayohusu masuala ya kazi na ajira na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Lengo la msingi la miongozo hiyo ni kuboresha maisha ya wananchi, kudumisha amani, utulivu na umoja, kuimarisha utawala bora, kujenga uchumi madhubuti na endelevu, kuboresha afya na kutunza mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imetekeleza miongozo hiyo kwa kuimarisha viwango vya kazi, kuhakikisha kuna mazingira yanayokidhi afya na usalama wa wafanyakazi mahali pa kazi, kuboresha maslahi ya wafanyakazi, kuimarisha ushirikishwaji wa wafanyakazi na kukuza ajira nchini.

Mafanikio yaliyopatikana yamewezesha kuendelea kuwa na utulivu katika Sekta ya Kazi, hali ambayo imesaidia kukua kwa uchumi na kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje, hivyo kukuza ajira kwa makundi mbalimbali ya wananchi katika nchi yetu na kuwapunguzia umasikini wa kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa kazi za Wizara yangu kwa mwaka 2014/2015 na malengo ya mwaka 2015/2016, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu - Mheshimiwa Dkt. Mary M. Nagu, Mbunge wa Jimbo la Hanang, kwa hotuba zao nzuri ambazo zimefafanua kwa kina utekelezaji wa sera, mipango na mikakati ya Serikali na kutoa mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Malengo, maelezo na vigezo vilivyomo kwenye hotuba hizo vimezingatiwa kikamilifu katika kuandaa bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza ni Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010, sehemu ya pili ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2014/2015 na sehemu ya tatu ni malengo ya Wizara kwa mwaka 2015/2016 na maombi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Malengo hayo.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imetekeleza ipasavyo Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 78, 80, 81 na 82 kuhusu masuala ya Ajira, Kazi na Hifadhi ya Jamii. Taarifa ya kina ya utekelezaji wa Ilani hiyo imeainishwa kwa kina katika Kitabu cha hotuba kuanzia ukurasa wa nane hadi ukurasa wa 23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kukabiliana na tatizo la ajira nchini hususan kwa vijana, imetekelezwa kazi zifuatazo:-

(a) Imeandaa na kuanza kutekeleza Programu ya miaka mitatu ya kukuza ajira kwa vijana inayolenga kutoa fursa za ajira kwa vijana 840,000. Programu hiyo inalenga kuwajengea vijana uwezo na ujuzi wa stadi mbalimbali za kazi na ujasiriamali; kuwawezesha kupata mitaji, nyenzo na vifaa vya uzalishaji mali; na kuwapatia vijana maeneo ya uzalishaji na biashara.

Katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015 jumla ya ajira 1,929,938 zilizalishwa nchini ikiwa ni karibu asilimia 200 ya lengo lililoweka la kuzalisha ajira milioni moja katika kipindi hicho cha miaka mitano. Idadi hii inajumuisha ajira katika sekta zifuatazo:-

Ø Sekta ya Umma zilisalishwa jumla ya ajira 991,890; Sekta ya Kilimo ajira 417,531, Sekta ya Elimu ajira 144,764; Sekta ya Afya ajira 29,444; Sekta ya Ujenzi wa Miundombinu ajira 200,484; Sekta ya Nishati ajira 1,479; Miradi ya Kijamii ajira 102,948; na Sekta nyingine Serikalini ajira 15,240.

Ø Jumla ya ajira zilizozalishwa katika Sekta binafsi ni 1,018,048. Mawasiliano ajira 184,030; Viwanda vidogo na vya kati (SMEs) ajira 26,098; na Miradi ya uwekezaji kupitia kituo cha TIC ajira 325,622; vituo vya EPZ ajira 67,646 na maeneo mengine ya uwekezaji ajira 414,652.

(b) Serikali imeandaa na kuanza kutekeleza Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi wa Nguvukazi (*Skill Development Program - SDP*) chini utaratibu wa Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa – BRN.

Wizara ya Kazi na Ajira kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani na Wadau wengine kuanzia mwezi Julai 2013, imeendesha mafunzo kwa vitendo kazini (*Apprenticeship/Intership*) kwa wahitimu wa vyuo ambao hawajaajiriwa. Utaratibu huo umeanza kwa majaribio na umeonyesha mafanikio makubwa katika Sekta ya Utalii. Kupitia Programu hiyo ya SDP, katika mwaka 2015/2016 kazi zitakazotekelezwa ni zifuatazo:-

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Ø Vijana 4,200 kupatiwa mafunzo ya vitendo kazini (*internship/Apprenticeship*) katika sekta sita za kipaumbele za maji, nishati na madini, kilimo, elimu, afya na utalii;

Ø Waajiri kuwezesha kutoa mafunzo ya ujuzi na ufanisi wa kazi kwa wafanyakazi 10,000; na

Ø Vijana 5,000 wa sekta isiyo rasmi wasio na vyeti vya ujuzi, kupatiwa mafunzo kuwawezesha kupatiwa vyeti vya ujuzi huo;

(c) Serikali imepitisha Sheria ya Ajira kwa wageni ya mwaka 2014 katika Bunge la 19 mwezi Machi, 2015 ili kusimamia ipasavyo ajira za wageni nchini kwa lengo la kulinda na kuongeza ajira za Watanzania katika maeneo ya uwekezaji. Sheria hiyo imeweka mamlaka moja ambayo ni Wizara ya Kazi na Ajira kuwa msimamizi wa utoaji wa vibali vya ajira kwa wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kuhakikisha yanakuwepo mahusiano mema baina ya waajiri na wafanyakazi na kuhamasisha uzuiaji na utatuzi wa migogoro kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kukuza tija mahali pa kazi katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015 imetekeleza yafuatayo:-

(a) Jumla ya kaguzi 220,350 zimefanyika ikiwa ni wastani wa kaguzi 40,000 kwa mwaka. Lengo la kaguzi hizo ni kuhakikisha waajiri wanafuata Sheria za Kazi ipasavyo.

(b) Jumla ya kaguzi za kawaida 26,412 na kaguzi maalum 53,807 kuhusiana na afya na usalama mahali pa kazi zimefanyika. Wafanyakazi 136,076 walipimwa afya zao ili kubaini matatizo na athari za kiafya zitokanazo na maeneo wanayofanyia kazi.

(c) Jumla ya migogoro 10,281 imesuluhishwa na jumla ya migogoro 6,057 imeamuliwa na Tume ya Usuhishi na Uamuzi (CMA).

Katika kipindi hicho muda wa kusikiliza na kusuluhisha umepungua kutoka siku 30 mwaka 2010 hadi siku 12 mwezi Aprili, 2014.

(d) Elimu kwa Umma kuhusu Sheria za Kazi ilitolewa kwa wafanyakazi wapatao 1,908,000 na waajiri 6,890.

(e) Jumla ya vyama vya wafanyakazi vilivyosajiliwa nchini hadi sasa ni 31, ikilinganishwa na vyama 24 vilivyokuwepo mwaka 2009. Kiambatisho katika kitabu changu kinaonesha idadi ya vyama vilivyosajiliwa.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2010 hadi 2015, Serikali imeendelea kuimarisha Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa lengo la kupanua wigo ili wananchi wengi zaidi wanufaike na huduma zinazotolewa na kufanya huduma zitolewazo kuwa endelevu. Kwa muhtasari kazi zilizotekelezwa kwa kipindi hicho ni ifuatavyo:-

(a) Serikali ilianzisha Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Hifadhi ya Jamii (SSRA) nchini mwaka 2010, kwa lengo la kuboresha Sekta ya Hifadhi ya Jamii.

(b) Serikali ilirekebisha Sheria ya Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii kupitia Sheria Na. 5 ya mwaka 2012 ili kuipa SSRA mamlaka ya kusimamia kikamilifu Sekta ya Hifadhi ya Jamii.

(c) Serikali kupitia SSRA imechukua hatua za kupanua wigo wa kinga ya jamii kuwezesha Watanzania wengi zaidi kufaidika na huduma ya hifadhi ya jamii na mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(i) Wanachama katika Sekta ya Hifadhi ya Jamii wameongezeka mara mbili kutoka 900,000 mwaka 2010 hadi kufikia zaidi ya 2,000,000 mwaka 2015;

(ii) Rasilimali za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii zimeongezeka kutoka trilioni 1.3 mwaka 2005 hadi kufikia trilioni nane mwaka 2015;

(iii) Mafao ya Wanachama walionufaika imekua kutoka Shilingi bilioni 131 mwaka 2005 hadi kufikia Shilingi trilioni 1.3 mwaka 2015;

(iv) Wastaafu (*pensioners*) wameongezeka toka 24,000 mwaka 2005 kufikia takribani 100,000 mwaka 2015;

(v) Jumla idadi ya watu wanaonufaika na huduma za hifadhi ya jamii imefikia watu milioni 6.5 mwaka 2015 kutoka watu 690,000 mwaka 2005; na

(vi) Uwekezaji wa Mifuko ya Hifadhi ya jamii katika miradi ya kijamii na kiuchumi umeongezeka kutoka Shilingi trilioni 1.6 mwaka 2006 hadi kufikia Shilingi trilioni saba mwaka 2015. Hili ni ongezeko la asilimia 250.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanzisha Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ili kutoa fidia kwa wafanyakazi wanaougua au kuumia kazini. Mfuko huu utanza kutekeleza wajibu wake katika mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imetekeleza majukumu yake ya kusimamia viwango vya kazi, ukuzaji wa ajira, ushirikishwaji wa wafanyakazi

mahali pa kazi, uboreshaji wa hifadhi ya jamii na kushughulikia migogoro ya kazi na usalama na afya mahali pa kazi. Kazi zilizotekelezwa katika mwaka 2014/2015 zimeainishwa kwa kina katika kitabu cha hotuba kuanzia ukurasa wa 23 hadi ukurasa wa 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 jumla ya Sh. 9,606,000/= zilikadiriwa kukusanywa ikiwa ni mapato ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2015 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha Sh. 3,120,000/= sawa na asilimia 33 ya makadirio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara (Fungu 65), ilikasimia Sh. 5,815,289,000/= kwa ajili ya kulipa mshahara wa Watumishi (PE), Sh. 8,914,105,000/= kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC); na Sh. 2,925,000,000/= fedha za Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2015, Sh. 4,744,071,997/= sawa na asilimia 82 ya fedha za Mshahara ya Watumishi (PE) na Sh. 2,692,134,371 sawa na asilimia 30 ya fedha za Matumizi Mengine (OC) zilitolewa na kutumika na Wizara. Hakuna fedha za bajeti ya miradi ya maendeleo zimetolewa mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi katika kuhakikisha yanakuwepo mahusiano mema baina ya waajiri na wafanyakazi na kuhamasisha uzuiaji na utatuzi wa migogoro ya kikazi kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kukuza tija mahali pa kazi. Katika mwaka 2014/2015 kazi zilizotekelezwa katika eneo hili ni zifuatazo:-

(a) Jumla ya kaguzi za kazi 1,754 zimefanyika katika maeneo mbalimbali ya kazi nchi. Kaguzi hizo zililenga katika kuangalia utekelezaji wa viwango vya kazi, uzingatiaji wa haki za msingi za kazi mahali pa kazi.

(b) Wizara iliendelea kutoa elimu kuhusu Sheria za Kazi kwa Wafanyakazi 3,536 na Waajiri 673 wa Sekta za Viwanda na Biashara, Afya, Kilimo, Ujenzi, Hoteli, Ulinzi binafsi na Usafirishaji.

(c) Wizara imeanza kuandaa mfumo sahihi wa kuwashirikisha wadau wengi zaidi katika kupanga kima cha chini cha mshahara katika Sekta Binafsi. Mfumo huo ni kuwa na na Bodi moja ya Kitaifa ya kupendekeza kima cha chini cha mshahara.

(d) Mikataba ya Hali Bora 67 ilisainiwa na kusajiliwa na Wizara. Mikataba hiyo inahusisha Sekta za Viwanda, Maji, Biashara pamoja na Hoteli.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuimarisha huduma za hifadhi ya jamii, katika kipindi kinachoishia Aprili, 2015 Wizara kupitia SSRA imetekeleza yafuatayo:-

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(a) Imetoa elimu ya hifadhi ya jamii kwa watu 517,951 na kwa makundi mbalimbali ambayo ni pamoja na Wabunge, Watumishi wa Serikali Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri na Makampuni binafsi;

(b) Elimu ya Hifadhi ya Jamii ilitolewa katika vipindi 173 vya runinga na redio na kupitia vyombo vya habari ikiwa ni pamoja na magazeti, mikutano na waandishi wa habari na ushiriki katika maonesho;

(c) Serikali, imetoa Kanuni mpya ya kuwianisha mafao ya pensheni (*benefits harmonization rule*) iliyoanza kutumika tarehe 01 Julai, 2014.

(d) Serikali imekamilisha taratibu zote muhimu za kuanza kuendesha Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi. Mfuko huo umeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 74(1) cha Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ya mwaka 2008 (*The Workers Compensation Act, 2008*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara katika mwaka 2015 kwa kushirikiana wadau mbalimbali imeendelea kupambana na utumikishwaji wa watoto kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Watoto 8,538 wamezuiwa kuingia kwenye utumikishwaji na kupatiwa shughuli mbadala ikiwa ni pamoja na Elimu ya Msingi kwa watoto 4,619, Elimu ya Sekondari watoto 1,884 na elimu kwa walioikosa 2,035.

(b) Kutoa elimu ya Sheria za Kazi hususan katika masuala yanayohusu katazo la utumikishwaji wa mtoto kwa Walimu 411; Wajumbe wa Kamati za shule 513, Wajumbe wa VICOBA 2,398, vijana 4,738 wenye umri kati ya miaka 15 hadi 17 na Maafisa wa Serikali za Mitaa 3,042.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuhimiza ushirikishwaji wa wafanyakazi mahali pa kazi. Hatua hii imesaidia sana kuboresha mahusiano mazuri na kuwepo hali ya utulivu mahali pa kazi nchini. Kazi zilizotekelezwa katika eneo hili kwa kifupi ni kama zifuatazo:-

(a) Wizara ilitatua jumla ya migomo tisa iliyopokelewa kutoka kwa waajiri wa Sekta za Viwanda, Ujenzi na Usafirishaji; na

(b) Wizara iliratibu kikao kimoja cha viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kujadili maslahi ya wafanyakazi nchini.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na juhudi za kuhamasisha wadau mbalimbali kushiriki katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ajira ya Mwaka 2008 kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Wizara iliandaa Kongamano la Wakuu wa Mikoa lililofanyika mwezi Novemba, 2014 kuhusu ukuzaji wa ajira nchini.

Kupitia Kongamano hilo, Wizara imewekeana Mkataba (*Memorandum of Understanding*) na Wakuu wa Mikoa wa kukuza ajira kwa vijana na kuweka mazingira wezeshi kwa vijana kujiajiri katika maeneo yao.

(b) Kupitia Sera na miongozo kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 jumla ya ajira 574, 040 zilizalishwa katika Sekta za Kilimo ajira 154,560; Elimu ajira 36,071; Afya ajira 3,452; Ujenzi wa Miundombinu ajira 107,527; Nishati ajira 378; na Miradi ya ya Kijamii ajira 9,455.

Sekta nyingine Serikalini zilizalisha ajira 5,274. Jumla ya ajira zilizozalishwa katika Sekta binafsi ni 257,322 kwa mchanganuo ufuatao:-

Mawasiliano ajira 6,809; Viwanda vidogo na vya kati; ajira 6,524 na miradi ya uwekezaji kupitia Kituo cha TIC ni 34,164; uwekezaji katika Vituo vya EPZ 16,911 na sekta nyingine za uwekezaji ni 192, 895. Viambatisho katika kitabu vinaonesha yote hayo.

(c) Mawakala 96 wanaotoa huduma za ajira walipewa usajili wa mwaka mmoja kuanzia tarehe 13/03/2015 hadi 12/03/2016.

(d) Wizara imeratibu uandaaji wa muswada wa kutunga Sheria ya Ajira za Wageni kwa lengo la kuimarisha na kuongeza ufanisi wa utoaji wa vibali vya ajira kwa wageni nchini. Sheria ya Ajira ya Wageni ya mwaka 2014 imetungwa na Bunge mwezi Machi, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kuhimiza na kufuatilia haki mbalimbali za Wafanyakazi na Waajiri, ikiwemo haki ya kuanzisha, kujiunga na kushiriki katika shughuli mbalimbali halali za Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri. Katika mwaka uliopita kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

(a) Kusajili Chama cha wafanyakazi cha Kutetea Haki na Maslahi ya Walimu Tanzania (CHAKAMWATA);

(b) Kukagua vyama nane katika ngazi ya Taifa katika kuhakikisha vyama hivyo vinatimiza masharti ya usajili kulingana na matakwa ya Sheria; na

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(c) Wafanyakazi 102 na Wajumbe 30 kutoka Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) walipatiwa elimu juu ya uhuru wa kujumuika na kujiunga na Vyama vya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2014/2015 tumetekeleza yafuatayo katika kujenga uwezo wa Wizara:-

(a) Kuajiri watumishi 21 kupitia Tume ya Ajira Serikalini;

(b) Watumishi 40 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi na watumishi wanne wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi; na

(c) Watumishi 100 wamepatiwa mafunzo ya Maadili katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kusimamia shughuli za taasisi saba za Umma zilizo chini yake. Taasisi hizo ni Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA), Shirika la Tija la Taifa (NIP), Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA), Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) na Mfuko wa Fidua ya Wafanyakazi.

Kazi zilizotekelezwa katika mwaka 2014/2015 kupitia Taasisi hizo ni kama ifuatavyo na nyingine zinapatikana katika kitabu chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi kwanza wamefanya kaguzi 4,862 za kawaida na kaguzi maalum 18,236 sawa na asilimia 151.9 ya ukaguzi 12,000 uliokuwa umepangwa; na Wafanyakazi 45,721 walipimwa afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara kupitia Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA) imetekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kusajili watafuta kazi 1,249 na kuunganisha watafuta kazi 503 kwa waajiri wenye fursa za ajira ndani ya nchi;

(b) Kusimamia na kuratibu ajira za Watanzania 1,116 nje ya nchi ikiwemo Oman 918, Dubai 164, India 21, Ujerumani sita, Japani watano na Qatar wawili; na

(c) Kutoa ushauri kwa watafuta kazi 1,157 juu ya uchaguzi wa fani, mafunzo na kazi stahiki kulingana na sifa zao na mahitaji ya soko la ajira.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Shirika la Tija la Taifa (*NIP*) katika mwaka 2014/2015, mafunzo 48 ya kuinua tija mahali pa kazi na mafunzo ya kujenga uwezo sawa na asilimia 60 ya lengo lililopangwa, yalitolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015, Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Hifadhi ya Jamii (*SSRA*) imetekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kufanya kaguzi 16 za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa Sheria zilizounda Mifuko hiyo;

(b) Kutoa elimu kwa watu 1,700,000 kuhusu Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa makundi mbalimbali ya kijamii; na

(c) Kufanya tafiti mbili zenye lengo la kupanua wigo wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016 Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi utatekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kuajiri watumishi katika ngazi ya Menejimenti na Wataalam;

(b) Kuandaa mifumo ya upatikanaji wa taarifa na ulipaji wa fidia wafanyakazi watakaoumia, kuugua au kufariki kutokana na mazingira ya kazi;

(c) Kufanya utafiti wa kubaini viwango sahihi kwa kila sekta kulingana na mazingira ya kazi (*Risk Assessment*); na

(d) Kutoa elimu kwa Umma kuhusu Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi na wajibu wa Waajiri kuchangia mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) limetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Limekusanya mapato ya kiasi cha Shilingi milioni 629,404.4 sawa na asilimia 60.3 ya lengo;

(ii) Shirika limeandikisha wanachama wapya 113,517 ambao ni asilimia 24.5 ya lengo lililokusudiwa ambapo wanachama 37,144 ni kutoka katika sekta isiyo rasmi;

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(iii) Mafao mbalimbali ya jumla ya Shilingi milioni 239,658.4 yalilipwa ambayo ni sawa na asilimia 145.2 ya lengo la kulipa Shilingi milioni 164,999.7. Jumla ya wanachama waliolipwa mafao ni 65,932;

(iv) Shirika limeendelea na utaratibu wa kutoa mikopo katika sekta isiyo rasmi (*Informal Sector*), na kwa wanachama wake katika vikundi vya SACCOS na VICOBA ambapo Shilingi bilioni 51.80 zimetolewa kwa Wanachama 6,506 katika maeneo mbalimbali nchini;

(v) Shirika limeendelea na ujenzi wa daraja la Kigamboni ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba na Mheshimiwa Rais kufanya ufunguzi mdogo wa awali wa daraja hilo.

(vi) Shirika limekamaliza miradi ya ujenzi wa ofisi na vitega uchumi katika Mikoa ya Morogoro, Kilimanjaro na Wilaya ya Ilala; na

(vii) Shirika limeendelea na uthaminishaji wa mradi wa uzalishaji umeme wa megawati 300 na sasa TANESCO wametupatia Megawati 100 katika eneo la Mkuranga. Taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi (*Cosultantants*) wa mradi huu zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaenda Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA). Katika mwaka 2014/2015, kazi zilizotekelezwa na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ambayo ni Taasisi ya Serikali iliyo chini ya Wizara yangu yenye jukumu la kusuluhisha migogoro ya kikazi na kuamua migogoro ya kikazi ni zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (Fungu15) ilikasimia Sh.1,824,223,550/= kwa ajili ya mishahara (PE) na Sh. 2,707,500,000/= kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2015, Sh. 982,966,133.84 sawa na asilimia 54 ya fedha za mishahara ya Watumishi (PE) na Sh. 668,047,148.16 sawa na asilimia 25 ya fedha za Matumizi mengine (OC) zilitolewa na kutumika na Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30/04/2015 Tume ilipokea Migogoro 11,435 na kusajiliwa. Kati ya migogoro hiyo iliyosajiliwa; migogoro 4,141 ilishughulikiwa na kumalizika, migogoro 2,657 ilisuluhishwa na migogoro 1,484 ilitolewa uamuzi. Migogoro 7,294 inaendelea kushughulikiwa katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi 35 zilipewa mafunzo kuhusu dhana ya ushirikishwaji wa wafanyakazi na matumizi sahihi ya Sheria za Kazi;

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016 Wizara ya Kazi na Ajira kwa kushirikiana na Taasisi kwa kushirikiana Taasisi zilizopo chini yake, itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kusimamia Sheria na Viwango vya kazi,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ushirikishwaji wa Wafanyakazi na kusuluhisha migogoro sehemu za kazi; kusimamia usalama na afya mahali pa kazi, kukuza na kutoa huduma za ajira; kuboresha ufanisi na tija kazini na kuboresha Sekta ya Hifadhi ya Jamii.

Kazi zitakazotekelezwa na Wizara na Taasisi zake zimeainishwa kwa kina katika Kitabu cha Hotuba kuanzia ukurasa wa 50 hadi ukurasa 70. Kwa muhtasari kazi zitakazotekelezwa ni zifuatazo:-

Kwanza, ni usimamizi wa kazi na huduma za ukaguzi.

(a) Wizara itafanya kaguzi 4,800 katika maeneo mbalimbali ya kazi nchini ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua waajiri watakaokiuka Sheria;

(b) Wizara itaboresha itaboresha upangaji wa kima cha chini cha mshahara katika sekta binafsi kwa kutumia Bodi moja ya Kitaifa ya Kima cha chini cha mshahara;

(c) Wizara itaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa kupambana na utumikishwaji wa watoto kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na wabia wa maendeleo;

(d) Wizara itahamasisha majadiliano ya pamoja kati ya waajiri na wafanyakazi pamoja na vyama vyao kwa lengo la kuboresha maslahi ya wafanyakazi na hatimaye kuongeza tija na uzalishaji na kuongeza ajira;

(e) Kuimarisha utekelezaji wa Kanuni ya Utatu ya masuala ya UKIMWI katika sehemu za kazi kwa lengo la kupambana na maambukizi na athari zake; na

(f) Kujenga uwezo wa Maafisa Kazi kuhusu mbinu za kisasa za kaguzi na usimamizi wa kazi ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa mashtaka Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016 Wizara itaendelea kuimarisha masuala ya hifadhi ya Jamii ambapo itaanzisha Idara mpya ya Hifadhi ya Jamii itakayokuwa na jukumu la kuratibu masuala yote ya huduma za hifadhi ya jamii kwa lengo la kuendelea kuziboresha. Kazi zitakazotekelezwa katika eneo hili ni zifuatazo:-

(a) Kuendelea na Mkakati wa Taifa wa kupanua wigo wa Hifadhi ya Jamii nchini;

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(b) Kuandaa kanuni za Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi Na. 20 ya mwaka 2008;

(c) Kuwezesha utendaji wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi; na

(d) Kuandaa Kanuni za Baraza la Rufaa la Hifadhi ya Jamii na kuwezesha utekelezaji wa majumuku ya Baraza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la ukuzaji wa Ajira nchini, Wizara yangu itaendelea kuratibu shughuli za kukuza ajira nchini kupitia Programu ya Kukuza Ajira kwa Vijana, Programu ya Kukuza Ujuzi uwekezaji katika Sekta ya Umma na Binafsi. Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kuratibu ukuzaji ajira kwenye Miradi na Programu za maendeleo za Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Jiji na Wizara mbalimbali;

(b) Kuendelea na utekelezaji wa Programu ya Kukuza Ajira kwa Vijana ambayo imelenga kuwajengea vijana uwezo wa stadi mbalimbali za ujasiriamali; kuwapatia vijana mitaji yenye masharti nafuu na nyenzo za uzalishaji; na Kutenga maeneo maalum ya uzalishaji na kufanyia biashara Bado dakika 5?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016 Wizara itaendelea na jukumu la kusajili na kusimamia Vyama vya Waajiri na Wafanyakazi nchini kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kushughulikia maombi ya usajili wa Vyama vya Wafanyakazi;

(b) Kuwaelimisha Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi; na

(c) Kushughulikia kesi Mahakamani zinazotokana na masuala yanayohusu mambo ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ya Kazi na Ajira itaendelea kusimamia Taasisi za Umma zilizo chini yake katika kutekeleza majukumu yao kama yalivyoainishwa katika kitabu chetu cha hotuba ikiwemo Wakala wa Usalama na Afya mahali pa kazi, wataendelea kufanya kaguzi; watafanya kaguzi 20,000; watapima afya za wafanyakazi 65,000; watasajili sehemu za kazi 3,000; na watatoa mafunzo mbalimbali kuhusu usalama wa Afya mahali pa kazi kwa wafanyakazi na waajiri 3,000; na wataanzisha mifumo mbalimbali ya utendaji kazi ikiwa ni pamoja na kuanzisha mifumo ya usambazaji wa taarifa ya Hifadhi ya Jamii.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, TaESA wataendelea kushiriki katika zoezi la kutoa mafunzo ya ujuzi *Internship* kwa watafutakazi 4,200; kusajili watafutakazi 3,000 na kutoa mafunzo elekezi .

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Tija la Taifa (*NIP*) wataendelea na mafunzo 80 ya uongozi yatakayohudhuriwa na watumishi 1,200; watatoa huduma za ushauri kwa wateja 30 na watafanya tafiti. SRA wataendelea kukamilisha tathmini ya mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii kwa kushirikiana na *ILO*, watatoa elimu kwa Hifadhi ya Jamii kwa Wanachama 2,000,000 na watafanya kaguzi 29,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, (*NSSF*) wataendelea kukusanya Sh. 2,561,032 na wataendelea kuelimisha kuhusu shughuli zao na wataendelea na ujenzi wa vitega uchumi na kukamilisha miradi wanayoendelea nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi wataendelea kusuluhisha na kuamua migogoro. Mwaka huu wamepanga kuamua migogoro 15,000 ya kikazi, wataendelea kujenga uwezo wa Tume kwa kuendeleza Watumishi Maalumu na kuendeleza mafunzo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana katika mwaka huu...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, omba pesa.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 38,883,129,000/= kwa Wizara ya Kazi na Ajira (Fungu 65) na jumla ya Sh. 8,097,054,000/= kwa Tume ya Ushuluhishi na Uamuzi (Fungu 15) kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ili kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii katika mchanganuo ufuatao:-

(a) Fungu 65: Wizara ya Kazi na Ajira

(i) Sh. 4,154,089,000/= zitatumika kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi wa Wizara;

(ii) Sh. 14,725,040,000/= zitatumika kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (OC);

(iii) Sh. 20,000,000,000/= zitatumika katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

(b) Fungu 15: Tume ya Usuluhishi na Uamuzi

(i) Sh.1,910,043,000/= zitatumika kulipa mishahara ya watumishi wa Tume; na

(ii) Sh. 2,187,011,000/= zitatumika kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (OC).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nitoe shukrani zangu kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa anwani: [www. Kazi.go.tz](http://www.Kazi.go.tz).

Baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante hoja imeungwa mkono.

**Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 -
Wizara ya Kazi na Ajira**

**HOTUBA YA WAZIRI WA KAZI NA AJIRA MHESHIMIWA GAUDENTIA M. KABAKA
(MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA
FEDHA KWA MWAKA 2015/2016 KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii iliyochambua bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira (Fungu 65) na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (Fungu 15), naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio na Mapato ya Wizara ya Kazi na Ajira na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hai na kuniwezesha kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu leo. Vile vile sina budi kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mkubwa walionipa ndani na nje ya Bunge katika kipindi chote cha Bunge hili la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, nikishukuru Chama changu cha CCM,

kwa imani kubwa kwangu katika kutekeleza Ilani ya Uchanguzi ya CCM ya mwaka 2010 nikiwa Mbunge na Waziri wa Kazi na Ajira.

3. Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiki ni kikao cha mwisho cha Bunge hili la Kumi kabla halijavunjwa, niruhusu nichukue nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwanza kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania **Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete** kwa kuniteua kuwa mmoja wa washauri wake wakuu katika masuala yahasuyo Kazi na Ajira. Katika kipindi hiki cha miaka mitano nimejifunza mengi sana kutoka kwake na mimi nategemea kuwa nimetoa mchango uliotegemewa katika kumsaidia yeye kutimiza majukumu yake kama kiongozi mkuu wa nchi yetu, na pia katika kutimiza malengo tuliyojiwekea katika Ilani yetu ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Pia, napenda nimshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Dkt. Gharib Bilal** ambaye katika kipindi hiki cha miaka mitano, amekuwa mfano mkubwa kwangu wa uelewa, umahiri na uvumilivu katika uongozi. Aidha, nachukua nafasi hii kumshukuru Waziri Mkuu **Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda** kwa uongozi wake na maelekezo yake mahiri katika utendaji wangu wa kazi wa siku hadi siku.

4. Mheshimiwa Spika, vile vile nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na maafisa wa Serikali wote ambao katika kipindi hiki wamenipa ushauri na ushirikiano mkubwa ulioniwezesha nitekeleze majukumu yangu kwa umakini kama Waziri wa Kazi na Ajira. Wote nawashukuru sana na nawaombea Mungu awabariki. Lakini kwa namna ya pekee kabisa napenda niwashukuru Mheshimiwa **Dkt Milton Makongoro**, Naibu Waziri wa Kazi na Ajira, Katibu Mkuu wa Wizara yangu, **Ndugu Eric Shitindi**; Wakurugenzi na Watumishi wote wa Wizara; Watendaji Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ambao nimefanya nao kazi kwa karibu sana na leo hii tumeifikisha Sekta ya Kazi na Ajira hapa tulipofika. Mwisho kabisa napenda niwashukuru sana Wasaidizi wangu katika Ofisi yangu kwa huduma, umakini na uvumilivu wao mkubwa. Wote hawa nawaombea Baraka za Mungu waendeleo kuwa na afya tele.

5. Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuungana na Wabunge wenzangu kuwapongeza Viongozi wetu wa Chama na Serikali kwa kazi nzuri waliyoifanya tangu wateuliwe kushika nyadhifa mbalimbali. Ni matumaini yangu kwamba wananchi wana imani na Chama cha Mapinduzi, pamoja na Wabunge wake. Hivyo, nina amini kwamba wataendelea kuwapigia kura ili waendeleo kuwawakilisha katika Awamu ijayo ya uongozi.

6. Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza na kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti **Mheshimiwa Said Mtanda**, **Mbunge wa Jimbo la Mchinga**, na Makamu Mwenyekiti **Mheshimiwa Albert Obama**, **Mbunge wa Jimbo la Manjovu** kwa

ushauri, maoni na ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wote wa uhai wa Kamati hii na hususan wakati wa maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2015/2016. Naishukuru sana Kamati kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina Taarifa ya Utekelezaji ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2014/2015 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2015/2016 katika kikao chake kilichofanyika Dar es salaam tarehe 6 na 7 Mei, 2015. Kadhalika, ninaishukuru Kamati hii kwa kutembelea Taasisi na Miradi mbalimbali inayotekelezwa na Taasisi hizo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa daraja la Kigamboni na ujenzi wa nyumba za kisasa zinazojengwa na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF). Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hiyo yamezingatiwa katika bajeti hii.

7. Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa napenda kujiunga na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole za dhafi kwa familia, ndugu na jamaa wa Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliofariki katika kipindi hiki cha Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwarehemu. Aidha, kwa namna ya pekee nichukue fursa hii kuungana na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii ambayo inasimamia Wizara yangu kwa kifo cha ghafla cha aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Marehemu Kapteni John Damiano Komba aliyekuwa Mbunge wa Mbinga Magharibi. Kifo hicho kimekuwa ni pigo kwa Kamati kwa kuwa Marehemu alikuwa nguzo imara katika Kamati hiyo. Nichukue fursa hii kuwapa pole familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu. Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ailaze Roho ya Marehemu Mahali Pema Peponi, **AMINA!**

8. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kutekeleza shughuli zake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Malengo ya Milenia (MDGs), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Awamu ya Pili, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano, Mikataba mbali mbali ya Kimataifa inayohusu masuala ya kazi na ajira na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Lengo la msingi la miongozo hiyo ni kuboresha maisha ya Wananchi; kudumisha amani; utulivu na umoja; kuimarisha utawala bora; kujenga uchumi madhubuti na endelevu; kuboresha afya na kutunza mazingira. Wizara yangu imetekeleza miongozo hiyo kwa kuimarisha viwango vya kazi, kuhakikisha kuna mazingira yanayokidhi afya na usalama wa wafanyakazi mahali pa kazi, kuboresha maslahi ya wafanyakazi, kuimarisha ushirikishwaji wa wafanyakazi na kukuza ajira nchini. Mafanikio yaliyopatikana yamewezesha kuendelea kuwa na utulivu katika sekta ya kazi, hali ambayo imesaidia kukua kwa uchumi na kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje hivyo kukuza ajira kwa makundi mbali mbali ya wananchi katika nchi yetu na kuwapunguzia umasikini wa kipato.

9. **Mheshimiwa Spika**, kabla sijaanza kutoa taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa kazi za Wizara yangu kwa mwaka 2014/2015 na malengo ya mwaka 2015/2016, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa **Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb.)** na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, Mheshimiwa **Dkt. Mary Nagu** Mbunge wa Jimbo la Hanang kwa hotuba zao nzuri ambazo zimefafanua kwa kina utekelezaji wa Sera, Mipango na Mikakati ya Serikali na kutoa mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Malengo, maelezo na vigezo vilivyomo kwenye hotuba hizo vimezingatiwa kikamilifu katika kuandaa bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2015/2016.

10. **Mheshimiwa Spika**, hotuba yangu imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza ni Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010, sehemu ya pili ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2014/2015 na sehemu ya tatu ni Malengo ya Wizara kwa mwaka 2015/2016 na maombi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Malengo hayo.

B. UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2010 KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO (2010 – 2015)

11. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imetekeleza ipasavyo Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, hususan **Ibara ya 78** vifungu (b na c), **Ibara ya 79** vifungu (a-b) na **Ibara ya 81** vifungu (i-j) kuhusu Ajira, **Ibara ya 80** vifungu (a-c) kuhusu Kazi na **Ibara 82** vifungu (a-e) kuhusu Hifadhi ya Jamii kama ifuatavyo:

Ibara ya 78, kifungu (b);

Kufanya utafiti wa kina wenye lengo la kuandaa mpango wa muda mrefu utakaowashirikisha vijana katika shughuli mbalimbali za kiuchumi ili kuwajengea uwezo wa kujitegemea.

12. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Taifa ya Takwimu imefanya uchambuzi wa hali halisi ya soko la ajira kupitia Utafiti wa Nguvu Kazi (*Integrated Labour Force Survey*). Pia, Wizara imefanya mashauriano na wadau wa sekta ya ajira ikiwemo Wakuu wa Mikoa, Sekta Binafsi, Waajiri, Vyama vya Wafanyakazi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs) kubaini changamoto za ukosefu wa ajira kwa vijana na namna ya kukabiliana nazo. Mashauriano haya yamebaini kuwa changamoto kubwa kwa sasa zinazowakabili vijana katika kujijajiri ni pamoja na ukosefu wa ujuzi, ukosefu wa miundombinu ya kuwezesha kujijajiri, ukosefu wa mitaji pamoja na mtazamo hasi kuhusu kujijajiri miongoni mwa vijana. Uchambuzi huu umewezesha Wizara kuandaa Programu ya Kukuza Ujuzi pamoja na Programu ya Kukuza Ajira kwa Vijana. Programu hizo zinalenga kuwajengea uwezo Vijana

wa kuajiriwa na kujajiri katika sekta mbalimbali za kiuchumi. Utekelezaji wa Programu hizo zitaendelea kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2015/16 na zinahusisha wadau mbalimbali.

Ibara ya 78, kifungu (c);

Kuimarisha Shirika la Tija la Taifa ili kuongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wa shughuli za uendeshaji wa uchumi nchini.

13. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuimarisha Shirika la Tija la taifa Wizara imefanya uteuzi wa Bodi ya Wakurugenzi na kuongeza idadi ya watumishi ikiwa ni pamoja na kujaza nafasi zilizokaimiwa kwa muda mrefu. Uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi umezingatia uzoefu na ujuzi wao katika masuala ya kiuchumi. Aidha, katika kipindi cha miaka 5 kuanzia mwaka 2011 hadi 2015, Shirika limetoa mafunzo 346 ya kuboresha tija kwa taasisi mbali mbali sawa na asilimia 87 ya lengo.

Ibara ya 79, kifungu (a);

Serikali kuibua Mpango Kabambe wa kuwawezesha kiuchumi vijana wasomi walio tayari kujituma kwa kujajiri ili watumie nguvu na maarifa waliyonayo katika kilimo, ufugaji na uvuvi wa kisasa.

14. Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa Programu ya kukuza ajira kwa vijana ya miaka mitatu itakayowawezesha kutoa fursa za ajira kwa vijana 840,000. Programu hii imelenga kuwajengea vijana uwezo na ujuzi wa stadi mbalimbali za kazi na ujasiriamali; kuwawezesha kupata mitaji, nyenzo na vifaa vya uzalishaji mali; na kuwapatia vijana maeneo ya uzalishaji na biashara. Pia, Wizara imeendelea kuhamasisha wadau mbalimbali kushiriki katika kukuza ajira kwa vijana. Miongoni mwa wadau wanaoshiriki katika ukuzaji ajira ni pamoja na Umoja wa Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUGECO), Shirika la TechnoServe kupitia Mradi wa kuwawezesha vijana kujajiri katika kilimo mkoani Mbeya; Baraza la Taifa Uwezeshaji kupitia “**Programu ya Kijana Jijiri**”; Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa kushirikiana na wadau wa Utalii na Chuo cha Taifa cha Utalii kupitia Programu ya Kukuza Ujuzi katika sekta ya hoteli pia kwa kushirikiana na VETA kwa kutekeleza programu ya kutambua ujuzi uliopatikana kupitia mfumo wa elimu usio rasmi. Miradi iliyotekelezwa imelenga kutoa mafunzo ya ujasiriamali na namna ya kuanzisha na kuendeleza biashara ikiwemo mradi wa Kazi Nje Nje ambapo mafunzo ya ujasiriamali yalitolewa kwa vijana 35,325; miongoni mwao vijana **11,825** ni wahitimu wa elimu ya juu. Katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015 jumla ya ajira **1,929,938** zilizalishwa nchini tofauti na lengo la kuzalisha ajira milioni moja katika kipindi hicho cha miaka mitano. Idadi hii inajumuisha ajira Kilimo ajira **417,531**; Elimu ajira **144,764**; Afya ajira **29,444**; Ujenzi wa Miundombinu ajira **200,484**; Nishati ajira **1,479**; Miradi ya Kijamii ajira

102,948; Sekta nyingine Serikalini ajira **15,240**. Jumla ya ajira zilizozaliwa katika Sekta binafsi ni **1,018,048** kwa mchanganuo ufuatao: Mawasiliano ajira **184,030**; Viwanda vidogo na vya kati (SMEs) ajira **26,098** na Miradi ya uwekezaji kupitia kituo cha TIC ni **325,622**; uwekezaji katika vituo vya EPZ **67,646** na sekta nyingine za uwekezaji ni **414,652 (Jedwali Na 1)**.

Ibara ya 80, kifungu (a);

Kuendelea kuboresha mishahara ya wafanyakazi kwa kadri hali ya uchumi wa nchi utakavyoruhusu.

15. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mishahara, Serikali iliunda Bodi za kima cha chini cha mishahara katika sekta binafsi kutoka Bodi 8 zilizokuwepo mwaka 2010 hadi Bodi 12 mwaka 2011. Kutokana na mapendekezo ya Bodi hizo, tangu mwaka 2010 hadi sasa kima cha chini cha mishahara katika Sekta Binafsi kimeongezwa mara mbili, mwaka 2010 na 2013. Nyongeza hizo zimezingatia vigezo vya kiuchumi na tija katika kila sekta. Aidha nyongeza ya mwaka 2013 ilikuwa kati ya asilimia 21 hadi 65 ya viwango vya mishahara vya mwaka 2010.

Ibara ya 80, kifungu (b);

Kuimarisha na kufanya kaguzi za kazi, ikiwa ni pamoja na masuala ya Afya na Usalama Mahala pa Kazi

16. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015 jumla ya kaguzi **220,350** zimefanyika ikiwa ni wastani wa kaguzi **40,000** kwa mwaka. Lengo la kaguzi hizo ni kuhakikisha waajiri wanafuata Sheria za Kazi ipasavyo. Jumla ya kaguzi za kawaida **26,412** na kaguzi maalum **53,807** kuhusiana na afya na usalama mahala pa kazi zimefanyika. Wafanyakazi **136,076** walipimwa afya zao ili kubaini matatizo na athari za kiafya zitokanazo na maeneo wanayofanyia kazi. Pia, Serikali imeendelea kuimarisha Ofisi za Kazi za Mikoa kwa kuziongezea bajeti na idadi ya watumishi kwa lengo la kuziwezesha kusimamia kikamilifu Sheria na viwango vya kazi katika maeneo yao. Katika mwaka 2014/2015 Wizara imeajiri watumishi **24** ili kuimarisha ukaguzi wa viwango vya kazi nchini.

Ibara ya 80, kifungu (c);

Kusuluhisha na kuamua kwa wakati migogoro yote ya kikazi na kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa wafanyakazi mahali pa kazi

17. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2010 hadi mwezi Aprili, 2015 jumla ya migogoro **10,281** imesuluhishwa na jumla ya migogoro **6,057** imeamuliwa na Tume ya Ushishi na Uamuzi (CMA). Katika kipindi hicho muda wa kusikiliza na

kusuluhisha umepungua kutoka siku **30** hadi siku **12** na muda wa kusikiliza na kuamua umepungua kutoka siku **90** hadi siku **85**. Pia, elimu kwa umma kuhusu Sheria za Kazi ilitolewa kwa wafanyakazi wapatao **1,908,000** na waajiri **6,890**. Hadi sasa jumla ya Mabaraza ya Wafanyakazi **265** yameundwa katika Taasisi za Umma ikiwa ni sawa na asilimia **86.6** ya lengo;

Wizara imeendelea kuhimiza na kufuatilia haki mbalimbali za wafanyakazi na waajiri, ikiwemo haki ya kuanzisha, kujiunga na kushiriki katika shughuli mbalimbali halali za vyama vya wafanyakazi na waajiri. Katika kipindi cha 2010 hadi 2015, jumla ya vyama **7** vya wafanyakazi vilisajiliwa na shirikisho moja la vyama vya wafanyakazi liliundwa na kusajiliwa. Lengo ni kuongeza na kuboresha wigo wa ushiriki wa wafanyakazi, majadiliano na utetezi wa haki za wafanyakazi na waajiri katika sehemu za kazi. Jumla ya vyama vya wafanyakazi vilivyosajiliwa nchini hadi sasa ni **31**, ikilinganishwa na vyama **24** vilivyokuwepo mwaka 2009. Hadi sasa tuna vyama **viwili** vya waajiri (ATE na TAACIME), Mashirikisho mawili ya vyama vya wafanyakazi (TUCTA na FEATU) na Shirikisho moja la vyama vya Waajiri wa Afrika Mashariki (EAEO) na Shirikisho la Mashirikisho ya Vyama vya Wafanyakazi wa Afrika Mashariki –EATUC. **(Rejea Kiambatisho Na. 2)**

Ibara ya 81, kifungu (i);

Serikali kuandaa mafunzo maalum kwa vijana ya kupenda kufanya kazi na kuwa waadilifu ili waweze kuajirika

18. Mheshimiwa Spika, Serikali imehuisha elimu ya kujitegemea katika mfumo wa elimu na mafunzo, pamoja na kurejesha mfumo wa vijana kupitia katika mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Aidha, Serikali imepitisha Sera ya Taifa ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 ambayo inazingatia utengenezaji wa mitaala inayozingatia mahitaji ya soko la ajira. Pia, kupitia Programu ya kukuza Ajira kwa Vijana ambayo ilianzishwa mwaka 2013; mafunzo maalum ya kubadili fikra kwa vijana (change of mind set) ni sehemu mojawapo ya mtaala wa mafunzo. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani na Wadau wengine tangu mwezi Julai 2014, zimeandaa Programu ya Mafunzo kwa vitendo kazini (*Apprenticeship*) kwa wahitimu wa vyuo ambao hawajaajiriwa ili kuwawezesha kupata stadi na sifa za kuajiriwa na kupenda kufanya kazi. Programu imeanza na imefanyiwa majaribio katika sekta ya utalii.

Ibara ya 81, kifungu (j);

Serikali kusimamia kikamilifu Sheria ya Ajira ya Wageni

19. Mheshimiwa Spika, Serikali imepitisha Sheria ya Ajira kwa wageni ya mwaka 2014 katika Bunge la 19 mwezi Machi, 2015. Sheria hiyo imeweka

mamlaka moja ambayo ni Wizara ya Kazi na Ajira kuwa msimamizi wa utoaji wa vibali vya ajira kwa wageni.

Ibara ya 82, kifungu (a);

Kufanya tathmini ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na kurekebisha viwango vya mafao vinayotoa ili visipishane mno.

20. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2010 tathmini ya mifuko ya hifadhi ya jamii ilifanyika ambapo matokea ya tathmin hiyo yalionesha kwamba hali ya mifuko ni nzuri isipokuwa Mfuko wa PSPF ambao hali yake ya kifedha si ya kuridhisha kutokana na deni la Serikali linalotokana na malipo ya pensheni kwa wastaafu ambao hawakuchangia kabla ya Julai 1999 (Pre 99). Kutokana na matokeo ya tathmin hiyo, Serikali imeanza kulipa deni la PSPF kwa awamu.

Aidha, kuanzia Julai 2014, Serikali imerekebisha kanuni za kukokotoa mafao ya pensheni, hatua ambayo imesaidia kuondoa tofauti ya malipo ya mafao ya pensheni kwa wanachama katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Mabadiliko haya ambayo yameambatana na vikokotoo vipya, yameboresha mafao ya kila mwezi ya pensheni kutoka 67% kwenda 72.5%. vile vile kanuni hizi zinathaminisha pensheni (indexation) na hivyo kuboresha pensheni kwa kiwango kikubwa.

Ibara ya 82, kifungu (b);

Kuanzisha na kuimarisha Mamlaka ya Udhhibiti na Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA)

21. Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Hifadhi ya Jamii (SSRA) nchini mwaka 2010, kwa lengo la kuboresha sekta ya hifadhi ya jamii. Aidha, Serikali ilirekebisha Sheria ya Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii kupitia Sheria Na. 5 ya mwaka 2012 ili kuipa SSRA mamlaka ya kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii. Sheria hiyo pamoja na mambo mengine imeimarisha Mamlaka na kuboresha utendaji wa Mifuko. Hadi kufikia Juni, Machi, 2015 SSRA imetoa jumla ya miongozo 11 ya kuongoza na kuimarisha Sekta. Miongozo na kanuni hizo ni:-

i) Mwongozo wa Uendeshaji wa Bodi za Wadhamini wa Mifuko (2012)

ii) Mwongozo wa Utunzaji wa Kumbukumbu na Takwimu (Data Management Guidelines) 2012

Nakala ya Mtandao (Online Document)

- iii) Mwongozo wa Utangamano wa Mifumo ya TEHAMA (2014)
- iv) Mwongozo wa Usalama wa TEHAMA (Security Electronic Information) of
- v) Mwongozo wa Majumuisho ya Vipindi Vya Uchangiaji (2013/2014)
- vi) Miongozo ya Tathmini (Actuarial guidelines)
- vii) Miongozo ya uwekezaji (Investment guidelines) ya 2012
- viii) Mwongozo wa Uandikishaji wanachama wa 2013
- ix) Mwongozo wa Uendeshaji wa Mikutano ya kila mwaka ya wanachama (2014)
- x) Mwongozo wa Uwasilishwaji wa Taarifa za Mwaka (2014)
- xi) Kanuni ya Kuhuisha Mafao ya pensheni (2014)

Ibara ya 82, kifungu (c);

Kuchukua hatua za makusudi za kupanua wigo wa kinga ya jamii ili Watanzania walio wengi waweze kufaidika na huduma ya hifadhi ya jamii

22. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia kifungu cha 30 cha Sheria Na. 8 ya mwaka 2008, kwa kuruhusu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuandikisha wanachama kutoka sekta yoyote kwa kuzingatia Sheria na Mwongozo wa Uandikishaji Wanachama wa mwaka 2013. Aidha, Sheria hiyo pia imetoa fursa kwa mifuko ya hifadhi ya jamii kusajili wanachama kutoka katika sekta isiyo rasmi, ambapo hadi sasa wanachama wapatao 40,000 wamejiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Pia, Serikali katika jitihada za kupanua wigo wa huduma ya hifadhi ya jamii kupitia Sheria Na. 8 ya mwaka 2013, imebadili GEPF kutoka Mfuko wa Akiba wa Wafanyakazi na kuwa Mfuko wa Pensheni ili kuwezesha mwananchi yoyote kujiunga na kufaidi mafao ya kila mwenzi ya uzeeni. Aidha, wanachama katika sekta ya Hifadhi ya Jamii wameongezeka mara mbili kutoka **900,000** mwaka 2010 hadi kufikia zaidi ya **2,000,000** mwaka 2015; Rasilimali za Mifuko ya hifadhi ya Jamii zimeongezeka kutoka **trillion 1.3** mwaka 2005 hadi kufikia **trilioni 8** mwaka 2015; Mafao ya wanachama walionufaika imekua kutoka shilingi **bilioni 131** mwaka 2005 hadi kufikia **shilingi trilioni 1.3** mwaka 2015; Wastaafu (pensioners) wameongezeka

toka 24,000 mwaka 2005 kufikia takribani 100,000 mwaka 2015. Kwa ujumla idadi ya watu wanaonufaika na huduma za hifadhi ya jamii imefikia watu **milioni 6.5** mwaka 2015 kutoka watu **690,000** mwaka 2005. Vile vile, mwaka 2014/2015 Serikali imeanzisha Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ili kutoa fidia kwa wafanyakazi wanaouguua au kuumia kazini. Mfuko huu utanza kutekeleza wajibu wake katika mwaka 2015/2016.

Ibara ya 82, kifungu (d);

Kuelimisha jamii ya wafanyakazi na waajiri juu ya umuhimu wa hifadhi ya jamii kwa maendeleo ya wafanyakazi na ya nchi kwa ujumla.

23. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia SSRA na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imeendelea kutoa elimu ya Hifadhi ya Jamii kupitia vyombo mbalimbali vikiwemo semina, warsha, radio, magazeti, mitandao ya kijamii, digitali, tovuti ya Mamlaka, machapisho, vipeperushi na runinga. Watu waliofikiwa ni zaidi ya **5,450,000**. Aidha, Mifuko yote imekuwa ikifanya mikutano ya mwaka ya wanachama, ambapo wanachama husika wamekuwa wakipatiwa taarifa mbalimbali zinazohusu uendeshwaji wa Mifuko. SSRA pia imetoa elimu kwa makundi maalum, wakiwemo vyama vya wafanyakazi, waajiri, waheshimiwa wabunge, wajasiriamali, wanafunzi wa vyuo, mabaraza ya wafanyakazi wa taasisi mbalimbali, waandishi na wahariri, wafanyakazi wa sekta ya umma na binafsi

Ibara ya 82, kifungu (e);

Kuendelea kutumia uwezo wa kifedha uliopo katika kila shirika la hifadhi ya jamii, kwa kuwekeza katika miradi mbalimbali ya nchi.

24. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015 Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imeendelea kubuni huduma na mafao mbalimbali kwa wanachama wake kwa lengo la kuongeza wigo wa hifadhi ya jamii, kuongeza ajira na kudumisha utulivu wa kisiasa nchini. Mifuko hiyo iliendelea kuwekeza rasilimali katika maeneo yanayolenga kujenga uchumi wa kisasa ikiwa ni pamoja na elimu, afya, makazi, michezo, miundombinu, mapinduzi ya viwanda na kilimo. Mwongozo wa Kusimamia Uwekezaji wa mwaka 2012 umeweka vipaumbele kwenye uwekezaji wa miradi mnyambuka (multiplier effect) kwa kuzingatia hadhari na kipato (risk and return). Aidha uwekezaji umeongezeka kutoka **shilingi trilioni 1.6** mwaka 2006 hadi kufikia **shilingi trilioni 7** mwaka 2015. Hili ni ongezeko la asilimia 250. Vile vile, mikopo ipatayo **shilingi bilioni 130** imetolewa kwa wanachama wa vikundi mbalimbali.

C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KAZI KWA MWAKA 2014/2015

25. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina jukumu la kuandaa, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali kuhusu viwango vya kazi, usawa na ajira ya staha, ukuzaji wa ajira, ushirikishwaji ukuzaji wa tija mahali pa kazi na hifadhi ya jamii nchini. Katika mwaka 2014/2015 tumefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

WIZARA YA KAZI NA AJIRA

26. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/15 Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imetekeleza majukumu yake ya kusimamia viwango vya kazi, ukuzaji wa ajira, ushirikishwaji wa wafanyakazi mahali pa kazi, uboreshaji wa hifadhi ya jamii na kushughulikia migogoro ya kazi na usalama na afya mahali pa kazi.

27. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 jumla ya **shilingi 9,606,000** zilikadiriwa kukusanywa ikiwa ni mapato ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali vya Wizara. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2015 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha **shilingi 3,120,000** sawa na **asilimia 33** ya makadirio.

28. Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara (**Fungu 65**), ilikasimiwa jumla ya **Shilingi 17,654,394,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 5,815,289,000** sawa na **asilimia 33** zilitengwa kwa ajili ya kulipa mshahara wa Watumishi (PE), **Shilingi 8,914,105,000** sawa na **asilimia 50** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengine (OC) na **Shilingi 2,925,000,000** fedha za Maendeleo sawa na **asilimia 17**.

29. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2015, **Shilingi 4,744,071,997** sawa na **asilimia 82** ya fedha za Mishahara ya Watumishi (PE) na **shilingi 2,692,134,371** sawa na **asilimia 30** ya fedha za Matumizi mengine (OC) zilitolewa na kutumika na Wizara. Hakuna fedha za Bajeti ya Miradi ya Maendeleo zimetolewa mpaka sasa.

Usimamizi wa Kazi na Huduma za Ukaguzi

30. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi ambazo ni Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya mwaka 2004. Utekelezaji umefanyika kwa kukagua sehemu za kazi, kutoa elimu ya Sheria za kazi kwa wafanyakazi na waajiri na kuchukua hatua za kisheria kwa wasiozingatia Sheria za kazi. Aidha, Wizara imeendelea kuwa karibu na wafanyakazi kupitia vyama vyao na kuhakikisha kuwa inashughulikia matatizo yao kwa wakati. Wizara imeendelea kuhimiza mahusiano mema baina ya waajiri na wafanyakazi na kuhamasisha uzuiaji na utatuzi wa migogoro ya kikazi kwa njia ya majadiliano ya pamoja kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kukuza tija mahali pa kazi.

31. Mheshimiwa Spika, jumla ya kaguzi za kazi **1,754** zimefanyika katika maeneo mbalimbali ya kazi nchi. Kaguzi hizo zililenga katika kuangalia utekelezaji wa viwango vya kazi, haki za msingi za kazi pamoja na haki za vyama vya wafanyakazi katika sehemu za kazi. Kupitia kaguzi hizo, waajiri **244** walipewa amri tekelezi (*compliance orders*) baada ya kubainika kuwa wanakiuka Sheria na waajiri **9** wamefikishwa mahakamani kwa kushindwa kutekeleza amri zilizotolewa. Vile vile, maafisa Kazi **11** wamejengewa uwezo wa namna ya kufanya ukaguzi wa viwango vya kazi kwa wafanyakazi wa majumbani.

32. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kutoa elimu kuhusu Sheria za Kazi kwa wafanyakazi na waajiri katika maeneo mbalimbali ya kazi nchini. Elimu hiyo ilitolewa kwa Wafanyakazi **3,536** na Waajiri **673** wa sekta za Viwanda na Biashara, Afya, Kilimo, Ujenzi, Hoteli, Ulinzi binafsi na Usafirishaji. Wizara pia, imeshiriki katika mikutano mbalimbali ya kimataifa na kikanda (Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya nchi za Kusini mwa Afrika - SADC, Umoja wa Afrika na Shirika la Kazi la Kimataifa) iliyohusu masuala mbalimbali ya kazi ikiwa ni pamoja na kuimarisha usimamizi wa sheria za kazi, kuimarisha jitihada za kukabiliana na utumikishwaji wa watoto ikiwa ni pamoja na kufanyika kongamano la kutokomeza ajira mbaya ya mtoto katika sekta ya kilimo na usafirishaji wa binadamu.

Kima cha Chini cha Mshahara katika Sekta Binafsi

33. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuandaa mfumo sahihi wa kuwashirikisha wadau wengi zaidi katika kupanga kima cha chini cha Mshahara katika Sekta Binafsi. Kwa sasa mfumo unaotumika katika upangaji wa Kima cha Chini cha Mshahara katika sekta binafsi ni kutokana na ushauri unaotolewa na Bodi za kissekta. Utaratibu huu umesababisha malalamiko kutoka kwa waajiri na wafanyakazi kwa kutozingatiwa kwa uwiano sahihi wa vigezo vya kiuchumi na tija katika kupanga kima hicho kwa kila sekta. Katika kuboresha mfumo huo, Wizara iliunda Kikosi Kazi cha Utatu cha wajumbe kutoka Serikalini, Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri ambacho kimependekeza mfumo sahihi wa kuwa na Bodi Moja ya kupendekeza Kima cha Chini cha Mshahara katika Sekta Binafsi.

34. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha wafanyakazi na waajiri kujadiliana kwa pamoja katika kuboresha maslahi ya wafanyakazi. Katika kipindi hiki jumla ya Mikataba ya Hali Bora **67** ilisainiwa na kusajiliwa na Kamishna wa Kazi. Mikataba hiyo inahusisha sekta za Viwanda, Maji, Biashara pamoja na Hoteli.

Hifadhi ya Jamii

35. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuimarisha huduma za hifadhi ya jamii, katika kipindi kinachoishia Aprili, 2015 Wizara kwa kushirikiana na SSRA imetoa elimu hifadhi ya jamii kwa watu **517,951** na kwa makundi mbalimbali ambayo ni pamoja na Wabunge, Watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, Watendaji wa Vyama vya Wafanyakazi, Vyama vya Waajiri, Vyama visivyo vya Kiserikali (NGOs) na Makampuni binafsi. Aidha, Mamlaka imeandaa na kutekeleza mkakati wa elimu kwa umma. Elimu ya Hifadhi ya Jamii ilitolewa katika vipindi 173 vya runinga na redio na kupitia vyombo vya habari ikiwa ni pamoja na magazeti, mikutano na waandishi wa habari na ushiriki katika maonesho. Pia, zilifanyika tafiti **tatu (3)** zenye lengo la kupanua wigo wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii hapa nchini. Hizi zilijumuisha huduma zisizo rasmi za bima ya afya (social health insurance) na misaada ya kijamii (social assistance). Vile vile Serikali, imetoa Kanuni mpya ya kuwianisha mafao ya pensheni (benefits harmonization rule) iliyoanza kutumika tarehe 01 Julai, 2014.

Fidia kwa Wafanyakazi (The Workers Compensation Fund)

36. Mheshimiwa Spika, Wizara katika mwaka 2014/2015 imekamilisha taratibu muhimu za kuanza kuendesha Mfuko wa Fidua wa Wafanyakazi. Mfuko huo unaanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 74(1) cha Sheria ya Mfuko wa Fidua kwa Wafanyakazi ya mwaka 2008 (*The Workers Compensation Act, 2008*). Hatua hizo muhimu zilizotekelezwa katika kuanzisha mfuko huo ni pamoja na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Kanuni kuhusu viwango vya michango kwa makundi ya Waajiri kwa mwaka 2015/16 ambapo Serikali itachangia **asilimia 0.5** ya mshahara wa kila mtumishi kila mwezi na Taasisi Binafsi watachangia **asilimia 1** ya mshahara wa kila Mfanyakazi kila mwezi. Hatua nyingine iliyotekelezwa katika kuanzisha Mfuko huo wa Fidua ni kuteuliwa kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidua pamoja na Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini wa Mfuko.

Vita dhidi ya Ajira Mbaya kwa Mtoto

37. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika lisilo la kiserikali la *International Rescue Committee-WEKEZA* imeendelea kupambana na utumikishwaji wa watoto katika mikoa ya Tanga na Kigoma. Kupitia Mradi huu, jumla ya watoto **8,538** wamezuiwa kuingia kwenye utumikishwaji na kupatiwa shughuli mbadala ikiwa ni pamoja na elimu ya shule ya msingi kwa watoto **4,619**, elimu ya Sekondari kwa watoto **1,884** na elimu kwa watoto **2,035** waliokosa elimu ya msingi. Aidha, kupitia Mradi huu, elimu ya sheria za kazi hususani katika masuala yanayohusu katazo la utumikishwaji wa mtoto ilitolewa kwa Walimu **411**, Wajumbe wa Kamati za shule **513**, Wajumbe wa VICOBA **2,398**, Vijana **4,738** wenye umri kati ya miaka 15 hadi 17 na Maafisa wa Serikali za Mitaa **3,042**.

Ushirikishwaji wa Wafanyakazi

38. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi kuhusu ushirikishwaji wa wafanyakazi mahali pa kazi. Hatua hii imesaidia sana kuboresha mahusiano na kuwepo hali ya utulivu mahali pa kazi. Aidha, kutokana na elimu iliyotolewa Wizara ilitatua jumla ya migomo 9 iliyopokelewa kutoka kwa waajiri wa sekta za Viwanda, Ujenzi na Usafirishaji walio katika mikoa ya Dar es salaam, Tanga, Mwanza, Musoma na Kigoma.

39. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ushirikishaji wa wafanyakazi nchini, Wizara iliratibu kikao kimoja cha viongozi wa vyama vya Wafanyakazi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Kikao hicho kilijadili masuala mbalimbali kuhusiana na hali na maslahi ya wafanyakazi nchini.

Ukuzaji wa Ajira Nchini

40. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na juhudi za kuhamasisha awadau mbalimbali kushiriki katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ajira ya Mwaka 2008 pamoja na kuratibu shughuli husika. Katika mwaka 2014/2015, wadau walioshiriki katika kuandaa na kutekeleza programu za kukuza ajira ni pamoja na: TechnoServe kupitia Mradi wa kuwezesha vijana kujijiri katika kilimo mkoani Mbeya; Baraza la Taifa Uwezeshaji kupitia “Programu ya Kijana Jijiri” inayowezesha vijana kujijiri; Shirika ka Kazi Duniani kwa kushirikiana na wadau wa Utalii na Chuo cha Taifa cha Utalii kupitia Programu ya Kukuza Ujuzi katika sekta ya hotel; Shirika ka Kazi Duniani kwa kushirikiana na VETA kwa kutekeleza programu ya kutambua ujuzi ulipatikana kupitia mfumo wa elimu usio rasmi. Aidha, katika kuweka msukumo zaidi kwa Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa kuendeleza juhudi za kukuza ajira hasa kwa vijana katika ngazi za Wilaya na Mikoa, wizara iliandaa Kongamano la Wakuu wa Mikoa lililofanyika mwezi Novemba, 2014 kuhusu ukuzaji wa ajira nchini.

Kupitia Kongamano hilo, Wizara imewekeana Mkataba (*Memorandum of Understanding*) na Wakuu wa Mikoa la kukuza ajira kwa vijana na kuweka mazingira wezeshi kwa vijana kujijiri. Pia, Wizara imeratibu ushiriki wa Wajasiriamali wadogo 120 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar kwenye Maonesho ya 14 ya Nguvu Kazi/Jua Kali ya Afrika Mashariki yaliyofanyika tarehe 1 hadi 7 mwezi Desemba, 2014 mjini Kigali nchini Rwanda.

Kuimarisha ukusanyaji taarifa na takwimu za ajira

41. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, **Wizara** imeendelea kuimarisha mfumo wa taarifa za soko la ajira nchini ambapo hadi kufikia mwezi

Aprili, 2015 jumla ya ajira **574, 040** zilizalishwa katika sekta za: Kilimo ajira **154,560**; Elimu ajira **36,071**; Afya ajira **3,452**; Ujenzi wa Miundombinu ajira **107,527**; Nishati ajira **378**; Miradi ya ya Kijamii ajira **9,455**; Sekta nyingine Serikalini ajira **5,274**. Jumla ya ajira zilizozalishwa katika Sekta binafsi ni **257,322** kwa mchanganuo ufuatao: Mawasiliano ajira **6,809**; Viwanda vidogo na vya kati (SMEs) ajira **6,524** na Miradi ya uwekezaji kupitia kituo cha TIC ni **34,164**; uwekezaji katika vituo vya EPZ **16,911** na sekta nyingine za uwekezaji ni **192, 895 (Kiambatisho Na. 3)**

Huduma za Ajira

42. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia Kanuni za huduma za ajira zinazotolewa na Wakala Binafsi, Wizara imefanya uchambuzi wa maombi ya usajili wa Mawakala Binafsi **126** wa Huduma za Ajira ambapo kati yao Mawakala **96** walipewa usajili wa mwaka mmoja kuanzia tarehe 13/03/2015 hadi 12/03/2016.

Uratibu wa Ajira za Wageni

43. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia ajira za wageni nchini kwa lengo la kuhakikisha ajira hizo ni kwa manufaa ya nchi na pia kulinda ajira za Watanzania; Wizara imeratibu utungaji wa Sheria ya Ajira za Wageni kwa lengo la kuimarisha na kuongeza ufanisi wa utoaji wa vibali vya ajira kwa wageni. Sheria hiyo imeweka mamlaka moja ambayo ni Wizara ya Kazi na Ajira kuwa msimamizi wa utoaji wa vibali vya ajira kwa wageni kwa kuzingatia ujuzi adimu nchini.

44. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2014/2015, Wizara ilipokea na kushughulikia jumla ya maombi **9,271** ya vibali vya ajira za wageni vya Daraja B. Kati ya maombi hayo, maombi **8,890** (96%) yalipendekezwa kupewa vibali na maombi **381** (4%) yalikataliwa (**Kiambatisho Na. 4**)

Usajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri

45. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kuhimiza na kufuatilia haki mbalimbali za Wafanyakazi na Waajiri, ikiwemo haki ya kuanzisha, kujiunga na kushiriki katika shughuli mbalimbali halali za Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri. Katika mwaka kazi zifuatazo zimetetelezwa:

i) Kusajili Chama kimoja cha wafanyakazi cha Kutetea Haki na Maslahi ya Walimu Tanzania (CHAKAMWATA);

ii) Kukagua taarifa za hesabu za vyama 5 vya wafanyakazi;

iii) Kukagua vyama 8 katika ngazi ya taifa katika kuhakikisha vyama hivyo vinatimiza masharti ya usajili kulingana na matakwa ya Sheria; na

iv) Kutoa elimu juu ya uhuru wa kujumuika na kujiunga na vyama vya wafanyakazi na waajiri na kuwakumbusha viongozi na wananchama wa vyama kuheshimu Katiba za vyama vyao kuepuka migogoro. Wafanyakazi 102 na wajumbe 30 kutoka Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) walipatiwa elimu hiyo.

Kujenga Uwezo wa Wizara

46. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2014/2015 tumetekeleza yafuatayo katika kujenga uwezo wa Wizara:-

i) Kuajiri watumishi 21 kupitia Tume ya Ajira Serikalini ambao ni Maafisa Kazi Daraja la II na tayari wameshapangiwa vituo vya kazi mikoani;

ii) Watumishi 40 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi na watumishi 4 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi. Aidha, jumla ya watumishi 100 wamepatiwa mafunzo ya Maadili katika Utumishi wa Umma; na

iii) Kusimamia zoezi la OPRAS kwa watumishi 262 wa Wizara kulingana na mwongozo wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

TAASISI ZA UMMA CHINI YA WIZARA

47. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia shughuli za taasisi **saba** za umma zilizo chini yake. Taasisi hizo ni Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA), Shirika la Tija la Taifa (NIP), Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA), Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) na Mfuko wa Fidia ya Wafanyakazi. Mapitio ya utekelezaji wa mipango na kazi kwa mwaka 2014/2015 kupitia taasisi hizi ni kama ifuatavyo:

Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA)

48. Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi una wajibu wa kusimamia na kufuatilia uzingatiaji wa masuala ya usalama na afya mahali pa kazi kwa kusajili sehemu za kazi, kufanya ukaguzi na kupima afya za wafanyakazi. Wizara katika mwaka 2014/2015 kupitia Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) imetekeleza kazi zifuatazo;

i) Kufanya ukaguzi **4,862** wa kawaida (*General Workplace inspection*) na ukaguzi maalum **18,236** sawa na asilimia **151.9** ya ukaguzi **12,000** uliopangwa

kufanyika. Ukaguzi huu ulifanywa kwenye maeneo ya Umeme, Mitambo ya kuzalisha mvuke (boilers), Mitungi ya hewa na Mvuke, Zana za kunyanyulia vitu vizito na Vipimo vya mazingira. Aidha wafanyakazi 45,721 walipimwa afya zao sawa na asilimia **101.6** ya lengo la kuwapima wafanyakazi **45,000**

ii) Kukamilisha taratibu za kupendekeza kuridhia mikataba 6 ya Shirika la Kazi la Kimataifa (ILO) kuhusu Usalama na Afya Mahali pa Kazi. Mikataba hiyo ni Mkataba Na.155 (Occupational Safety and Health Convention, 1981), Mkataba Na.187 (Promotional Framework for Occupational Safety and Health Convention, 2006) Mkataba Na.167 (Occupational Safety in Construction Convention, 1988), Mkataba Na.161 (Occupational Health Services Convention, 1995), Mkataba Na.176 (Safety and Health in Mines Convention, 1995) na Mkataba Na.184 (Safety and Health in Agriculture Convention, 2001);

iii) Kusajili mahali pa kazi **1,847** sawa na asilimia **123** ya sehemu za kazi 1,500 zilizopangwa zilisajiliwa. Mahali pa kazi **137** zilipewa leseni za kukidhi vigezo vya Sheria namba 5 ya mwaka 2003 ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi rejea Kiambatisho Na. 5); na

iv) Mafunzo na kozi mbalimbali kuhusu Usalama na Afya Mahali pa Kazi yamefanyika kwa maafisa **1,700** wa afya na usalama mahali pa kazi kutoka sekta mbalimbali. Kozi hizi zinajumuisha kozi ya Taifa ya Usalama na Afya (*National Occupational Safety and Health Course (NOSHC)*), Utoaji wa Huduma ya Kwanza Makazini (*industrial first aid*), Usalama katika Kufanya kazi za Juu (safety in working at height), na namna ya kuunda na kuendesha Kamati za Afya na Usalama Mahali pa kazi. Aidha, OSHA iliandaa mikutano **6** na wamiliki wa viwanda mbalimbali na semina moja kwa Kamati **2** za Kudumu za Bunge kuhusu masuala ya usalama na afya mahali pa kazi rejea Kiambatisho Na. 6).

Wakala wa Huduma za Ajira (TaESA)

49. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara kupitia Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA) imetekeleza kazi zifuatazo:

i) Kusajili watafutakazi **1,249** na kuunganisha watafutakazi **503** kwa waajiri wenye fursa za ajira ndani ya nchi na kutoa mafunzo elekezi kwa watafutakazi 584 kwa lengo la kuwajengea uwezo wa jinsi ya kuweza kuajiriwa;

ii) Kusimamia na kuratibu ajira za Watanzania **1,116** nje ya nchi ikiwemo Oman **918**, Dubai **164**, India **21**, Ujerumani **6**, Japani **5** na Qatar **2**;

iii) Kutoa mafunzo ya jinsi ya kukabiliana na soko la ajira kwa wahitimu watarajiwa 665 kupitia Taasisi 2 za elimu ya juu ambazo ni Mwalimu Nyerere Memorial Academy na Taasisi ya Uhasibu Tanzania;

iv) Kutoa ushauri kwa watafuta kazi **1,157** juu ya uchaguzi wa fani, mafunzo na kazi stahiki kulingana na sifa zao na mahitaji ya soko la ajira (*Vocational Guidance and Employment Counseling*) ili kuwajengea uwezo wa kujiajiri na kuajirika;

Shirika la Tija la Taifa (NIP)

50. Mheshimiwa Spika, Shirika la Tija la Taifa (NIP) lina jukumu la kutoa mafunzo mbalimbali, kufanya tafiti zenye lengo la kuinua tija pamoja na kutoa huduma ya ushauri ili kuinua tija sehemu za kazi nchini. Katika mwaka 2014/2015, Shirika liliendesha mafunzo **48** ya kuinua tija mahali pa kazi na mafunzo ya kujenga uwezo sawa na asilimia **60** ya lengo lililopangwa. Mafunzo hayo yalitolewa kwa washiriki **820** kutoka taasisi mbalimbali. Pia NIP ilifanya tafiti moja sawa na asilimia **25** ya lengo na kutoa huduma ya ushauri katika kukuza tija kwa mteja mmoja.

Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Hifadhi ya Jamii (SSRA)

51. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/15, Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Hifadhi ya Jamii (SSRA) imetekeleza kazi zifuatazo:

i) Kufanya kaguzi **kumi na sita** (16) za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa Sheria zilizounda Mifuko hiyo na pia Sheria ya Mamlaka, Kanuni na Miongozo yake kama inafuatwa ipasavyo. Kati ya hizo, kaguzi **tano** (5) zilifanyika eneo la kazi (onsite inspection) na kumi na mbili (12) zilifanyika kwa njia ya taarifa (offsite inspection);

ii) Kutoa elimu kwa watu **1,700,000** kuhusu Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa makundi mbalimbali ambayo ni pamoja na Wabunge, Watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, Watendaji wa Vyama vya Wafanyakazi, Vyama vya Waajiri, Vyama visivyo vya Kiserikali (NGOs) na Makampuni binafsi.

Aidha, elimu ya Hifadhi ya Jamii ilitolewa katika njia mbalimbali ikiwemo, Makala ya magazeti **102**, vipindi **13** vya televisheni, vipindi **326** vya redio na mitandao mingine ya digitali **20**, ikiwa ni pamoja na ushiriki katika maonesho;

iii) Kufanya tafiti **mbili (2)** zenye lengo la kupanua wigo wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii hapa nchini. Hizi zilijumuisha huduma zisizo rasmi za bima ya afya (social health insurance) na misaada ya kijamii (social assistance);

iv) Kutoa Kanuni mpya ya kuwianisha mafao ya pensheni (pension benefits harmonization rules) iliyoanza kutumika tarehe 01 Julai, 2014; Kanuni hizi zimewezesha mafao ya pensheni kuongezeka kutoka **67%** kwenda **72.5%**,

kuthaminisha penshen (indexation) na kutumia watan wa mshahara wa miaka **3** badala ya miaka **5**;

v) Kusajili Mifuko **miwili (2)** ya hiyari na kutoa miongozo na kanuni za utendaji wao wa kila siku;

vi) Kusimamia na kufanikisha zoezi la kuhuisha michango (reconciliation of contributions) ya wanachama wa vyuo vikuu pamoja na mashirika ya umma yaliyokuwa na matatizo. Vyuo **11** na mashirika **35** yalifanyiwa kazi, ambapo kiasi cha shilingi **1,104,319,525** kilihuishwa;

vii) Kupokea na kutatua malalamiko mbalimbali ya wanachama, ambapo kati ya malalamiko **509** yaliyopokelewa, malalamiko **501** yalifanyiwa kazi na kutatuliwa;

viii) Kufanya marekebisho ya muongozo wa kujumuisha vipindi vya uchangiaji ili kuwezesha wanachama waliochangia mfuko zaidi ya mmoja kujumlisha vipindi vyake vifikie kigezo cha kupata pensheni; Muongozo huu utasaidia wanachama zaidi ya **11,070** ambao waliathirika na muundo wa kuchangia zaidi ya Mfuko mmoja wa lazima, wakati wa utumishi wao;

ix) Kuandaa Mfumo hadhari wa kusimamia na kukagua Mifuko na watoa huduma (Risk Based Supervision Framework);

x) Kutengeza mfumo wa kielektroniki wa kupokea na kutoa taarifa kati ya Mifuko na Mamlaka (Electronic Submission Portal); na

xi) Kufanya tathmini ya Mifuko yote ya pensheni kwa kushirikiana na shirika la Kazi duniani (ILO) kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji wa Mifuko, kuanda fao la wasio na ajira (unemployment benefit). Pia, tathmini hii inaendelea kuangalia uwezekano wa kupunguza idadi ya Mifuko ya pensheni iliyopo.

Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF)

52. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) limetekeleza kazi zifuatazo:-

i) Limekusanya mapato ya kiasi cha shilingi milioni **629,404.4** sawa na asilimia **60.3** ya lengo na kutumika katika kulipa mafao ya wanachama, kuwekeza katika vitenga uchumi, gharama za uendeshaji na miradi ya maendeleo (**Jedwali Na. 7**);

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ii) Limeendesha semina **3,066** kwa waajiri na wanachama nchi nzima ili waweze kuelewa vizuri mfumo mpya wa Hifadhi ya Jamii;

iii) Shirika limeandikisha wanachama wapya **113,517** ambao ni asilimia **24.5** ya lengo lililokusudiwa ambapo wanachama **37,144** ni kutoka katika sekta isiyo rasmi (Informal Sector), vikundi vya akiba ya kuweka na kukopa (SACCOS) na Vikoba;

iv) Mafao mbalimbali ya jumla ya shilingi milioni **239,658.4** yalilipwa ambazo ni sawa na asilimia **145.2** ya lengo la kulipa shilingi milioni **164,999.7**. Jumla ya wanachama waliolipwa mafao ni **65,932**;

v) Katika kuboresha Huduma kwa Wateja wake; Shirika limepata Cheti cha Kimataifa cha Utoaji Huduma Bora Kwa Wateja (**ISO 9001: 2008 Certification**).

Aidha Shirika limekamilisha Mpango wa Biashara Endelevu (*Business Continuity Plan*) na pia limeweza kuunganisha Ofisi zake zote za Mikoa na Wilaya katika Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa (*Fibre Cable*), Shirika liko katika hatua za mwisho za maandalizi ya mpango wake wa kupima afya za baadhi ya wanachama wake (*Preventive Health Checks*) na kufanya Mkutano Mkuu wa Nne wa wadau wa NSSF mwezi Mei 2015;

vi) Shirika limeshiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii (Corporate Social Responsibility) katika maeneo yafuatayo: Mchango kusaidia shughuli za kijamii katika jimbo la Mwabara (Nuru ya Maendeleo ya Jinsia), udhamini michezo ya Ramadhan Bonanza (*Union sports Club*), udhamini wa mkutano wa kila mwaka wa TAPSEA, kusaidia Mwenge wa uhuru Kilwa (DAS Kilwa), udhamini wa mchezo wa mpira wa miguu (*Mwidau Foundation*), Udhamini mkutano mkuu wa mwaka (*Tanzania Editors Forum*), mchango wa kuendesha kambi ya waogeleaji (Champion rise swim club), kusaidia mkutano mkuu wa mwaka ma mkutano wa kisayansi (*Tanzania Surgical Association*), Mchango kusaidia Iftar ya wabunge (Ngurdoto Mountain Lodge), Ulinzi na Uhifadhi wa Mazingira (DAS Kilwa), udhamini wa gharama za Traksuti **100** Mwenge Pangani, Udhamini wa gharama za kila mwaka za mikutano ya kisayansi (*Tanzania Dental Association*), (*sponsoring africa corporate governance network meeting*), kusaidia watoto wa mitaani (*Retention home upanga*) na Rukwa, msaada kwa Taasisi ya maendeleo kwa viziwi Tanzania, Kampeni ya kuongeza muamko wa utunzaji wa mazingira, kusaidia wasiojiweza, kusaidia Mkapa HIV/AIDS Foundation, kuchimba visima ukerewe, udhamini wa mwanamke na uchumi campaign, udhamini wa rock city marathon, kusaidia mchango ya makazi ya nyumba za wazee, usaidizi kwa SOS children village, mchango kusaidia ununuzi wa "Patient monitor" (Muhimbili), Mchango kwa ajili ya kuondoa umaskini (*Kisesa Development Fund*), *Rufiji Social Development*, Mkapa Fellows Program, pia michango kwa Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu cha Bagamoyo,

Zanzibar legal Services na shughuli zinginezo nyingi ambazo ni kwa manufaa ya jamii nzima kwa ujumla;

vii) Shirika limeendelea na utaratibu wa kutoa mikopo katika sekta isiyo rasmi (Informal Sector), kwa wanachama wake katika vikundi vya SACCOS na VICOBA ambapo **shilingi bilioni 51.80** zimetolewa kwa wanachama **6,506** katika Wilaya zifuatazo: Temeke, Ilala, Kinondoni, Arumeru Mashariki, Singida Mjini, Kigoma Vijijini, Masasi na Karagwe. Shirika linatoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, mtumie fursa hii kuwafahamisha watu wajijunge na NSSF ili wapate mikopo;

viii) Shirika linaendelea na Ujenzi wa Daraja la Kigamboni ambao unatarajiwa kukamilika Disemba 2015;

ix) Shirika limekamilisha miradi ya ujenzi wa ofisi na vitega uchumi katika mkoa ya Morogoro, Kilimanjaro na Wilaya ya Ilala kwa mwaka wa Fedha 2014/2015. Aidha, Shirika limeendelea na ujenzi wa jengo la ofisi na kitega uchumi mkoani Shinyanga, hoteli ya kisasa katika mkoa wa Mwanza ambao umefikia asilimia **30** na kuendelea na ujenzi wa jengo la Mzizima, Kijiji cha Kisasa Kigamboni (Tuangoma na Dungu Farm) - nyumba mchanganyiko na ujenzi wa nyumba za bei nafuu Mtoni Kijichi awamu ya tatu ambao unatarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 2015/2016;

x) Katika miradi inayofanywa kwa ushirikiano na Wadau wengine (*Joint Venture Projects*); miradi ya ujenzi wa Hospitali ya "Clinic" ya Apollo jijini Dar es Salaam na ujenzi wa ofisi za RITA (*Registration, Insolvency and Trusteeship Agency*) itakamilika mwaka wa Fedha 2014/2015; Ujenzi wa Kijiji cha Bunge Dodoma (*MP's Village*), mtaalamu/mwelekezi anakamilisha kuandaa michoro. Aidha, Shirika linasubiri udhamini kutoka Serikali ili kuanza Miradi ya Jengo la Maadili. Na pia katika ujenzi wa nyumba za Watumishi wa Serikali Nchi nzima, Kampuni ya Watumishi "*Housing Limited*" inasubiriwa kukamilisha taratibu, ili Shirika liweze kushiriki; na

xi) Shirika limeendelea na uthaminishaji mradi wa uzalishaji umeme wa megawati 300 katika eneo la Mkuranga, taratibu za ununuzi na taratibu za kupata Washauri Elekezi (*Cosultantants*) wa mradi huu zinaendelea.

TUME YA USULUHISHI NA UAMUZI (CMA)

53. Mheshimiwa spika, kama ambavyo nimeshaeleza katika aya zilizotangulia, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*Commission for Mediation and Arbitration*) ni Taasisi ya Serikali iliyo chini ya Wizara yangu yenye jukumu la kusuluhisha migogoro ya kikazi, kuamua migogoro ya kikazi na kuratibu shughuli

za Kamati ya Huduma Muhimu (*Essential Services Committee*). Vile vile Tume ina jukumu la kutoa elimu ya kuzuia migogoro mahali pa kazi.

54. Mheshimiwa spika, katika mwaka 2014/15, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (**Fungu15**) iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **4,531,723,550** kati ya fedha hizo shilingi **1,824,223,550** ni kwa ajili ya mishahara (PE) na shilingi **2,707,500,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2015, **Shilingi 982,966,133.84** sawa na **asilimia 54** ya fedha za Mishahara ya Watumishi (PE) na **shilingi 668,047,148.16** sawa na **asilimia 25** ya fedha za Matumizi mengine (OC) zilitolewa na kutumika na Tume.

Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu na Kazi ya Tume kwa Mwaka 2014/15:

55. Mheshimiwa spika, katika mwaka 2014/15, Tume imeendelea kutekeleza majukumu yake kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Taasisi za Kazi Na.7 ya mwaka 2004. Kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

Migogoro **11,435** ilipokelewa na kusajiliwa hadi tarehe 30/04/2015. Jumla ya migogoro **4,141** ilishughulikiwa na kumalizika sawa na asilimia **36**. Migogoro 2,657 ilisuluhishwa sawa na asilimia **23** na migogoro **1,484** ilitolewa uamuzi sawa na asilimia **13**. Migogoro **7,294** sawa na asilimia **64** inaendelea kushughulikiwa katika hatua mbalimbali za uamuzi;

Kuwezesha Kamati ya Huduma Muhimu kutembelea na kuifanyia uchunguzi kampuni ya Songas ambapo Kamati ilibaini kuwa Kampuni hiyo ina sifa ya kuwa sekta inayotoa Huduma Muhimu; na

Taasisi **35** zilipewa mafunzo kuhusu dhana ya ushirikishwaji wa wafanyakazi, matumizi sahihi ya Sheria za Kazi, wajibu wa wajumbe katika Baraza na namna bora ya kutatua migogoro ya kikazi.

D. MPANGO WA KAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

WIZARA YA KAZI NA AJIRA

56. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016 Wizara ya Kazi na Ajira kwa kushirikiana na Taasisi zilizopo chini yake, itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kusimamia Sheria na Viwango vya kazi, ushirikishwaji wa Wafanyakazi na kusuluhisha migogoro sehemu za kazi; kusimamia usalama na afya mahali pa kazi, kukuza na kutoa huduma za ajira; kuboresha ufanisi na tija kazini na kuboresha sekta ya hifadhi ya jamii. Utekelezaji kwa mwaka 2015/2016 ni kama ifuatavyo:-

Usimamizi Kazi na Huduma za Ukaguzi

- i) Kufanya jumla ya kaguzi **4,800** katika maeneo mbalimbali ya kazi nchi nzima ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua waajiri wanaokiuka sheria;
- ii) Kuboresha upangaji wa kima cha chini cha mishahara katika sekta binafsi kwa kuunda Bodi moja ya mishahara;
- iii) Kuimarisha majadiliano ya utatu kwa kujenga uwezo wa Wajumbe wa Baraza la Kazi, Uchumi na Jamii (**LESCO**) na Wajumbe wa Bodi ya mishahara ikiwa ni pamoja na kuwezesha vikao vyake;
- iv) Kuimarisha na kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa kupambana na utumikishwaji wa watoto (*National Action Plan on Elimination of Child Labour*) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na wabia wa maendeleo;
- v) Kufanya uelimishaji kwa wadau na umma kwa ujumla kuhusu Sheria za Kazi;
- vi) Kuhamasisha majadiliano ya pamoja kati ya waajiri na wafanyakazi pamoja na vyama vyao kwa lengo la kuboresha maslahi ya wafanyakazi, hatimaye kuongeza tija na uzalishaji;
- vii) Kuimarisha utekelezaji wa Kanuni ya Utatu ya masuala ya UKIMWI katika sehemu za kazi (*Tripartite HIV and AIDS Code of Conduct at Workplaces*) kwa lengo la kupambana na maambukizi na athari zake; na
- viii) Kujenga uwezo wa Maafisa Kazi kuhusu mbinu za kisasa za kaguzi na usimamizi wa kazi ikiwa ni pamoja na uendeshaaji wa mashtaka mahakamani.

Hifadhi ya Jamii

57. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016 Wizara itaendelea kuimarisha masuala ya hifadhi ya Jamii ambapo itaanzisha Idara mpya ya Hifadhi ya Jamii itakayokuwa na jukumu la kuratibu masuala yote ya huduma za hifadhi ya jamii kwa lengo la kuendelea kuziboiresha, kupanua wigo na kuzifanya kuwa endelevu. Kazi zitakazotekelezwa katika eneo hili ni zifuatazo:

- i) Kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Taifa wa kupanua wigo wa Hifadhi ya Jamii nchini;
- ii) Kuandaa kanuni za Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi Na.20 ya mwaka 2008;

- iii) Kuwezesha utendaji wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi;
- iv) Kushughulikia tatizo la wanachama kujitoka katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kabla ya umri wa kustaafu;
- v) Kuandaa Kanuni za Baraza la Rufaa la Hifadhi ya Jamii na kuwezesha utekelezaji wa majumuku Baraza hilo; na
- vi) Kuridhia Mkataba Na. 102 wa Shirika la Kazi la Kimataifa (ILO).

Ukuzaji wa Ajira Nchini

58. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuratibu shughuli za kukuza ajira nchini; ambapo jumla ya ajira **500,000** zinategemewa kuzalishwa katika mwaka 2015/2016 kutokana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo itakayotekelezwa na Taasisi za Umma, kupitia Programu ya Kukuza Ajira kwa Vijana, Programu ya Kukuza Ujuzi pamoja na uwekezaji katika Sekta Binafsi.

59. Mheshimiwa Spika, ili kukuza ajira na kazi za staha nchini, katika mwaka 2015/2016, Wizara imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

- i) Kuratibu uhuishaji wa masuala ya ukuzaji ajira kwenye mipango na programu za maendeleo za Halmashauri za Wilaya/Manispaa/Jiji kwenye mikoa 5, Mashirika ya Umma 6 na Wizara/Idara/Wakala za Serikali 5;
- ii) Kusimamia utekelezaji wa Programu ya Kukuza Ajira kwa Vijana ambayo imelenga kuwajengea vijana uwezo wa stadi mbalimbali za ujasiriamali; kuwapatia vijana mitaji yenye masharti nafuu na nyenzo za uzalishaji; na Kutenga maeneo maalum ya uzalishaji na kufanyia biashara;
- iii) Kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008 na Sera ya Tija, Mapato na Bei;
- iv) Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na utoaji wa taarifa za soko la ajira nchini,
- v) Kuratibu utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi wa Nguvukazi (**Skill Development Program**) chini ya Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa - BRN ambapo utekelezaji utahusu (a) Vijana 4,200 kupatiwa mafunzo ya vitendo kazini (internship/Apprenticeship katika sekta sita (maji, nishati & madini, kilimo, elimu, afya na utalii), (b) Waajiri kuwezesha kutoa mafunzo ya ujuzi na ufanisi wa kazi kwa wafanyakazi 10,000 na (c) Vijana 5,000 wa sekta isiyo rasmi wasio na vyeti vya ujuzi, kupatiwa mafunzo kuwawezesha kupatiwa vyeti vya ujuzi huo;

- vi) Kuratibu maonesho ya 16 ya Afrika Mashariki ya Nguvu Kazi/Jua Kali yatakayofanyika Dar es salaam mwezi Desemba 2015;
- vii) Kufanya Utafiti wa Hali ya Rasilimali Watu Nchini (Manpower Survey);
- viii) Kusimamia utoaji wa huduma za ajira zinazotolewa na Mawakala wa Huduma za Ajira nchini;
- ix) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Maazimio ya Wakuu wa Mikoa kuhusu ukuzaji wa ajira kwa vijana.

Usajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri

60. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016 Wizara itaendelea na jukumu la kusajili na kusimamia vyama vya waajiri na wafanyakazi nchini kama ifuatavyo:

- i) Kushughulikia maombi ya usajili wa vyama vya Wafanyakazi na Waajiri na Mashirikisho;
- ii) Kufanya kaguzi za vyama ikiwa ni pamoja na kuhakiki taarifa za fedha za vyama;
- iii) Kuwaelimisha viongozi wa vyama na wadau wake juu ya wajibu wa vyama na namna ya kushughulikia masuala mbalimbali kwa mujibu wa Sheria za Kazi na Kanuni zake;
- iv) Kushughulikia migogoro ya vyama inayojitokeza; na
- v) Kushughulikia kesi mahakamani zinazotokana na maamuzi ya Msajili na masuala yanayohusu katiba za vyama.

Kujenga Uwezo wa Wizara

61. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara imepanga kujenga uwezo wa Wizara kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

- i) Kuwajengea uwezo watumishi **hamsini** (50) wa wizara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na wengine **kumi** (10) kuwezesha kupata mafunzo ya muda mrefu katika fani mbalimbali;

Nakala ya Mtandao (Online Document)

- ii) Kuimarisha mahusiano kazini kwa kufanya vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi na kushiriki katika matamasha ya michezo;
- iii) Kuboresha mazingira ya kazi kwa kununua nyenzo na vitendea kazi pamoja na kushirikisha Sekta Binafsi katika utoaji wa huduma za ulinzi, usafi na matengenezo ya vifaa vya ofisi;
- iv) Kuendelea kutoka mafunzo ya Utawala Bora, Maadili, Vita dhidi ya rushwa mahali pa kazi na mapambano dhidi ya UKIMWI kwa watumishi **150** wa Wizara kulingana na Sheria na Miongozo ya Utumishi wa Umma. Aidha, Wizara itaendelea kuwahudumia watumishi watano (5) wanaoishi na virusi vya UKIMWI;
- v) Kufanya vikao vinne vya Kamati ya Ajira ya Wizara (mara moja kila Robo ya Mwaka) kwa kuajiri, kuthibitisha kazini na kupandisha vyeo watumishi wenye sifa za Kimuundo na utendaji mzuri wa kazi;
- vi) Kuimarisha Ofisi za Kazi za Mikoa ili ziweze kusimamia viwango vya kazi kwa mujibu wa Sheria;
- vii) Kuratibu na kusimamia ujazaji wa fomu za OPRAS na utekelezaji wake kwa watumishi **262** wa Wizara;
- viii) Kujibu Hoja za Ukaguzi, Taarifa ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuandaa Taarifa kwa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC);
- ix) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2015/2016 na Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN);
- x) Kuendelea kufuatilia mwenendo wa bajeti kwa kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi;
- xi) Kuandaa Mafunzo juu ya sheria Mpya ya Manunuzi kwa Wajumbe wa Bodi ya Zabuni ya Wizara pamoja na Wakuu wa Idara na Vitengo;
- xii) Kuendelea kuelimisha umma juu ya shughuli mbalimbali za Wizara kupitia vyombo mbali mbali vya habari pamoja kuunganisha mtandao wa Mawasiliano wa Wizara na Mkongwa wa mawasiliano wa Taifa; na
- xiii) Kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kusimamia kesi zinazohusu Wizara.

TAASISI ZA UMMA CHINI YA WIZARA

62. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara ya Kazi na Ajira itaendelea kusimamia Taasisi za Umma zilizo chini yake katika kutekeleza majukumu yao kama ifuatavyo:-

Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA)

63. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara kupitia Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

i) Kufanya ukaguzi **20,000** wa kawaida na ukaguzi **21,000** maalum kuhusu afya na usalama mahali pa kazi na kupima afya za wafanyakazi **65,000** katika sehemu mbalimbali za kazi;

ii) Kusajili sehemu **3,000** mpya za kazi ili ziweze kukidhi viwango na kanuni za Afya na Usalama Mahali pa Kazi pamoja na kutoa leseni ya kukidhi matakwa ya chini ya Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi (*The Occupational Health and Safety Act, 2003*);

iii) Kuendelea kutoa mafunzo na kozi mbalimbali za Afya na Usalama Mahali pa Kazi ambapo mafunzo hayo yatajumuisha kozi ya Taifa ya usalama na afya (*NOSHC*), kozi ya utoaji wa huduma ya kwanza makazini (*industrial first aid*), kozi ya usalama katika kufanya kazi za juu (*safety in working at height*), na kozi ya namna ya kuunda na kuendesha Kamati za Afya na Usalama Mahali pa kazi. Wafanyakazi na Waajiri **3,000** wanatarajiwa kupata mafunzo haya.

iv) Kuanzisha mifumo mbalimbali ya utendaji kazi ikiwa ni pamoja na kuanzisha mfumo wa kuripoti na kutoa taarifa za magonjwa na ajali zitokanazo na kazi, mfumo wa kutunza kumbukumbu, mfumo wa usimamizi wa fedha na mfumo wa usimamizi wa vifaa (*Asset tracking system*);

v) Kuendelea kuelimisha wafanyabiashara wadogo na wa kati pamoja na sekta isiyo rasmi ili waweze kuboresha mazingira yao ya kazi kwa kuendesha warsha, semina na makongamano mbalimbali katika mikoa ya Tanzania Bara;

vi) Kukamilisha uandaaji wa rasimu za kanuni tatu ambapo kanuni mbili ni kuhusu gesi "*Occupational health and safety (Oil and Gas) rules*", na "(Vessel under pressure regulations na kanuni moja kuhusu utoaji taarifa za magonjwa na ajali zitokanazo na kazi "*Recording and reporting of occupational diseases, injuries and dangerous occurrences rules*"; na

vii) Kushiriki katika taratibu za kuridhia mikataba **sita (6)** ya Kimataifa (ILO Conventions) inayohusiana na Usalama na afya mahali pa kazi. Mikataba

hiyo ni Mkataba Na. 155 (*Occupational Safety and Health Convention, 1981*), Mkataba Na.187 (*Promotional Framework for Occupational Safety and Health Convention, 2006*) Mkataba Na.167 (*Occupational Safety in Construction Convention, 1988*), Mkataba Na.161 (*Occupational Health Services Convention, 1985*), Mkataba Na.176 (*Safety and Health in Mines Convention, 1995*) and Mkataba Na.184 (*Safety and Health in Agriculture Convention, 2001*).

Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA)

64. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA) umepanga kufanya yafuatayo:-

i) Kushiriki katika zoezi la kutoa mafunzo ya ujuzi (Internship Program) kwa watafutakazi **4,200** ili kuwajengea uwezo wa kushindania fursa katika soko la ajira;

ii) Kusajili watafutakazi **3,000** na kuunganisha watafutakazi **1,000** kwa waajiri wenye fursa za ajira ndani ya nchi;

iii) Kutembelea waajiri **1,000** kwa lengo la kubaini idadi na aina ya fursa za ajira;

iv) Kusimamia na kuratibu ajira za Watanzania **1,000** nje ya nchi;

v) Kuendelea kukusanya, kuchambua na kusambaza Taarifa za Soko la Ajira;

vi) Kutoa mafunzo elekezi (Job search workshops) kwa watafutakazi **1,500** na kutembelea Taasisi **20** za elimu ya juu kwa lengo la kutoa mafunzo ya jinsi ya kukabiliana na ushindani wa soko la ajira kwa wahitimu watarajiwa; na

vii) Kutoa ushauri wa kitaalam (*consultancy services*) kwa wadau juu ya masuala ya huduma za ajira hapa nchini.

Shirika la Tija la Taifa (NIP)

65. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/16, Wizara kupitia Shirika la Tija la Taifa (NIP) imepanga kutekeleza kazi zifuatazo katika kuongeza Tija sehemu za kazi:

i) Kuendesha mafunzo **80** ya uongozi yatakayohudhuriwa na watumishi **1,200** kutoka taasisi za umma, binafsi na taasisi zisizokuwa za Kiserikali (NGO's);

Nakala ya Mtandao (Online Document)

- ii) Kutoa huduma za ushauri elekezi kwa wateja **30** katika sekta za umma, binafsi na taasisi zisizokuwa za Kiserikali (NGO's);
- iii) Kufanya tafiti nne katika maeneo mbalimbali yanayolenga kuboresha tija;
- iv) Kuanzisha mahusiano na kushirikiana na taasisi nyingine za tija duniani; na
- v) Kuanzisha mahusiano na kushirikiana na wadau wa maendeleo (Development Partners) na taasisi za kimataifa (International Agencies) kwenye huduma za mafunzo, utafiti na ushauri elekezi.

Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Hifadhi ya Jamii (SSRA)

66. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Hifadhi ya Jamii (SSRA) itaendelea kutekeleza hatua za kuboresha Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

- i) Kukamilisha tathmini ya Mifuko yote inayofanywa kwa kushirikiana na ILO
- ii) Kuendelea kutekeleza Mkakati wa elimu kwa umma kwa lengo la kuongeza uelewa wa masuala ya hifadhi ya jamii. Elimu hiyo itafanyika zaidi kikanda, ambapo zaidi ya wanachama 2,000,000 wataelimishwa na wanafunzi 100,000 wa vyuo vikuu wataelimishwa. Aidha, Mamlaka itaendelea kutumia Runinga, Redio na Magazeti kuwafikia wananchi wengi zaidi nchi nzima;
- iii) Kuendelea na zoezi la ukaguzi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuhakikisha kuwa Mifuko hiyo inaendesha shughuli zake kwa mujibu wa sheria na kwa manufaa ya wanachama wake ambao ndio msingi wa kuanzishwa kwao. Kaguzi 29 zitafanyika, 5 zikiwa ni za eneo la kazi (onsite supervision) na 24 zikiwa si za eneo la kazi (offsite surveillance);
- iv) Kufanya tafiti tano (5) katika maeneo ya ubora wa huduma, mafao mbadala kwa sekta isiyo rasmi na bima za afya ya jamii. Kutokana na tafiti hizi Mamlaka itabuni program na mafao maalum ya hifadhi ya jamii kwa sekta isiyo rasmi mijini na vijijini;
- v) Kutekeleza mageuzi katika sekta ya hifadhi ya jamii yaliyoainishwa katika Mpango wa Mageuzi ya Sekta hiyo katika kipindi cha 2012-19.
- vi) Kuendelea na kazi ya usajili wa Mifuko ya hiyari 4 (Supplementary Schemes), Mameneja Wawekezaji 2 (Fund Managers) na Watunza nyaraka (Custodians) na kutoa miongozo na kanuni za utendaji wao wa kila siku; na

vii) Kuboresha Mfumo wa usimamizi unaotumia vipimo vya hathari (Risk Based Supervision) kwa kuandaa miongozo.

Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF)

67. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16 Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii litatekeleza kazi zifuatazo:-

i) Kukusanya jumla ya Shilingi milioni **1,561,032.15** na kutumia kiasi hicho cha fedha kulipia mafao ya wanachama, kuwekeza kwenye vitega uchumi mbalimbali, gharama za uendeshaji na miradi ya maendeleo;

ii) Kuimarisha uandikishaji na ukusanyaji michango ya Wanachama katika sekta isiyo rasmi (*informal sectors*), kuendelea na ukusanyaji wa madeni kwa waajiri na pango kwa wapangaji wa majengo ya NSSF;

iii) Kuendelea kutoa elimu kwa wanachama, waajiri na umma kwa ujumla ili waweze kuelewa vizuri mfumo mpya wa hifadhi ya jamii;

iv) Shirika litaendelea na mpango wa kupima afya za wanachama wake (*Preventive Health checks*);

v) Kufanya mkutano mkuu wa tano wa wadau wa NSSF;

vi) Kukamilisha tathimini ya uwezo wa mfuko kifedha ili kulipa mafao kwa wanachama wake kwa muda mrefu ujao;

vii) Kukamilisha ujenzi wa daraja la Kigamboni mwezi Desemba, 2015;

viii) Kuendelea na ujenzi wa vitega uchumi; Hospitali ya Apollo, Mradi wa nyumba za bei nafuu mia nane Mtoni Kijichi awamu ya Tatu, Ujenzi wa Kijiji cha Kisasa Kigamboni (*Tuangoma na Dungu Farm*), ujenzi wa kijiji cha kisasa Kigamboni (*Azimio Satellite town*), ujenzi wa Kijiji cha Bunge Dodoma (MP's Village) na Ofisi za Bunge Dar es Salaam na Tanga (*Commercial Complex*), kituo cha kimataifa cha Magari Mwandiga Kigoma, Ujenzi wa Majengo ya NSSF/Maadili, NSSF/TBC; na

ix) Kuanza ujenzi wa jengo kwa ajili ya ofisi Makao Makuu katika Mkoa wa Dar es Salaam, ofisi katika Wilaya za Kinondoni, Temeke, Tarime na Kasulu, na kuendelea na ujenzi wa majengo ya ofisi na vitega uchumi katika mikoa ya Mbeya, Mwanza, wilaya za Temeke na Kinondoni. Pia kuanza ujenzi wa kituo cha michezo (*Sports Academy*).

TUME YA USULUHISHI NA UAMUZI (CMA)

68. Mheshimiwa spika, naomba sasa nitoe maelezo kuhusu mpango wa kazi za Tume ya Usuluhishi na Uamuzi, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16. Tume imeweka kipaumbele katika kutekeleza yafuatayo:-

- i) Kusuluhisha na kuamua migogoro **15,000** ya kikazi na kuandaa taarifa;
 - ii) Kufanya tafiti juu ya migogoro ambayo haijasajiriwa katika Tume na kuishughulikia;
 - iii) Kuendesha mafunzo **200** ya uelewa na ushauri wa kisheria kwa waajiri na wafanyakazi juu ya kuzuia na kutatua migogoro mahali pa kazi;
 - iv) Kuandaa na kusimamia vikao vya Makamishna wa Tume na vikao vya Kamati ya Huduma Muhimu (*Essential Services Committee*);
 - v) Kuandaa na kusambaza juzuu ya tatu ya kitabu cha rejea cha maamuzi mbalimbali ya Tume (*Case Management Guide Vol. 3.*) yaliyorejewa na Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi kwa matumizi ya wadau wa Tume;
 - vi) Kuwezesha uanzishwaji wa vyombo vya ushirikishwaji wa wafanyakazi mahala pa kazi;
 - vii) Kupokea na kusajili mikataba ya kuunda mabaraza ya wafanyakazi sehemu za kazi;
 - viii) Kufanya tathmini ya hali ya ushirikishwaji Tanzania Bara;
 - ix) Kujenga uwezo wa Tume kwa kuwaendeleza watumishi kitaaluma;
- na
- x) Kuendeleza mafunzo ya maadili, vita dhidi ya rushwa na utawala bora sehemu za kazi na mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI.

E. SHUKRANI

69. Mheshimiwa spika, mafanikio yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2014/2015 yametokana na ushirikiano wa hali ya juu wa viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara yangu. Napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru viongozi wote wa Wizara ya Kazi na Ajira pamoja na Mashirika na Taasisi zake, kwa juhudi zao kubwa walizoonyesha katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa. Shukrani zangu za kipekee nazielekeza kwa **Mheshimiwa Dkt. Milton**

Makongoro Mahanga (Mb), Naibu Waziri wa Kazi na Ajira na Mbunge wa Jimbo la Segerea kwa ushirikiano na ushauri wake wa karibu. Aidha, napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu **Bwana Eric Shitindi** pamoja na Wakuu wa Idara, Vitengo na Watumishi wote wa Wizara yangu, Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu yangu pamoja na michango yao iliyowezesha kuandaa hotuba hii.

70. Mheshimiwa Spika, kwa njia ya pekee naomba niwashukuru Wajumbe wa Baraza la Kazi, Uchumi na Jamii (*LESCO*), Chama cha Waajiri Tanzania (*ATE*) na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (*TUCTA*) kwa michango na ushauri wao mzuri walionipatia katika kutekeleza majukumu na malengo ya Wizara yangu. Nazishukuru pia Wizara na Taasisi, Mashirika na Idara mbalimbali za Serikali na Taasisi zisizo za Kiserikali ambazo tumeshirikiana nazo.

71. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua na itaendelea kuthamini michango mbalimbali ya Washirika wa Maendeleo ambayo inasaidia kwa kiwango kikubwa kutekeleza majukumu ya Wizara. Naomba nitumie fursa hii kuzishukuru kwa dhati nchi na Washirika wa maendeleo ambao wamechangia katika utekelezaji na mafanikio ya Wizara yangu. Hivyo, napenda shukrani zangu za dhati ziende kwa Shirika la Kazi Duniani (*ILO*), *UNDP*, *UNICEF*, *UNFPA*, Shirika la Misaada la Kimataifa la Denmark (*DANIDA*), Idara ya Kazi ya Marekani, Serikali ya Brazil na Benki ya Dunia (*WB*).

72. Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge letu kwa kuendesha shughuli za Bunge kwa viwango stahiki. Natoa pia shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa michango yao ndani ya Bunge na nje ya Bunge inayolenga kuboresha utendaji katika Wizara yangu.

73. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba niishukuru tena Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Said Mtanda, Mbunge wa Jimbo la Mchinga na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Albert Obama, Mbunge wa Manjovu kwa kuendelea kuisimamia vyema Wizara yangu. Wizara itaendelea kutekeleza ushauri na maelekezo ya Kamati kwani yanalenga kuboresha utendaji wa kazi wa Wizara.

74. Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wote wa mkoa wangu wa Mara kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia. Aidha, kwa namna ya pekee naishukuru familia yangu kwa upendo wao na mchango mkubwa ninaoupata.

F. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016

75. Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi **38,883,129,000** kwa Wizara ya Kazi na Ajira (**Fungu 65**) na jumla ya Shilingi **4,097,054,000** kwa Tume ya Ushuluhishi na Uamuzi (Fungu 15) kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ili kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii katika mchanganuo ufuatao:-

(a) Fungu 65: Wizara ya Kazi na Ajira

i) Shilingi **4,158,089,000** zitatumika kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi wa Wizara;

ii) Shilingi **14,725,040,000** zitatumika kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (OC);

iii) Shilingi **20,000,000,000** zitatumika katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

(b) Fungu 15: Tume ya Usuluhishi na Uamuzi

(iii) Shilingi **1,910,043,000** zitatumika kulipa mishahara ya watumishi wa Tume; na

(iv) Shilingi **2,187,011,000** zitatumika kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (OC).

76. Mheshimiwa Spika, naomba tena nitoe shukrani zangu kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa anwani: www.kazi.go.tz

77. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Dkt. Maua. Mheshimiwa Dkt. Maua subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, kuna mgeni wa Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mbunge wa Kibaha ambaye tulisahau kumtangaza jina lake, ambaye ni Mzee Mguta, Mwenyekiti wa Tawi wa CCM Mlandizi. Karibu Bungeni! (*Makofi*)

MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI (K.n.y. KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAENDELEO YA JAMII): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara

ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 pamoja na maoni ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba nichukue nafasi hii kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kuhusu Utekelezaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Maua subiri kidogo. Kutokana na sababu zisizoweza kuelezeka, namwita Mwenyekiti, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o aweze kuendelea na Kikao.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Lediana M. Mng'ong'o) Alikalialia Kiti

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, endelea.

MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI (K.n.y. KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba kuchukua fursa hii kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu na kwa Familia ya Marehemu Mheshimiwa Capt. John Damian Komba, aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, aliyefariki mwezi Februari, 2015. Hakika Kamati itamkumbuka sana kwa mchango wake mkubwa aliutoa katika kuendeleza Taifa hili. Bwana ametoa na Bwana ametwaa, jina lake lihimidiwe. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ilikutana na Wizara ya Kazi na Ajira tarehe 6 na 7 Mei, 2015 katika kikao chake kilivyofanyika Dar es Salaam. Kamati ilipokea na kujadili kwa kina utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015, pamoja na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uchambuzi wa Makadirio ya Wizara hiyo, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa mafungu mawili yaliyo chini ya Wizara ambayo ni Fungu 65 – Wizara ya Kazi na Ajira na Fungu 15 – Tume ya Usuluhishi na Uamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Taarifa za Kamati za miaka iliyopita zinazohusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii, inaonekana kwamba kwa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

zaidi ya miaka mitano mfululizo, Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti inayotengwa kwa Wizara bado ni ndogo ikilinganishwa na majukumu yanayopaswa kutekelezwa. Kwa mfano, mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilikasimiwa jumla ya Sh.17,654,394,000/= . Kati ya hizo Sh. 5,825,289,000/= sawa na asilimia 33 zilitengwa kwa ajili ya kulipia mishahara ya watumishi. Sh. 8,924,105,000/= zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na Sh. 2,925,000,000/= sawa na asilimia 17, fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 Wizara imepokea jumla ya Sh. 4,744,071,997/= sawa na asilimia 80 ya fedha za mishahara ya watumishi na Sh. 2,692,134,371/= sawa na asilimia 30 ya fedha za matumizi mengineyo (OC). Aidha, hakukuwa na fedha yoyote ya bajeti ya maendeleo iliyotolewa. Kwa mantiki hii, inaonyesha kwamba hakuna kazi yoyote ya maendeleo iliyofanywa na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kukosekana kabisa kwa bajeti ya maendeleo katika Wizara hii ni kumaanisha kwamba Wizara hii haina jipya katika kuiendeleza nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kueleza wasiwasi wake juu ya kutokuwepo kwa nia ya dhati ya Serikali kwa kutotenga fedha za kutosha au kuinyima kabisa fedha za miradi ya maendeleo na kuifanya isimame pale ilipo na kutosonga mbele hata kwa hatua moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha unaoishia Juni 30, 2015, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo mbalimbali hasa katika nyanja zifuatazo:-

- (i) Uanzishwaji wa Mfuko wa Pensheni kwa Wazee;
- (ii) Migogoro ya Wafanyakazi;
- (iii) Ukuzaji wa Ajira kwa Vijana Nchini;
- (iv) Ufuatiliaji wa masuala yanayohusu Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA);
- (v) Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, itekeleze masuala mbalimbali ya kijamii na kiuchumi; na
- (vi) Uanzishwaji wa Idara/Kurugenzi ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza ushauri wa Kamati kwenye maeneo ambayo bado hayajafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuelezea utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha uliopita, naomba sasa nizungumzie Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 nikianza na makadirio ya ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilitarajia kukusanya jumla ya Shilingi milioni 9.606 kama maduhuli. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha Shilingi milioni 3.12 na hivyo kutokukusanya kiasi cha Shilingi milioni 6.486 sawa na asilimia 67.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya Sh. 7,484,334,000/= kama maduhuli. Hili ni ongezeko la Sh. 7,474,728,000/=. Vyanzo vya mapato haya ya Wizara ni pamoja na vibali vya kazi kwa wananchi wasio Watanzania na ada kutoka kwa Wakala wa Ajira Binafsi. Kamati inaipongeza sana Wizara hii kwa kupata chanzo hiki kipya cha mapato.

katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara imetengewa jumla ya Sh. 18,280,136,000/=. Kati ya fedha hizo Sh. 14,725,041,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 4,158,089,000/= ni kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara inatarajia kutumia kiasi cha Shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yaliyopewa kipaumbele katika miradi ya maendeleo kwa mwaka ujao wa fedha 2015/2016 ni pamoja na kukuza ajira kwa vijana na kuwezesha ukuzaji ujuzi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua ufinyu wa bajeti ya Serikali. Hata hivyo, inapongeza sana Serikali kwa kutenga kiasi hicho.

Aidha, baada ya kufanya uchambuzi wa bajeti ya miradi, Kamati imebaini kuwa bado ni ndogo ikilinganisha na wimbi kubwa la vijana waliopo nchini ambao hawana ajira.

Kamati inasikitishwa kwa kitendo cha Serikali kutenga bajeti ndogo kwa Wizara hii bila kujali umuhimu wa Wizara hasa katika kukuza ajira kwa vijana

ukizingatia hatari inayoweza kuligharimu Taifa kwa kuwa na vijana wengi wasio na ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia na kuichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015, pamoja na maombi ya fedha yanayojumuisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Kwanza, Uanzishwaji wa Mfuko wa Pensheni kwa Wazee. Kwa miaka mingi sasa wazee wamekuwa wakielezwa kuwa kundi hili ni muhimu katika jamii nyingi duniani na hata kwenye jamii yetu. Kutokana na umuhimu wao ndiyo maana Serikali nyingi duniani hasa za Mataifa yaliyoendelea yamekuwa yakiwatengea bajeti. Thamani ya wazee imekuwa kubwa nchini kwetu kwa miaka mingi na ndiyo maana Serikali iliamua kutunga Sera ya Wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyotoa katika Bunge lako Tukufu tarehe 12 Mei, 2015, alitambua mchango wa wazee na umuhimu wao kama hazina na chemchemi ya busara katika jamii, katika kuhimiza maadili, malezi bora, usalama na kuwa washauri wakuu katika masuala mengine muhimu ya Kitaifa hasa katika kipindi hiki ambacho jamii inapitia mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kiutamaduni.

Kamati inakubaliana na Mheshimiwa Waziri Mkuu juu ya ukweli huu lakini inahoji kwamba kama Serikali inaona wazee ni sehemu muhimu sana katika jamii: Je, inashindwa vipi kuunda Mfuko wa Pensheni ya Wazee? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi za Mwaka 2012, idadi ya wazee nchini Tanzania kwa sasa imefikia 5,056,825 kati ya watu takriban milioni 49. Hii ni sawa na kusema kwamba idadi ya wazee ni sawa na asilimia 11 ya idadi ya watu wote nchini Tanzania. Idadi hii siyo ya kuipuzia hata kidogo. Hata hivyo, Kamati inaitaka Serikali kutatua matatizo mbalimbali ya wazee. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 Kamati ilishauri Serikali ikamilishe mchakato wa uanzishwaji wa Pensheni ya Wazee ili waweze kuboresha hali zao za kimaisha. Wizara imeiarifu Kamati kuwa imekamilisha Rasimu ya Mapendekezo ya Kuanzisha Pensheni ya Wazee na kupanga jinsi utekelezaji wake utakavyokuwa.

Hata hivyo, uhalisia wa utekelezaji unaonekana kuwa mgumu kutokana na ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, ambapo zimetengwa Shilingi milioni 41 tu wakati mahitaji halisi yaliyopendekezwa ni Shilingi bilioni 136. Kiwango hiki ni sawa na asilimia tatu ya mahitaji halisi. Asilimia hii ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imesikitishwa na majibu ya Serikali kwamba inaendelea kujifunza kutoka TASAF. Kamati inashindwa kuelewa nia thabiti ya Serikali kwa kuwa hata katika taarifa ya Kamati hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Kamati ilipokea majibu ya Serikali kuendelea kujifunza kutoka maeneo, idara na sekta mbalimbali za Serikali ndani na nje ya nchi. Kamati inapenda kueleza wasiwasi wake kuhusu utekelezaji wa upatikanaji wa Pensheni ya Wazee kwa sababu takriban muda wa miaka mitano mfululizo Kamati imekuwa ikishauri juu ya kuwapatia wazee Pensheni bila mafanikio yoyote mpaka sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutilia maanani suala hili la Pensheni ya Wazee na kuanzisha Mfuko wa Pensheni ya Wazee. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi imekuwa ikisimamia utekelezaji wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004. Aidha, Tume imekuwa ikiratibu migogoro yote ya kikazi inayowasilishwa kwake ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wafanyakazi sehemu za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi imetengewa kiasi cha Sh. 4,830,800,000/= kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Tume ya Usuluhishi na Uamuzi imetengewa kiasi cha Sh. 4,097,054,000/=. Ni wazi kuwa kwa bajeti hii ndogo, bado Wizara itaendelea kuathiri utekelezaji wa majukumu ya Tume hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Tume ilipokea na kusajili migogoro 6,776. Katika mwaka huo huo (2014/2015) Tume ilishughulikia migogoro 4,141. Aidha, ikilinganishwa migogoro iliyopokelewa kwa mwaka wa fedha na idadi ya migogoro iliyoshughulikiwa kwa mwaka utaona kuwa kuna ongezeko kubwa la migogoro ambayo inahitaji fedha na rasilimali watu ili kushughulikiwa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa uwezo wa CMA kufanya kazi unazidi kupungua kutokana na kiasi cha fedha kinachotengwa ukilinganisha na idadi ya kesi zinazopokelewa na kusajiliwa. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuwaongezea bajeti ili Tume iweze kutenda kazi zake ya kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la migogoro ya muda mrefu katika Sekta ya madini nchini ni miongoni mwa migogoro inayolisumbua Taifa. Migogoro hiyo ni pamoja na mgogoro kati ya wafanyakazi zaidi ya 200 na Uongozi wa Mgodu wa *African Barrick* Bulyanhulu. Kamati iliwahi kupata fursa ya kukutana

na wawakilishi wa wafanyakazi wa Mgodu wa *African Barrick* na kuzungumza nao. Pamoja na mambo mengine, suala la kuachishwa kazi bila kupimwa afya zao kama sheria inavyoelekeza, walililalamikia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Wizara kupitia *OSHA*, kati ya wafanyakazi zaidi ya 250 wa Bulyankhulu walioachishwa kazi mwaka 2007, wafanyakazi 79 tu ndio waliopimwa afya zao mara baada ya kuachishwa kazi kama sheria inavyotaka. Aidha, kati ya wafanyakazi waliorudi kazini baada ya mgomo na kugundulika kupata athari za kiafya baadaye na kuachishwa kazi, ni wafanyanyakazi 10 tu ndio walipimwa afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Chama cha Wafanyakazi wa Migodi (*TAMICO*) kuwabaini wafanyakazi ambao hawajapimwa afya zao kwa idadi kamili ya wafanyakazi hao na kama ikibainika wana matatizo ya kiafya, kama inavyobainishwa na sheria, walipwe haki zao endapo watahindwa kuendelea na kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwezi Machi na Aprili, 2015, kumekuwa na migomo ya madereva wa mabasi ya abiria hapa nchini. Migomo hii imekuwa na athari kubwa sana kwa kuwa imesababisha kazi nyingi za uzalishaji kusimama. Sababu za migomo hii ni pamoja na madereva kutokuwa na mikataba ya ajira, mpango wa Serikali wa kuwataka madereva wa mabasi ya abiria kwenda shule kila wanapotaka kujaza maombi ya kupata leseni mpya.

Aidha, madereva wanailalamikia Serikali kwa kushindwa kutatua kero zao za ajira ambazo wamekuwa wakizitoa mara kwa mara bila kupata ufumbuzi. Kamati inaishauri Serikali kukaa chini na kuangalia kwa undani suala hili na kulipatia ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ajira kwa vijana limekuwa ni changamoto kubwa na liinasumbua Taifa. Kwa muda mrefu sasa, Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kupanga bajeti ya kutosha kwa Wizara ya Kazi na Ajira ili kuiwezesha Wizara hii kufanya kazi ipasavyo na kuwawezesha vijana kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake aliyoitoa Bungeni tarehe 12 Mei, 2015, alikiri wazi kuwa upatikanaji wa ajira bado ni changamoto kubwa inayowakabili vijana, siyo tu nchini kwetu, bali duniani kote.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, idadi ya vijana nchini ni milioni 16.2, sawa na asilimia 35.1 ya Watanzania wote. Takwimu hizo zinabainisha kuwa, vijana walioajiriwa katika Sekta ya Umma ni 188,000; walioajiriwa katika Sekta Binafsi ni milioni 1.03. Hivyo, sehemu kubwa ya

vijana takriban milioni 15 wamejiajiri katika shughuli za kilimo, mifugo, uvuvi na biashara ndogo ndogo ambako hata hivyo hawajaandaliwa mazingira rafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu hizi, inaonesha wazi kuwa Serikali imeshindwa kuwasaidia vijana. Katika hali ya kawaida, vijana milioni 15 kati ya milioni 16.2 kujajiri wenyewe ni kuongeza mzigo katika kunyang'anyana rasilimali chache zinazoshindaniwa kuendeleza na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi wanakabiliwa na changamoto ya tija ndogo kwenye uzalishaji na biashara kutokana na matumizi ya teknolojia duni, ukosefu wa mitaji, miundombinu ya uwekezaji mdogo mdogo katika ngazi za awali za ujasiriamali na uwekezaji na elimu ya ujasiriamali.

Ili kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imekuwa ikitoa elimu ya ujasiriamali na mikopo kwa vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na mifuko mingine ili kuwawezesha kuanzisha au kupanua miradi yao ya uzalishaji mali. Hata hivyo, Mfuko huu wa Maendeleo ya Vijana hautengewi asilimia tano kutoka Halmashauri na Serikali Kuu kama inavyotakiwa. Athari ya kutotengwa kwa asilimia tano kutoka katika kila Halmashauri inasababisha vijana kushindwa kukabiliana na changamoto zinazowakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuja na mpango mkakati utakaoonesha Serikali itakavyowezesha kuwepo mazingira mazuri na bora katika kutengeneza ajira binafsi na za kijamii kwa ajili ya vijana nchini. Kamati inaamini kwamba hili linawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza sana Wizara kwa kuweza kuanzisha Idara ya Hifadhi za Jamii kama Idara inayojitegemea ndani ya Wizara. Kamati ina imani kubwa kwamba kuwepo kwa Idara ya Mashirika ya Hifadhi ndani ya Wizara ya Kazi na Ajira kutasaidia sana kutatua migogoro na mambo mengine madogo madogo yaliuyojitokeza katika mashirika haya.

Hata hivyo, Idara hii haijajitosheleza kabisa kirasilimali na hivyo uwezo wake kutekeleza majukumu kuwa mdogo. Kamati inaishauri Serikali kuiongezea bajeti Wizara hii ili iweze kuiimarisha idara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA), hii ni taasisi inayosimamia na kudhibiti masuala yote ya hifadhi ya jamii na kuishauri Serikali ipasavyo juu ya uimarishaji na uboreshaji wake.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhika na utekelezaji wa maoni yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kwa Mamlaka ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuiboresha taasisi hii ili iweze kuendelea kuisimamia Mifuko ya Hifadhi za Jamii kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza NSSF kwa kuendelea kuwahudumia wateja wake kwa ufanisi mkubwa. Pamoja na pongezi hizo, Kamati inaushauri Mfuko huu kuweka mkakati wa kuongeza juhudi za kutoa elimu hasa kwa wakulima, wafugaji na watu wengine wasio katika ajira rasmi ili waweze kuona umuhimu wa kujiunga kwenye mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliarifiwa kuwa katika mwaka wa fedha 2014/2015, NSSF ilikuwa katika majadiliano na Ofisi ya Bunge kwa ajili ya kuingia mkataba wa ujenzi wa Ofisi za Wabunge katika Majimbo ya Uchaguzi nchini. Jambo hili tuliliunga mkono na Kamati kutokana na umuhimu wake. Hata hivyo utekelezaji wa jambo hili haujaleta matumaini. Kamati inashauri jambo hili lipewe umuhimu na lifanywe kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inashuhudia ongezeko kubwa la uwekezaji kutoka kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Uwekezaji huu unakwenda pamoja na ajira mbalimbali kwa Watanzania hali ambayo inachangia pia kuwepo ongezeko la matatizo ya afya za wafanyakazi.

Katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) umepanga kutekeleza kazi kadhaa ikiwa ni pamoja na kufanya kaguzi 41,000 maalumu na za kawaida kuhusu afya mahali pa kazi. Aidha, Wakala katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 unatarajia kupima afya za wafanyakazi 65,000 katika Sehemu mbalimbali za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri upimaji huu ufanyike mapema, pamoja na kuwabaini waliokuwa wafanyakazi wa mgodi wa Bulyakhulu ambao wamekuwa wakilalamikia suala hili kwa muda mrefu sana. Kamati pia inashauri kuwa kaguzi hizi zifanyike kwa kina na kila mara ili kubaini upungufu uliopo katika sehemu hizo ili kulishughulikia ipasavyo.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Naomba umalizie! Mheshimiwa naomba umalizie muda umekwisha. Malizia!

DKT. MAUA ABEID DAFTARI (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KAZI NA AJIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kuwashukuru Watendaji wote, Waheshimiwa Wabunge, Spika na Katibu wa Bunge pamoja na Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwa kazi wanazoendelea kuzifanya katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KAZI NA AJIRA KWA MWAKA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba nichukue nafasi hii kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kuhusu Utekelezaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba kuchukua fursa hii kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu na kwa Familia ya Marehemu Mheshimiwa Capt. John Damian Komba, (Mb) Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii aliyefariki mwezi Februari mwaka 2015.

Ni kweli kwamba Kamati itamkumbuka kwa mchango wake mkubwa alioutoa katika kuendeleza taifa hili. Bwana ametoa na bwana ametwaa, jina lake lihimidiwe. Amina.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ilikutana na Wizara ya Kazi na Ajira tarehe 6 na 7 Mei, 2015 katika vikao vyake vilivyofanyika Dar es salaam. Kamati ilipokea na kujadili kwa kina utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, pamoja na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa Makadirio ya Wizara hiyo, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa mafungu mawili yaliyo chini ya Wizara ambayo ni **Fungu 65 – Wizara ya Kazi na Ajira na Fungu 15 – Tume ya Usuluhishi na Uamuzi.**

2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA

MWAKA 2013/2014

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa za Kamati za miaka iliyopita zinazohusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii inaonekana kwamba kwa zaidi ya miaka mitano mfululizo Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya Wizara hii. Bajeti inayotengwa kwa Wizara bado ni ndogo ikilinganishwa na majukumu yanayopaswa kutekelezwa. Kwa mfano, Mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilikasimiwa jumla ya Shilingi bilioni kumi na saba milioni mia tatu tisini na nne **(17,654,394,000/=)**. Kati ya hizo Shilingi bilioni tano milioni mia nane ishirini na tano laki mbili themanini na tisa elfu **(5,825,289,000/=)** sawa na asilimia 33, zilitengwa kwa ajili ya kulipia mishahara ya watumishi, ambazo ni Shilingi bilioni nane milioni mia tisa ishirini na nne laki moja elfu tano **(8,924,105,000/=)** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengine (OC) na Shilingi bilioni mbili milioni mia tisa ishirini na tano **(2,925,000,000/=)** sawa na asilimia 17 fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 Wizara imepokea jumla ya Shilingi bilioni nne milioni mia saba arobaini na nne elfu sabini na moja mia tisa tisini na saba **(4,744,071,997/=)** sawa na **asilimia 82** ya fedha za mishahara ya watumishi na Shilingi bilioni mbili milioni mia sita tisini na mbili laki moja thelathini na nne mia tatu sabini na moja **(2,692,134,371/=)** sawa na asilimia 30 ya fedha za matumizi mengine (OC). Aidha, hakukuwa na fedha yoyote ya bajeti ya maendeleo iliyotolewa. Kwa mantiki hii, inaonesha kwamba hakuna kazi yoyote ya maendeleo iliyofanywa na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, kukosekana kabisa kwa bajeti ya maendeleo katika Wizara hii ni kumaanisha kwamba Wizara hii haina jipya katika kuiendeleza nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kueleza wasiwasi wake juu ya kutokuwepo kwa nia ya dhati ya Serikali kwa kutotenga fedha za kutosha au kuinyima kabisa fedha za miradi ya maendeleo na kuifanya isimame pale ilipo na kutosonga mbele hata kwa hatua moja.

3.0 UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha unaoishia Juni 30, 2015, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo mbalimbali hasa katika nyanja zifuatazo:-

- (vii) Uanzishwaji wa Mfuko wa Pensheni kwa Wazee.
- (viii) Migogoro ya Wafanyakazi.

- (ix) Ukuzaji wa Ajira kwa Vijana Nchini.
- (x) Ufuatiliaji wa masuala yanayohusu Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA).
- (xi) Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) itekeleze masuala mbalimbali ya kijamii na kiuchumi.
- (xii) Uanzishwaji wa Idara/Kurugenzi ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza ushauri wa Kamati kwenye maeneo ambayo bado hayajafanyiwa kazi.

4.0. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA KWA FEDHA 2015/2016

4.1 Makadirio ya Ukusanyaji wa Mapato

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha uliopita, naomba sasa nizungumzie makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 nikianza na makadirio ya ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilitarajia kukusanya jumla ya Shilingi milioni 9.606 kama maduhuli. Hata hivyo hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha Shilingi milioni 3.12 na hivyo kutokusanya kiasi cha shilingi milioni 6.486 sawa na asilimia 67.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi bilioni saba milioni mia nne themanini na nne laki tatu thelathini na nne **(7,484,334,000/=)** kama maduhuli. Hili ni ongezeko la Shilingi bilioni saba milioni mia nne sabini na nne laki saba ishirini na nane **(7,474,728,000/=)**. Vyanzo vya mapato haya ya Wizara ni pamoja na vibali vya kazi kwa wananchi wasio Watanzania na ada kutoka kwa Wakala wa Ajira Binafsi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza sana Wizara hii kwa kupata chanzo hiki kipyacha mapato.

4.2 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Wizara imetengewa jumla ya Shilingi bilioni kumi na nane milioni mia mbili themanini laki moja thelathini na sita elfu **(18,280,136,000/=)**, kati ya fedha hizo Shilingi bilioni kumi na nne milioni mia saba ishirini na tano na arobaini na moja elfu **(14,725,041,000/=)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (OC) na Shilingi bilioni nne milioni mia moja hamsini na nane themanini na tisa elfu **(4,158,089,000/=)** kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi.

4.3 Makadirio ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016, Wizara inatarajia kutumia kiasi cha Shilingi bilioni ishirini **(20,000,000,000/=)** kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyopewa kipaumbele katika Miradi ya Maendeleo kwa mwaka ujao wa fedha 2015/2016 ni pamoja na:-

- (i) Kukuza ajira kwa vijana,
- (ii) Kuwezesha Ukuzaji Ujuzi Nchini

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua ufinyu wa bajeti ya Serikali, hata hivyo, inapongeza sana Serikali kwa kutenga kiasi hicho. Aidha, baada ya kufanya uchambuzi wa bajeti ya miradi, Kamati imebaini kuwa bado ni ndogo ikilinganisha na wimbi kubwa la vijana waliopo nchini ambao hawana ajira.

Kamati inasikitishwa kwa kitendo cha Serikali kutenga bajeti ndogo kwa Wizara hii bila kujali umuhimu wa Wizara hasa katika kukuza ajira kwa vijana ukizingatia hatari inayoweza kuligharimu Taifa kwa kuwa na vijana wengi wasio na ajira.

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia na kuichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na maombi ya fedha yanayojumuisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

i. Uanzishwaji wa Mfuko wa Pensheni kwa Wazee

Mheshimiwa Spika, nikianza na uanzishwaji wa Mfuko wa Pensheni ya Wazee. Kwa miaka mingi sasa wazee wamekuwa wakielezwa kuwa kundi muhimu

katika jamii nyingi duniani na hata kwenye jamii yetu. Kutokana na umuhimu wao ndiyo maana Serikali nyingi duniani hasa za mataifa yaliyoendelea yamekuwa yakiwatengea bajeti.

Thamani ya wazee imekuwa kubwa nchini kwetu kwa miaka mingi na ndiyo maana Serikali iliamua kutunga Sera ya ya Wazee.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyoitoa katika Bunge lako Tukufu tarehe 12 Mei, 2015, alitambua mchango wa wazee na umuhimu wao kama hazina na chemchemi ya busara katika jamii katika kuhimiza maadili, malezi bora, usalama na kuwa washauri wakuu katika masuala mengine muhimu ya kitaifa hasa katika kipindi hiki ambacho jamii inapitia mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kiutamaduni.

Kamati inakubaliana na Mheshimiwa Waziri Mkuu juu ya ukweli huu lakini inahoji kwamba kama Serikali inaona wazee ni sehemu muhimu sana katika jamii; je, inashindwa vipi kuunda Mfuko wa Pensheni ya Wazee?

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za sensa ya watu na makazi za mwaka 2012, idadi ya wazee nchini Tanzania kwa sasa imefikia 5,056,825 kati ya watu takriban milioni 49. Hii ni sawa na kusema kwamba, idadi ya wazee ni sawa na asilimia 11 ya idadi ya watu wote nchini Tanzania. Idadi hii si ya kuiuuzia hata kidogo. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikipuuzia kutatua matatizo mbalimbali ya wazee.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 Kamati ilishauri Serikali ikamilishe mchakato wa uanzishwaji wa Pensheni ya Wazee ili waweze kuboresha hali zao za kimaisha. Wizara imeiarifu Kamati kuwa imekamilisha Rasimu ya Mapendekezo ya Kuanzisha Pensheni ya Wazee na kupanga jinsi utekelezaji wake utakavyokuwa. Hata hivyo, uhalisia wa utekelezaji unaonekana kuwa mgumu kutokana na ukomo wa bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 ambapo zimetengwa Shilingi milioni 41 wakati mahitaji halisi yaliyopendekezwa ni Shilingi bilioni 136. Kiwango hiki ni sawa na asilimia 3 ya mahitaji halisi. Asilimia hii ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, Kamati imesikitishwa na majibu ya Serikali kwamba inaendelea kujifunza kutoka TASAF. Kamati inashindwa kuelewa nia thabiti ya Serikali kwa kuwa hata katika taarifa ya Kamati hii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Kamati ilipokea majibu ya Serikali kuendelea kujifunza kutoka maeneo, idara na sekta mbalimbali za Serikali ndani na nje ya nchi. Kamati inapenda kueleza wasiwasi wake kuhusu utekelezaji wa upatikanaji wa Pensheni ya Wazee kwa sababu, takriban muda wa miaka mitano mfululizo Kamati imekuwa ikishauri juu ya kuwapatia Wazee Pensheni bila mafanikio yoyote mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutilia maanani suala hili la Pensheni ya Wazee na kuanzisha Mfuko wa Pensheni ya Wazee.

ii. **Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA)**

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) imekuwa ikisimamia utekelezaji wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Namba 6 ya mwaka 2004. Aidha, Tume imekuwa ikiratibu migogoro yote ya kikazi inayowasilishwa kwake ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wafanyakazi sehemu za kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ilitengewa kiasi cha Shilingi bilioni nne milioni mia nane thelathini na saba thelathini elfu mia nane **(4,837,030,800/=)** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake. Kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi imetengewa kiasi cha Shilingi bilioni nne milioni fisini na saba hamsini na nne elfu **(4,097,054,000/=)**. Ni wazi kuwa kwa bajeti hii ndogo bado Wizara itaendelea kuathiri utekelezaji wa majukumu ya Tume hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Tume ilipokea na kusajiri migogoro 6,776, katika Mwaka huo huo (2014/2015) Tume ilishughulikia migogoro 4,141. Aidha, ikilinganishwa migogoro iliyopokelewa kwa mwaka na idadi ya migogoro iliyoshughulikiwa na mwaka utaona kuna ongezeko kubwa la migogoro ambayo inahitaji fedha na rasilimali watu ili kuweza kushughulikiwa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake kamati imebaini kuwa uwezo wa CMA kufanya kazi unazidi kupungua kutokana na kiasi cha fedha inachotengewa ukilinganisha na idadi ya kesi zinazopokelewa na kusajiriwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Kamati inashauri kuwa Serikali iitazame tena Tume hii kwa kuwaongezea bajeti ili Tume iweze kutenda kazi yake ya kuwasaidia wananchi.

iii. **Mgogoro wa wafanyakazi katika sekta ya madini**

Mheshimiwa Spika, suala la migogoro ya muda mrefu katika sekta ya madini nchini ni miongoni mwa migogoro inayolisumbua taifa. Migogoro hiyo ni pamoja na mgogoro kati ya wafanyakazi zaidi ya 200 na uongozi wa Mgodu wa *African Barrick Bulyanhulu*. Kamati iliwahi kupata fursa ya kukutana na wawakilishi wa wafanyakazi wa Mgodu wa *African Barrick Bulyanhulu* na kuzungumza nao, pamoja na mambo mengine, suala la kuachishwa kazi bila kupimwa afya zao kama sheria inavyoelekeza, walililalamikia sana.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Wizara kupitia OSHA, kati ya wafanyakazi zaidi ya 250 wa Bulyankhulu walioachishwa kazi mwaka 2007, wafanyakazi 79 tu ndio waliopimwa afya zao mara baada ya kuachishwa kazi kama sheria inavyotaka. Aidha, kati ya wafanyakazi waliorudi kazini baada ya mgomo na kugundulika kupata athari za kiafya baadaye na kuachishwa kazi, ni wafanyanyakazi 10 tu ndio walipimwa afya zao

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Chama cha Wafanyakazi wa Migodi (TAMICO) kuwabaini wafanyakazi ambao hawajapimwa afya zao kwa idadi kamili ya wafanyakazi hao na kama ikibainika wana matatizo ya kiafya, kama inavyobainishwa na sheria walipwe haki zao endapo watahindwa kuendelea na kazi.

iv. **Mgogoro wa Wafanyakazi wa mabasi ya abiria.**

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi wa Machi na mwezi Aprili, 2015, kumekuwa na migomo ya madereva wa mabasi ya abiria hapa nchini. Migomo hii imekuwa na athari kubwa sana kwa kuwa imesababisha kazi nyingi za uzalishaji kusimama. Sababu za migomo hii ni pamoja na madereva kutokuwa na mikataba ya ajira, mpango wa Serikali wa kuwataka madereva wa mabasi ya abiria kwenda shule kila wanapotaka kujaza maombi ya kupata leseni mpya (*license renewal*). Aidha, madereva wanailalamikia Serikali kwa kushindwa kutatua kero zao za ajira ambazo wamekuwa wakizitoa mara kwa mara bila kupata ufumbuzi wowote.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kukaa chini na kuangalia kwa undani suala hili na kulipatia ufumbuzi wa kudumu.

v. **Ajira kwa vijana**

Mheshimiwa Spika, suala la ajira kwa vijana limekuwa ni changamoto kubwa inayolisumbua taifa. Kwa muda mrefu sasa Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kupanga bajeti ya kutosha kwa Wizara ya Kazi na Ajira ili kuiwezesha Wizara hii kufanya kazi ipasavyo na kuwawezesha vijana kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Hotuba yake aliyoitoa kwa Bunge lako Tukufu tarehe 12 Mei, 2015 alikiri wazi kuwa, upatikanaji wa ajira bado ni changamoto kubwa inayowakabili vijana, si tu nchini kwetu bali duniani kote. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, idadi ya Vijana nchini ni Milioni 16.2, sawa na asilimia 35.1 ya Watanzania wote. Takwimu hizo zinabainisha kuwa, Vijana walioajiriwa katika Sekta ya Umma ni 188,087, walioajiriwa katika Sekta Binafsi ni Milioni 1.03. Hivyo, sehemu kubwa ya

vijana takriban milioni 15 wamejiajiri katika shughuli za kilimo, mifugo, uvuvi na biashara ndogo ndogo ambako hata hivyo hawajaandaliwa mazingira rafiki.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu hizi inaonesha wazi kuwa Serikali imeshindwa kuwasaidia vijana. Katika hali ya kawaida vijana milioni 15 kati ya milioni 16.2 kujiajiri wenyewe ni kuongeza mzigo katika kunyang'anyana rasilimali chache zinazoshindwa kuendelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Vijana wengi wanakabiliwa na changamoto ya tija ndogo kwenye uzalishaji na biashara kutokana na matumizi ya teknolojia duni, ukosefu wa mitaji, miundombinu ya uwekezaji mdogo mdogo katika ngazi za awali za ujasiriamali na uwekezaji na elimu ya ujasiriamali. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imekuwa ikitoa elimu ya ujasiriamali na mikopo kwa vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na mifuko mingine ili kuwawezesha kuanzisha au kupanua miradi yao ya uzalishaji mali. Hata hivyo, Mfuko huu wa Maendeleo ya Vijana hautengewi asilimia 5 kutoka Halmashauri na Serikali kuu kama inavyotakiwa. Athari ya kutotengwa kwa asilimia 5 kutoka katika kila Halmashauri inasababisha vijana kushindwa kukabiliana na changamoto zinazowakabili.

Mheshimiwa Spika, Kamati inendelea kuishauri Serikali kuja na mpango mkakati utakaonesha Serikali itakavyowezesha kuwepo mazingira mazuri na bora katika kutengeneza ajira binafsi na za kijamii kwa ajili ya vijana nchini. Kamati inaamini hili linawezekana.

(vi) **Kuanzisha idara ya Hifadhi za Jamii Wizarani.**

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza sana Wizara kwa kuweza kuanzisha Idara ya Hifadhi za Jamii kama idara inayojitegemea ndani ya Wizara. Kamati ina imani kubwa kwamba kuwepo kwa Idara ya Mashirika ya Hifadhi ndani ya Wizara ya Kazi na Ajira kutasaidia sana kutatua migogoro na mambo mengine madogo madogo yanayojitokeza katika mashirika haya. Hata hivyo, Idara hii haijajitosheleza kabisa ki-rasilimali na hivyo uwezo wake kutekeleza majukumu kuwa mdogo. Kamati inashauri Serikali kuiongezea bajeti Wizara hii ili iweze kuiimarisha idara hii muhimu.

(vii) **Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA)**

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA). Hii ni taasisi inayosimamia na kudhibiti masuala yote ya hifadhi ya jamii na kuishauri Serikali ipasavyo juu ya uimarishaji na uboreshaji wa sekta hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhika na utekelezaji wa maoni yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kwa Mamlaka ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuiboresha taasisi hii ili iweze kuendelea kuisimamia Mifuko ya Hifadhi za Jamii kwa ufanisi zaidi.

(viii) **Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)**

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza NSSF kwa kuendelea kuwahudumia wateja wake kwa ufanisi mkubwa. Pamoja na pongezi hizo, Kamati inaushauri Mfuko huu kuweka mkakati wa kuongeza juhudi za kutoa elimu hasa kwa wakulima wafugaji na watu wengine wasio katika ajira rasmi ili waweze kuona umuhimu wa kujiunga kwenye mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliirifiwa kuwa katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 NSSF ilikuwa katika majadiliano na Ofisi ya Bunge kwa ajili ya kuingia mkataba wa ujenzi wa Ofisi za Wabunge katika Majimbo ya Uchaguzi nchini. Jambo hili liliungwa mkono na Kamati kutokana na umuhimu wake. Hata hivyo utekelezaji wa jambo hili haujaleta matumaini. Kamati inashauri jambo hili lipewe umuhimu na lifanywe kwa haraka.

(ix) **Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA)**

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inashuhudia ongezeko kubwa la uwekezaji kutoka kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Uwekezaji huu unakwenda pamoja na ajira mbalimbali kwa Watanzania hali ambayo inachangia pia kuwepo ongezeko la matatizo ya afya za wafanyakazi. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) umepanga kutekeleza kazi kadhaa ikiwa ni pamoja na kufanya kaguzi 41,000 maalumu na za kawaida kuhusu afya mahali pa kazi. Aidha, Wakala katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 unatarajia kupima afya za wafanyakazi 65,000 katika Sehemu mbalimbali za kazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri upimaji huu ufanyike mapema pamoja na kuwabaini waliokuwa wafanyakazi wa mgodi wa Bulyakhulu ambao wamekuwa wakilalamikia suala hili kwa muda mrefu sasa.

Kamati pia inashauri kuwa kaguzi hizi zifanyike kwa kina na kila mara ili kubaini upungufu uliopo katika sehemu hizo ili kulishughulikia ipasavyo tatizo hili na hivyo kuwa sehemu ya motisha kwa watumishi kwa kujali afya zao na usalama katika maeneo yao ya kazi.

Mheshimiwa Spika, ingawa ni jukumu la waajiri na waajiriwa kuhakikisha afya na usalama wao mahali pa kazi, bado Serikali ina wajibu wa kuhakikisha inaweka viwango vya usalama na kusimamia kikamilifu utekelezwaji wake ili kunusuru

afya za wananchi na hivyo kukuza kipato cha wananchi na kulinda ukuaji wa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa Wakala wa Usalama Mahala pa Kazi (OSHA) uandae mwongozo utakaotumika katika kuwaongoza wafanyakazi kumkumbusha mwajiri juu ya haki zao za kiafya kila mara, na kuelimisha wananchi juu ya kujua haki zao za kiafya ambazo zinapaswa kutolewa na mwajiri mahala pa kazi. Mwongozo huo upelekwe kwa kila chama cha wafanyakazi kila mahali lilipo tawi la chama hicho.

Mheshimiwa Spika, pamoja na OSHA kuandaa kanuni Kamati inaisisitizia Serikali kuendelea kutoa elimu kuhusiana na sheria, kanuni na taratibu za afya na usalama mahali pa kazi na kusimamia utekelezaji wake kwa nguvu zote ili kuweza kuliokoa taifa la Tanzania kwa miaka ijayo.

6.0 MWISHO

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia maelekezo ya mara kwa mara yaliyonisaidia kuongoza Kamati hii katika kutekeleza majukumu yake. Niwapongeze pia Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa namna ambavyo wanavyokusaidia kutekeleza majukumu yako.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Kazi na Ajira - Mheshimiwa Gaudencia Mugosi Kabaka, (Mb), Naibu Waziri - Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga, (Mb), Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu Erick Francis Shitindi na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa wanaoipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Kamati pia kwa michango yao ya kina iliyosaidia kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Said Mohamed Mtanda, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Mohamed Said Mohamed, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Kiumbwa Makame Mbaraka, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Mary Pius Chatanda, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Moza Abedi Saidy, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Dkt Maua Abeid Daftari, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Juma Othman Ali, Mb - Mjumbe

11. Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Salum Khalfan Barwany, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Nassib Suleiman Omary, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Salvatory Naluyaga Machelemi, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Jaddy Simai Jaddy, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Rose Kamili Sukum, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Rosemary Kisimbi Kirigini, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Mustafa Haidi Mkulo, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Joshua Samweli Nassari, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Ridhiwani J. Kikwete - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashillilah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Charles Mloka na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Emmanuel Mmidi na Ndugu Ruth Makungu kwa ushauri na kuandaa taarifa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kumaliza kwa kuunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati Maendeleo ya Jamii; Mwakilishi wake, Mheshimiwa Agnes Hokororo, dakika 20.

MHE. AGNESS E. HOKORORO (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kabla sijaanza kusoma Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, naomba nichukue fursa hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kusimama mahali hapa nikiwa mzima wa afya njema.

Pili, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Mtwara hasa kupitia Chama cha Mapinduzi kwa kuendelea kushirikiana nami pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano mkubwa walionipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kibunge. Nawaahidi kuendelea kushirikiana nao na tutaendelea kufanya kazi kwa pamoja kuhakikisha Mtwara yetu itakuwa kuchele mpaka ngwe! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na Kanuni ya 117(11) za Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba kuchukua fursa hii kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu na kwa familia ya marehemu Mheshimiwa Capt. John Damian Komba aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, aliyefariki mwezi Februari, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Kamati itamkumbuka kwa mchango wake mkubwa aliutoa katika kuendeleza Taifa hili. Bwana ametoa na Bwana ametwaa, jina lake lihimidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilikutana na Wizara tarehe 30 Aprili, 2015 Jijini Dar es Salaam na kupokea taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu na malengo yaliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2014/2015, pamoja na kujadili bajeti iliyohusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Aidha, Kamati ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Maagizo ya Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoeleza mtoa hoja, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara ilipangiwa bajeti ya Shilingi bilioni 29.4. Kati ya fedha hizo, Sh. 12,818,434,000/= zilikuwa ni fedha za mishahara na Shilingi bilioni 7.7 ni matumizi mengineyo na Shilingi bilioni 8.9 ni kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2015 Wizara ilikuwa imepokea Shilingi bilioni 3.1 ikiwa ni sawa na asilimia 40 ya bajeti ya matumizi mengineyo. Aidha, katika fedha za miradi ya maendeleo, hadi Aprili, 2015 Wizara ilikuwa imepokea Shilingi shilingi bilioni mbili na milioni thelathini na nane ikiwa ni sawa na asilimia 22.8 ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ambapo Shilingi bilioni 1.7 ni fedha za ndani na Shilingi milioni 338.6 ni fedha za nje. Uchambuzi wa Kamati umeelezewa kwa mchanganuo zaidi katika jedwali namba moja, ukurasa wa tatu wa taarifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wa Bajeti, Kamati imebaini kwamba miradi ya maendeleo haikupewa kipaumbele kabisa. Kamati inaona kwamba hali hii inaathiri sana ustawi wa shughuli za kijamii zinazosimamiwa na Wizara. Aidha, katika mwaka wa fedha 2014/2015 miradi iliyopangwa kutekelezwa na kupangiwa bajeti ilikuwa ni pamoja na:-

- (a) Ujenzi na Ukarabati wa jengo Makao Makuu ya Wizara;
- (b) Programu ya Sekta ya Maendeleo ya Elimu;
- (c) Ulinzi na Ushiriki wa Watoto;

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(d) Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi;

(e) Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii;

(f) Utetezi na Maendeleo ya Jamii;

(g) Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi (Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake);

(e) Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi (Benki ya Wanawake); na

(i) Uhai na Maendeleo ya Mtoto.

Mheshimiwa Spika, miradi yote hiyo pamoja na ile ambayo haikutajwa hapo juu ikilinganishwa na fedha iliyotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Wizara hii ni ndogo hali ambayo ilisababisha miradi mingi ya msingi ya maendeleo kutotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutopatikana kwa fedha hizo, Kamati inaishauri Serikali ikamilishe utoaji wa fedha hizi kwa kipindi kilichosalia ili Wizara iweze kutekeleza majukumu iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaoisha Juni 30, 2015, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo mbalimbali, hususan kwenye maeneo yafuatayo:-

(1) Kuongeza fedha za ndani kwenye miradi ya maendeleo;

(2) Serikali kurudisha mfumo wa zamani wa kutumia fedha inazopata (*retention at source*) kwa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vya Maendeleo ya Wananchi;

(3) Wizara kwa kushirikiana na TANESCO kufanya tathmini ya gharama za kuingiza umeme wa Gridi ya Taifa katika majengo ya vyuo ambavyo havina umeme;

(4) Kuvipatia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vyombo vya usafiri;

(5) Wizara iharakishe upatikanaji wa hatimiliki katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Wananchi;

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(6) Serikali kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya kutoa ajira moja kwa moja na kuajiri wataalamu wa Maendeleo ya Jamii wanaomaliza Vyuo;

(7) Wizara kupeleka Muswada wa Sheria Bungeni kwa ajili ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kuwa Taasisi ya Elimu ya Juu;

(8) Kufanya marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971; na

(9) Asilimia tano ya fedha za maendeleo ya mfuko wa wanawake ziende katika Mfuko wa Wanawake kupitia Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa.

Hata hivyo, kuna maeneo ambayo bado hayajafanyiwa kazi. Maeneo hayo ni Halmashauri kutenga asilimia tano ya fedha za maendeleo ya Mfuko wa Wanawake, upatikanaji wa hatimiliki katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971. Kamati inapenda kujua, kwa nini Serikali imeshindwa kutekeleza maagizo haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijulishwa kuwa katika Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 1.6 kutokana na ada za wanafunzi kutoka katika vyuo vinane vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Uyole, Rungemba, Mlale, Misungwi, Ruaha, Mabughai na Monduli na vyanzo vingine kama ada za usajili wa NGOs na uzaji wa zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijulishwa kuwa ili Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha wa 2015/2016, Wizara imetengewa jumla ya Shilingi bilioni 31.4.

Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 11.38 thelathini na nane ni mishahara; Shilingi milioni 10.9 ni miradi ya maendeleo; na Shilingi bilioni 9.4 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Aidha, kati ya fedha za miradi ya maendeleo, Shilingi bilioni nane ni fedha za ndani na Sh. 2,923,419,650/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yaliyopewa kipaumbele kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ni pamoja na:-

(i) Kutoa msukumo wa kuwezesha na kuwaendeleza wanawake kwa kuwajengea uwezo wa kutekeleza Ajenda ya Maendeleo ya Afrika Tunayoipenda (*Agenda 2063 The Africa We Want*);

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(ii) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitatu wa Kuzuia na Kupambana na Ukatili dhidi ya Watoto pamoja na Ukatili wa Kijinsia ikiwemo kukabiliana na kutokomeza ukeketaji wa wanawake na hivyo kukuza ustawi wa jamii;

(iii) Kuanza kutumia mfumo wa ufuatiliaji wa Tathmini kuhusu utekelezaji wa Sera, Mikataba, Programu na Mipango ya Wizara na Taifa;

(iv) Kuondoa migongano baina wananchi wanaozunguka Vyuu na Vyuu vya Maendeleo ya Wananchi na Vyuu vya Maendeleo ya Jamii kwa kupima na kuchora ramani na kuvipatia hatimiliki Vyuu vyenye migogoro ya ardhi;

(v) Kuendelea na ukarabati wa majengo ya Vyuu vya Maendeleo ya Wananchi na Vyuu vya Maendeleo ya Jamii;

(vi) Kuvipa umeme Vyuu vya Maendeleo ya Wananchi; Bunguri, Ulembwe, Rubondo, Msingi, Mwanahala na Malya; na

(xvii) Kulipa madeni ya watumishi, wazabuni na makandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mtiririko wa bajeti ulivyo, kwa mara nyingine Kamati inasikitishwa na bajeti ndogo inayotengwa kwa Wizara hii kila mwaka bila kujali umuhimu wa Wizara katika kuimarisha masuala yote yanayohusu maendeleo ya jamii, usawa wa jinsia, haki za watoto na ustawi wa familia.

Hata hivyo, licha ya Bunge kuidhinisha fedha kwa Wizara hii, bado fedha hizo zimekuwa hazitolewi kwa wakati na wakati mwingine hazipelekwi kabisa. Aidha, bajeti hii ndogo inaathiri uwezo wa Wizara katika kutekeleza vipaumbele ilivyojiwekea katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nitumie fursa hii kutoa maoni na ushauri wa Kamati katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kuwa Bajeti inayotengwa kwa ajili ya Wizara kila mwaka ni ndogo, bado kumekuwa na ucheleweshaji wa fedha hizo kutoka Hazina. Hali hii imekuwa ikiathiri Wizara katika kutekeleza majukumu yake na hasa miradi ya maendeleo.

Katika mwaka wa fedha unaomalizika Juni 30, 2015 hadi kufikia mwezi Aprili, 2015, Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha Shilingi bilioni mbili ikiwa ni sawa na asilimia 22. Shilingi bilioni 8.9 ya bajeti za fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 1.7 ni fedha za ndani na Shilingi

milioni 338.6 ni fedha za nje. Aidha, hali hiyo imeathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya wizara kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa, kiasi cha fedha kilichosalia kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kinapatikana na kupelekwa Wizarani. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuainisha vyanzo vipya vya mapato na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ili kuweza kutenga fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo na siyo kama ilivyo sasa ambapo fedha nyingi za miradi ya maendeleo zinategemea vyanzo vya nje na ambavyo upatikanaji wake umekuwa siyo wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo Wananchi nchini vimekumbwa na migogoro ya ardhi na vipo vyuo ambavyo havina hatimiliki ya ardhi.

Aidha, kutokana na vyuo hivyo kukosa umiliki wa maeneo hayo, wananchi wamevamia na kufanya shughuli za kilimo na ujenzi wa makazi. Kwa mfano, katika Chuo cha Wananchi Rungemba Mkoani Iringa, kuna mgogoro kati ya wananchi wawili na Chuo. Wananchi hao wamejenga makazi ya kudumu ndani ya eneo la Chuo na hawataki kuondoka katika eneo hilo na kudai kuwa ni haki yao kuwepo katika eneo hilo. Aidha, mchakato wa kukipatia Chuo hicho hati umechukua muda mrefu na hivyo kusababisha Chuo kushindwa kupanga mipango yake ya muda mrefu na mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kufanya utafiti wa umiliki wa maeneo na majengo yote ya Vyuo vya Wananchi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ili kuwa na taarifa sahihi za umiliki.

Aidha, Kamati inazidi kuishauri Serikali kuharakisha upatikanaji wa hati hizo licha ya kuwa Kamati imekuwa ikitoa ushauri wake mara kwa mara pasipo Serikali kutekeleza. Pia, Kamati inashauri kuwa utafutwe muafaka baina ya vyuo na wananchi ili wananchi waliovamia eneo la Chuo waondoke bila kuleta athari ya ushirikiano kwa wanaozunguka eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu mkubwa wa wataalamu wa Maendeleo ya Jamii katika kuharakisha maendeleo na kutatua migogoro inayoendelea kujitokeza, bado Sekta ya Maendeleo ya Jamii ina upungufu mkubwa wa Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii katika ngazi za Wilaya na Kata.

Kwa mfano, kwa sasa kuna jumla ya Kata 3,339 nchini. Jumla ya Maafisa Maendeleo ya Jamii waliopo katika Kata ni 1,310, hivyo kufanya Kata kuwa na upungufu wa wataalamu 2,029, sawa na asilimia 61 ya mahitaji ikiwa kila Kata

itapata Afisa Maendeleo ya Jamii mmoja, kama Sera ya Maendeleo ya Jamii inavyosisitiza kuwa na mtaalamu angalau mmoja katika kila Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu huo na ili kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, iangalie uwezekano wa kuwaajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii moja kwa moja kutoka vyuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake Tanzania ni Kampuni ya Umma inayomilikiwa kwa kiasi kikubwa na Serikali ya Tanzania na pia ina wanahisa wadogo wanaokadiriwa kufikia 160. Benki hii ilianzishwa kwa lengo la kuwakomboa wanawake kiuchumi kwa kuwawezesha kupata mikopo kwa riba nafuu na kwa ajili ya kukuza mitaji ya biashara.

Hata hivyo, lengo hilo linaonekana kutofikiwa kikamilifu katika siku za karibuni hasa kutokana na ukweli kwamba kiwango cha fedha ambacho kinatolewa kwa ajili ya benki kama sehemu ya kukuza mtaji wake, ni kidogo sana ikilinganishwa na matarajio ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete akielezea madhumuni ya kuanzishwa kwa Benki hii, alisema kwamba Serikali itatoa jumla ya Shilingi bilioni mbili kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo ili kuiwezesha Benki hii kuimarika kimtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 na mwaka 2011/2012 Benki ya Wanawake ilipokea kiasi cha Shilingi bilioni mbili kama ilivyoelezwa. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2012/2013 kiasi cha Shilingi bilioni 1,300 tu ndiyo kilitolewa na kiasi cha Shilingi milioni 700 bado hakijatolewa na Serikali. Kipindi cha mwaka 2013/2014 kiasi cha Shilingi milioni 450 tu ndiyo kimetolewa na Serikali na kiasi cha Shilingi bilioni 1.5 bado hakijatolewa mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2014/2015 hakuna fedha yoyote iliyopelekwa na kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Shilingi bilioni 4.5 zimeombwa kwa ajili ya Benki ya Maendeleo ya Wanawake (TWB) na Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Benki ianzishwe mpaka sasa ni kiasi cha Sh. 8.7 tu ndicho kilichopo kama mtaji. Kutokana na changamoto ya mtaji, Benki imekuwa ikitafuta fursa mbalimbali za kupata fedha za kujiendesha na kutanua mtaji wake ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kuuza hisa zake kupitia Soko la Hisa la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imearifiwa na Wizara kuwa kwa mwaka 2015 Benki ya Wanawake imetengeneza faida ya Shilingi milioni 141 kabla ya kodi. kwa hiyo, Menejimenti na Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya Wanawake wanaona mwaka 2015 ni kipindi muafaka cha kuanza mchakato wa kuuza hisa ili kukuza mtaji wa Benki na kuiwezesha Benki kujiendesha pasipo kutegemea mtaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kutoa kiasi chote cha fedha ambacho hakikupelekwa kwenye Benki ya Wanawake ili kutimiza azma ya kauli ya Mheshimiwa Rais ya kuifanya Benki hii kujiendesha kibiashara na kutoa fursa kwa wanawake wengi nchini kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati inashauri Serikali kutoa fedha zote walizoomba mwaka 2015/2016 ili Benki ya Wanawake Tanzania iweze kuorodhesha hisa zake katika Soko la Hisa la Dar es Saalam ili ziweze kuuzwa na hivyo kuongeza mtaji utakaosaidia kufungua matawi nchi nzima na kuwawezesha wanawake wote Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1993 Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto, ilianzisha mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kwa lengo la kuwawezesha wanawake kiuchumi kwa kuwapatia mikopo. Mfuko huo ulianzishwa kwa Tamko la Serikali la Mwaka 1993 na Bunge lilipitisha maazimio kwa Sheria ya *The Exchequer and Audit Ordinance* ya mwaka 1961.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la mfuko ni kutoa mikopo midogo midogo kwa wanawake wajasiriamali ili kuwawezesha kiuchumi. Chanzo kikuu cha mapato ya mfuko ni kutoka Serikali Kuu (Wizara ya Fedha) pamoja na Serikali za Mitaa, ambapo kila Halmashauri inatakiwa kuchangia asilimia tano ya mapato kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya mfuko huu na kuzitoa kwa wakati ili kuwawezesha wanawake kujiendeleza katika nyanja mbalimbali kama za kilimo na biashara na kujikomboa kutoka katika lindi la umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa umahiri na busara zako katika uendeshaji wa Vikao vya Bunge. Nawapongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi ambavyo mnatekeleza majukumu yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumshukuru Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto - Mheshimiwa Sophia Mathayo Simba, Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana - Naibu Waziri wake; Katibu Mkuu wa Wizara - Ndugu Anna T. Maembe; Naibu Katibu Mkuu - Ndugu Nuru H. M. Milao na Wakurugenzi; Wakuu wa Idara; Wakuu wa Vitengo; na Taasisi pamoja na Watumishi wote

Wizara kwa ushirikiano wao mkubwa uliwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge na kwa umuhimu wa pekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Kama wanavyoonekana na kutambuliwa katika kitabu chetu cha hotuba ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas Kashillillah, akisaidiwa na Mkurugenzi wa Kamati za Bunge - Ndugu Charles Mloka, Makatibu wa Kamati - Ndugu Ruth Makungu, Ndugu Emmanuel Mmidi pamoja na Msaidizi kwa ushauri na uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Naomba kuwasilisha. (Makofi)

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na Kanuni ya 117(11) za Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilishataarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake Kamati ilikutana na Wizara (**Fungu 53**) tarehe 30 Aprili, 2015 Jijini Dar es salaam na kupokea taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu na malengo yaliyopangwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na kujadili bajeti iliyohusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Aidha, Kamati ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Maagizo ya Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI YA MWAKA 2014/2015

Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza mtoa hoja, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015, Wizara ilipangiwa bajeti ya Shilingi bilioni ishirini na tisan milioni mia nne hamsini na tatu laki tano tisini na tisa elfu (**29,453,599,000/=**) kati ya fedha hizo Shilingi bilioni kumi na mbili milioni mia nane kumi na nane laki nne thelathini na nne elfu (**12,818,434,000/=**) inajumuisha mishahara na Shilingi bilioni saba milioni mia saba na saba laki sita ishirini na moja elfu (**7,707,621,000/=**) ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Shilingi bilioni nane milioni mia tisa ishirini na saba laki tano arobaini na nne elfu (**8,927,544,000/=**) kwa ajili ya Miradi mbalimbali ya Maendeleo ambapo Shilingi bilioni sita milioni mia tisa na kumi (**6,910,000,000/=**) ni fedha za ndani na Shilingi bilioni mbili milioni kumi na saba laki tano arobaini na nne elfu (**2,017,544,000/=**) ni fedha za nje. Hadi kufikia Machi, 2015 Wizara ilikuwa imepokea Shilingi bilioni tatu milioni mia moja kumi na moja elfu sabini mia tano tisini na moja na senti thelathini na tano (**3,111,070,591.35/=**) sawa na **asilimia 40** ya bajeti ya matumizi mengineyo. Aidha, katika fedha za Miradi ya Maendeleo hadi Aprili, 2015 Wizara ilikuwa imepokea Shilingi shilingi bilioni mbili milioni thelathini na nane laki sita thelathini na nne elfu (**2,038,634,000/=**) sawa na **asilimia 22.8** ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge ambapo Shilingi bilioni moja milioni mia saba (**1,700,000,000/=**) ni fedha za ndani na Shilingi milioni mia tatu thelathini na nane laki sita thelathini na nne (**338,634,000/=**) ni fedha za nje. Uchambuzi wa Kamati umeelezewa kwa mchanganuo zaidi katika jedwali lifuatalo;

Jedwali Namba 1. Uchambuzi wa fedha iliyoidhinishwa na iliyotolewa

Na. Dhima	Bajeti iliyoidhinishwa	%	Fedha iliyotolewa	%
1. mishahara	12,818,434,000	43.5	7,796,097,271	60
2. matumizi mengineyo	7,707,621,000	26.1	3,111,070,591.35	40
3. Miradi ya Maendeleo	8,927,544,000	30.3	2,038,634,000	22.8

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa Bajeti, Kamati imebaini kwamba katika mwaka wa fedha 2014/2015 Miradi ya maendeleo haikupewa kipaumbele kabisa. Kamati inaona kwamba hali hii kama itaendelea itaathiri sana ustawi wa shughuli za kijamii zinazosimamiwa na Wizara.

Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 miradi iliyopangwa kutekelezwa na kupangiwa bajeti ilikuwa ni pamoja na;

- Ujenzi na Ukarabati wa jengo Makao Makuu ya Wizara
- Programu ya Sekta ya Maendeleo ya Elimu

- c) Ulinzi na Ushiriki wa Watoto
- d) Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi
- e) Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii
- f) Utetezi na Maendeleo ya Jamii
- g) Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi (Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake)
- h) Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi (Benki ya Wanawake)
- i) Uhai na maendeleo ya Mtoto.

Mheshimiwa Spika, miradi yote hiyo pamoja na ile ambayo haikutajwa hapo juu ikilinganishwa na fedha iliyotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Wizara hii ni ndogo hali ambayo ilisababisha miradi mingi ya msingi ya maendeleo kutotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutopatikana kwa fedha hizo Kamati inaishauri Serikali ikamilishe utoaji wa fedha hizi kwa kipindi kilichosalia ili Wizara iweze kutekeleza majukumu iliyojipangia kwa Mwaka wa Fedha **2014/2015**.

3.0 UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha unaoisha Juni 30, 2015, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo mbalimbali, hususan kwenye maeneo yafuatayo:-

1. Kuongeza fedha za ndani kwenye miradi ya maendeleo.
2. Serikali kurudisha mfumo wa zamani wa kutumia fedha inazopata (*retention at source*) kwa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vya Maendeleo ya Wananchi.
3. Wizara kwa kushirikiana na TANESCO kufanya tathmini ya gharama za kuingiza umeme wa Gridi ya Taifa katika majengo ya vyuo ambavyo havina umeme.
4. Kuvipatia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vyombo vya usafiri.
5. Wizara iharakishe upatikanaji wa hatimiliki katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Wananchi.
6. Serikali kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya kutoa ajira moja kwa moja na kuajiri wataalamu wa Maendeleo ya Jamii wanaomaliza Vyuo.

7. Wizara kupeleka Muswada wa Sheria Bungeni kwa ajili ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kuwa Taasisi ya Elimu ya Juu.

8. Kufanya marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.

9. Asilimia tano (5%) ya fedha za maendeleo ya mfuko wa wanawake ziende katika mfuko wa wanawake kupitia Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa, hata hivyo kuna maeneo ambayo bado hayajafanyiwa kazi. Maeneo hayo ni, Halmashauri kutenga asilimia 5 ya fedha za maendeleo ya mfuko wa wanawake, upatikanaji wa hati miliki katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kujua kwa nini Serikali imeshindwa kutekeleza maagizo haya.

4.0. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

4.1 Makadirio ya Ukusanyaji wa Mapato

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa katika Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi **bilioni moja milioni mia tisa ishirini na saba laki tatu sabini na nne elfu (1,927,374,000/=)** kutokana na ada za wanafunzi kutoka katika vyuo vinane vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Uyole, Rungemba, Mlale, Misungwi, Ruaha, Mabughai na Monduli na vyanzo vingine kama ada za usajili wa NGOs na uzaji wa zabuni.

4.2 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa ili Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha wa **2015/2016**, Wizara imetengewa jumla ya shilingi bilioni ishirini na tisa milioni mia tatu na nane laki nne hamsini elfu laki mbili arobaini na tano elfu **(29,308,450,245,000/=)** kati ya fedha hizo Shilingi bilioni kumi na nane milioni mia tatu themanini na tano elfu thelathini mia tano tisini na tano **(18,385,030,595/=)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi bilioni kumi milioni mia tisa ishirini na tatu laki bbe kumi na tisa elfu mia sita hamsini **(10,923,419,650/=)** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida Shilingi bilioni kumi milioni mia tatu themanini na nane laki saba kumi na nne elfu **(10,388,714,000/=)** ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi bilioni saba milioni mia tisa tisini na sita laki tatu kumi na sita mia tano tisini na tano **(7,996,316,595/=)** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, kati ya fedha za Miradi ya Maendeleo, shilingi bilioni nane **(8,000,000,000/=)** ni fedha za ndani na shilingi bilioni mbili milioni mia tisa ishirini na tatu laki nne kumi na tisa elfu mia sita hamsini **(2,923,419,650/=)** ni fedha za nje.

Mheshimwa Spika, maeneo yaliyopewa kipaumbele kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ni pamoja na:-

i. Kutoa msukumo wa kuwezesha na kuwaendeleza wanawake kwa kuwajengea uwezo wa kutekeleza Ajenda ya Maendeleo ya Afrika Tunayoipenda (*Agenda 2063 The Africa We Want*);

ii. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitatu wa Kuzuia na Kupambana na Ukatili dhidi ya Watoto pamoja na Ukatili wa Kijinsia ikiwemo kukabiliana na kutokomeza ukeketaji wa wanawake na hivyo kukuza ustawi wa jamii;

iii. Kuanza kutumia mfumo wa ufuatiliaji na Tathmini kuhusu utekelezaji wa Sera, Mikataba, programu na Mipango ya Wizara na Taifa;

iv. Kuondoa migongano baina wananchi wanaozunguka vyo na Vyo vya Maendeleo ya Wananchi na Vyo vya Maendeleo ya Jamii kwa kupima na kuchora ramani na kuvipatia hati miliki vyo vyenye migogoro ya ardhi;

v. Kuendelea na ukarabati wa majengo ya Vyo vya Maendeleo ya Wananchi na Vyo vya Maendeleo ya Jamii;

vi. Kuvipa umeme Vyo vya Maendeleo ya Wananchi-Munguri, Ulembwe, Rubondo, Msingi, Mwanhala na Malya; na

vii. Kulipa madeni ya watumishi, wazabuni na makandarasi.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na mtiririko wa bajeti ulivyo, kwa mara nyingine Kamati inasikitishwa na bajeti ndogo inayotengwa kwa Wizara hii kila mwaka bila kujali umuhimu wa Wizara katika kuimarisha masuala yote yanayohusu maendeleo ya jamii, usawa wa jinsia, haki za watoto na ustawi wa familia.

Hata hivyo licha ya Bunge kuidhinisha fedha kwa Wizara hii, bado fedha hizo zimekuwa hazitolewi kwa wakati na wakati mwingine hazipelekwi kabisa. Aidha, bajeti hii ndogo inaathiri uwezo wa Wizara katika kutekeleza vipaumbele ilivyojiwekea katika mwaka huu wa fedha.

5.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nitumie fursa hii kutoa maoni na ushauri wa Kamati katika maeneo yafuatayo:

a) Bajeti ndogo ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwa Bajeti inayotengwa kwa ajili ya Wizara kila mwaka ni ndogo, bado kumekuwa na ucheleweshaji wa fedha hizo kutoka Hazina. Hali hii imekuwa ikiathiri Wizara katika kutekeleza majukumu yake na hasa Miradi ya Maendeleo. Katika Mwaka wa Fedha unaomalizika Juni 30, 2015 hadi kufikia mwezi Aprili, 2015, Wizara ilikuwa imepokea Shilingi bilioni mbili milioni thelathini na nane laki sita thelathini na nne elfu **(2,038,634,000/=)** sawa na asilimia ishirini na mbili, kati ya Shilingi bilioni nane milioni mia tis ishirini na saba laki tano arobaini na nne elfu **(8,927,544,000/=)** ya bajeti ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni moja milioni mia saba **(1,700,000,000/=)** ni fedha za ndani na shilingi milioni mia tatu thelathini na nane laki sita thelathini na nne elfu **(338,634,000/=)** ni fedha za nje. Aidha, hali hiyo imeathiri utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa kiasi cha fedha kilichosalia kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kinapatikana na kupelekwa. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuainisha vyanzo vipya vya mapato na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ili kuweza kutenga fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo na si kama ilivyo sasa ambapo fedha nyingi za miradi ya maendeleo zinategemea vyanzo vya nje ambavyo upatikanaji wake umekuwa sio wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 imebainika kuwa Bajeti ya mwaka huu imepungua kwa kiasi cha Shilingi milioni mia mbili arobaini na tano laki moja arobaini na nane mia saba hamsini na tano **(245,148,755/=)** .

b) Vyuvo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuvo vya Maendeleo ya Wananchi

i. Hatimiliki

Mheshimiwa Spika, Vyuvo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuvo vya Wananchi nchini vimekumbwa na migogoro ya ardhi na vipo vyuo ambavyo havina hatimiliki ya ardhi. Aidha, kutokana na vyuo hivyo kukosa umiliki wa maeneo hayo wananchi wamevamia na kufanya shughuli za kilimo na ujenzi wa makazi. Kwa mfano, katika Chuo cha Wananchi Rungemba Mkoani Iringa kuna mgogoro kati ya wananchi wawili na Chuo. Wananchi hao wamejenga makazi ya kudumu ndani ya eneo la chuo na hawataki kuondoka katika eneo hilo na kudai kwamba haki yao kuwepo katika eneo hilo. Aidha, mchakato wa kukipatia chuo hicho hati umechukua muda mrefu na hivyo kusababisha Chuo kushindwa kupanga mipango yake ya muda mrefu na muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kufanya utafiti wa umiliki wa maeneo na majengo yote ya Vyuo vya Wananchi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ili kuwa na taarifa sahihi za umiliki. Aidha, Kamati inazidi kuishauri Serikali kuharakisha upatikanaji wa hati hizo licha ya kuwa Kamati imekuwa ikitoa ushauri wake mara kwa mara pasipo Serikali kutekeleza. Pia, Kamati inashauri kuwa utafutwe muafaka baina ya vyuo na wananchi ili wananchi waliovamia eneo la Chuo waondoke bila kuleta athari ya ushirikiano na wananchi wanaozunguka eneo hilo.

ii. Ajira kwa Wahitimu wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu mkubwa wa wataalamu wa Maendeleo ya Jamii katika kuharakisha maendeleo na kutatua migogoro inayoendelea kujitokeza, bado Sekta ya Maendeleo ya Jamii ina upungufu mkubwa wa wataalamu wa maendeleo ya jamii katika ngazi za Wilaya na Kata. Kwa mfano, kwa sasa kuna jumla ya Kata 3,339 nchini. Jumla ya Maafisa Maendeleo ya Jamii waliopo katika Kata ni 1,310, hivyo kufanya Kata kuwa na upungufu wa wataalam 2,029 sawa na asilimia 61 ya mahitaji ikiwa kila Kata itapata Afisa Maendeleo ya Jamii mmoja kama Sera ya Maendeleo ya Jamii inavyosisitiza kuwa na mtaalamu walau mmoja katika kila Kata. Kutokana na upungufu huo na ili kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, iangalie uwezekano wa kuwaajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii moja kwa moja kutoka vyuoni.

d. Benki ya Wanawake Tanzania

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wanawake Tanzania ni Kampuni ya umma inayomilikiwa kwa kiasi kikubwa na Serikali ya Tanzania na pia ina wanahisa wadogo wadogo wanaokadiriwa kufikia 160. Benki hii ilianzishwa kwa lengo la kuwakomboa wanawake kiuchumi kwa kuwawezesha kupata mikopo kwa riba nafuu na kwa ajili ya kukuza mitaji ya biashara. Hata hivyo, lengo hilo linaonekana kutofikiwa kikamilifu katika siku za karibuni hasa kutokana na ukweli kwamba kiwango cha fedha ambacho kinatolewa kwa ajili ya benki kama sehemu ya kukuza mtaji wake, ni kidogo sana ikilinganishwa na matarajio ya awali. Wakati Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, akielezea madhumuni ya kuanzishwa kwa benki hii, alisema kwamba Serikali itatoa jumla ya shilingi bilioni mbili **(2,000,000,000/=)** kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo ili kuiwezesha benki hii kuimarika kimtaji.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 na mwaka 2011/2012 Benki ya Wanawake ilipokea kiasi cha Shilingi bilioni mbili **(2,000,000,000/=)** kama ilivyoielezwa. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2012/2013 kiasi cha Shilingi bilioni moja milioni mia tatu **(1,300,000,000/=)** tu ndiyo kilitolewa na kiasi cha Shilingi milioni mia saba **(700,000,000/=)** bado hakijatolewa na Serikali. Kipindi cha mwaka 2013/2014 kiasi cha Shilingi milioni mia nne hamsini **(450,000,000/=)**

tu ndiyo kimetolewa na Serikali na kiasi cha Shilingi bilioni moja milioni mia tano hamsini (**1,550,000,000/=**) bado hakijatolewa mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, Mwaka wa Fedha 2014/2015 hakuna fedha yoyote iliyopelekwa na kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 Shilingi bilioni nne milioni mia tano (**4,500,000,000/=**) zimeombwa kwa ajili ya Benki ya Maendeleo ya Wanawake (TWB) na Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake.

Mheshimiwa Spika, tangu Benki ianzishwe mpaka sasa ni kiasi cha shilingi bilioni nane milioni mia saba arobaini na sita elfu hamsini na tatu (**8,746,053,000/=**) tu ndicho kilichopo kama mtaji, na kufuatia Sheria za Benki Kuu ya Tanzania ili Benki iweze kujiendesha kibiashara inapaswa iwe na mtaji wa kuanzia, shilingi bilioni kumi na tano (**15,000,000,000/=**). Kutokana na changamoto ya mtaji, Benki imekuwa ikitafuta fursa mbalimbali za kupata fedha za kujiendesha na kutanua mtaji wake ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kuuza hisa zake kupitia Soko la Hisa la Dar es salaam. (*Dar es Salaam Stock Exchange*).

Mheshimiwa Spika, Kamati imearifiwa na Wizara kuwa mwaka 2015 Benki ya Wanawake imetengeneza faida ya shilingi milioni 141 kabla ya kodi. kwa hiyo, Menejimenti na Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya Wanawake wanaona mwaka 2015 ni kipindi muafaka cha kuanza mchakato wa kuuza hisa ili kukuza mtaji wa Benki na kuiwezesha Benki kujiendesha pasipo kutegemea mtaji kutoka Serikalini. Hata hivyo, hali hii itawezekana tu endapo Serikali itatoa mtaji wa shilingi bilioni tatu zinazombwa katika bajeti ya Serikali kwa mwaka 2015/2016 fedha ambazo zitatumika kuongeza kima cha mtaji wa benki na kugharamia gharama za mchakato wa kuuza hisa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kutoa kiasi chote cha fedha ambacho hakikupelekwa kwenye Benki ya Wanawake ili kutimiza azma ya kauli ya Rais ya kuifanya Benki hii kujiendesha kibiashara na kutoa fursa kwa wanawake wengi nchini kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati inashauri Serikali kutoa fedha zote walizoomba mwaka 2015/2016 ili Benki ya Wanawake Tanzania iweze kuorodhisha Hisa zake katika Soko la Hisa la Dar es Saalam (*Dar es Salaam Stock Exchange*) ili ziweze kuuzwa na hivyo kuongeza mtaji utakaosaidia kuweza kufungua matawi nchi nzima na hivyo kuwawezesha wanawake wa Tanzania kiuchumi na hatimaye kupanua wigo wa huduma zake hadi vijijini.

e. Mfuko Wa Maendeleo Wa Wanawake

Mheshimiwa Spika, mwaka 1993 Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto ilianzisha mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kwa lengo la kuwawezesha wanawake kiuchumi kwa kuwapatia mikopo. Mfuko huo ulianzishwa kwa Tamko la Serikali la Mwaka 1993 na Bunge lilipitisha maazimio

kwa Sheria ya *The Exchequer and Audit Ordinance* ya mwaka 1961 ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2001 na 2004 chini ya Sheria ya Fedha (*Public Finance Act*).

Mheshimiwa Spika, lengo la mfuko ni kutoa mikopo midogo midogo kwa wanawake wajasiriamali ili kuwawezesha kiuchumi. Chanzo kikuu cha mapato ya mfuko huu ni kutoka Serikali Kuu (Wizara ya Fedha) pamoja na Serikali za Mitaa ambapo kila Halmashauri inatakiwa kuchangia asilimia tano ya mapato yake ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu mfuko huu umekuwa ukisuasua kutokana na Serikali kutotenga pesa na asilimia tano kutoka Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya mfuko huu na kuzitoa kwa wakati ili kuwawezesha wanawake kujiendeleza katika nyanja mbalimbali kama za kilimo na biashara na kujikomboa kutoka katika lindi la umasikini.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa umahiri na busara zako katika uendeshaji wa Vikao vya Bunge. Nawapongeza pia Naibu Spika na Wenyevidi wa Bunge kwa jinsi wanavyokusaidia katika kutekeleza majukumu yako.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumshukuru Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto - Mheshimiwa Sophia Mattayo Simba (Mb); Naibu Waziri - Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb); Katibu Mkuu wa Wizara – Ndugu Anna T. Maembe; Naibu Katibu Mkuu Ndugu - Nuru H. M. Milao na Wakurugenzi, Wakuu wa Idara, Wakuu wa Vitengo na Taasisi pamoja na watumishi wote Wizara kwa ushirikiano wao mkubwa uliowezesha Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Said Mohamed Mtanda, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Mohamed Said Mohamed, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Nasib Suleiman Omar, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Mustafa Haidi Mkulo, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Salum Khalfan Barwany, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Kiumbwa Makame Mbaraka, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Salvatory Naluyaga Macheili, Mb- Mjumbe

Nakala ya Mtandao (Online Document)

10. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Moza Abedi Saidy, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Agness Elias Hokororo, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Mary Pius Chatanda, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Juma Othman Ali, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Jaddy Simai Jaddy, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Dkt. Maua Abeid Daftari, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Rose Kamili Sukum, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Joshua Samweli Nassari, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Rosemary Kasimbi Kirigini, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashillilah akisaidiwa na Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndugu Charles Mloka, Makatibu wa Kamati, Ndugu Ruth Makungu, Ndugu Emmanuel Mdidi pamoja na msaidizi wa Kamati Ndugu Mwimbe John kwa ushauri na uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

Said Mohamed Mtanda, Mb

MWENYEKITI

KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII

25 Mei, 2014

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Hokororo. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani Wizara ya Kazi na Ajira, Mheshimiwa Cecilia Paresso, dakika 20.

MHE. CECILIA D. PARESSO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WIZARA YA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani ya Wizara ya Kazi na Ajira kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunilinda na kunitunza ili niweze kulitumikia Taifa langu. Napenda kuishukuru familia yangu kwa msaada mkubwa na uvumilivu hasa ninapokuwa katika shughuli zangu za kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii, kuwashukuru Watanzania wote kwa kupokea na kulea harakati za mabadiliko nchini.

Shukrani hizi pia ziwafikie Wenyekiti wenza wa vyama vinavyounda UKAWA na Makatibu Wakuu viongozi wa UKAWA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru kwa nafasi ya kipekee wananchi wa Wilaya ya Karatu na wananchi na wote wa Mkoa wa Arusha kwa ushirikiano na imani kubwa kwangu wakati nikitokeleza majukumu kama mwakilishi wao. Niliahidi daima nitakuwa mtumishi wa watu, kwa maslahi ya watu na kwa maendeleo ya watu na daima nitabaki kuwa hivyo. Nawashukuru na nawaomba wazidishe imani hiyo kwangu kwani haiwezi kupotea bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Shukrani hizo, napenda kuanza hotuba yangu kwa kunukuu maneno machache kutoka kwa Baba wa Taifa; ningependa Watanzania kuyatafakari hasa kipindi hiki tunapoelekea Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba 2015: “Na hakutakuwa na watu wa kizazi hiki na karne hii ambao watatakiwa kujitoa muhanga kwa ajili ya maisha bora kwa siku zijazo wakakubali, wakati wanaona watu wachache wakiendelea kuneemeka machoni pao bila kujali wakati ujao, wakati wananchi na watoto wao wakiendelea kuishi katika maisha duni na dhalili.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu tumekuwa tukionesha jinsi ambavyo Serikali imekuwa haina mikakati endelevu ya kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira nchini. Aidha, Serikali ya CCM imekuwa ikitumia mikakati ya kupaka mafuta kwa mgongo wa chupa kama nadharia iliyozoeleka kwa nia yenye kuwapumbaza wananchi kwa kuwapa matumaini yasiyokuwa na matokeo chanya juu suala zima la utengenezaji wa ajira hapa nchini na hivyo kulifanya tatizo la ajira kuwa ni wimbo uliozoeleka ndani ya masikio ya Watanzania. Hili ni jambo la aibu kwa nchi iliyojaliwa utajiri mkubwa wa rasilimali na maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere amewahi kutamka maneno yafuatayo, naomba kunukuu: “Amini nawaambieni enyi Waswahili wachache mnaotawala, mnategemea kweli mtawaongoza Watanzania kwa lazima wakati wamepoteza matumaini; na mtegemee kuwa wanasalia wamekaa kimya kwa amani na utulivu?” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo wa uongozi wa mazoea na wa kuongoza na kuamua mambo kwa matukio, ni kuonesha jinsi gani Serikali ya CCM ilivyochooka na kwamba inahitaji kukaa pembeni na kujifunza namna ya kuongoza nchi kwa viwango vya uwajibikaji wenye maslahi mapana kwa jamii ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya CCM imeshindwa kuzioanisha sera, sheria, mikakati na mipango mbalimbali ambayo kwa pamoja ingeweza kutatua matatizo sugu ya ukosefu wa ajira nchini. Ni Serikali hii ambayo imeua

falsafa ya kujitegemea ambayo Baba wa Taifa aliipigania kwa ajili ya watanzania wote. Je, ni kiongozi gani wa CCM atakayeweza kusimama na kusema kuwa Serikali ya CCM imekua mdau nambari moja wa Azimio la Arusha? Je, ni nani kati yenu anayeweza kusema mfumo wa elimu tulionaoleo, unampa mhitimu uwezo wa kujitegemea? Ni nani anaweza kusimama na kueleza mafanikio ya Serikali ya CCM kuhakikisha kuwa kilimo alichokipigania Baba wa Taifa kinatoa ajira kwa makundi yote? (Makofi)

Je, ni nani kati yenu atakayeweza kusimama na kujinasibu kuwa Vyyo Vikuu mlivyojenga kwa fedha za wachangiaji ambao wengi ni wafanyakazi na wakulima wa nchi hii vimemwandaa Mtanzania kukabiliana na changamoto za ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Serikali ya Tanzania inayoongozwa na CCM kuwa na utaratibu wake, hakika huu ni utaratibu wa kushindwa kuendana na mahitaji ya kiuchumi na ya kijamii ya watu wake, utaratibu wa kushindwa kuleta maendeleo kwa watu wake, utaratibu wa kushindwa kuleta maendeleo ya amani kwa watu wake na taratibu nyinginezo zenye kunyonya nguvu za watu wake.

Hivyo basi, Serikali ya UKAWA itakapoingia madarakani imekusudia kudhibiti na kuondoa changamoto hizi kwa kuhakikisha kuwa wananchi wa Taifa hili la Tanzania wanatengenezewa ajira za kutosha, wanaishi na kufanya kazi kwa amani na utulivu, kuondoa umasikini; na kuhakikisha kuwa watu wanaishi kwa uhuru na wanafurahia haki za msingi za kidemokrasia na kwa ufanisi mkubwa.

Pia kuhakikisha kuwa mfumo wa uendeshaji Serikali kiutawala na kisiasa unaendana na maendeleo endelevu ya kiuchumi na zaidi mabadiliko hayo ya kiuchumi yanafikiwa katika nchi hii yenye utajiri mkubwa wa rasilimali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika historia ya sasa, Tanzania imekuwa chini ya utawala wa CCM uliovaa koti la shari, vitisho na mabavu chini ya CCM; na sasa Watanzania wanatambua juu ya matokeo ya utawala wa namna hii. Hata hivyo, tangu uhuru, Watanzania wamekuwa wakiishi kwa pamoja na kujenga urafiki na ushirikiano baina yao, Serikali na watu wa nchi nyingine katika msingi wa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli hiyo ya utawala wa sheria uliovaa koti la shari, vitisho na mabavu, unadhihirishwa pia na kauli za Kiongozi wa nchi alizowahi kuzitoa huko nyuma mwezi Mei, 2010 alisema hivi, naomba kunukuu: "wafanyakazi wanaotaka kugoma waache kazi, kwa kuwa kuna watu wengi wanahitaji kazi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba soko la ajira Tanzania limefurika wanaotafuta kazi, lakini siyo kweli kwamba watu wote wanaotafuta kazi wana sifa stahiki kwa kila kazi. Kiongozi yeyote awaye mwenye mamlaka ya juu ya kiutendaji ana wajibu wa kuchagua maneno yenye hekima, kwa kuwa hekima ni uhuru. Wafanyakazi wanapodai haki zao ni vema wasijione wanyonge mbele ya Mwajiri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitumie fursa hii kunukuu maneno ya Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere aliyowahi kuyatoa kwenye sherehe za Mei Mosi mwaka 1974, naomba kunukuu: "Tulipoanzisha vyama wafanyakazi; na halafu baada ya Uhuru kwa uamuzi wa Serikali ya TANU, wafanyakazi wa Tanzania wamelindwa wasinyonywe na matajiri wao, watu binafsi na hata Mashirika ya Umma. Ulinzi huo umezidishwa siku hata siku. Kima cha chini cha mishahara kimewekwa na kimekuwa kikiongezwa mara kwa mara. Sasa ni vigumu sana kumfukuza mfanyakazi, na kila mfanyakazi apate heshima yake kama binadamu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Baba wa Taifa inatufundisha msimamo wa viongozi wanaojali maslahi ya watu na wafanyakazi kwa ujumla na kuwahakikishia wafanyakazi ulinzi wa ajira zao dhidi ya unyonyaji unaofanywa na matajiri, watu binafsi na Mashirika ya Umma; pia kuweka kima cha chini cha mishahara na kukiongeza mara kwa mara kuendana na mwenendo wa uchumi; lakini pia kuondoa vitisho vya wafanyakazi kufukuzwa na waajiri wao na kuwapa wafanyakazi heshima yao kama binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli za viongozi zisizokidhi matarajio ya wafanyakazi zinazotolewa katika siku za zama hizi zinaonesha wazi kuwa wafanyakazi wa Tanzania sio kama wa Enzi za Mwalimu. Soko la ajira limewapa nafasi matajiri, watu binafsi, Mashirika ya Umma na Serikali yenyewe kunyonya jasho la wafanyakazi, kuendesha vitisho, kulipa mishahara isiyokidhi maisha na vitisho vya kufukuzwa kazi na ukosefu wa heshima kwa wafanyakazi. Inawezekana haya ni matunda ya kuliua Azimio la Arusha na mahali pake kuliweka "Azimio la Zanzibar."

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala usiozingatia maslahi ya watu wake wake kwa kiwango cha juu kwa jinsi unavyoendeshwa na CCM, unazuia amani na maendeleo ya pamoja. CHADEMA na washirika wake, UKAWA wanatambua kuwa amani na utulivu katika nchi yoyote hujenga na kuleta maendeleo ya Kitaifa na hatimaye maisha bora kwa watu wake.

Halikadhalika, amani katika dunia inalinda maendeleo ya pamoja na ustawi wa watu wake na mgawanyo halali katika mafanikio ya maendeleo. Katika njia ya kujenga jamii yenye demokrasia yenye mpangilio mzuri na wa kuridhisha, UKAWA watakapotwaa madaraka au mamlaka ya kuongoza nchi

hii, watachukulia umuhimu wa kwanza kwa masuala ya maendeleo na ushirikiano na wananchi wa Tanzania na kutambua kuwa ajira na ujira wenye staha ni muhimu katika kujenga jamii yenye ustawi wa kisasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere aliwahi kusema, *“To measure a country’s wealth by its gross National Product is to measure things, not satisfaction.”*. Kwa maana isiyo rasmi ya Kiswahili amesema: “Kupima utajiri wa nchi kwa kutumia pato lake, ni kupima vitu na siyo mahitaji toshelezi ya wananchi wake.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa uchumi na uzalishaji wa ajira ni vitu ambavyo haviwezi kutenganishwa katika mahusiano yake. Katika hotuba ya Waziri Mkuu, inaeleza kuwa katika mwaka 2014, uchumi ulikua kwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na asilimia 4.7 mwaka 2006; ukuaji ambao ni mzuri ikilinganishwa na nchi nyingine zinazoendelea. Lakini ni vizuri kujua uchumi umekuwa ukikua bila kuzalisha ajira nyingi na bila kupunguza umasikini. Hii inatokana na aina ya ukuaji wa uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta zinazokua kwa kasi ni zile zinazotumia mashine na mitambo ambazo ukuaji wake kwa asilimia ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi asilimia 14, usafirishaji na uhifadhi asilimia 12, fedha na bima asilimia 10 na nyinginezo. Sekta zinazotumia mashine na mitambo haziajiri wafanyakazi wengi kama zile zinazotumia misuli mfano kilimo, uvuvi na ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kilikua kwa asilimia 3.4 tu. Pia Sekta zilizokua kwa kasi, hazina mwingiliano na sekta zisizokua. Jambo lingine linaloweza kufanya ukuaji wa uchumi usipunguze umaskini ni mgawanyo mbovu wa sehemu ya uchumi iliyokua.

Aidha, Serikali itakayoundwa na UKAWA itaandaa programu za mafunzo na kuunganisha jamii ya baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi; pia italetta viwango vya juu vya ubora wakati huo huo ikiongeza ushiriki wa wafanyabiashara wa maeneo hayo katika shughuli za utalii.

Pia Serikali yetu itafanya mapitio ya mfumo wa sasa wa kodi na ushuru ambao ni mgumu kuelewa. Mapitio hayo pia yatagusa usimamizi wa matumizi yasiyo ya wazi ya mapato yaliyokusanywa kutoka utalii.

Vilevile, UKAWA tutakapopewa ridhaa ya kuongoza nchi hii, tutahakikisha kuwa masuala ya kisheria, sera na udhibiti, yaliyo rafiki yanazingatiwa kwa kuwa na bajeti zinazojikita katika maendeleo ya miundombinu kwa upana wake,

kuondoa urasimu Serikalini na kukuza rasilimali watu inayohitajika katika sekta binafsi kuwa na ushindani wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, UKAWA tutajenga mfumo imara utakaoweza kujenga uwezo katika utengenezaji wa ajira hapa nchini na kuipaisha Tanzania katika modeli za ukuaji wa ajira ukilinganisha na hali ya sasa ya kufanya kazi kwa mazoea bila kuendana na mabadiliko ya dunia ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ajira kwa Vijana; kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mataifa, watu milioni 200 miongoni mwa wakazi wa Afrika ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 na 24. Hii ni katika hali ambayo Umoja wa Mataifa unasema kuwa, idadi ya vijana wasio na ajira barani Afrika ni mara mbili zaidi ya watu wazima. Ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana unawafanya washawishike kujiunga na makundi yenye misimamo mikali tena kwa ujira mdogo na hata kwa hasira za kukata tamaa na maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kwa vijana ni suala nyeti katika uchumi wa Tanzania. Ni bahati mbaya kuwa vijana wengi hawajaajiriwa katika sekta rasmi. Katika Hotuba ya Waziri Mkuu aliyoiwasilisha mnamo tarehe 12 Mei, 2015 katika Bunge hili ni kwa masikitiko makubwa hakueleza kabisa hali ilivyo hivi sasa. Hotuba ya Waziri Mkuu ingepaswa kueleza kwa nini hali iko hivi sasa na nini kinafanyike kupambana na hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo sababu nyingi za vijana kutoajiriwa na kujiajiri ikiwa ni pamoja na upungufu wa nafasi za ajira na kukubalika katika soko la ajira. Upungufu huo na kutokukubalika katika soko la ajira una sababu zake ambazo bajeti ilipaswa kuelezea lakini imekaa kimya. Pia uwezo mdogo wa vijana kujiajiri ungepaswa kuelezwa pamoja na hatua zinazochukuliwa na ambazo zimeshachukuliwa miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, CHADEMA na washirika wake wa UKAWA watakapopewa ridhaa ya kuongoza nchi hii Oktoba mwaka huu, pamoja na kiwango cha mchango wa pato letu kwenye kaya za jamii zetu kuwa ni ndogo, tunaweza kupunguza utegemezi na mgawanyo wa hovyoyote wa rasilimali na kupiga hatua katika utafiti na uendelezaji na kuweka jitihada kubwa ili kuhakikisha kuwa rasilimali tulizonazo zinatumiwa kwa kiwango cha juu. Utawala wa UKAWA utajenga uwezo mkubwa wa viwanda vyake vya malighafi, vifaa vya uzalishaji na uzalishaji wa bidhaa za mlaji ili kutosheleza mahitaji ya walaji wa Tanzania na kutoa bidhaa na huduma bora katika soko la Kimataifa. Kwa kufanya hivyo pia tutaongeza ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mishahara yenye staha katika sekta mbalimbali nchini; kwa miaka yote mitano ya uhai wa Bunge hili Kambi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiwatetea watumishi wa umma katika nyanja mbalimbali, lakini cha

kusikitisha ni kwamba Serikali hii ya CCM inayojiita sikivu mara zote imekuwa ikipuuza na kubeza mapendekezo mazuri yanayotolewa na Kambi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Rais anaondoka madarakani watu wake wakiwa hawana shauku tena na sherehe nyingi za Mei Mosi zaidi ya Taasisi za Serikali kwa kuwa, maadhimisho haya hayana maana tena kwao. Maadhimisho haya kwa muda wa miaka 10 hayajakata kiu ama shauku ya mfanyakazi kupunguziwa kodi ya mapato wala kusikia ongezeko la mshahara wenye staha. Je, ni nani kati yetu anayeweza kuishi kwa sh. 265,000 kwa mwezi, akalipia kodi ya nyumba, ada ya watoto na huduma nyingine za umeme, maji, afya na kujikimu kwa chakula kwa kiasi hicho? Ipo wapi azma ya baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere ya kujenga Taifa la wafanyakazi? CCM inaondoka madarakani ikiwa imeharibu misingi iliyojengwa na Mwalimu, ni nani wa kusimama na kujivunia hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala Binafsi wa Ajira Nchini; kwa muda mrefu Kambi ya Upinzani imekuwa ikiwasilisha malalamiko ya Watanzania ambao wamekua wakinyonywa nguvu zao na makampuni binafsi yenye kutoa huduma za wakala wa ajira huku wakala hawa binafsi wakinufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yetu ya mwaka 2014/2015, tulielezea kuwa, mawakala hawa binafsi wamekuwa wakitumia kampuni zao kuwaajiri watafuta kazi na si kuwaunganisha watafuta kazi na mwajiri. Hali hii imewakosesha wafanyakazi wanaounganishwa na wakala hawa haki zao za msingi ikiwemo likizo, huduma za matibabu, huduma za Mifuko ya Hifadhi za Jamii na kuwanyima mishahara na posho zao pamoja na stahiki zao nyingine. Kwa muda mrefu tumeelezea ni jinsi gani Wizara imezembea kuchukua hatua mbalimbali za kiutawala, ili kuhakikisha wakala hawa wa ajira wanafanya kazi kwa kuzingatia sheria na kanuni za nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya Uwakala wa Ajira inayojulikana kwa jina la *ISON BPO* imelalamikiwa kwa muda mrefu na wafanyakazi kutokana na kunyimwa haki zao ambapo wafanyakazi wapatao 500 wa kitengo cha huduma kwa wateja wa *Airtel* waliopo jengo la *Quality Plaza*, Makao Makuu Dar es Salaam, pamoja na Makao Makuu ya *Airtel* yaliyopo Moroko. Kampuni hii ni kampuni ya uwakala wa ajira inayotokea nchini India na imepewa jukumu la kusimamia kitengo cha Huduma kwa Wateja na kampuni ya mawasiliano ya *Airtel* tangu mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu kumekuwepo na mgogoro baina ya wafanyakazi wa *Airtel* na Kampuni ya *ISON* ulioplekea kuwepo kwa mazungumzo baina ya Wizara ya Kazi na Ajira. Hata hivyo tarehe 17 na 18 Aprili, 2015 kulitokea mgomo ambapo ulilenga kushinikiza kampuni hiyo kuwalipa

wafanyakazi hao wa *Airtel* malimbikizo yote ya mishahara na stahiki zao, kama ilivyoagizwa na Serikali kupitia Wizara ya Kazi, lakini mpaka leo hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani tunataka kupata majibu ya malalamiko ya wafanyakazi wapatao 500 kama ifuatavyo;

ISON BPO, ilisajiliwa kwa leseni na sheria ipi ya nchi? *ISON BPO*, kwa nini wanaendelea kukaidi agizo la Serikali kwa kukataa kulipa mishahara stahiki na inayopendekezwa na Serikali? Wizara ya Kazi na Ajira, kwa nini inakuwa na kigugumizi na kushindwa kuchukua hatua madhubuti dhidi ya Wakala wa Ajira wajulikanao kama *ISON BPO* katika mgogoro huu ilhali inajua kinachoendelea kufanywa na wakala hawa ni ukiukwaji wa sheria za nchi na kuisababishia Serikali kupoteza pato la Taifa kupitia *P.A.Y.E.* ya wafanyakazi hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii; Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa *NSSF*; Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa *NSSF* ni mojawapo ya Mifuko ambayo mbali ya kutoa mafao ya kustaafu na huduma nyinginezo kadiri ya dira na dhima yake, lakini bado inajishughulisha katika uwekezaji wa miradi mbalimbali kama ambavyo inaoneshwa katika Hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani si kama inapinga uwekezaji unaofanywa na *NSSF* bali tunachohoji na kuliza je, uwekezaji huo unafanywa kwa kuangalia kipindi ambacho miradi itarejesha faida?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 3.12 cha Mwuongozo wa Msimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wa *SSRA* kwa mwaka 2013, pamoja na kanuni zake kuhusu uwekezaji salama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa Mwaka 2012 ni kwamba, Mifuko inatakiwa kuwekeza asilimia 70 ya mali zake kwenye dhamana na hati fungani, asilimia 25 ya mali zake kwenye miundombinu na asilimia 30 ya mali zake kwenye mali isiyohamishika. Je, ni kwa kiasi gani *NSSF* imefuata Sheria na kanuni kuhusu uwekezaji wake mpaka sasa kwa kufuata mgawanyo uliotajwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NSSF* walinunua majengo ya Manji kwa jumla ya shilingi bilioni 47.5 mwaka 2006. Kwa mujibu wa taarifa mbalimbali ni kuwa majengo haya hayakuwa na thamani hiyo wakati *NSSF* inayanunua! Pamoja na hayo, mradi huu unasemekana mpaka sasa kutokurudisha thamani ya uwekezaji kwa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahusisha upandishaji huo wa thamani usiokuwa halisi kuwa ni mojawapo ya mianya ya watendaji wa *NSSF* kujipatia kinachoitwa 10% katika miradi hiyo isiyokuwa na

tija. Aidha, kodi ya mwaka ya Jengo hilo inayotokana na upangaji, haijaweza kuakisi marejesho ya faida ya uwekezaji huo kwa kuwa, mradi huo mpaka sasa umeshindwa kurudisha hata nusu ya fedha zilizowekezwa na hivyo kuhatarisha uwezo wa Mfuko kutoa marejesho kwa wanachama wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuonesha kuwa uwekezaji wa NSSF umekuwa ukiongozwa na matakwa ya watu binafsi, kuna jengo la ghorofa nne lililojengwa Kigoma kwa gharama ya shilingi bilioni saba na limekamilika sasa ni miaka miwili, lakini hadi sasa halijapata mpangaji. Kambi ya Upinzani inahitaji kupata majibu ya uhakika kuhusu uwekezaji huu usiokuwa na tija na ni nini hatma yake ikiwemo suala la uwajibikaji kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa kushindwa kuusimamia ipasavyo Mfuko huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani Bungeni, inataka majibu ya kina kutoka kwa Wizara juu ya uwekezaji mzima unaofanywa na NSSF bila kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo kwa kuwa, ni dhahiri kuwa uwekezaji mkubwa usiokuwa na tija unaofanywa na NSSF unahatarisha kwa kiwango kikubwa uhai wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa ujumla wake; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika kipindi chote cha miaka mitano tumeshauri mambo yafuatayo kuhusiana na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hapa nchini;

kwanza, kuunganisha Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii kubaki chini ya usimamizi wa Wizara ya Kazi na Ajira lengo, likiwa ni kuirahisishia Mamlaka ya Usimamizi wa Hifadhi ya Jamii (SSRA) katika kutekeleza Sheria moja na kuunda vifungu sawa vya kisheria vitakavyosimamia utekelezaji na uendeshaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Pia, tumeitaka Serikali kuwa na jitihada za haraka kunusuru uhai wa Mifuko ya Hifadhi za Jamii kwa kulipa fedha walizochota kwa ajili ya uwekezaji katika miradi...

MWENYEKITI: Malizia, muda umekwisha, *summarise*, muda umekwisha!

MHE. CECILIA D. PARESSO – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba, tunahitaji kupata majibu ya kina juu ya masuala yote tuliyoyasema kuhusiana na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na pia tunahitaji kupata majibu ya kina kuhusiana na suala zima la kuinusuru Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo imekuwa ikiidai Serikali fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Taarifa yangu iingie yote katika Hansard kama ilivyo na naomba kuwasilisha. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante.

**HOTUBA YA MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (MB), MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KAZI NA AJIRA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016
(Inatolewa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge kanuni ya 99(9) toleo la mwaka 2013)
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 Utangulizi

Mheshimiwa Spika,

Kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunilinda na kunitunza ili niweze kutumikia Taifa langu. Napenda kuishukuru familia yangu kwa msaada mkubwa na uvumilivu hasa ninapokuwa katika shughuli zangu za kisiasa.

Mheshimiwa Spika,

Napenda kutumia fursa hii, kuwashukuru wataanzania wote kwa kupokea na kulea harakati za mabadiliko nchini. Shukurani hizi za pekee ziwafikie wenyeviti wenza wa vyama vinavyounda UKAWA, Mh. Freeman Mbowe, Mh. Prof. Ibrahimu Lipumba, Mh. James Mbatia na Mh. Dr. Emanuel Makaidi. Vile vile, shukurani zangu ziwafikie Makatibu wakuu viongozi wa UKAWA; Mhe. Wilbrod P. Slaa, Mhe. Seif Shariff Hamad, Mhe. Masena Nyambabe na Mhe. Tozi Matwange. Sambamba na hao, shukurani zangu ziende kwa timu ya wataalamu wa UKAWA, viongozi, watendaji, wanachama na wapenzi wa vyama vyote vinavyounda UKAWA. Mwisho japo si kwa kumaliza shukurani zangu ziwaendee wabunge wote wa Kambi ya Upinzani bungeni wanaounda UKAWA kwa kazi nzuri ya kutetea na kusimamia maslahi ya wananchi wa Tanzania. Aidha, bila kuwasahau watendaji wa Kambi ya Upinzani ambao wamekuwa ni msaada mkubwa katika utekelezaji wa shughuli zetu.

Mheshimiwa, Spika,

Napenda kuwashukuru kwa nafasi ya pekee wananchi wa wilaya ya Karatu na wananchi na wote wa mkoa wa Arusha kwa ushirikiano na imani kubwa kwangu wakati nikiteteleza majukumu kama mwakilishi wao. Niliahidi daima nitakuwa “Mtumishi wa watu, kwa Maslahi ya watu na kwa Maendeleo ya watu” na daima nitabaki kuwa hivyo. Ninawashukuru na nawaomba wazidishe imani hiyo kwangu kwani haiwezi kupotea bure.

Baada ya Shukrani hizo napenda kuanza hotuba yangu kwa kunukuu maneno machache kutoka kwa Baba wa Taifa, ningependa watanzania kuyatafakari hususan kipindi cha kuelekea Uchaguzi Mkuu mwezi oktoba 2015;

“Na hakutakuwa na watu wa kizazi hiki na karne hii ambao watatakiwa kujitoa muhanga kwa ajili ya maisha bora katika siku zijazo wakakubali, wakati wanawaona watu wachache wakiendelea kuneemeka machoni pao bila kujali wakati ujao, wakati wananchi na watoto wao wakiendelea kuishi katika maisha duni na dhalili.”

UKOSEFU WA AJIRA NCHINI

Mheshimiwa Spika,

Kwa muda mrefu tumekua tukionesha jinsi ambavyo Serikali imekua haina mikakati endelevu ya kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira nchini. Aidha, Serikali ya CCM imekuwa ikitumia mikakati ya ‘kupaka mafuta kwa mgongo wa chupa’ kama nadharia iliyozeleka kwa nia yenye kuwapumbaza wananchi kwa kuwapa matumaini yasiyo na matokeo chanya juu suala zima la utengenezaji wa ajira hapa nchini na hivyo kulifanya tatizo la ajira kuwa ni wimbo uliozeleka ndani ya masikio ya watanzania. Hili ni jambo la aibu kwa nchi iliyojaliwa utajiri mkubwa wa maliasili na rasilimali.

Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere amewahi kutamka maneno yafuatayo;

“Amini nawaambieni enyi waswahili wachache mnaotawala; mnategemea kweli kuwa mtawaongoza watanzania kwa lazima wakati wamepoteza matumaini, na mtegemee kuwa wanasalia wamekaa kimya kwa amani na utulivu?” (Reflections on Leadership in Africa -VUB – University Press, 2000)

Mheshimiwa Spika,

Mwelekeo wa uongozi wa mazoea na wa kuongoza na kuamua mambo kwa matukio ni kuonesha jinsi gani Serikali ya CCM ilivyochoka na kwamba inahitaji kukaa pembeni na kujifunza namna ya kuongoza nchi kwa viwango vya uwajibikaji wenye maslahi mapana kwa jamii ya watanzania. Serikali ya CCM imeshindwa kuzioanisha Sera, Sheria, Mikakati na mipango mbalimbali ambayo kwa pamoja ingeweza kutatua matatizo sugu ya ukosefu wa ajira nchini. Ni Serikali hii ambayo, imeua falsafa ya kujitegemea ‘self reliance’ ambayo Baba wa Taifa aliipigania kwa ajili ya watanzania wote. Je, ni kiongozi yupi wa CCM atakayeweza kusimama na kusema kuwa Serikali ya CCM imekua mdau nambari moja wa azimio la Arusha? Je ni nani kati yenu anayeweza kusema mfumo wa elimu tulionao leo unampa mhitimu uwezo wa kujitegemea? Ni nani anaweza kusimama na kueleza mafanikio ya Serikali ya CCM kuhakikisha kuwa kilimo alichokipigania Baba wa Taifa kinatoa ajira kwa makundi yote? Je, ni nani

kati yenu atakayeweza kusimama na kujinasibu kuwa vyuo vikuu mlivyojenga kwa fedha za wachangiaji ambao wengi ni wafanyakazi na wakulima wa nchi hii vimemuandaa mtanzania kukabiliana na changamoto za ajira?

Mheshimiwa Spika,

Serikali yoyote katika hali halisi ya kiutendaji na utawala, itakuwa na walakini kama itaangalia tu utawala au mfumo bila kujielekeza kuangalia pia mchakato mzima katika utawala na mfumo wake. Ni wazi kwamba, Tanzania inahitaji kufanya mageuzi makubwa kwa sababu nchi inahitaji mabadiliko na hii ni kwa kuwa serikali hii inayoongozwa na CCM ina mambo ambayo hayaendani na kasi ya mabadiliko ya sasa ya kidunia.

Mheshimiwa Spika,

Pamoja na kwamba Serikali ya Tanzania inayoongozwa na CCM kuwa na utaratibu wake, hakika huu ni utaratibu wa kushindwa kuendana na mahitaji ya kiuchumi na kijamii ya watu wake, utaratibu wa kushindwa kuleta maendeleo kwa watu wake, utaratibu wa kushindwa kuleta maendeleo ya amani kwa watu wake na taratibu nyinginezo zenye kunyonya nguvu za watu wake.

Hivyo basi, Serikali ya UKAWA itakapoingia madarakani imekusudia kudhibiti na kuondoa changamoto hizi kwa kuhakikisha kuwa wananchi wa taifa hili la Tanzania wanatengenezewa ajira za kutosha na wanaishi na kufanya kazi kwa amani na utulivu na kuondoa umaskini, kuhakikisha kuwa watu wanaishi kwa uhuru na wanafurahia haki za msingi za kidemokrasia na kwa ufanisi mkubwa, kuhakikisha kuwa mfumo wa uendeshaji serikali kiutawala na kisiasa unaleta maendeleo endelevu ya kiuchumi, na zaidi, mabadiliko hayo ya kiuchumi yanafikiwa katika nchi hii yenye utajiri mkubwa wa rasilimali.

Mheshimiwa Spika,

Katika historia ya sasa; Tanzania imekuwa chini ya utawala wa sheria uliovaa koti la shari, vitisho na mabavu chini ya CCM, na sasa watanzania wanatambua juu ya matokeo ya utawala wa namna hiyo. Hata hivyo, tangu uhuru, watanzania wamekuwa wakiishi kwa pamoja na kujenga urafiki na ushirikiano baina yao, serikali na watu wa nchi nyingine katika msingi wa amani.

Mheshimiwa Spika,

Kauli hiyo ya utawala wa sheria uliovaa koti la shari, vitisho na mabavu unadhihirishwa pia na kauli za Kiongozi wa nchi alizowahi kuzitoa huko nyuma Mwezi Mei 2010 alisema:

“.....wafanyakazi wanaotaka kugoma waache kazi.....kwa kuwa kuna watu wengi wanahitaji kazi....”

Mheshimiwa Spika,

Ni ukweli usiopingika kwamba “soko la ajira” Tanzania limefurika wanaotafuta kazi; lakini si kweli kwamba watu wote wanaotafuta kazi wanasifa stahiki kwa kila kazi. Kiongozi yeyote awaye mwenye mamlaka ya juu ya kiutendaji ana wajibu wa kuchagua maneno yenye hekima; kwa kuwa “hekima ni uhuru”. Wafanyakazi wanapodai haki zao ni vema wasijione wanyonge mbele ya “Mwajiri Mkuu”

Mheshimiwa Spika,

Naomba pia nitumie fursa hii kunukuu maneno ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius K. Nyerere aliyoyatoa Dar es Salaam kwenye sherehe za Mei mosi mwaka 1974:

“.....tulipoanzisha vyama wafanyakazi, na halafu baada ya uhuru kwa uamuzi wa serikali ya TANU, wafanyakazi wa Tanzania wamelindwa wasinyonywe na matajiri wao, watu binafsi, na hata mashirika ya umma. Na ulinzi huo umezidishwa siku hata siku. Kima cha chini cha mishahara kimewekwa na kimekuwa kikiongezwa mara kwa mara. Sasa ni vigumu sana kumfukuza mfanyakazi, na kila mfanyakazi apate heshima yake kama binadamu.....” (Julius K.Nyerere (1974): UHURU NI KAZI, National Printing Company Ltd, Dar es Salaam, ukurasa 15)”

Mheshimiwa Spika,

Kauli ya Baba wa taifa inatufundisha msimamo wa viongozi wanaojali maslahi ya wafanyakazi na watu wao kwa ujumla na kuwahakikishia wafanyakazi :(1) ulinzi wa ajira zao dhidi ya unyonyaji unaofanywa na matajiri, watu binafsi, na mashirika ya umma; (2) kuweka kima cha chini cha mishahara na kukiongeza kila mara kuendana na mwenendo wa uchumi;(3) kuondoa vitisho vya wafanyakazi kufukuzwa na waajiri;(4)kuwapa wafanyakazi heshima yao kama binadamu[ibara ya 12(2), Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977(2005)]

Mheshimiwa Spika, kauli za viongozi zisizokidhi matarajio ya wafanyakazi zinazotolewa katika siku za dhama hizi zinaonesha wazi kuwa leo wafanyakazi wa Tanzania si kama “Enzi za Mwalimu.” Soko la ajira limewapa nafasi matajiri, watu binafsi, mashirika ya umma na serikali (yenyewe) kunyonya jasho la wafanyakazi, kuendesha vitisho, kulipa mishahara isiyokidhi maisha (na mafao duni ya uzeeni na/au kiinua mgongo), vitisho vya kufukuzwa kazi, na ukosefu wa heshima kwa wafanyakazi! Inawezekana haya ni matunda ya kuliua Azimio la Arusha na mahala pake kuliweka “Azimio la Zanzibar”

Mheshimiwa Spika,

Utawala usiozingatia maslahi ya wafanyakazi wake kwa kiwango cha juu kwa jinsi unavyoendeshwa na CCM, unazuia amani na maendeleo ya pamoja.Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na washirika wake (UKAWA) wanatambua kuwa amani na utulivu katika nchi yoyote

hujenga na kuleta maendeleo ya kitaifa na hatimaye maisha bora kwa watu wake, hali kadhalika amani katika dunia inalinda maendeleo ya pamoja na ustawi wa watu wote na mgawo halali katika mafanikio ya maendeleo yao. Katika njia ya kujenga jamii yenye demokrasia yenye mpangilio mzuri na wa kuridhisha, UKAWA watakapotwaa mamlaka ya kuongoza nchi hii watachukulia umuhimu wa kwanza masuala ya maendeleo na ushirikiano na wananchi wa Tanzania na kutambua kuwa ajira na ujira wenye staha ni njia muhimu ya kujenga jamii yenye ustawi wa kisasa.

UKUAJI WA SEKTA YA AJIRA

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere aliwahi kusema:

“To measure a country’s wealth by its gross national product is to measure things, not satisfaction.”¹

Kwa maana isiyo rasmi ya Kiswahili anasema:

“Kupima utajiri wa nchi kwa kutumia pato lake (yaani maana ya namba ya GNP), ni kupima vitu na si mahitaji toshelezi ya wananchi wake”.

Mheshimiwa Spika,

Ukuaji wa Uchumi na Uzalishaji wa Ajira (Economic growth and Employment creation) ni vitu viwili ambavyo haviwezi kutenganishwa katika mahusiano yake. Katika hotuba ya Waziri Mkuu, inaeleza kuwa ‘kwa mwaka 2014, uchumi ulikua kwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na asilimia 4.7 mwaka 2006, ukuaji ambao ni mzuri ikilinganishwa na nchi nyingi zinazoendelea’. Lakini ni vizuri kujua kuwa umekuwa ukikua bila kuzalisha ajira nyingi na bila kupunguza umaskini. Hii inatokana na aina ya ukuaji wa uchumi wa Tanzania. Sekta zinazokua kwa kasi ni zile zinazotumia mashine na mitambo ambazo ukuaji wake kwa asilimia katika mabano ni ujenzi(14.1), usafirishaji na uhifadhi(12.5), fedha na bima(10.8) na nyinginezo. Sekta zinazotumia mashine na mitambo haziajiri wafanyakazi wengi kama zile zinazotumia misuli mfano kilimo, uvuvi, na ufugaji. Kilimo kilikua kwa asilimia 3.4 tu. Pia Sekta zilizokua kwa kasi hazina mwingiliano na sekta zisizokua. Jambo lingine linaloweza kufanya ukuaji wa uchumi usipunguze umaskini ni mgawanyo mbovu wa wa sehemu ya uchumi iliyokua.

¹ J.K. Nyerere, The Rational Choice given on 2 January 1973 in Khartoum)

Mheshimiwa Spika,

Kimsingi, bajeti lazima zingatiae si tu kukua kwa uchumi bali pia kuhakikisha kuwa ukuaji huu unakuwa shirikishi, unazalisha ajira na kupunguza umaskini. Ni muhimu pia kuisitiza ukuaji wa kijani (green production growth) ambao ni ukuaji usioharibu mazingira (ikolojia).

Mheshimiwa Spika,

Maendeleo ya sekta binafsi na uwekezaji ni muhimu sana katika ukuaji wa sekta ya ajira na kujenga ustawi wa maisha ya watu. Japokuwa Bajeti ya Waziri Mkuu imezungumzia mambo mengi kuhusu maendeleo ya sekta binafsi, ingekuwa vizuri kutambua mambo ya msingi katika sekta binafsi, Uchambuzi katika sekta binafsi unaonesha kuwa sekta hii si kitu kimoja, ina vipande vingi. Hivi ni pamoja na: sekta binafsi ya nje na ya ndani; sekta binafsi kubwa, ya kati na ndogo na sekta binafsi isiyo rasmi. Hatua za kibajeti lazima zitambue ukweli huu kuhusu sekta binafsi. Aina zote za sekta binafsi zikiwekwa katika kapu moja haitakuwa sahihi kwa maendeleo ya sekta hii hasa ile ya ndani, ndogo na isiyo rasmi. Ni vema CCM wakajiuliza maswali na kuachana na mazoea ya utengenezaji hotuba za bajeti kwa namna ambayo haitoi taswira halisia tena kwa fikra zile zile, za miaka ile ile na kwa ujanja ule ule.

Mheshimiwa Spika,

Aidha hatuwezi kupigia kelele ukosefu wa ajira bila kujielekeza katika kuangalia sekta ya uwekezaji. Suala kuu katika sekta ya uwekezaji ambayo CCM imekuwa ikipata ganzi kulifanyia kazi na kuchukua hatua makini za makusudi ni uboreshaji wa mazingira kwa wawekezaji wa ndani na nje, wakubwa kwa wadogo. Hatua mahsusi za kibajeti zinatakiwa katika kuleta na kuboresha mazingira rafiki na wezeshi ya uwekezaji ili kuongeza ajira na ustawi wa maisha ya watanzania.

Mheshimiwa Spika,

eneo lingine ni maboresho katika sekta ya utalii yanaweza kujenga ajira nyingi kwa watanzania. Tayari sekta ya utalii ni mchangiaji mkubwa kwa uchumi wa Tanzania. *Chapisho la Hali ya Uchumi wa Tanzania linalochapishwa Na Benki ya Dunia* libainisha kwamba sekta ya utalii inaweza kukua na kujenga ajira zaidi, hususan katika ajira zinazolipa vizuri, pia inaweza kuunganisha biashara na wana jamii wa maeneo husika. Ili kutumia fursa hii, serikali inapaswa kupitia upya wajibu wake kwa kurahisisha mfumo wa kodi na ushuru, na kufanya mgawanyo wa mapato kuwa wazi zaidi.

Mheshimiwa Spika,

sekta ya utalii huajiri moja kwa moja takribani watanzania nusu milioni na huchangia karibu asilimia 20 ya bidhaa zinazouzwa nje. Huwakilisha takribani asilimia 3.4 ya Pato Ghafi la Tanzania (GDP), lakini kiwango hiki kinaweza kufikia makadirio asilimia 10 unapochukuliwa mchango wake ambao si wa moja kwa moja katika sekta nyingine kama kilimo na uchukuzi. Pamoja na kwamba sekta ina lengo la kuongeza mapato yatokanayo na utalii mara nane ifikapo mwaka 2025, au kuongeza kiwango cha ukuaji wa sekta mara dufu kwa kila mwaka kama inavyoonekana katika miaka hivi karibuni, Lengo hili litafikika endapo tu kutakuwa na mabadiliko katika sera na mitazamo miongoni mwa wadau wote.

Mheshimiwa Spika,

kama nilivyokwisha sema awali, bila kujenga uwezo wa kitaasisi katika sekta zetu mbalimbali hapa nchini ni vigumu kuzalisha ajira na kuleta maisha ya ustawi kwa watu wetu. Katika kuboresha sekta hii ya utalii ambayo ni moja ya sekta zenye mchango mkubwa wa ajira katika nchi yetu mambo kadhaa yanahitajika. Serikali itakayoundwa na UKAWA imejipanga (1) kupanua shughuli za utalii kuwa anuai tofauti na msisitizo wa sasa ambao unatoa umuhimu kwa watalii wa gharama kubwa katika kanda ya kaskazini na kuzunguka Arusha na Zanzibar ambako asilimia 90 ya shughuli za utalii ndiko ziliko sasa;(2)kuongeza juhudi za kuwaunganisha wana jamii wa maeneo husika na wafanyabiashara wadogo wa utalii katika shughuli za utalii, kupitia michakato ya kugawana faida.

Aidha, Serikali itakayoundwa na UKAWA itaandaa programu za mafunzo na kuunganisha jamii baina ya sekta za umma na binafsi, hii italeti viwango vya juu vya ubora wakati huo huo ikiongeza ushiriki wa wafanyabiashara na wafanyakazi wa maeneo hayo katika shughuli za utalii; na (3) Serikali yetu itafanya mapitio ya mfumo wa sasa wa kodi na ushuru ambao ni mgumu kuuelewa, mapitio hayo pia yatagusa usimamizi wa matumizi yasiyo ya wazi ya mapato yaliyokusanywa kutoka utalii. Vilevile, mfumo wa kodi na ushuru utafanywa kuwa rahisi na kutekelezwa kwa usawa zaidi kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji wa biashara na kuziba mianya ambayo inatoa nafasi kufanya malipo haramu. Aidha, mgawanyo wa mapato utarasimishwa ili uwe rahisi kufuatilia na kuongeza manufaa kwa wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Spika,

Pamoja na kiwango cha ukuaji wa uchumi wa Tanzania kukua kwa asilimia 7 bado hakiakisi maendeleo halisi ya watu kwenye kaya zao. Hivi sasa maisha yako juu. Bei ya bidhaa na huduma mbalimbali za jamii, ziko juu. Kwa kifupi hali ya maisha ni ngumu. Kambi rasmi ya upinzani inaona kuwa tatizo kubwa la viongozi wa CCM ni kuona kuwa “wizara husika inapaswa kufa kivyake” bila kutambua na kuona pia jitihada za makusudi zinatakiwa kuchukuliwa ili kuwepo na “mfumo unaounganisha wizara, idara, wakala za serikali, na uongozi wa sekta binafsi kufanya kazi kwa umoja” utakaoweza kusaidia kujenga uwezo wa uelewa wa jinsi gani ajira zinaweza kutengenezwa katika nchi.

Serikali ya UKAWA inaahidi kuifanya Wizara ya Kazi na Ajira kuwa bunifu na kuioanisha na vitengo vingine vya utawala pamoja na wataalamu mbalimbali wa wizara zingine katika kufikia lengo la kuongeza ajira kwa wataanzania.

Mheshimiwa Spika,

UKAWA tutakapopewa ridhaa ya kuongoza nchi hii tutahakikisha kuwa masuala ya kiseria, kisheria na ya udhibiti yaliyo rafiki yanazingatiwa, kwa kuwa na bajeti zinazojikita katika maendeleo ya miundo mbinu kwa upana wake, kuondoa

urasimu serikalini na kukuza rasilimali watu inayohitajika kwa sekta binafsi kuwa na ushindani wa kimataifa. UKAWA tutaweza kujenga mfumo imara utakaoweza kujenga uwezo katika utengenezaji wa ajira hapa nchini na kuipaisha Tanzania katika modeli za ukuzaji wa ajira ukilinganisha na hali ilivyo ya sasa ya kufanya kazi kwa mazoea bila kuendana na mabadiliko ya dunia ya sasa.

AJIRA KWA VIJANA

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mataifa, watu milioni 200 miongoni mwa wakazi wa Afrika ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 na 24. Hii ni katika hali ambayo Umoja wa Mataifa unasema kuwa, idadi ya vijana wasio na ajira barani Afrika ni mara mbili zaidi ya watu wazima. Ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana unawafanya washawishike kujiunga na makundi yenye misimamo mikali tena kwa ujira mdogo tu au hata kwa hasira za kukata tamaa na maisha. Mfano wa hali hiyo unashuhudiwa katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Nigeria na Mali. Inaonekana kuwa, vijana wasio na ajira ni mawindo mazuri kwa makundi yenye kutishia amani. Leo hii siku za karibuni tumeshuhudia kijana wa kitanzania Rashid Charles Mberesero (21), akituhumiwa kuwa mmoja wa wanamgambo wa Al-Shabaab ambao walifanya mauaji katika Chuo Kikuu cha Garissa nchini Kenya na kuua wanafunzi 148. Haya ni matokeo ya kushindwa kwa mfumo wa utawala katika sekta ya elimu unaosimamiwa na Serikali ya CCM ambao ndio msingi wa kumuandaa kijana kifikra na hata kimtazamo.

Mheshimiwa Spika,

Ajira kwa vijana ni suala nyeti katika uchumi wa Tanzania. Ni bahati mbaya kuwa vijana wengi hawajaajiriwa katika sekta rasmi. Katika Hotuba ya Waziri Mkuu aliyowasilisha mnamo tarehe 12 Mei 2015 katika bunge hili ni kwa masikitiko makubwa haikueleza kabisa hali ilivyo hivi sasa. Hotuba ya Waziri Mkuu ingepaswa kueleza kwa nini hali iko hivi na nini kinafanyika kupambana na hali hiyo. Zipo sababu nyingi za vijana kutoajiriwa na kujajiri ikiwa ni pamoja na upungufu wa nafasi za ajira na kukubalika katika soko la ajira. Upungufu huo na kutokubalika katika soko la ajira vina sababu zake ambazo bajeti ilipaswa kuelezea lakini imekaa kimya. Pia uwezo mdogo wa vijana kujajiri ungepaswa kuelezewa pamoja na hatua zinazochukuliwa na ambazo zimeshachukuliwa miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, wakati wa majadiliano ya bajeti ya wizara ya kazi na ajira mwaka jana tarehe 24 Mei 2014, Waziri Kabaka alieleza kuwa vijana wa kitanzania hasa wahitimu wanategemea kuajiriwa serikalini na mashirika binafsi na hawako tayari kujajiri. Haya ni ghiriba kwa watoto wa masikini na waziri anapaswa kufuta kauli yake kwa kuwa inavyoonekana leo hii kuwa ni watoto

wa vigogo pekee ndio wana haki ya kupata ajira serikalini na watoto wa kimasikini ndio wajajiri.

Mheshimiwa Spika,

Ajira 200 za uhamiaji zilitangazwa Februari 17, mwaka 2014 ambapo watu 15,707 walijitokeza kuwania nafasi hizo 200, miongoni mwao, waombaji 1,005 waliitwa kwenye usaili na 200 waliothibitishwa waliitwa kazini. Hata hivyo, baada ya tangazo la kuitwa kazini malalamiko yaliibuka kupitia vyombo vya habari na baadhi ya mitandao ya kijamii, kwamba baadhi ya walioitwa katika ajira hizo walikuwa ni watoto, jamaa na ndugu wa maofisa wa Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa si kosa kwa ndugu na jamaa kuajiriwa katika nafasi yoyote iwapo wanakidhi vigezo vyote, lakini inapotokea kwamba hakuna uwazi (transparency) ni dhahiri kwamba kunakuwa na upendeleo kama ilivyotokea. Hii inatokana na ukweli kuwa idara hiyo haichukui watumishi kutoka Sekretarieti ya Ajira, kwa kuwa wanaohitajika ni askari. Lakini hii ni mojawapo ya ushahidi kuwa nafasi za kazi nchini zimeendelea kutolewa kwa upendeleo na wanaonufaika na nafasi hizo ni vigogo na ndugu zao au watu wenye mahusiano ya karibu na wenye mamlaka hayo.

Mheshimiwa Spika,

Kukosekana kwa takwimu sahihi na taarifa za nguvu kazi nchini kunaleta sintofahamu kubwa katika kutatua matatizo ya ajira nchini. Kukosekana huko kwa taarifa sahihi ndio kunakofanya CCM itake kuwaaminisha wataanzania kuwa Mabilioni ya Rais Kikwete yameweza kutatua changamoto za ajira nchini. Tukiwa tunamaliza miaka 10 ya utawala usio wa kimkakati, vijana na nguvukazi ya Tanzania inawakumbuka watawala wa CCM kama wazee wa ahadi, ahadi zenye mashaka! Leo hii tuna Serikali inayokiri kutokua na takwimu za ajira nchini, ni vipi mikakati na sera hizi zitapimwa utekelezaji wake ikiwa takwimu sahihi zinakosekana?

Mheshimiwa Spika,

Mabilioni ya Kikwete ni mojawapo ya mikakati iliyoshindwa kwa kuwa haikua na nia ya dhati ya kumfundisha mtanzania kuvua bali kuwapatia samaki wa siku moja na lilenga kuwadumaza wataanzania kwa kuwaaminisha kuwa Rais Kikwete ana mahela ambayo yanaweza kutatua shida zao na si kuwainua kiuchumi. Kwa bahati mbaya sana Serikali za CCM za *Awamu ya Pili, Tatu na hata hii ya Nne, zimekuwa siku zote zikisema zinafufua uchumi. Kila uongozi unaokuja hauishi kutamba kuwa unataka kufufua uchumi. Swali la kujiuliza ni kwamba, ni nani aliyepua uchumi na kuuzika? Na ni nani anayetaka kuufufua? Jibu la haraka ni serikali hiyo hiyo, tena ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) toka Baba wa Taifa akabidhi madaraka kwa marais waliomfuatia.*

Mheshimiwa Spika,

Mkazo wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na washirika wake (UKAWA) watakapopewa ridhaa ya kuongoza nchi hii Oktoba mwaka huu ni kwamba, pamoja na kiwango cha mchango wa pato letu kwenye kaya za jamii zetu kuwa ni kidogo, tunaweza kupunguza utegemezi na mgawanyo wa ovyo wa rasilimali na kupiga hatua katika utafiti na uendelezaji (Research and Development) na kuweka jitihada kubwa ili kuhakikisha kuwa rasilimali tulizonazo zinatumika kwa kiwango cha juu. Utawala wa UKAWA utajenga uwezo mkubwa wa viwanda vyake vya malighafi, vifaa vya uzalishaji (capital goods) na uzalishaji wa bidhaa za mlaji ili kutosheleza mahitaji ya walaji wa Tanzania na kutoa bidhaa na huduma bora katika soko la kimataifa. Kwa kufanya hivyo pia kutaongeza ajira kwa wataanzania.

Mheshimiwa Spika,

Uchumi wa taifa hili unaongozwa na CCM na CCM ndiyo yenye jukumu la kuu au kukuza uchumi. Serikali ya Awamu ya nne baada ya kuingia madarakani, ilikuja na mkakati mahususi wa kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Ili kuondoa umaskini, mbali ya kutoa ahadi ya ajira milioni moja kila mwaka kwa vijana, Rais Jakaya Kikwete pia alikuja na mpango wa kutoa mabilioni ya fedha kwa ajili ya kukopesha vikundi vya ujasiriamali. Fedha hizo zilisemekana kuwa zingetolewa kupitia benki, vyama vya akiba na mikopo (SACCOS) na taasisi nyingine za fedha zilizoruhusiwa na Serikali kupitishia mikopo hiyo. Chini ya mpango huo, kila mkoa uliahidiwa kumwagiwa sh bilioni moja.

Mheshimiwa Spika,

Hivi karibuni wakati akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalumu, Faida Mohamed Bakari (CCM) ambaye alitaka kufahamu ni wafanyabiashara wangapi wenye ulemavu walipatiwa mikopo kupitia fedha hizo. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uwekezaji na Uwezeshaji, Christopher Chiza alisema kuwa mpango huo ulikuwa na madhumuni ya kuwezesha wananchi kiuchumi na kuongeza ajira kwa wanawake na vijana vijijini na mijini kwa kuwapatia mikopo bila kujali maumbile yao. Alisema chini ya mpango huo, mikopo ilitolewa katika awamu mbili kupitia benki na asasi za kifedha, zilizoteuliwa na serikali baada ya kukidhi vigezo ambapo jumla ya Sh bilioni 43.69 zilitolewa na kunufaisha wajasiriamali 74,593. Vilevile, cha kusikitisha zaidi ni kuwa Waziri Chiza alieleza kuwa mikopo hiyo haikuwa na kipengele cha utambuzi cha watu wenye ulemavu. Hii inaonesha ni jinsi gani Serikali ya CCM imeshindwa kuwapa vipaumbele walemavu katika mikakati yake ya kuwawezesha kiuchumi na kukuza ajira. Ni hatari kuona kuwa, walemavu kwa muda wa miaka 10 ya utawala wa Kikwete hawajapewa kipaumbele cha kujijiri wala kuajiriwa bali Serikali imekua ikiwakumbuka kipindi cha uchaguzi pekee. Ndio maana Serikali siku zote hutoa idadi ya walemavu walionufaika na nafasi za kuongozi na kisiasa na wala si walionufaika na fursa za ajira nchini. Kambi rasmi ya Upinzani inaendelea kuwa mtetezi nambari moja wa haki za walemavu katika masuala ya ajira kwa kuwa

watu wenye ulemavu ni sehemu ya jamii yetu na wana haki sawa na watu wote.

Mheshimiwa Spika,

Sasa inatosha! Kambi ya Upinzani Bungeni inapenda kuwaambia watanzania kuwa kwa muda wa miaka 10, matatizo yao yametumika kama mtaji wa Serikali ya CCM na hivyo utatuzi wa matatizo hayo ni sawa na ahadi hewa. Ikumbukwe kuwa Mheshimiwa Kikwete pia katika muendelezo wa ahadi zake zilezile, alitoa agizo mahsusi kwa Wizara hii Jumatano, Aprili 10, 2013 baada ya kuwa ameelezwa na kuonyeshwa video ya Mpango wa Kuwawezesha Wajasiriamali Vijana Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine cha Morogoro katika shughuli iliyofanyika Ikulu, Dar es Salaam. Mpango huo unaogharimiwa na Benki ya CRDB na kuendeshwa kwa pamoja kwa kushirikiana na SUA pamoja na Ushirika wa Wahitimu Wajasiriamali wa Chuo Kikuu cha Sokoine (SUGECO).

Mheshimiwa Spika,

Rais Kikwete aliitaka Wizara ya Kazi na Ajira kuwasilisha haraka iwezekanavyo kwenye Kikao cha Baraza la Mawaziri mapendekezo ya kuboresha na kupanua mpango mpya wa uwezesaji na ajira kwa vijana wanaomaliza vyuo vikuu ambao unalenga kupanua fursa za ajira kwa kutoa mitaji kwa vijana ili waanzishe shughuli zao za uzalishaji. Hii ni kauli ya Kiongozi Mkuu wa Serikali kukubali kuwa mikakati yake dhidi ya tatizo la ajira imekosa vipaumbele vya muda mfupi na mrefu.

“Huu mpango nimeupenda sana. Huu ni bora zaidi kuliko hata ule mwingine wenye mafanikio wa Mabilioni ya Bwana Fulani kwa sababu huu unamwandaa vizuri mjasiriamali ili aweze kukopeshwa. Huu ndiyo aina ya mpango ambao nimekuwa nauzungumzia na kutaka uanzishwe ambako wasomi na wasio wasomo wanajiunda katika vikundi kulingana na ujuzi na elimu ili Serikali iweze kuwawezesha.”

Ikiwa imepita mwaka mmoja toka Rais atoe ahadi ya utekelezaji wa wazo hilo, wizara ina majibu gani? Aidha, Rais Kikwete aliendelea kusema kuwa

“Serikali yangu iko tayari kuchangia kiasi cha sh. bilioni tano katika mfuko wa kuunga mkono mpango huu. Hii ni modeli nzuri ya kuwezesha vijana, kuzalisha ajira na kuboresha maisha ya watu. Tuendeleo kuwezesha vijana katika sekta ya kilimo lakini sasa tuanze kufikiria namna ya kupanuka na kuingia katika maeneo mengine ili kusudi anayetaka kukopa kufanya biashara ya mitumba na ya teknolojia ya habari naye aweze kukopeshwa.”

Mheshimiwa Spika,

Ni jambo la kusikitisha kuona kuwa Rais anakubali kuwa modeli aliyooneshwa ni bora kuliko mabilioni yake ambayo anashindwa kutaja hata jina lake kwa kuwa,

mpango wa Mabilioni ya Kikwete si tu umeshindwa kuwa na matokeo mazuri lakini pia umeshindwa kutatua tatizo la ajira nchini na kuwainua wananchi kiuchumi.

MISHAHARA YENYE STAHA KATIKA SEKTA MBALIMBALI NCHINI

Mheshimiwa Spika, kwa miaka yote mitano ya uhai wa Bunge hili Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiwatetea watumishi wa umma katika nyanja mbalimbali lakini cha kusikitisha ni kwamba Serikali hii ya CCM inayojiita sikivu mara zote imekuwa ikipuuza na kubeza mapendekezo mazuri yanayotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Spika,

Miongoni mwa masuala muhimu tuliyopendekeza na serikali kuyapuuza ni kama ifuatavyo:

1.Kima cha Chini cha Mshahara:

Mheshimiwa Spika,

Kambi Rasmi ya Upinzani kwa muda mrefu imekua ikiishauri Serikali kupandisha kiima cha chini cha mshahara kwa watumishi wa umma kufikia shilingi 315,000/= kwa mwezi lakini Serikali imeamua kuziba masikio na mpaka sasa haijatekeleza pendekezo hilo. Inashangaza sana kuona Serikali ikijigamba kuwa imepandisha kima cha chini cha mshahara kutoka shilingi 240,000/= hadi shilingi 265,000/= sawa na ongezeko la shilingi 25,000 tu.

Mheshimiwa Spika,

Pamoja na matumaini ambayo Rais Kikwete aliwapa wafanyakazi mwaka 2005 na 2010, leo hii anapoondoka madarakani hata walimu ambao waliamini Rais kwa nafasi yake kama mkuu wa nchi atawapa alichowaaahidi, leo wanambebea bango na kumuuliza kwa machungu 'Shemeji unatuachaje'? hii inasikitisha sana .

Mheshi miwa Spika,

Leo hii Rais anaondoka madarakani watu wakiwa hawana shauku tena na Mei Mosi zaidi ya Taasisi za Serikali kwa kuwa maadhimisho haya hayana maana tena kwao. Maadhimisho haya kwa muda wa miaka 10 hayajakata kiu ama shauku ya mfanyakazi kupunguziwa kodi ya mapato wala kusikia ongezeko la mshahara wenye staha. Je ni nani kati yetu anayeweza kuishi kwa shilingi 265,000 kwa mwezi, akalipia kodi ya nyumba, ada ya watoto, huduma za umeme, maji na afya na kujikimu kwa chakula kwa kiasi hicho? Ipo hapi azma ya baba wa Taifa ya kujenga Taifa la wafanyakazi? CCM inaondoka madarakani ikiwa imeharibu misingi iliyojengwa na Mwalimu, ni nani wa kusimama na kujivunia hayo?

Pamoja na kuahidi kuwa Serikali itaongeza mshahara, Mhe. Raisi anashindwa kutamka hadharani iwapo ongezeko la mshahara litafikia 315000, na hata kama halitafikia bado anatoa matumaini kwa watanzania kuwa ataongeza. Hii ni mbinu ya kudaka kura za watanzania kwa mara nyengine.

KODI YA PATO LA MSHAHARA (PAYE)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa utaratibu wa kodi ya mapato ya wafanyakazi ni kati ya asilimia 12 na 35 ya mshahara wa mfanyakazi. Kwa mujibu wa CAG katika mwaka 2013/2014 mamlaka ya kodi ta Tanzania ilikusanya jumla ya triloni 15 kama kodi itokanayo na mapato (PAYE). Aidha, mdhibiti na mkaguzi mkuu wa serikali alionesha kwamba katika kipindi hicho, serikali ilitoa msamaha kwa walipa kodi wakubwa na makampuni ya nje liliyofikiwa kiasi cha shilingi triloni 1.5 sawa na kodi iliyokusanywa na Serikali kutoka kwa wafanyakazi. Hii ina maana kwamba kama Serikali isingetoa misamaha hiyo ya kodi, mapato ya serikali kutoka kwa walipa kodi wakubwa nchini yangeongezeka maradufu na hivyo kumpunguzia mfanyakazi mzigo wa kodi.

Mheshimiwa spika,

Kutokana na ukuaji mbaya wa uchumi, mfumuko wa bei pamoja na kupanda kwa gharama za maisha, kodi itokanayo na mapato ya wafanyakazi imekuwa mzigo mkubwa na maumivu kwa wafanyakazi wa Tanzania waliopo katika ajira rasmi. Katika maoni yake ya mwaka toka kuanza kwa Bunge lako la 10, Kambi rasmi ya Upinzani, imekuwa ikipendekeza kwamba viwango vya kodi ya mapato ya wafanyakazi vipunguzwe kufikia asilimia 9 hadi 27 respectively. Pendekezo hili bado lina nguvu mpaka leo. Leo Rais anaondoka madarakani akiacha kiwango cha asilimia 12 huku akiwa hana uhakika wa kutekeleza ahadi zake za kupunguza kodi kwa wafanyakazi. Akihutubia Maadhimisho ya Mei Mosi, Rais Kikwete alisema:

'Na mwaka huu tutapunguza sijui tutafikia asilimia 9 kama mnavyotaka ila tutakapofikia si pabaya'

Haya ni maneno ya Rais ambayo si tu hayatoi mwelekeo bali hayajibu njaa ya miaka mingi ya punguzo la kodi ili Tanzania iwe sawa na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ni ahadi yetu kwa wafanyakazi wote nchini ambao Mwalimu Nyerere aliwapigania kwa moyo wake wote bila kujali itikadi zao kuwa, UKAWA itayatekeleza haya kwa kuwa maoni ya CAG kwa mwaka 2013/2014 yalieleza dhahiri kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kupunguza misamaha ya kodi bila kuathiri mapato ya Serikali kwa namna yoyote ile.

WAKALA BINAFSI WA AJIRA NCHINI

Mheshimiwa Spika,

Kwa muda mrefu sasa Kambi ya upinzani imekua ikiwasilisha malalamiko ya watanzania ambao wamekua wakinyonywa nguvu zao na makampuni binafsi yenye kutoa huduma za wakala wa ajira huku wakala hawa binafsi wakinufaika. Katika hotuba yetu ya mwaka 2014/2015 tulielezea kuwa mawakala hawa binafsi wamekua wakitumia kampuni zao kuwaajiri watafuta kazi na si kuwaunganisha watafuta kazi na mwajiri. Hali hii imewakosesha wafanyakazi wanaounganishwa na wakala hawa haki zao za msingi ikiwemo likizo, huduma za matibabu, huduma za mifuko ya hifadhi za jamii na kuwanyima mishahara na posho zao pamoja na stahiki zao nyingine.

Mheshimiwa Spika,

Kwa muda mrefu tumeelezea ni jinsi gani wizara imezembea kuchukua hatua madhubuti za kiutawala ili kuhakikisha wakala hawa wa ajira wanafanya kazi kwa kuzingatia sheria na kanuni za nchi yetu ikiwemo Sheria ya Huduma za Ajira Na. 9 ya mwaka 1999. Aidha, wakala hawa binafsi wengi wameendelea kufanya kazi zao bila kulipa kodi na hivyo kulikosesha Taifa mapato. Mojawapo ya makampuni yaliyokuwa yakiendesha huduma za ajira ni pamoja na Erolink ambayo kwa mujibu wa Waziri wa Kazi na Ajira, Mhe. Gaudensia Kabaka alieleza kuwa ilikosesha Serikali mapato ya takribani Bilioni 3 kwa muda wa miaka mitatu. Na katika kipindi hiki, makampuni takribani 56 ya wakala binafsi wa ajira yalituma barua za kuomba kibali mara baada ya Serikali kupiga marufuku makampuni ambayo hayana kibali kujihusisha na kazi za huduma za ajira. Ikiwa kampuni moja ya Huduma za ajira imeikosesha Serikali kiasi cha Shilingi za Kitanzania Bilioni 56 kwa miaka mitatu, je makampuni 56 ambayo yalituma maombi ya vibali yatakuwa yameikosesha Serikali kiasi gani cha mapato?

Mheshimiwa Spika,

Ikumbukwe kuwa wakala binafsi wa ajira pamoja na kuendelea kufanya kazi bila kibali pia zimeendelea kuwanyima haki za msingi wafanyakazi wanaowamiliki kinyume na Sheria na utaratibu uliowekwa.

Mheshimiwa Spika,

Kampuni ya Uwakala wa Ajira inayojulikana kwa jina la ISON BPO (zamani SPANCO BPO) imelalamikiwa kwa muda mrefu kutotoa haki kwa wafanyakazi wapatao 500 wa kitengo cha huduma kwa wateja wa Airtel waliopo jengo la Quality Plaza na Makao Makuu ya Airtel, Morocco jijini Dar Es Salaam. Kampuni hii (ISON BPO), ni kampuni ya uwakala wa ajira inayotokea nchini India, na imepewa jukumu la kusimamia kitengo cha Huduma kwa Wateja na kampuni ya mawasiliano ya Airtel, tangu mwaka 2011 katika mambo yanayohusu voice (sauti), data (internet), na Airtel Money (huduma za kibenki kwa njia ya simu).

Mheshimiwa Spika,

Mnamo mwaka 2013, kupitia Wizara ya Kazi na Ajira, Serikali iliagiza na kutoa maelekezo kuwa wafanyakazi katika Sekta ya Mawasiliano wanatakiwa walipwe kiima cha chini cha Tshs. 400,000/- (laki nne) kama mshahara (basic salary). Lakini la ajabu, la kushangaza na la kusikitisha, ni kuwa kampuni hii ya kigeni imekuwa ikipuuzia maagizo na maelekezo hayo ya Serikali kwa kuendelea kuwalipa wafanyakazi wake mishahara kati ya 150,000/- na 270,000/- kinyume na agizo la Serikali. Aidha, ISON BPO, wamekuwa wakilipa kiwango hicho kwa madai kuwa wao (ISON BPO) hawaendeshi kampuni inayojihusisha na mambo ya mawasiliano, vilevile kwa dai lao lingine ni kuwa hawana hela za kuwalipa wafanyakazi kwa kiwango hicho cha 400,000/- (laki nne) kama ilivyoelekezwa na Serikali. Lakini wakati wakidai hayo kuwa hawana pesa ya kuwalipa wafanyakazi kwa kiwango hicho cha laki nne (400,000/-), wafanyakazi wenye asili ya India wamekuwa wakilipwa mishahara minono ya kati ya milioni tano na milioni kumi.

Mheshimiwa Spika,

Kutokana na mgomo wa wafanyakazi wa Airtel waliopo chini ya Kampuni ya ISON BPO uliotokea siku mbili kati ya tarehe 17 na 18, Aprili, 2015 ili kushinikiza wafanyakazi hao wa Airtel kulipwa malimbikizo yote na mshahara stahiki kama ilivyoagizwa na Serikali kupitia Wizara ya Kazi na Ajira; kwa kuamini watu wa Wizara ya Kazi na Ajira kuwa wangeweza kutatua mgogoro huo ambao umedumu kwa takribani miaka miwili sasa, wafanyakazi hao waliwasiliana na maafisa kazi (labour officers) ili kupata msaada. Maafisa hao wa Wizara ya Kazi walipofika, kwanza waliongea na wafanyakazi, na baadae waliongea na uongozi wa ISON BPO, baada ya mazungumzo ya pande mbili kufanyika katika nyakati tofauti, walikaa wote meza moja ya majadiliano na katika kuhitimisha, maafisa kazi walimpa ISON BPO (mwajiri) njia mbili;

1. ISON BPO awalipe mshahara wa laki nne (400,000/-) na kama hawezi kulipa kiwango hicho cha fedha, basi ISON BPO wasitische mkataba na Airtel ili idara au kitengo cha huduma kwa wateja kirudishwe Airtel. au;
2. ISON BPO kama mwajiri ajadiliane na wafanyakazi ili angalau awalipe laki tatu na nusu 350,000/-; na wakamalizia kwa kusema wao kama Wizara hawana mamlaka ya kumlazimisha ISON BPO alipe kiwango hicho cha mshahara, na huo ukawa mwisho wa kazi yao kama Wizara.

Mheshimiwa Spika,

Kambi Rasmi ya Upinzani tunataka kupata majibu ya malalamiko ya wafanyakazi hao wapatao 500 kama ifuatavyo;

1. ISON BPO, ilisajiliwa kwa leseni na sheria ipi ya nchi? 2. ISON BPO, kwa nini wanaendelea kukaidi agizo la Serikali kwa kukataa kulipa mishahara stahiki na iliyopendekezwa na Serikali yaani 400,000/- TZs. na badala yake wanalipa mishahara kwa kiwango wanachojua na kutaka wenyewe? 3. Wizara ya Kazi na Ajira, kwa nini inakuwa na kigugumizi na kushindwa kuchukua hatua madhubuti dhidi ya ISON BPO katika mgogoro huu ilhali inajua kinachoendelea kufanywa na hawa ISON BPO ni ukiukwaji wa sheria za nchi na kuisababishia Serikali kupoteza pato la Taifa kupitia P.A.Y.E. ya wafanyakazi hawa?

USALAMA MAHALI PA KAZI (OSHA)

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu katika hotuba zetu tumekua tukionesha wasiwasi wetu juu ya masuala yanayohusu usalama na afya mahali pa Kazi. leleweke kuwa, kwa muda mrefu tumekua tukiwasilisha malalamiko mbalimbali yanayoletwa na wafanyakazi lakini Serikali imeendelea kuyapuuza. Maeneo mbalimbali ya kazi yamekua hayazingatii usalama na afya za wafanyakazi wake na hivyo kuhatarisha maisha yao. Leo hii kuna watanzania wengi waliopoteza maisha, watanzania waliopata ulemavu na matatizo makubwa ya kiafya kutokana na kukosa usalama makazini. Lakini watanzania hawa, hawajapewa fidia kutokana na madhara waliyopata na mbaya zaidi wengi wamekua wakiachishwa kazi hasa pale wanapokua wakidai haki zao dhidi ya waajiri.

Mheshimiwa Spika,

Sehemu za migodini, viwanda pamoja na sekta ya ujenzi ndio maeneo yanayoongoza kwa ajali mbaya na za kusikitisha zinazotokea mahala pa kazi. Ikumbukwe kuwa mpaka leo hii Serikali yako baada ya kupokea malalamiko ya wafanyakazi 79 walioachishwa kazi na kampuni ya uchimbaji iliyokuwa ikijulikana kama African Barrick Gold Mining, ni wafanyakazi 10 tu pekee ambao walipimwa afya na Wizara kupitia OSHA. Je, ni nini hatma ya wafanyakazi 69 ambao mpaka leo hawajapimwa? Ni nini hatma ya wafanyakazi wote 79 ambao wanaendelea kupata madhara pamoja na ahadi ya Serikali ya kuwapima wafanyaaazi hao na kuhakikisha wanapata haki zao kwa mujibu wa Sheria?

Mheshimiwa Spika,

Wakati Serikali ikiwa busy kuandaa mikutano na semina kwa wenye viwanda mbalimbali nchini, inasahau kuwa baadhi ya viwanda na mahali pa kazi hawatekelezi Sheria kwa kiwango kinachotakiwa. Leo hii Serikali inaeleza kuwa imefanikiwa kufanya kaguzi za kushtukiza sehemu za kazi huku ni ukweli usiopingikiza kuwa baadhi za makampuni na viwanda yana ulinzi mkali na iwapo maafisa wa OSHA watafanya ukaguzi, vikwazo vya ulinzi pekee vinatosha kumuandaa muajiri kukwepa wajibu wake na kujiandaa na ukaguzi kwa kuficha mapungufu yaliyopo mahali pa kazi.

MIFUKO YA HIFADHI YA JAMII

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika kipindi chote cha miaka mitano tumeshauri mambo yafuatayo kuhusiana na mifuko ya hifadhi ya jamii hapa nchini;

1. Kuunganisha mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii na kubaki chini ya usimamizi wa Wizara ya Kazi na Ajira lengo likiwa ni kuirahisishia Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Hifadhi za Jamii katika kutekeleza Sheria moja nakuunda vifungu sawa vya kisheria vitakavyosimamia utekelezaji na uendeshaji wa mifuko hii. Tulipendekeza PPF na NSSF iunganishwe na kuwa mfuko mmoja kwa ajili ya Sekta Binafsi vilevile LAPF, PSPF na GEPF iunganishwe na kuwa mfuko mmoja kwa ajili ya Sekta ya Umma.

2. Tumeitaka serikali kuwa na jitihada za haraka kunusuru uhai wa Mifuko ya Hifadhi ya jamii kwa kulipa fedha walizochota kwa ajili ya uwekezaji katika miradi mikubwa kama ambavyo imeonyeshwa katika Ripoti za Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2012/2013, 2013/2014 lakini ripoti ya CAG ambayo imetolewa hivi karibuni ya 2014/2015.

Mheshimiwa Spika,

Ni kweli kuwa sikio la kufa halisikii dawa. Madeni sugu ya serikali yanatishia uhai wa mifuko ya hifadhi ya jamii nchini huku Mamlaka ya Usimamizi ya Mifuko hiyo (SSRA) ikitoa angalizo kwa serikali kuhusiana na hali hiyo kufuatia kuidai Sh. trilioni 8.43 kuwa hali hiyo inaweza kukwamisha mifuko hiyo kuwalipa mafao wanachama wake, kujiendesha yenyewe na kuwekeza katika miradi mbali mbali. Mkurugenzi wa SSRA, Irene Isaka alitoa tahadhari hiyo Oktoba mwaka jana mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa kuwakutanisha wakurugenzi wa mifuko ya hifadhi ya jamii, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi wa Mkuu wa Hesabu za Serikali, SSRA na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ambapo alieleza kuwa iwapo serikali itaendelea kukopa na kutopeleka michango ya wanachama wake, mifuko hiyo itaathirika kiasi cha kushindwa kulipa mafao kwa wanachama wake.

“ tuliyonayo, mifuko yetu ni ya pensheni, hasara ni ya mifuko. Mwanachama hatamsamehe mwenye mfuko kwa kushindwa kumlipia, kadri deni linavyoongezeka ndivyo Mfuko unaumia na baadaye kushindwa kulipa mafao yanayotakiwa.”

Mheshimiwa Spika,

Kauli hii ni ya msimamizi mkuu wa mifuko ya hifadhi ya jamii ambaye ndiye mwenye dhamana ya uhai wa mifuko hii. Mara kadhaa Kambi ya upinzani imeeleza na kuonya jinsi ambavyo madeni haya ambayo ni pamoja na PPF (bilioni 192), NHIF (bilioni 107), NSSF (bilioni 467), PSPF (bilioni 4.29), LAPF (bilioni

170) na GEPF (bilioni 6.86) yanavyohatarisha uhai wa mifuko hii. Si Raisi Kikwete wala viongozi waandamizi wa CCM wenye kuelewa kuwa, hili ni bomu litakapolipuka muda wowote. leleweke kuwa hakuna mpinzani yeyote anayepinga miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa chuo kikuu cha Dodoma (UDOM). Tunachokipinga ni kitendo cha Serikali kutumia fedha za wachangiaji wa mifuko kwa miradi yake ambayo ingeweza kutekeleza ipasavyo kwa kutumia fedha nyingine na kama ingefuta misamaha ya kodi, ingepigana ipasavyo kuzuia ufisadi na ubadhirifu kama wa ESCROW, EPA, RICHMOND-DOWANS na/ au kama ingeweza kupunguza matumizi makubwa ya serikali.

Mheshimiwa Spika,

Huwezi kuukataa ukweli kuwa utawala wa awamu ya nne umeshindwa kuipa wizara ya fedha uwezo wa kitaasisi wa kukusanya kodi matokeo yake, serikali inakuwa inakodolea macho fedha za mifuko ya hifadhi ya jamii na hii ni dhambi ambayo haitafutika machoni pa watanzania. Na sasa tunaelewa ni kwa nini serikali ilikuwa inaishinikiza wachangiaji wa mifuko wasichukue pensheni zao mpaka wafikishe umri wa kustaafu ambao ni miaka 60, kwa kuwa wanajua umri wa maisha ya wa watanzania ni miaka 52. Hatuwezi kuwa na serikali ambayo ina trade-off na ustawi wa maisha ya watu wake, hii ni aibu kubwa!

MFUKO WA TAIFA WA HIFADHI YA JAMII (NSSF)

Mheshimiwa Spika, mfuko wa hifadhi ya jamii, NSSF, ni mojawapo ya mifuko ambayo mbali ya kutoa mafao ya kustaafu na huduma zingine kwa kadri dira na dhima yake lakini bado inajishughulisha katika uwekezaji kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa takwimu zilizopo ni kwamba mbali ya kuwekeza kwenye ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu cha Dodoma na Daraja la Kigamboni, pia NSSF ina miradi ifuatayo ya ujenzi wa nyumba;

- i. Nyumba 300 za Mtoni Kijichi (PHASE I &II) –Nyumba hizo zilikwisha uzwa tayari
- ii. Nyumba 800-Flats 500 na Villas 300 (PHASE III) ambao umegharimu shilingi bilioni 137.
- iii. Mradi wa AZIMIO SATELITE -Kigamboni wenye Nyumba 7160 (Flats &Villas) –Utagarimu shilingi bilioni 871
- iv. Mradi wa Dungu Farm-Kigamboni (Flats 568) Utagarimu shilingi bilioni 140
- v. Mradi wa MZIZIMA TOWER nyumba ya Ghorofa 32 unaotarajiwa kumalizika Juni 2017, ambao utagarimu shilingi bilioni 233. Lakini hadi sasa bado mradi haujaanza.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi sio kama inapinga uwekezaji unaofanywa na NSSF, je uwekezaji huo unafanywa kwa kuangalia kipindi ambacho miradi hiyo itarejesha faida za uwekezaji (return on investment)?

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 3.12 cha mwongozo wa Msimamizi wa Mifuko ya Hifadhi(SSRA) wa mwaka 2003, pamoja na kanuni zake kuhusu uwekezaji salama wa mifuko na marejeo yake ya mwaka 2012 ni kwamba, mifuko inatakiwa kuwekeza asilimiai 70 ya mali zake kwenye dhamana (T-Bills) na hati fungani (T-Bonds), asilimia 25 ya mali zake kwenye Miundombinu, asilimia 30 ya mali zake kwenye mali isiyohamishika (Real Estates). Je, ni kwa kiasi gani NSSF imefuata Sheria na kanuni kuhusu uwekezaji wake mpaka sasa kwa kufuatia mgawanyo uliotajwa?

Mheshimiwa Spika, NSSF walinunua majengo ya Manji (EPZ-Project) kwa jumla ya shilingi bilioni 47.5 mwaka 2006, kwa mujibu wa taarifa mbalimbali, ni kuwa majengo hayo hayakuwa na thamani hiyo wakati NSSF inayanunua. Pamoja na hayo, mradi huu unasemekana mpaka sasa kutorudisha thamani ya uwekezaji kwa muda. Kambi ya Upinzani Bungeni inahusisha upandishaji huo wa thamani isiyo halisi kuwa ni mojawapo ya mianya ya watendaji wa NSSF kujipatia 10% kwa miradi isiyo na tija. Aidha, kodi ya mwaka ya Jengo hilo inayotokana na upangaji, haijaweza kuakisi marejesho ya faida ya uwekezaji huo kwa kuwa mradi huo mpaka sasa umeshindwa kurudisha hata nusu ya fedha zilizowekezwa na hivyo kuhatarisha uwezo wa mfuko kutoa marejesho kwa wanachama wake.

Kwa mujibu wa sheria ya SSRA, Benki Kuu ndio mamlaka ya kuhakikisha mifuko inafanya uwekezaji makini, je kwa uwekezaji huu ambao taarifa ya CAG ilisema kuwa unauweka mfuko katika hali ya kuweza kufilisika na hivyo wanachama kukosa mafao, Wizara ya Fedha inatoa majibu gani?

Mheshimiwa Spika, kuonesha kuwa uwekezaji wa NSSF umekuwa ukiongozwa na matakwa ya watu binafsi, kuna jengo la ghorofa 4 lililojengwa Kigoma kwa gharama ya shilingi Bilioni 7 na limekamilika sasa ni miaka 2, lakini hadi muda huu halijapata mpangaji. Kambi ya Upinzani inahitaji kupata majibu ya uhakika kuhusu uwekezaji huu usio na tija ni nini hatma ikiwemo uwajibikaji wa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi kwa kushindwa kuusimamia mfuko ipasavyo?

Mheshimiwa Spika, NSSF imenunua ardhi mikoa kadhaa kwa bei ambayo ni zaidi ya ile ya soko (Inflated price) na mwishowe viwanja hivyo vinakosa wanunuzi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa NSSF kukataa kuwekeza kwenye dhamana za Serikali na kuwekeza kwenye majengo ni wa kutia shaka na ni mwanya wa watendaji wake kupokea rushwa au makampuni yanayopewa kandarasi za ujenzi ni makampuni yao na hivyo uwekezaji huo kuwanufaisha wao binafsi na si wanachama wa mfuko.

Kambi ya Upinzani Bungeni, inataka majibu ya kina kutoka kwa Wizara juu ya uwekezaji mzima unaofanywa na NSSF bila kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo kwa kuwa ni dhahiri kuwa uwekezaji mkubwa usio na tija unaofanywa na NSSF unahatarisha kwa kiwango kikubwa uhai wa mfuko huu.

PENSHENI KWA WAZEE.

Mheshimiwa Spika, Wazee nchini wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kutokupata matibabu bure, kupoteza mali zao na haki ya kurithi, kuuwawa kwa imani za kishirikina ikiwemo wazee 2,866 waliuwawa katika mikoa 10 kwa kipindi cha miaka 5 iliyopita sawa na wastani wa wazee 573 kila mwaka au takribani mzee mmoja anauwawa kila siku. Tumeendelea kushuhudia wazee katika nchi hii kupuuzwa, kunyanyasika na kudharauliwa huku wakijisahau kuwa na wao pia ni wazee watarajiwa. Ikumbukwe kuwa ilikua ni ahadi ya uchaguzi ya Rais Kikwete kuwa wazee watalipwa pensheni.

Mheshimiwa Spika,

Kwa mujibu wa sensa ya Watu na Makazi, 2012 wazee nchini ni milioni 2,507,568 sawa na asilimia 5.6 ya idadi yote ya watanzania. Ongezeko la wazee nchini na duniani ni jambo lisilowezwa kupuuzwa tena kwani mtu mmoja katika watu tisa ni mzee, hata hivyo idadi hii inategemewa kuongezeka hadi kufikia mzee mmoja katika watu watano ifikapo 2050.

Katika hotuba zetu za miaka mitano mfululizo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tumeendelea kusisitiza umuhimu wa wazee kupewa pensheni, na Serikali imekua ikitoa kauli kuwa utoaji wa pensheni kwa wazee unafanyiwa utafiti ama uko katika hatua za mwisho. Aidha, kauli za Serikali kuwa wazee wapatiwe matibabu bure imekua ni changa la macho kwa kuwa wazee wengi wamepata usumbufu katika kupata huduma za afya na wengine wameshindwa kabisa kupata huduma hizo. Kwa kuwa kauli ya kuwapa wazee pensheni ilitumiwa na CCM katika uchaguzi, tunawataka wazee kuwa makini kwa kuwa CCM hawa hawa, watarudi tena na kauli ya kuwalipa pensheni kwenye kampeni za Uchaguzi Mkuu kwa nia ya kuwaomba kura. Tunapenda kuwakumbusha wazee wetu kuwa *'zimwi likujalo halikuli likakishwa'*. Na iwapo itatokea CCM kuwafata kuomba kura wasisahau kuwakumbusha CCM kuwa *'baniani mbaya kiatu chake dawa'*.

Mheshimiwa Spika,

Baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni naomba kuwasilisha.

**CECILIA DANIEL PARESSO (MB)
MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI
WIZARA YA KAZI NA AJIRA
25.05.2015**

MWENYEKITI: Sasa namwita Msemaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Esther Matiko! Dakika 20!

**HOTUBA YA MHESHIMIWA SALUM KHALFAN BARWANY (MB) MSEMAJI MKUU WA
KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA
WATOTO KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI
KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016
(Inatolewa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za
Bunge kanuni ya 99(9) toleo la mwaka 2013)
KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

MHE. ESTHER N. MATIKO (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote naomba kutoa pole kwa ndugu zangu, jamaa na marafiki maana weekend hii tumeweza kuwapoteza ndugu zetu watatu; kwanza kabisa baba yetu Mpendwa, Richard Msingi, ambaye alikuwa ni Mtumishi wa TAMISEMI aliyefariki siku ya Jumamosi, lakini pia, kaka yetu mpendwa, ndugu Julius Nyanabwa, aliyefia Mwanza, Sekoutoure na bibi yetu Mpendwa, Robi Chacha Chaboka, aliyegongwa na pikipiki Mjini Tarime na kupoteza maisha. Tunaomba Mwenyezi Mungu, azilaze roho zao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(9) ya Mwaka 2013, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuwasilisha Hotuba hii napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuungana na wananchi wa Burundi na wapenda amani duniani kote kulaani mauaji ya Kiongozi wa Upinzani huko Burundi, Z. Ferouz, Mkuu wa Chama cha Umoja wa Amani na Demokrasia (UPD-Zingamibanga) aliyeuawa kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana Mjini Bujumbura, huku machafuko yakiendelea nchini humo.

Kiongozi huyo aliuawa Jumamosi usiku alipokuwa akiingia nyumbani kwake katika eneo la Ngagara; mlinzi wake pia, ameuawa katika tukio hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani Bungeni inalaani mauaji haya kwa kuwa, ni mwendelezo wa Vyama Tawala kudhuru na hata kutoa uhai wa Wapinzani. Wao pale wanapoonwa wameshindwa ama hawakubaliki tena kwa wananchi. Ni wajibu wetu Wapinzani kusemea haya kwa kuwa, hata nchini kwetu Tanzania hatupo salama na tunaamini kuwa, Mungu atatusimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa damu yetu itamwagika katika dhuluma na haki, vizazi vyetu vitasimama na kupaza sauti zao dhidi ya watawala dhalimu. Mwenyezi Mungu azilaze roho za wahanga hawa kwa dhuluma ya kisiasa, mahali pema peponi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Kivuli...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther?

Mheshimiwa Esther, hayo yamo kwenye Hotuba yako?

MHE. ESTHER N. MATIKO (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO): Mheshimiwa Mwenyekiti, No! Nimeona Taarifa ya Habari jana usiku, nimeyaweka mimi kwenye Hotuba yangu...

MWENYEKITI: Unayoendelea kusema yamo kwenye hotuba yako, soma yaliyomo kwenye Hotuba!

MHE. ESTHER N. MATIKO (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Kivuli wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Barwany, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na kunisimamia katika maisha yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii pia kuwashukuru, ndugu, jamaa na marafiki wa familia ya Mheshimiwa Barwany kwa kuendelea kuwa pamoja naye kwa hali na mali. Nawashukuru vile vile wananchi wa Lindi Mjini kwa kumpa ushirikiano mkubwa Mbunge wao na napenda kuwahakikishia kwa niaba yake kuwa Oktoba 2015, ataendelea kuwatumikia kama mwakilishi wao kwa ushindi mnono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanaharakati wa Haki za Kiraia na Mkulima maarufu wa Marekani Cesar Chavez aliwahi kusema, *“Hatuwezi kutaka mafanikio kwa ajili yetu tu na kusahau maendeleo na ustawi wa jamii yetu.*

Malengo yetu ni lazima yawe makubwa kiasi ili kujumuisha matarajio na mahitaji ya wengine kwa ajili yao na kwa ajili yetu pia”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni tafsiri ya maneno ya Cesar Chavez kwa nukuu ya lugha ya Kiingereza ni kama ifuatavyo; *“if we cannot seek achievement for ourselves and forget about progress and prosperity for our community, our ambitions must be broad enough to include the aspirations and needs to others, for their sakes and for our own.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa tumebakiza miezi michache takribani miezi minne mpaka ufanyike uchaguzi mkuu ni dhahiri kuwa tutasikia kauli nyingi zenye kulenga kuwaaminisha Watanzania kuwa Serikali ya CCM itakwenda kutekeleza matarajio ya Watanzania waliyokuwa nayo chini ya utawala wa Rais Jakaya Mrisho Kikwete yalitolewa wakati wa Uchaguzi wa mwaka 2005 na pia uchaguzi Mkuu wa 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tuikumbushe Serikali ya CCM usemi kuwa mla ndizi husahau ila mtupa maganda hasahau. Pamoja na kuwa Serikali ya CCM ilitoa ahadi kemkem zikiwemo za kuinua maisha ya Watanzania kwa kauli ya maisha bora kwa kila Mtanzania, mpaka kufikia leo mwaka 2015, hali za Watanzania zimeendelea kuwa duni tangu kuanza kwa utawala wa Awamu ya Nne hasa kwenye Sekta ya Maendeleo ya Jamii , Jinsia na Watoto. Ni wajibu wetu kuwakumbusha wanaoachia madaraka kuwa Watanzania ambao kwao ni watupa maganda, hawajasahau ulaghai na ahadi zilizotolewa kwao mwaka 2005 na 2010 kwa kuzingatia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maendeleo ya Jamii; ni dhahiri kuwa kwa hali iliyopo sasa, Taifa letu limekumbwa na mporomoko mkubwa wa maadili unaochangiwa na kasi kubwa ya utandawazi. Tanzania ni moja kati ya Mataifa ya Afrika yenye uwezo wa kutumia historia na utamaduni wake katika kukuza maadili na jamii yenye staha. Hata hivyo, katika miaka ya karibuni, Taifa letu limeshuhudia vitendo vya kuporomoka kwa maadili ambavyo vimechangia kukithiri kwa vitendo vya ubakaji na ulawiti, wizi na ujambazi, mauaji, biashara ya ngono, ulevi, ngoma na sherehe zisizo na staha, waathirika wa madawa ya kulevya na ongezeko kubwa la maambukizi ya UKIMWI na magonjwa mengine ya zinaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuvo vya Maendeleo ya Jamii na Wataalam wa Maendeleo ya Jamii; kwa muda mrefu sasa Kambi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiitaka Serikali kuhakikisha kuwa masuala ya kimkakati ya kuzuia ama kupunguza mmomonyoko wa maadili kwa kuvipa uwezo Vyuvo vya Maendeleo ya Jamii pamoja na vya Maendeleo ya Wananchi ili kuongeza idadi ya wataalam na kuwatumia wataalam hao kwa maendeleo ya jamii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa Vyuo vilivyopo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Wananchi havikidhi ongezeko la watu nchini na pia havipewi kipaumbele katika kuviwezesha kutoa elimu na ujuzi unaofaa kwa wataalam wa maendeleo ya jamii nchini kwa kuwa Serikali imeendelea kutenga bajeti finyu. Vyuo vingi vimeendelea kuwepo katika majengo ambayo ni chakavu, vyenye ukosefu wa miundombinu bora na ambavyo haviwezi kuendelea kutokana na gharama kubwa za uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upungufu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii Nchini; tukiwa tunajadili bajeti ya mwaka ujao wa 2015/2016, huku randama za Wizara hii zikionesha kuwa Maafisa wa Maendeleo ya Jamii Nchini wanakadiriwa kufikia asilimia 29 tu, huku Sera ya Maendeleo ya Jamii ikitaka kuwepo kwa mtaalam ama Afisa Maendeleo ya Jamii katika kila Kata. Hii ni mojawapo ya sababu inazofanya jamii za Kitanzania kukumbana na changamoto kama nilivyoorodhesha awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kushangaza kuwa pamoja na kuwa na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ambavyo kwa mwaka 2014/2015, pekee vilikadiriwa kudahili jumla ya wanafunzi 3,594, lakini bado kuna upungufu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii nchini. Ikiwa Serikali inajivunia ongezeko la wanafunzi katika Vyuo hivi, je ni nini kinachowashinda Serikali kuajiri wahitimu wa vyuo hivi ili kukabiliana na upungufu wa Maafisa wa Maendeleo wa Jamii nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi duni katika fani za maendeleo ya jamii na wananchi ni mojawapo ya sababu zinazosababisha kuwe na uhaba wa wataalam hao hasa katika ngazi za Kata. Baadhi ya wahitimu wameshindwa kujiunga na kazi zinazohusiana na fani hii na kukimbilia katika kada nyingine ili waweze kujikwamua kiuchumi. Hii ni mojawapo ya sababu zinazofanya Serikali ya CCM isiwe na tija kwa muda wa miaka 10 ya kipindi cha Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kumbukumbu Rasmi za Bunge lako zinaonesha kuwa kwa kipindi cha miaka mitano toka kuanza kwa Mkutano wa Kumi, Kambi ya Upinzani katika kila mjadala wa bajeti imekuwa ikiishauri Serikali kuajiri wahitimu wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii moja kwa moja na kuwapangia vituo katika Kata mbalimbali nchini. Kwa kuwa Serikali imeendelea kupuuza maoni yetu ya Kambi ya Upinzani Bungeni, ni dhahiri kuwa Serikali imeshindwa kutekeleza jukumu lake la kuwa mlezi wa jamii zetu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la aibu kubwa kwa Serikali ya CCM ambayo toka utawala wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Nyerere, haijaviendeleza hata Vyuo vilivyoanzishwa na kujengwa kati ya miaka 1950 na 1963. Ni aibu kwa Serikali inayojivunia mafanikio, kujivunia kuchakaa kwa

majengo ya vyuo vilivyoanzishwa kwa nguvu ya Baba wa Taifa na kusababisha uchakavu mkubwa. Leo CCM inaposema inamuenzi Mwalimu Nyerere, je, inamuenzi kwa kuchakaza juhudi zake na kugeuza vyuo hivyo magofu? Ikiwa Serikali ya CCM imeweza kuacha kutumia magari ya zamani chakavu na kununua mashangingi kwa ajili ya viongozi wa Serikali, inashindwaje kuvipa hadhi vyuo hivyo vilivyojengwa toka enzi za Mwalimu? Hii ni aibu kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa matumizi makubwa ya Serikali, misamaha ya kodi isiyo na tija kwa Taifa, imekuwa chanzo kikubwa cha kudumaza Taifa. UKAWA inajipanga kukabiliana na matumizi makubwa ya Serikali pamoja na kupunguza misamaha ya kodi ili kujenga Vyuo vya Maendeleo pamoja na kuvikarabati vyuo chakavu kwa mustakabali wa Taifa letu na vizazi vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa, ili kuendeleza jamii yoyote kuwa jamii bora na yenye maendeleo, basi kipaumbele kikubwa kiwe kuhusisha masuala ya wanawake katika mikakati ya kiseru na ujumuishaji wake katika shughuli mbalimbali za maendeleo. Pamoja na kuwa na ongezeko la wanawake katika ngazi mbalimbali za maamuzi ikiwemo ongezeko la Majaji, Mawaziri, Wakuu wa Wilaya pamoja na Wabunge ni dhahiri kuna changamoto kubwa katika kuhakikisha wanawake wanapewa nafasi kutokana na sifa walizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwezeshaji wa Kiuchumi; kwa mujibu wa Sensa iliyofanyika mwaka 2012 inaonesha kuwa kati ya Watanzania milioni 45, wanawake ni milioni 23. Pamoja na kuwa kundi hili la wanawake limechanganywa na watu walio chini ya umri wa miaka 18, inaleta taswira kuwa idadi ya wanawake nchini ni kubwa na hivyo takwimu za uwezeshaji kwa kundi hili la wanawake zinazotolewa na Serikali zinaacha kundi kubwa la wanawake likiwa halijafikiwa na mafunzo na mikopo ya uwezeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwa mujibu wa takwimu za Wizara hii zinaonesha kuwa ni wanawake 11,350 tu walioweza kufikiwa na Benki ya Wanawake Tanzania ambao kwa mujibu wa taarifa hii ni sawa na asilimia 87 na wanaume 1,642 sawa na asilimia 13 kati ya mwaka 2009 na 2014. Hii ni kiini macho cha mchana kweupe kwa kuwa ikiwa kwa mujibu wa Sensa, wanawake na wanaume wenye umri juu ya miaka 15 ni takribani 25,200,000, basi kwa muda wa miaka mitano, Benki hii imeweza kuwanufaisha kwa asilimia 0.49 ya wanawake na wanaume wa Tanzania nzima kwa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoandikwa katika Mwongozo wa Sera ya Ukatili wa Kijinsia ya mwaka 2011, ukatili wa kijinsia ni tatizo kubwa ambalo linawanyima uhuru wanaume, wanawake na watoto kufurahia haki za msingi za

binadamu na kufanya wapendavyo. Licha ya tatizo hilo kuwepo katika nchi nyingi duniani lakini halipewi kipaumbele wala halishughulikiwi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukatili wa kijinsia unatokana na tofauti za kijinsia na baadhi ya mila na desturi potofu ambazo mara nyingi zinasababisha kuwepo kwa tofauti za kijinsia katika ngazi mbalimbali za jamii. Wanawake kutothaminiwa katika familia, hali duni ya uchumi na kutofahamu sheria kunawafanya washindwe kupata msaada pindi kunapotokea ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa asilimia 45 ya wanawake wametendewa ukatili wa kijinsia. Pia, kwamba wasichana watatu kati ya 10 wametendewa angalau tendo moja la ukatili wa kijinsia kabla ya kufikia umri wa miaka 18. Vile vile, asilimia 13 ya watoto wa kiume wenye umri ule ule wamefanyiwa matendo ya ukatili kabla ya kufikisha umri wa miaka 18. Leo Serikali inapoongelea kuhusu kufanikiwa kudhibiti ukatili wa kijinsia, unazungumzia kufanikiwa katika kuyalinda makundi haya ama katika kuandaa semina na warsha zinazowanufaisha watu wachache?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mimba za Utotoni; kutokana na taarifa ya umaskini ya maendeleo ya watu ya 2011, mimba za utotoni zilifikia 1,056 kwa mwaka mmoja tu. Wasichana wote hawa waliacha shule. Leo hii tukimaliza miaka kumi ya utawala wa Rais Jakaya Kikwete, tunamaliza na maumivu ya kauli yake aliyoitoa mwaka 2010 akiwa katika ziara Mkoani Mwanza akisema kuwa matukio ya mimba kwa wanafunzi wa kike nchini yanasababishwa na viherehere vya wanafunzi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Rais kutoa kauli inayowatupia lawama wanafunzi wa kike bila uchambuzi, kunaenda kinyume na azma ya Serikali kuwajibika kwa wananchi kuhusu kufanyia kazi matatizo ya msingi yanayosababisha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kupata ujauzito. Ikumbukwe kuwa, kwa mujibu wa Wizara ya Elimu, mpango wa Serikali kuhusu shule za sekondari za Kata ulilenga shule hizo zijengwe karibu na makazi ya wananchi ili watoto waweze kutoka nyumbani na kwenda shuleni na kurudi nyumbani kwa urahisi kwa lengo la kuhakikisha kuwa watoto wengi wanapata elimu nzuri na bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa asilimia kubwa utekelezaji wa mpango huo haujafanyika kama ilivyokusudiwa kwa sababu kuna maeneo mengi nchini ambapo wanafunzi wengi tena wenye umri mdogo chini ya miaka 17, bado wanalazimika kutembea zaidi ya kilomita kumi kila siku kwenda shuleni huku wakipita katikati ya mapori, mabonde na milima yenye hatari mbalimbali kwa maisha yao ukiwemo ubakaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wanafunzi hawa wanaopata mimba za utotoni ambao wanakaa katika maeneo ambayo yana shida za maji na hivyo kulazimika kutembea umbali mrefu baada ya masomo ili kupata maji kwa matumizi ya majumbani mwao. Kushindwa kwa sera ya Serikali ya CCM ndiyo kumpelekea watoto wa kike kukumbwa na mimba za utotoni. Kushindwa kwa Serikali kusimamia utekelezaji wa ahadi zake za kipindi cha uchaguzi ndizo zinazosababisha ongezeko la mimba za utotoni, hivyo kauli ya Rais Kikwete si tu iliwaumiza waathirika wa mimba za utotoni bali pia iliwadhalilisha wazazi maskini wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la watoto wa mitaani na athari zake katika Taifa. Wakati piramidi ya idadi ya watu nchini Tanzania inaonesha kuwa idadi kubwa ya watu nchini Tanzania ni watoto wenye umri wa chini ya miaka 15 na vijana. Asilimia 44 ya watu wote hapa nchini ni watoto wenye umri chini ya miaka 15, ambapo ongezeko la watoto wa mitaani limeendelea kuwa na athari huku sababu mbalimbali kama umaskini katika familia, mifarakano na ukosefu wa amani kwenye familia na wazazi kutowajibika katika malezi na makuzi ya watoto wao vikipelekea watoto hao kuishi katika mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine ni vitendo vya ukatili, udhalilishaji na unyanyasaji wa watoto kutoka kwa familia na jamii kwa ujumla. Nyingine ni kufariki kwa wazazi hasa kutokana na magonjwa mbalimbali, pia huchangiwa na ndoa za umri mdogo pamoja na mimba zisizotarajiwa. Kambi ya Upinzani Bungeni imenuia kujenga mfumo wa utambuzi wa miji inayoongoza kwa watoto wa mitaani na kuwaweka watoto hawa wa mitaani chini ya uangalizi wa walezi watakaokuwa wakiwezesha na Serikali yaani *Foster Parents* ili kupunguza idadi ya watoto wa mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi ya Upinzani imejiandaa kuhakikisha kuwa vituo vya kulelea watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi hasa yatima, wanaweka mfumo wa kumbukumbu na taarifa kamili ili kufuatilia maendeleo yao popote walipo nchini Tanzania kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ya watoto kwa kuwa vituo vingi vimeendeshwa bila kuwanufaisha watoto hasa wanaoishi katika vituo hivyo na kwenye mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya masikitiko, napenda kuzungumzia hali ya maendeleo ya watoto wenye ulemavu mbalimbali hapa nchini. Pamoja na kuwa Wizara imepewa dhamana ya kuhakikisha maendeleo ya watoto wenye ulemavu ni endelevu, bado mikakati ya Serikali imeendelea kuweka kundi hili la watoto katika hatari kubwa. Kundi hili la watoto wenye uhitaji maalumu kama walemavu wa viungo, macho, usikivu na ngozi hawajawekewa uzito wa kutosha na hivyo kuwafanya wanyonge na washindwe kuendelea kwa kasi ile ile kama watoto wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mawasilisho ya Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Barwany ambaye ni Waziri Kivuli wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto lakini akiwa ni mlemavu wa ngozi alionesha wasiwasi wake juu ya dhamira ya Serikali katika kuwalinda watu wenye ulemavu wa ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Sera, Uratibu na Bunge Mheshimiwa Jestina Mhagama alisimama na kutoa maelezo kuwa Serikali imeandaa utaratibu wa kuwalinda watu wenye ulemavu wa ngozi kwa kuwaandalia *tracking devices system* yaani mfumo wa kutambua mienendo ya mlengwa ambayo inafanywa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa watu wenye ulemavu wa ngozi na masuala ya usalama. Mheshimiwa Barwany hakuridhishwa na kauli ile kwa kuwa yeye pia ni mmoja wa watu wanaoishi kwa wasiwasi kwenye Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zikiwa zimepita siku mbili toka Mheshimiwa Barwany kuonesha wasiwasi wake juu ya mfumo wa ulinzi kwa watu wenye ulemavu wa ngozi nchini mwanamama Remi Luchoma alikatwa mkono na watu wasiojulikana Mkoani Katavi. Hii ni aibu kubwa kwa Serikali na ni dhahiri kuwa, imeshindwa kuwalinda watu wenye ulemavu kwa kuwa kwa masikitiko na uchungu mkubwa, miezi mitatu (3) iliyopita mwili wa mtoto Yohana Bahati aliyekuwa na umri wa mwaka mmoja tu ambaye alikuwa ni mlemavu wa ngozi maarufu kama *Albino*, ambaye alitekwa siku ya Jumapili Februari, 2015 ulipatikana akiwa ameuawa kikatili katika eneo la Shilabela Mapinduzi kilomita kadhaa kutoka nyumbani kwao Kijiji cha Ilelema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayazungumza haya leo kwa kuwa tunapozungumzia maendeleo ya jamii, jinsia na watoto, huwezi kuepuka kuzungumzia wanawake na watoto ambao nao wana ulemavu na hasa uliosababishwa na vitendo vya kikatili. Huwezi kuacha kuzungumzia matukio ya kikatili na ya kusikitisha yanayoelekezwa kwa kundi hili muhimu katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa maelezo haya nikiwa na masikitiko makubwa na huzuni nyingi na huku nikiwa natafakari hatma ya watu wenye ulemavu nchini kwetu wenyewe. Je, waikimbie Tanzania? Je, ni nani atamfunga paka kengele? Ni nani atawasaka na kuwazuia watekaji, watesaji na wauaji wa watu wenye ulemavu hasa wa ngozi? Napinga kwa nguvu zangu zote na kuendelea kusikitishwa na vitendo vya kikatili vinavyoendelea dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nitoe wito kwa Watanzania wote kutowabagua watu wenye ulemavu wa ngozi na kuchukua jukumu la kwanza la kuwa walinzi wa haki ya watu wenye ulemavu wa ngozi kuishi kwa kuwa

Serikali ya CCM imeshindwa kuwazuia wauaji na watesaji wa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; Serikali ya CCM imeendelea kuuma na kupuliza kuhusu usimamizi wa mashirika yasiyo ya Kiserikali. Ni Serikali hii ambayo kwa miaka kadhaa imekuwa ikiyapa usajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, lakini Serikali hiyo hiyo ikashindwa kufuatilia utendaji wake kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa kuna baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambayo yamelenga kutumia mwanya uliopo kufanya kazi kinyume na utaratibu uliowekwa, lakini ni ukweli usiopingika kuwa mashirika ambayo yamegeuka kuwa mwiba kwa Serikali hasa kwa kufichua uozo na uovu wa Serikali hii, ndiyo yamekuwa walengwa wa mkakati wa Serikali wa kuyafuta kwa kuwa yanafanya kazi bila kufuata mashinikizo ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kuamini kuwa Serikali inatekeleza mpango wa kuyafutia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hasa kutokana na hofu ya kazi inayofanywa na mashirika hayo, kutoa elimu kwa umma na hasa tunapoelekea Uchaguzi Mkuu wa Oktoba. Ni jambo la kushangaza kuwa Serikali inaeleza changamoto mojawapo za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni kujikita mijini na siyo vijijini kwenye wananchi wengi wenye huhitaji, ikiwa nayo inashindwa kutekeleza wajibu na majukumu yake ya kuhakikisha maendeleo ya jamii yanafuata vijiji na si miji peke yake, inawezaje kuyafuta mashirika haya? Ni nini kinachoifanya Serikali ya CCM ifute mashirika kwa kushindwa kujikita vijijini na nini kitaizua UKAWA kuifuta CCM ambayo imeshindwa kutimiza wajibu wake kwa Watanzania? Tunapenda kuikumbusha CCM kuwa, mwenzako akinyolewa upara, nawe tia maji kichwa chako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ni jambo la kushangaza kuona kuwa taarifa ya Wizara ya utekelezaji unaelezea changamoto kuwa mashirika haya yanategemea ufadhili wa nje katika kutimiza majukumu yao, je, si Serikali hii hii ya CCM ambayo inategemea fedha za nje kuendesha miradi ya maendeleo nchini? CCM imechoka na hii ndio lala salama yao. Amkani si shwari *No Longer at Ease!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, ni katika kadhaa hizi ndipo tunaamini kuwa, kwa kuwa ushauri wetu kwa miaka mingi umepuuzwa; Serikali ya CCM ijijandae kuachia ngazi ifikapo Oktoba, 2015 kwa kuwa Serikali itakayoongozwa na UKAWA imepangwa na imetarajia kurudisha maendeleo ya jamii katika ngazi ambayo Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, alitarajia kutufikisha Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kunukuu maneno ya Baba wa Taifa aliyowahi kusema; “Uhuru na Maendeleo ni vitu vinavyohusiana sana; uhusiano wao ni sawa na uhusiano baina ya kuku na yai! Bila ya kuku hupati mayai na bila mayai kuku watakwisha. Vile vile, bila ya uhuru hupati maendeleo na bila ya maendeleo ni dhahiri kwamba uhuru wako utapotea”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante.

HOTUBA YA MHESHIMIWA SALUM KHALFAN BARWANY (MB) MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 (Inatolewa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge kanuni ya 99(9) toleo la mwaka 2013) KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa kanuni za kudumu za Bunge, Kanuni ya 99 (9) naomba kuwasilisha maoni ya Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Kivuli wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Mhe. Salum Barwany, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na kuendelea kunisimamia katika maisha yangu. Napenda kuchukua fursa hii pia kuwashukuru, ndugu, jamaa, marafiki na familia ya Mheshimiwa Barwany kwa kuendelea kuwa pamoja naye kwa hali na mali. Niwashukuru vilevile wananchi wa Lindi mjini kwa kumpa ushirikiano mkubwa mbunge wao na napenda kuwahakikishia kwa niaba yake kuwa Oktoba 2015, ataendelea kuwatumikia kama mwakilishi wao kwa ushindi wa kishindo.

Aidha, napenda kuchukua fursa kuwashukuru wabunge wote wa Kambi ya Upinzani na watendaji wake kwa ushirikiano mkubwa, viongozi na wanachama wa vyama vinavyounda UKAWA kwa nia yao ya dhati ya kuwakomboa watanзания hasa kuelekea uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2015.

Mheshimiwa Spika, Mwanaharakati wa Haki za Kiraia na Mkulima maarufu wa Marekani Cesar Chavez aliwahi kusema;

“Hatuwezi kutaka mafanikio kwa ajili yetu tu na kusahau maendeleo na ustawi wa jamii yetu... Malengo yetu ni lazima yawe makubwa kiasi ili kujumuisha matarjio na mahitaji ya wengine kwa ajili yao na kwa ajili yetu pia”.

Hii ni tafsiri ya maneno ya Cesar Chavez kwa nukuu ya lugha ya kiingereza ni kama ifuatavyo;

“We cannot seek achievement for ourselves and forget about progress and prosperity for our community... Our ambitions must be broad enough to include the aspirations and needs of others, for their sakes and for our own”

Mheshimiwa Spika, ikiwa tumebakiza miezi michache takribani miezi minne mpaka ufanyike uchaguzi mkuu ni dhahiri kuwa tutasikia kauli nyingi zenye kulenga kuwaaminisha watanzania kuwa Serikali ya CCM itaenda kutekeleza matarajio ya watanzania waliyokuwa nayo chini ya utawala wa Raisi Jakaya Mrisho Kikwete yalitolewa wakati wa Uchaguzi wa mwaka 2005 na pia uchaguzi Mkuu wa 2010.

Mheshimiwa Spika, labda tuikumbushe Serikali ya CCM usemi kuwa ‘Mla ndizi husahau ila si mtupa maganda’. Pamoja na kuwa Serikali ya CCM ilitoa ahadi kemkem zikiwemo za kuinua maisha ya watanzania kwa kauli ya maisha bora kwa kila mtanzania, mpaka kufikia leo mwaka 2015, hali za watanzania zimeendelea kuwa duni tangu kuanza kwa utawala wa awamu ya nne hasa wenye sekta ya maendeleo ya jamii , jinsia na watoto.

Mheshimiwa Spika,ni wajibu wetu kuwakumbusha wanaoachia madaraka kuwa watanzania ambao kwao ni watupa maganda, hawajasahau ulaghai na ahadi zilizotolewa kwao mwaka 2005 na 2010 kwa kuzingatia yafuatayo;

MAENDELEO YA JAMII

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa kwa hali iliyopo sasa, Taifa letu limekumbwa na mporomoko mkubwa wa maadili unaochangiwa na kasi kubwa ya utandawazi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni moja kati ya mataifa ya Afrika yenye uwezo wa kutumia historia na utamaduni wake katika kukuza maadili na jamii yenye staha. Lakini katika miaka ya karibuni, taifa letu limeshuhudia vitendo vya kuporomoka kwa maadili ambavyo vimechangia kukithiri kwa vitendo vya ubakaji na ulawiti, wizi na ujambazi, mauaji, biashara ya ngono, ulevi, ngoma na sherehe zisizo na staha, waathirika wa madawa ya kulevya na ongezeko kubwa la maambukizi ya UKIMWI na magonjwa mengine ya zinaa.

Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa Kambi ya Upinzani Bungeni imekua ikiitaka Serikali kuhakikisha kuwa masuala ya kimkakati ya kuzuia ama kupunguza mmomonyoko wa maadili kwa kuvipa uwezo vyuo vya maendeleo ya jamii pamoja na vya maendeleo ya wananchi ili kuongeza idadi ya

wataalamu na kuwatumia wataalamu hao kwa maendeleo ya jamii nchini. Ni dhahiri kuwa vyuo vilivyopo vya maendeleo ya na vyuo vya wananchi havikidhi ongezeko la watu nchini na pia havipewi kipaumbele katika kuviwezesha kutoa elimu na ujuzi unaofaa kwa wataalamu wa maendeleo ya jamii nchini kwa kuwa Serikali imeendelea kutenga bajeti finyu. Vyuo vingi vimeendelea kuwepo katika majengo ambayo ni chakavu, yenye ukosefu wa miundombinu bora na ambavyo haviwezi kuendelea kutokana na gharama kubwa za uendeshaji.

Upungufu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii Nchini

Mheshimiwa Spika, tukiwa tunajadili bajeti ya mwaka ujao wa 2015/2016 huku randama ya Wizara hii ikionesha kuwa maafisa wa maendeleo ya jamii nchini wanakadiriwa kufikia asilimia 29 tu, huku Sera ya Maendeleo ya Jamii ikitaka kuwepo kwa mtaalamu ama afisa maendeleo ya jamii kwa kila kata nchini. Hii ni mojawapo ya sababu inazofanya jamii ya Kitanzania kukumbana na changamoto kama nilivyoorodhesha awali. Ni jambo la kushangaza kuwa pamoja na kuwa na vyuo vya maendeleo ya jamii ambavyo kwa mwaka 2014/2015 pekee vilikadiriwa kudaili jumla ya wanafunzi 3594 lakini bado kuna upungufu wa maafisa maendeleo ya jamii nchini. Ikiwa Serikali inajivunia ongezeko la wanafunzi katika vituo hivi, je ni nini kinachowashinda Serikali kuajiri wahitimu wa vyuo hivi ili kukabiliana na upungufu wa maafisa wa maendeleo ya jamii nchini?

Mheshimiwa Spika, maslahi duni katika fani za maendeleo ya jamii na wananchi ni mojawapo ya sababu zinazosababisha kuwe na uhaba wa wataalamu hao hasa katika ngazi za kata. Baadhi ya wahitimu wameshindwa kujiunga na kazi zinazohusiana na fani hii na kukimbilia katika kada nyengine ili waweze kujikwamua kiuchumi. Hii ni mojawapo ya sababu zinazofanya Serikali ya CCM isiwe na tija kwa muda wa miaka 10 ya kipindi cha awamu ya nne.

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu rasmi za Bunge lako zinaonesha kuwa kwa kipindi cha miaka mitano toka kuanza kwa Mkutano Wa Kumi (10), Kambi ya Upinzani katika kila mjadala wa bajeti imekua ikiishauri Serikali kuajiri wahitimu wa vyuo vya maendeleo ya jamii mojakwamoja na kuwapangia vituo katika kata mbalimbali nchini. Lakini kwa kuwa Serikali imeendelea kupuuza maoni yetu ya Kambi ya Upinzani Bungeni, ni dhahiri kuwa Serikali imeshindwa kutekeleza jukumu lake la kuwa mlezi wa jamii zetu nchini.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la aibu kubwa kwa Serikali ya CCM ambayo toka utawala wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Nyerere, haijaviendeleza hata vyuo vilivyoanzishwa na kujengwa kati ya miaka 1950 na 1963. Ni aibu kwa Serikali inayojivunia mafanikio, kujivunia kuchakaza majengo ya vyuo vilivyoanzishwa kwa nguvu za Baba wa Taifa na kusababisha uchakavu mkubwa. Leo CCM inaposema inamuenzi Mwalimu Nyerere, je inamuenzi kwa kuchakaza juhudi zake na kugeuza vyuo hivyo magofu? Ikiwa Serikali ya CCM imeweza kuacha

kutumia magari ya zamani chakavu na kununua mashangingi kwa ajili ya viongozi wa Serikali, inashindwaje kuvipa hadhi vyuo vilivyojengwa toka enzi za Mwalimu? Hii ni aibu kubwa.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa kukithiri kwa vitendo kama kangamoko, vigodoro, singo n.k (ambavyo pamoja na Kambi ya Upinzani kushauri kuvipiga marufuku na kuwatia hatiani wahusika), vitendo hivi vinaelekea kuota mizizi na kusababisha mmomonyoko wa maadili kutokana na Serikali kushindwa kutatua changamoto za maendeleo ya jamii nchini! Ni imani yetu kuwa wananchi wamekua mashahidi wa jinsi tulivyojitahidi kusimamia bajeti za Serikali ikiwemo mapendekezo ya kuinua na kuipa hadhi sekta ya maendeleo ya jamii kwa muda mrefu lakini tumepuuzwa. Ni kwa imani hiyo ambayo wataanzania wanayo kwetu UKAWA, tunaamini kuwa mwaka 2016/2017 tutatoa vipaumbele wa kutatua changamoto za maendeleo ya jamii ikiwemo ufinyu wa bajeti, uhaba wa waalimu na wataalamu wa vyuo vya maendeleo ya jamii na vyuo vya maendeleo ya wananchi vyenye kuleta mabadiliko chanya kwa wataanzania wote.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa matumizi makubwa ya Serikali na misamaha ya kodi isiyo na tija kwa taifa, imekua chanzo kikubwa cha kudumaza Taifa. UKAWA inajipanga kukabiliana na matumizi makubwa ya Serikali pamoja na kupunguza misamaha ya kodi ili kujenga vyuo vya maendeleo pamoja na kuvikarabati vyuo chakavu kwa mustakabali wa Taifa letu na vizazi vyetu.

Maendeleo ya Jinsia Nchini

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa ili kuendeleza jamii yoyote kuwa jamii bora na yenye maendeleo basi kipaumbele kikubwa kiwe kuhusisha masuala ya wanawake katika mikakati ya kiseru na ujumuishaji wake katika shughuli mbalimbali za maendeleo. Pamoja na kuwa na ongezeko la wanawake katika ngazi mbalimbali za maamuzi ikiwemo ongezeko la majaji, mawaziri na wakuu wa wilaya pamoja na wabunge ni dhahiri kuna changamoto kubwa katika kuhakikisha wanawake wanapewa nafasi hizo kutokana na sifa. Aidha, changamoto kubwa pia ipo katika ngazi muhimu hasa katika ngazi za chini ambazo zinamuathiri mwanamke moja kwa moja. Ngazi hizi za maamuzi ni pamoja na ngazi za familia na vijijini ambapo mwanamke anaonekana kama mzigo ama chombo kisicho na umuhimu katika maamuzi.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la ukatili dhidi ya wanawake nchini ni mojawapo wa viashiria kuwa, ongezeko la viongozi wanawake katika ngazi za juu hakujamkomboa mwanamke hasa wanaotoka katika mazingira duni kwa namna yoyote ile.

Uwezeshaji wa Kiuchumi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sensa iliyofanyika mwaka 2012 inaonesha kuwa kati ya watanzania milioni 45, wanawake ni milioni 23. Pamoja na kuwa kundi hili la wanawake limechanganywa na watu walio chini ya miaka 18, inaleta taswira kuwa idadi ya wanawake nchini ni kubwa na hivyo takwimu za uwezeshaji kwa kundi la wanawake zinazotolewa na Serikali, zinaacha kundi kubwa la wanawake likiwa halijafikiwa na mafunzo na mikopo ya uwezeshaji.

Kwa mfano, kwa mujibu wa takwimu za Wizara hii zinaoesha kuwa ni wanawake 11350 tu walioweza kufikiwa na Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) ambao kwa mujibu wa taarifa hii ni sawa na asilimia 87% na wanaume 1642 sawa na asilimia 13 kati ya mwaka 2009 na 2014. Hiki ni kiini macho cha mchana kweupe kwa kuwa ikiwa kwa mujibu wa Sensa; wanawake na wanaume wenye umri juu ya miaka 15 ni takribani 25,200,000, basi kwa muda wa miaka 5, Benki hii imeweza kunufaisha asilimia 0.49% ya wanawake na wanaume wa Tanzania nzima kwa miaka 5.

Ukatikili wa Kijinsia

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoandikwa katika Mwongozo wa Sera ya Ukatili wa Kijinsia (MOHSW 2011), ukatili wa kijinsia (GBV) ni tatizo kubwa ambalo linawanyima uhuru wanaume, wanawake na watoto kufurahia haki za msingi za binadamu na kufanya wapendavyo. Licha ya tatizo hilo kuwepo katika nchi nyingi duniani lakini halipewi kipaumbele wala halishughulikiwi ipasavyo. Ukatili wa kijinsia unatokana na tofauti za kijinsia na baadhi ya mila na desturi potofu ambazo mara nyingi zinasababisha kuwepo kwa tofauti za kijinsia katika ngazi mbalimbali za jamii. Wanawake kutothaminiwa katika familia, hali duni ya uchumi na kutofahamu sheria kunawafanya washindwe kupata msaada pindi kunapotokea ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa asilimia 45 ya wanawake wametendewa ukatili wa kijinsia. Pia, kwamba wasichana watatu kati ya 10 wametendewa angalau tendo moja la ukatili wa kijinsia kabla ya kufikia umri wa miaka 18. Vilevile, zaidi ya asilimia 13 ya watoto wa kiume wenye umri ule ule wamefanyiwa matendo ya ukatili kabla ya kufikisha umri wa miaka 18. Leo Serikali inapoongelea kuhusu kufanikiwa kudhibiti ukatili wa kijinsia, unazungumzia kufanikiwa katika kuyalinda makundi haya ama katika kuandaa semina na warsha zinazowanufaisha watu wachache?

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha hata kuona na kusikia Waziri mwenye dhamana akifurahia kujengea kamati ya Kitaifa uwezo wa kukabiliana na ukatili wakati huu ambao ukatili na unyanyasaji dhidi ya wanawake majumbani na sehemu za kazi umeendelea kuongezeka, kati ya wanawake watatu, wawili wanatendewa ukatili wa kijinsia na wanaume.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kuona Serikali ya CCM inajivunia kuwa mtetezi wa wanawake na watoto wakati kama nchi, bado tuna changamoto kwenye sheria za urithi na ndoa ambazo zinarudisha nyuma juhudi za kupigania usawa wa kijinsia.

Mimba za Utotoni

Mheshimiwa Spika, Kutokana na taarifa ya umaskini na maendeleo ya watu ya 2011, mimba za utotoni zilifikia 1,056 kwa mwaka mmoja tu. Wasichana wote hawa waliacha shule. Leo hii tukimaliza miaka kumi ya utawala wa Rais Kikwete, tunamaliza na maumivu ya kauli yake aliyoitoa mwaka 2010 akiwa katika ziara mkoani Mwanza akisema kuwa matukio ya mimba kwa wanafunzi wa kike nchini yanasababishwa na viherehere vya wanafunzi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa Rais kutoa kauli inayowatupia lawama wanafunzi wa kike bila uchambuzi, kunaenda kinyume na azma ya Serikali kuwajibika kwa wananchi kuhusu kufanyia kazi matatizo ya msingi yanayosababisha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari za Serikali kupata ujauzito. Ikumbukwe kuwa kwa mujibu wa Wizara ya Elimu, mpango wa Serikali kuhusu shule za sekondari za kata ulilenga shule hizo zijengwe karibu na makazi ya wananchi ili watoto waweze kutoka nyumbani na kwenda shuleni na kurudi nyumbani kwa urahisi kwa lengo la kuhakikisha kuwa watoto wengi wanapata elimu nzuri na bora zaidi. Lakini kwa asilimia kubwa utekelezaji wa mpango huo haujafanyika kama ilivyokusudiwa kwa sababu kuna maeneo mengi nchini ambapo wanafunzi wengi tena wenye umri mdogo chini ya miaka 17, bado wanalazimika kutembea zaidi ya kilomita kumi kila siku kwenda shuleni huku wakipita katikati ya mapori, mabonde na milima yenye hatari mbalimbali kwa maisha yao ukiwemo ubakaji.

Mheshimiwa Spika, ni wanafunzi hawa wanaopata mimba za utotoni ambao wanakaa katika maeneo ambayo yanashida za maji na hivyo kulazimika kutembea umbali mrefu baada ya masomo ili kupata maji kwa matumizi ya majumbani mwao. Kushindwa kwa sera za Serikali ya CCM ndio kumepelekea watoto wa kike kukumbwa na mimba za utotoni. Kushindwa kwa Serikali kusimamia utekelezaji wa ahadi zake za kipindi cha uchaguzi ndizo zinazosababisha ongezeko la mimba za utotoni, hivyo kauli ya Rais Kikwete si iliwaumiza waathirika wa mimba za utotoni bali pia iliwadhalilisha wazazi masikini wa kitanzania.

Kambi ya Upinzani Bungeni, inaelewa kuwa kuna baadhi ya mimba za utotoni zinazosababishwa na kuporomoka kwa maadili kwa baadhi ya watoto wa kike lakini asilimia kubwa ya wasichana waliopata mimba za utotoni, wanahitaji nafasi kwa ajili ya kurekebisha makosa. Mtoto akinyea mkono, 'hauukati' ni kauli ambayo sisi wazazi tunatumia katika kurekebisha watoto wetu, hivyo kulitenga kundi hili na kutolipa kipaumbele ni kuongeza mzigo katika taifa hasa watoto

wa mitaani. Ni rai yetu kwa watoto wote wa kike nchini, kutumia nafasi finyu waliyopewa katika elimu ili kujikwamua. Sisi UKAWA tunaamini kuwa, kufanya kosa si kosa bali kosa ni kurudia kosa. Tunawataka wazazi wote nchini kuwa walezi na marafiki nambari moja wa watoto wao ili kujenga jamii yenye kuwajibika ili kuondokana na umasikini na matusi ya viongozi wasio na uchungu na maisha yao.

Maendeleo ya Watoto Nchini

Mheshimiwa Spika, tafiti mbalimbali zilizofanyika zinazohusu watoto hapa nchini, zimeonesha kuongezeka kwa idadi ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, wakati watoto yatima wakifikia milioni 2.4. Katika tafiti hizo, zimeonesha kuwa, tatizo la watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi limeonekana Mijini na Vijijini na zaidi kwenye Miji mikubwa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Tanga, Moshi, Dodoma na Mbeya. Idadi ya watoto wanaoishi mitaani imeendelea kuongezeka kutoka 1,579 mwaka 2007 hadi 2,010 mwaka 2011, wakati watoto 11,216 wanaoishi katika Vituo vya Kulelea Watoto kati yao 6,089 ni wavulana na 5,127 ni wasichana. Aidha, idadi ya Watoto Yatima waliopo nchi nzima wamefikia 2,400,000 kati ya hao Wasichana ni 1,055,000 na Wavulana ni 1,345,000, ambapo idadi ya watoto 2,700 kati ya miaka 0-14 wanaoishi na Virusi vya Ukimwi nchini.¹

Mheshimiwa Spika, takwimu hizo zinatoa viashiria na taswira pana juu ya watoto wanaoishi katika Mazingira hatarishi hali ambayo inachangia kwa ongezeko la watoto mitaani pamoja na kukithiri kwa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Katika taarifa ya jumla ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali juu ya ufanisi kwa mwaka 2014, inaonesha kua mfumowa udhibiti takwimu na taarifa za watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi ni dhaifu na haukidhi matakwa ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi²

Ongezeko la Watoto wa Mitaani na Athari zake katika Taifa

Mheshimiwa Spika, wakati piramidi ya Idadi ya Watu nchini Tanzania inaonesha kuwa idadi kubwa ya watu nchini Tanzania ni watoto wenye umri wa chini ya miaka 15 na vijana. Asilimia 44 ya watu wote hapa nchini ni watoto wenye umri chini ya miaka 15, ambapo ongezeko la watoto wa mitaani limeendelea kuwa na athari huku sababu mbalimbali kama umasikini katika familia, mifarakano na ukosefu wa amani kwenye familia na Wazazi kutowajibika katika malezi na makuzi ya watoto wao vikipelekea watoto hao kuishi katika mazingira hatarishi.

¹ Ripoti ya "Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania. Matokeo ya Utafiti wa Kitaifa, 2009: Muhtasari wa Kuenea kwa Ukatili wa Kijinsia, Kimwili na Kiakili, Mukhadha wa matukio ya Ukatili wa Kijinsia, Afya na Athari ya Tabia ya Ukatili iliyotokea utotoni, Dar es Salaam, Tanzania", UNICEF Tanzania

² Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali Hadi Machi 2014 ukurasa wa 11

Sababu nyingine ni vitendo vya ukatili, udhalilishaji na unyanyasaji wa watoto kutoka kwa familia na jamii kwa ujumla, nyingine ni kufariki kwa wazazi hasa kutokana na magonjwa mbalimbali, pia huchangiwa na ndoa za umri mdogo pamoja na mimba zisizotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni imenuia kujenga mfumo wa utambuzi wa miji inayoongoza kwa watoto wa mitaani na kuwaweka watoto hawa wa mitaani chini ya uangalizi wa walezi watakaokuwa wakiwezesha na Serikali (Foster Parents) ili kupunguza idadi ya watoto wa mitaani. Aidha, Kambi ya Upinzani imejiandaa kuhakikisha kuwa vituo vya kulelea watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi hasa yatima, wanaweka mfumo wa kumbukumbu na taarifa kamili ili kufuatilia maendeleo yao popote walipo nchini Tanzania kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ya watoto kwa kuwa vituo vingi vimeendeshwa bila kuwanufaisha watoto hasa wanaoishi katika vituo hivyo na kwenye mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya masikitiko napenda kuzungumzia hali ya maendeleo ya watoto wenye ulemavu mbalimbali hapa nchini. Pamoja na kuwa Wizara imepewa dhamana ya kuhakikisha maendeleo ya watoto wenye ulemavu ni endelevu, bado mikakati ya Serikali imeendelea kuweka kundi hili la watoto katika hatari kubwa. Kundi hili la watoto wenye uhitaji maalumu kama walemavu wa viungo, macho, usikivu na ngozi hajawekewa uzito wa kutosha na hivyo kuwafanya wanyonge na washindwe kuendelea kwa kasi ile ile kama watoto wengine.

Mheshimiwa Spika, wakati wa mawasilisho ya hotuba ya Bajeti ya ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Barwany ambaye ni waziri kivuli wa maendeleo ya jamii, jinsia na watoto lakini akiwa ni mlemavu wa ngozi alionesha wasiwasi wake juu ya dhamira ya Serikali katika kuwalinda watu wenye ulemavu wa ngozi. Waziri wa Sera, Uratibu na Bunge Mheshimiwa Jestina Mhagama alisimama na kutoa maelezo kuwa Serikali imeandaa utaratibu wa kuwalinda watu wenye ulemavu wa ngozi kwa kuwaandalia tracking devices system (mfumo wa kutambua mienendo ya mlengwa) ambayo inafanywa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa watu wenye ulemavu wa ngozi na masuala ya usalama. Mhe. Barwany hakuridhishwa na kauli ile kwa kuwa yeye pia ni mmoja wa watu wanaoishi kwa wasiwasi kwenye taifa hili.

Mheshimiwa Spika, zikiwa zimepita siku mbili toka Mhe. Barwany kuonesha wasiwasi wake juu ya mfumo wa ulinzi kwa watu wenye ulemavu wa ngozi nchini Mwanamama Remi Luchoma alikatwa mkono na watu wasiojulikana mkoani Katavi. Hii ni aibu kubwa kwa Serikali na ni dhahiri kuwa imeshindwa kuwalinda watu wenye ulemavu kwa kuwa kwa masikitiko na uchungu mkubwa, miezi mitatu (3) iliyopita mwili wa mtoto Yohana Bahati aliyekuwa na

umri wa mwaka mmoja ambaye alikuwa ni mlemavu wa ngozi maarufu kama Albino, ambaye alitekwa siku ya Jumapili Februari 15, 2015 ulipatikana akiwa ameuawa katika eneo la Shilabela Mapinduzi kilomita kadhaa kutoka nyumbani kwao kijiji cha Ilemelema.

Mheshimiwa Spika, nayazungumza haya leo kwa kuwa tunapozungumzia maendeleo ya jamii, jinsia na watoto, huwezi kuepuka kuzungumzia wanawake na watoto ambao wana ulemavu na hasa uliosababishwa na vitendo vya Kikatili. Huwezi kuacha kuzungumzia matukio ya kikatili na ya kutisha yanayoelekezwa kwa kundi hili muhimu katika jamii. Natoa maelezo haya nikiwa na masikitiko makubwa na huzuni nyingi na huku nikiwa natafakari hatma ya watu wenye ulemavu nchini kwetu wenyewe. Je, waikimbie Tanzania? Je ni nani atamfunga paka kengele? Ni nani atawasaka na kuwazuia watekaji, watesaji na wauaji wa watu wenye ulemavu hasa wa ngozi? Napinga kwa nguvu zangu zote na kuendelea kusikitishwa na vitendo vya kikatili vinavyoendelea dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Waziri Jenista Mhagama kueleza kuwa jambo la ulinzi wa watu wenye ulemavu wa ngozi haliwezi kuzungumzwa hadharani kwa kuwa Serikali ipo katika Mkakati, je leo hii anaweza kujibu ni idadi ya watu wangapi wenye ulemavu wa ngozi wauwawe ili mfumo huo uanze kufanya kazi? Anawaambia nini watu wenye ulemavu kuhusu kitendo cha kikatili cha ukataji wa kiungo cha mwanamke mwenzake kilichotokea siku mbili tu baada ya yeye kama waziri mwanamke kuhakikisha kuwa Serikali inawalinda watu wenye ulemavu wa ngozi?

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuiomba jamii kubadilika na kuachana na imani potofu ambazo zinahatarisha maisha na usalama wa watu wengine na ambazo zinarudisha nyuma jitihada zinazofanywa za kupiga vita ukatili kwa watu wenye ulemavu wa ngozi, wanawake na watoto. Hali kadhalika, tunawataka wananchi wote, kuwafichua wale wote wanaojishughulisha na vitendo hivyo na kutoa taarifa kwa vyombo vya dola na mamlaka sahihi ili hatua zaidi ziweze kuchukuliwa kwa mujibu wa sheria.

Aidha, nitoe wito kwa watanzania wote kutowabagua watu wenye ulemavu wa ngozi na kuchukua jukumu la kwanza la kuwa walinzi wa haki ya walemavu wa ngozi kuishi kwa kuwa Serikali ya CCM imeshindwa kuwazuia wauaji na watesi wa watu wenye ulemavu.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Mheshimiwa Spika, Serikali ya CCM imeendelea kuuma na kupuliza kuhusu usimamizi wa mashirika yasiyo ya Kiserikali. Ni Serikali hii ambayo kwa miaka kadhaa imekua ikiyapa usajili mashirika yasiyo ya Kiserikali lakini Serikali hiyohiyo ikashindwa kuyafuatilia utendaji wake kama inavyotakiwa kwa mujibu wa

Sheria. Ni kweli kuwa kuna baadhi ya mashirika yasiyo ya Kiserikali ambayo yamelenga kutumia mwanya uliopo kufanya kazi kinyume na utaratibu ulioekwa lakini ni ukweli usioplingika kuwa mashirika ambayo yamegeuka kuwa mwiba kwa Serikali hasa kwa kufichua uozo na uovu wa Serikali hii ndiyo yamekuwa walengwa wa mkakati wa Serikali wa kuyafuta kwa kuwa yanafanya kazi bila kufuata mashinikizo ya CCM.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kuamini kuwa Serikali inatekeleza mpango wa kuyafutia mashirika yasiyo ya Kiserikali hasa kutokana na hofu ya kazi inayofanywa na mashirika hayo kutoa elimu kwa umma na hasa tunapoelekea uchaguzi mkuu wa Oktoba. Ni jambo la kushangaza kuwa Serikali inaeleza changamoto mojawapo za mashirika yasiyo ya Kiserikali ni kujikita mijini na sio vijijini kwenye wananchi wengi wenye huhitaji, ikiwa nayo inashindwa kutekeleza wajibu na majukumu yake ya kuhakikisha maendeleo ya jamii yanafuata vijiji na si miji peke yake inawezaje kuyafuta mashirika haya? Ni nini kinachofanya Serikali ya CCM ifute mashirika kwa kushindwa kujikita vijijini na nini kitaizua UKAWA kuifuta CCM ambayo imeshindwa kutimiza wajibu wake kwa watanzania? Tunapenda kuikumbusha CCM kuwa, 'mwenzako akinyolewa upara, nawe tia maji kichwa chako'.

Aidha, ni jambo la kushangaza kuona kuwa taarifa ya Wizara ya utekelezaji unaelezea changamoto kuwa mashirika haya yanategemea ufadhili wa wa nje katika kutimiza majukumu yao, Je, si Serikali hii hii ya CCM ambayo inategemea fedha za nje kuendesha miradi ya maendeleo nchini? CCM imechoka na hii ndio lala salama yao. Amkani si shwari 'No Longer at Ease'!

HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, ni katika kadhia hizi ndipo tunaamini kuwa, kwa kuwa ushauri wetu kwa miaka mingi umepuuzwa; Serikali ya CCM ijiandae kuachia ngazi ifikapo Oktoba 2015 kwa kuwa Serikali itakayoongozwa na vyama vinavyoundwa UKAWA imepanga na inatarajia kurudisha maendeleo ya jamii katika ngazi ambayo Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, alitarajia kutufikisha watanzania. Nimalizie kwa kunukuu maneno ya Baba wa Taifa aliyowahi kusema

'Uhuru na Maendeleo ni vitu vinavyohusiana sana; uhusiano wao ni sawa na uhusiano baina ya kuku na yai! Bila ya kuku hupati mayai; na bila mayai kuku watakwisha. Vile vile, bila ya uhuru hupati maendeleo, na bila ya maendeleo ni dhahiri kwamba uhuru wako utapotea'

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha.

Khalfan Barwany Salum (MB)
MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WA
MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO.
25 MEI 2015.

MWENYEKITI: Sasa naomba niwatambue wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira ambao hawakutambuliwa asubuhi. Yupo Dkt. Aggrey Mlimuka, Mkurugenzi Mtendaji wa ATE, halafu wapo Wenyeviti na Makatibu wa Vyama vya Wafanyakazi nchini karibuni wote.

Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Agness Hokororo, atafuatiwa na Mheshimiwa Suleiman Nchambi na Mheshimiwa Maulida Komu ajiandae. Mheshimiwa Agness Hokororo dakika saba!

MHE. AGNESS E. HOKORORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja lakini pia naunga mkono hoja na ushauri uliotolewa na Kamati na mimi ni Mjumbe wa Kamati, kwamba fedha zinazotolewa katika Wizara hii hazikidhi mahitaji ya Wizara na hasa ukizingatia jina la Wizara lilivyo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kwa mwaka wa fedha 2015/2016, fedha ambazo Wizara imeomba na Bunge leo litapitisha shilingi bilioni 31, ni imani kwamba fedha hizo zinaweza zikatoka ili waweze kutekeleza majukumu yao na hasa katika miradi ya maendeleo tofauti na ile bajeti ambayo tunaimalizia Juni, 30 ambapo waliweza kupata asilimia 22 tu na hiyo inakwamisha kwa kiasi kikubwa kutekeleza miradi ya maendeleo katika Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, naomba nijikite kwenye Vyu vya Maendeleo ya Wananchi. Katika Kitabu cha Waziri ukurasa wa 13, inaonekana Vyu vya Maendeleo ya Wananchi kwa Tanzania jumla yake viko 55, lakini utakubaliana na mimi na katika Hotuba ya Waziri pia ameonesha kwamba wana changamoto nyingi, lakini pia ameonesha mikakati ya kuweza kutatua hizo changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze katika Mkoa Mtwara. Katika Mkoa wa Mtwara tuna Vyu vya Maendeleo ya Wananchi vitatu, kimoja kiko

Masasi, cha pili kiko Kiduni kwenye Kata ya Mtonya pale Newala na cha tatu kiko Mtawanya Wilaya ya Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo kitabu cha Mheshimiwa Waziri zimeonekana changamoto hizo na katika Vyuo hivi kuna upungufu mkubwa wa watumishi, hakuna fedha kabisa za uendeshaji ambazo zinakwenda na hivyo kufanya mafunzo katika Vyuo vyote hivyo vitatu kuwa magumu. Kwa mfano, katika Chuo kilichopo Masasi kuna jengo pale, kuna karakana iliezuliwa tangu mwaka 2006, lakini mpaka ninavyozungumza hivi sasa lile jengo halijafanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Vyuo vilivyopo Newala na Mtawanya, yale mafunzo yao kwa vitendo badala ya kufanyia kwenye karakana, wanalazimika kufanya nje na wakati mwingine sasa kama hali ya hewa hairuhusu, ina maana mafunzo yao kwa vitendo yanakuwa hayawezi kufanyika kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna upungufu mkubwa wa watumishi, wa walimu na wale wasio walimu, pia hakuna vitendea kazi. Natambua Sera ya Serikali kwa nini ilianzisha hivi Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na hasa sasa hivi tumekuwa tukilalamikia kwamba vijana wanaosoma katika vyuo vyetu na vyuo vikuu kwamba hawapati ajira. Kwa hiyo, wale vijana wanaomaliza darasa la saba na wanakwenda kwenye Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi tulikuwa tunatarajia kwamba waweze kupata ujuzi na maarifa kule waweze kujijiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali yangu, pamoja na kwamba Waziri ameonesha katika Kitabu chake kwamba wanaendelea na kutatua hizi changamoto na nimeona katika Chuo cha Newala bajeti hii ya 2015/2016 kutakuwa na ukarabati wa madarasa na kutakuwa na ukarabati wa majengo ya utawala. Hata hivyo, niombe sasa kwamba, kwa hali iliyopo sasa kwenye Vyuo vyote hivyo vitatu hali ni mbaya na kwa kweli vijana wapo lakini je, wanakwendaje kujifunza useremala na ufundi mwingine na *study* zingine za kazi kama miundombinu na vitendea kazi haviko kwenye hayo maeneo? Je, tunatarajia kweli vijana wanaotoka katika hivyo Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi waweze kupata ujuzi na maarifa ya wao kuweza kujitegemea na ya wao kuweza kujijiri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nina mashaka, niombe Serikali yangu kwamba, wakati Serikali inaelekeza nguvu katika Vyuo Vikuu ni wakati sasa pia kuelekeza nguvu za kutosha katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ili vijana ambao wanajiunga katika vyuo hivyo wanapohitimu waweze kufanya shughuli zao, waweze kujiongezea kipato na waweze kijijiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyoonekana kwamba, vipo vitendo vingine ambavyo sisi wenyewe kama wanajamii tunatakiwa kuchukua hatua. Kuna vitendo vingi vya ukatili wa kijinsia, lakini mara nyingi tumekuwa tukielekeza kwa Serikali. Nitumie nafasi hii kuwaomba wananchi wote na wanajamii kwa ujumla, ipo haja ya kuhakikisha kwamba jamii zetu zinakuwa sawa na hasa katika kuhakikisha kwamba vitendo vya ukatili wa kijinsia vinatokomezwa kama Serikali ambavyo imeendelea kuwekeza kwa ajili ya kutoa elimu na mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kwamba huo ukatili unakomeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, niombe Serikali na hasa niungane na hoja ya Kamati, katika Kata zetu kumekuwa na upungufu mkubwa wa Maafisa wa Maendeleo ya Jamii, kama Wizara ya Utumishi inaweza ikaajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii moja kwa moja kama ambavyo sasa hivi Walimu wanachukuliwa, hiyo itakuwa inaturahisishia sana hasa katika kuchakata maendeleo katika maeneo yetu ya Kata. Wote tunatambua Maafisa Maendeleo ya Jamii ndiyo waliosoma fani ya kuhamasisha mikakati ya kimendeleo na miradi ya maendeleo katika maeneo yetu. Sasa kwa upungufu huu tuliokuwano wa hawa watumishi 2000 haitakuwa rahisi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala hili lipewe uzito na Maafisa Maendeleo ya Jamii waliopo katika vyuo vyetu vyote nchini waweze kupata ajira moja kwa moja ili wakatuhamasishie. Hata wale wanaopita kuhakikisha kwamba miradi ya maendeleo, maabara hazijengwi, zahanati watu hawajitolei na michango mingine haitolewi, Maafisa Maendeleo ya Jamii watatusaidia kuhakikisha kwamba miradi hii inahamasishwa kwa sababu wanajua na wao ni chachu katika maendeleo yetu. Watu wengine wamekuwa wakipuuza, lakini hawa ni watu muhimu. Niombe Serikali iwaajiri moja kwa moja wakafanye kazi katika Kata na katika Halmashauri husika ili tuweze kusaidia kuchakata maendeleo katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua dakika saba ni chache, nirudie tena kuunga mkono hoja. Niwapongeze Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya, lakini niombe Serikali safari hii tuendeleo kuwatengea fedha na ni kwa Wizara zote, Wizara hii pamoja na Wizara ya Kazi na wao pia wanafanya kazi nzuri lakini niombe pia kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, niombe Watanzania tupate pia elimu sahihi na hasa kwenye lile suala la mafao ambapo nimeona kwa kipindi kirefu kwamba tumekuwa sasa kuna hoja mkanganyiko kwamba, watu wanasema mafao yamechakatwa na kwamba watu wanapunjwa, lakini niwaombe SSRA kwamba tuendeleo kutoa elimu kwa Watanzania na hasa wafanyakazi ili hizi hoja zinazochanganywa zieleweke vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa nitamwita Suleiman Nchambi dakika saba!

MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, wabeja sana. Awali ya yote, naomba niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kishapu kwa kuniamini mimi Mbunge wao kwa kipindi chote hiki ambacho nimeweza kuifanya kazi yao kwa uaminifu mkubwa sana. Naomba nianze kwa kuwasema wenzetu hawa wa UKAWA. Unajua maneno hata kwenye kanga yapo na maneno haya husemwa siku zote, maana wenzetu wamekuwa na maneno mengi kuliko watenda kazi, watenda kazi ni Viongozi wa Chama cha Mapinduzi waliomo humu ndani, wenyewe kazi yako imekuwa ni kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawafananisha hawa na wakati fulani Firauni wakati alipokuwa akimlea Mussa, alikuwa akimuona yule kijana yuko *bright* sana na ana akili ya ziada na anaweza kuwa mtu hatari sana baadaye kwa maana ya kazi alizokuwa akizifanya Farao za kuwakandamiza wanadamu. Akajua huyu kijana atakuwa tatizo na Firauni ni miongoni mwa wanadamu ambao walijaliwa akili nyingi sana, na inasadikiwa kuwa miongoni mwa wanadamu wa kawaida yeye ana akili nyingi kuliko pengine katika ulimwengu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nitoe mfano mmoja kwa wenzetu, Firauni wakati anataka kumteketeza yule kijana mke wake alikataa, mwisho akasema hebu mwite huyu kijana akaweka tende juu ya meza nyekundu na kijinga cha moto. Alipokichukua kile kitende na kijinga cha moto akaweka juu ya meza akamwambia Mussa chukua tende ule, Mussa akachukua kijinga cha moto akaweka katika ulimi akaungua akikutupa, mke wake akamwambia unaona huyu ni mtoto mdogo matendo yake tu, lakini Farao hakushangaa kwa nini vidole vya Mussa havikuguungua, ulimi umeungua. Bwana Yesu Asifiwe!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, wenzetu hawa katika *Quran* kuna maandiko yanasema: “*Wakhalakina I-jina wal-insa imma kafura wa imma shukuru.*”

Tafsiri yake: “Na tumekuumbeni wanadamu na majini aidha mtashukuru au mtakufuru.” Wenzetu hawa hakuna kilichofanywa cha maana na Chama cha Mapinduzi.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tulieni, tulieni.

MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN: Hakuna cha maana kilichofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kaa ndugu yangu utafika wakati wako utasema... *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Hayo ni matusi.

MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN: Subira yavuta heri, mbona ninyi mkiguswa kidogo tu mnainuka mnatetemeka, wewe tulia tu utapata muda wa kusema.

MWENYEKITI: Waheshimiwa naomba tukae, sijamruhusu mtu kusema.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Lakini anaisoma Quran sivyo yule, hawezi kutufananisha na Firauni sisi, hawezi kutufananisha na Firauna.

MWENYEKITI: Kaa basi sijakuruhusu.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Haya hata kama hujaniruhusu, anaisoma Quran sivyo.

MWENYEKITI: Kaa nasema, endelea Mheshimiwa Suleiman.

MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uulinde muda wangu, tatizo la wenzetu hawana subira na sifa mojawapo ya kiongozi lazima uwe na subira, kiongozi lazima uwe na uvumilivu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa endelea na hoja yako, endelea na hoja.

MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, muunganiko wa hawa ni sawa kuwaunganisha paka, dawa yako ni kutupa panya mikia inabaki wanaondoka bila mikia. *(Makofi)*

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: *Wamakhalakita l-jina wal-insa illal-yaabuduna*, sivyo unavyosoma wewe usisome Quran unavyotaka wewe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa naomba ukae.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Anatufananisha na paka...

MWENYEKITI: Tulieni tuvumiliane, naomba mkae, mimi ndiyo Mwenyekiti hapa, heshimuni kiti tukae tuendelee. Endelea Mheshimiwa Nchambi!

MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN: Watanzania wanashuhudia viongozi ambao wanajiandaa kuchukua nchi wasio na subira, UKAWA hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, wanasema kabisa Wizara ya Kazi matatizo ni mengi, lakini tunapotaka kuainisha matatizo lazima tutaje pia na mafanikio tuliyonayo. Ni katika awamu ipi amesema Msemaji wa Kambi ya Upinzani pale, awamu ya hovyoo kabisa ni Awamu ya Nne, lakini leo Awamu hii ya Nne, imewezesha hata watumishi Walimu, Wabunge, Madiwani na wote kupata hata mikopo mizuri ambayo inaweza kuwakidhi kusomesha watoto wao, kujenga nyumba na kufanya mambo mengi ni awamu ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema Wizara ya Kazi haijifanya chochote, hawa Watumishi leo wanaokopeshwa, wanadhaminiwa wanapata hata kujenga nyumba, wanapata kusomesha watoto, hiyo Mifuko ya Jamii inayosomesha watoto na kukopesha, hakuna kilichofanyika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya mwili siyo kubeba kichwa niliwahi kusema hapa, kichwa kinabebwa katika mwili ili kitafakari kiweze kurahisha maisha ya mwili na kichwa chenye. Pia mwanadamu huponzwa na ulimi, ulimi wa wenzetu ni hapana hatuwezi kuwashangaa. Wanasema nimewafananisha na paka, hapana, kama wanakataa na maandiko pia waseme, binadamu tuko wa aina tofauti, binadamu mzuri ni yule anayekwenda Msikitini au Kanisani, anafika kwanza anamshukuru Mungu na kumsifu, Ee Mungu umenijalia mimi kuwa Mbunge, umenijalia mimi kuwa mwanamume au mwanamke, umenijalia mimi watoto na mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye baada ya kumsifu na kumshukuru, unaomba mengine. Wenzetu hakuna la kusifu, hakuna la kushukuru, hakuna chochote kilichofanywa kwa kipindi chote hiki. Ndugu zangu hii siyo kufuru? Hii siyo kufuru? Serikali hii mnayoipiga madongo, imewafanya ninyi mmeingia humu Bungeni, Serikali hii mnayoipiga madongo, imewasomesheni mmeingia humu mnasoma vitabu, hii siyo kufuru? Anakataa vipi maandiko? Binadamu amekuja hapa binadamu akaachwa huru, aidha amshukuru Mungu au akufuru, hayo ndiyo niliyoyasema. Mimi *Quran* ama maandiko ya Biblia sikufundishwa hivi hivi nimesoma, najua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipongeze sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, tunafanya kazi nzuri na siku zote mavuno ni mengi, watenda kazi ni wachache. Sisi tunafanya kazi, wenzetu hawa kazi yao kupiga blabla, wanazunguka huko, wanawatukana wazee, Mheshimiwa Waziri Mkuu kila siku anatukanwa, Mheshimiwa Rais kila siku anatukanwa. Angalieni ni katika zama zipi watoto walitukana wazee wao na Mungu alileta hukumu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema dhaifu, wanasema mizigo, mbona wao wanao viongozi ambao waliwahi kuwa ma-DJ sisi tumesema? Hatujasema! Wanao pia viongozi na wao katika historia walikuwa ma-DJ!

Maana mtu akishakuwa na *disco* ni *DJ*, mimi nimekuwa na mabasi ni mpiga debe. Unamsema Waziri Mkuu ameanza kufanya kazi 1972, hili ndiyo Taifa tunalolihitaji la kesho?

MBUNGE FULANI: Hapana.

MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN: Hawa ndiyo tunahitaji wawe Mawaziri, Mawaziri Wakuu na Marais, ndugu zangu Watanzania na mwenye macho hatoona na mwenye masikio kamwe hatosikia. Kwa sababu kama hutendi haki, hutapata haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Watanzania sana, wajaribu kuangalia mwenendo wa viongozi, kiongozi mzuri ni yule anayetokana na jamii nzuri, nendeni mkasome Luka 6:43 – 45, kwa maana hakuna mti mzuri ukazaa matunda mabaya na hakuna mti mbaya ukazaa matunda mazuri.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Nchambi.

MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Maulidah Komu atafuatiwa na Mheshimiwa Agness Mkanga.

MHE. MAULIDAH ANNA VALERIAN KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Bismillah-r-Rahmani-r-Rahim*, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu wangu kwa kunipa uwezo na uzima na leo nikaweza kusimama kwenye ukumbi huu mtukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote na kabla sijatoa mchango wangu, naomba niwaambie wenzangu wote wa UKAWA na wale wasio wa UKAWA ambao wanasubiri mabadiliko ya nchi hii kitu kidogo tu *Innallah maa swabiriina, innallah ghafurur rahim* kila mwenye kusubiri Mwenyezi Mungu humpa fungu lake, Oktoba si mbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Wizara hii ni Wizara nzuri sana, naipenda sana Wizara ya Maendeleo ya Jamii, lakini masikitiko yangu makubwa kwamba siku zote Wizara inaongozwa na dada yangu akapewa na mwanangu. Kwa hiyo, nawasikitikia kwamba wana mipango mizuri, wanataka kufanya vizuri, lakini wanachopewa ni kiduchu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema maendeleo ya jamii una maana unaingia kwenye Wizara zote zilizoko katika nchi hii. Maendeleo ya jamii ni ya kila mmoja aliyeko katika nchi hii, kuanzia mtoto mpaka mzee, lakini kama yule

uliyemkabidhi kile chombo unamwambia tekeleza maendeleo watu hawa wapate maendeleo ili waweze kuendelea, halafu humpi kitu cha kufanya hiyo kazi; unategemea afanye nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Wizara ya Maendeleo ya Jamii naomba mtazame Kitabu cha Kamati au hotuba ya Kamati imeeleza kila kitu, nawapa hongera Kamati. Ukiangalia hotuba ambayo imetolewa na Upinzani, ina baadhi ya vitu vya kufuata, lakini leo ukisema maendeleo ya jamii halafu Wizara yenyewe hujaipa hata thumni kwenye maendeleo; unataka wafanye nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukisema sisi kwamba hakuna kitu hapa na huwa nasema kwa kweli iliyochoka siyo Serikali, siyo hawa waliochoka, aliyechoka ni mwananchi aliyeko kijiji. Naambiwa nitakwenda ofisi ya Serikali, nitapewa chai na korosho, nani anaruhusiwa kuingia kwenye ofisi ya Serikali mpaka akapewe hiyo chai, ina maana anachosubiri chai imfuate kule. Nani anampelekea chai kule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wao ndiyo waliochoka, hapa hatujachoka kwa sababu tunapanda magari mazuri, tunavaa matenge mazuri, tunapendekeza kwa hiyo, tunasema kidumu Chama cha Mapinduzi, ili tuendelee kustarehe na wengine waendeleo kwisha. Tatizo kubwa sana liko kwenye nchi hii. Na kuna siku nilichangia nikasema, tukileta ushabiki kwenye kutetea haki ya mwananchi, basi hatutaifikisha mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dada alikuwa na maneno akisema hapa ndani kwamba tuendeleo kuvuta subira kwa sababu sungura ni mdogo. Kwa hiyo, nawaambia wananchi, subira imefika mwisho na yule sungura kafa, hayuko tena. Kwa hiyo, tusimsubiri na kuzikwa keshazikwa kwa sababu hata shilingi ya maendeleo haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye jinsia, huwezi ukasema jinsia wakati baba hana kazi, huwezi ukasema jinsia wakati yeye mama anapika mama nitilie, anachukuliwa vitu vyake vinamwagwa anafurushwa na mgambo na wakismama akina Zungu hapa kupiga kelele kuhusu Machinga, kupiga kelele akinamama nitilie au mama lishe, hakuna kitu kinaendelea, ni kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye watoto yatima, hiki ndiyo kitu kilichonikaa rohani. Watoto mayatima, watoto wa mitaani ni watoto wanaopata tabu na sisi tunasema ndiyo hao tunawategemea kwa baadaye. Leo watoto wa mitaani nimemsikia mwanangu hapa Naibu Waziri anasema mipangilio mirefu ya Serikali kutekeleza hao watoto. Hivi kweli unawekwa mipangilio mirefu ya watoto zaidi ya 2000 wako barabarani wanafanyiwa vibaya wanajifundisha ujambazi, wanajifundisha tabia mbaya unaweka mipango mirefu wakati wao wanaendelea kukua, wanakusubiri wewe na hiyo

mipango yako, siyo kitu cha kuchukuliwa hatua haraka iwezekanavyo, wakaweza kukusanywa wale watoto wakaweza kufikiriwa nini la kufanya, kama kurudishwa kwa wazazi wao wakarudishwa, kama nini Serikali inafanya ikafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapanga mipango mirefu hawa watoto kesho majambazi, wasenge, vitu vya ajabu vitajaa kwenye nchi hii. Naomba kama kweli tunatekeleza, hizi nyumba ambazo wamekusanywa hawa watoto, kwanza ijulikane idadi ya nyumba Tanzania nzima ziko ngapi. Pili, mahali zilipo hizo nyumba dada.

Tatu, wahusika halisi, walezi ambao wanalea hao watoto, wamepewa mafunzo, wanajua nini wanafanya au basi tu wana mipango yao, sisemi wote, baadhi yao. Wapi wanapata fedha za kujikimu na kuwalisha hawa watoto na kuwapa elimu? Wapi wanapata hizo fedha?

Nne, kuangalia kwa umakini, kuwaangalia watu hawa kwa umakini mrefu kwa sababu kuna nyumba ya kulea mayatima ilikuwa Morogoro wakati fulani nilisikia watoto wale walikuwa wanafanyiwa vitu vibaya vya ajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kukagua kwa umakini na kuangalia kila wakati, muweke hasa hili desk la kukaa kwenye Halmashauri kila wakati nyumba hizi zikipitiwa na kuangalia malezi ya hawa watoto. Hao waliobakia huko mitaani wanahangaika ndugu zanguni pia tuwafanyie shauri la haraka, kwa sababu wanaumia, wanateseka na ninyi ndiyo Serikali. Yule sungura tukikaa kumsubiri hayupo, ile subira tulishavuta subira haipo tena! Sijui sasa mnatuambia tufanye nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna tena cha kufanya na mnakubali wenyewe. *Percent* kubwa hapa tukisimama tunachangia, tunasema naunga mkono mia kwa mia, lakini ukiunga mia kwa mia inafika mahali unaanza sasa, kwangu hakuna hiki, kwangu kuko hivi naomba hiki, naomba hiki, naomba hiki! Kwa hiyo, wote hapa tuna malalamiko, wote mia tatu na, tuna malalamiko. Sasa tutafika wapi? Mkiambiwa mmechoka msikasirike, msikasirike kabisa, kakaeni mfikirie nini la kufanya kuondokana na balaa mbaya iliyopo katika nchi hii...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. MAULIDAH ANNA VALERIAN KOMU: Oktoba kesho kutwa, kazi mkononi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, kengele ya pili hiyo. Namwita Mheshimiwa Margareth Mkanga, atafuatiwa na Mendrad Kigola.

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie machache. Kwa bahati nzuri niliomba Wizara zote mbili na zimewekwa pamoja kwa hiyo nitajihidi kuzungumza kifupi kwa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kuwapongeza viongozi Mawaziri wa Wizara hizi mbili na Manaibu wao na watendaji wao wote kwa kujitahidi kufanya kazi kikamilifu, lakini Wizara zote mbili kwa muda wote naona zinapunjwa kweli pesa za kushughulikia. Kwa hiyo, hata kuwalaumu naona tabu. Nisifu tu zaidi kwa sababu katika hali hiyo hiyo ya pesa ndogo na uwezesho mdogo, wanajitahidi kutekeleza yale ambayo kwa miaka yote huwa wanajipangia kuyafanya. Mengine yanafanikiwa na mengine ndiyo hayo yako *pending* yanangoja uwezesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza Wizara ya Kazi nimefurahishwa sana kwamba mwaka ujao kuna kuzalishwa kazi kama laki tano hivi, sasa naendelea tu kusihi na kuomba Wizara husika, je, katika kazi hizi, najua mtu unaomba unasahiliwa, ndipo unapoweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kushawishi kwamba, watu wenye ulemavu jamani, wengine sasa hivi wamesoma, wengi wana *skills* mbalimbali zinapotengwa kazi hizi, basi hasa zile umma mjitahidi sana kuwafikiria wale ambao wamekidhi vigezo kuweza kuwaajiri. Kuwaajiri wao ndiko mtasaidia kuleta maendeleo katika familia zao kwa sababu watawalisha, watawasaidia, watawasomesha na watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni ombi la kudumu, lakini nipongeze Wizara husika inajitahidi, lakini tatizo hasa lipo kwenye ajira za watu binafsi, bado wanaona wenye ulemavu labda hawako *productive*, labda hawawezi, lakini mtu anategemea kiungo alichoumia au kilicho tatizo, viungo vilivyo hai anaweza akavitumia kikamilifu kuweza kumudu kufanya hiyo kazi. Kwa mfano, viziwi ni mahodari sana kwa shughuli za kompyuta, kwani akiwekwa ofisini, akashughulika mambo haya ya mawasiliano na nini tatizo ni kitu gani? Kwa hiyo, hili Serikali naomba isaidie kwamba hawa watu waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko huko huko Wizara ya Kazi, Wizara ya Kazi inashughulika na kukagua viwandani na nini ili kuona matatizo ya wafanyakazi. Kuna viwanda na maeneo mbalimbali hasa ya hawa wenzetu wawekezaji, uonezi ni mkubwa bado wala hawafuati yale masharti ya kazi, wala hawafuati vima vile vya mishahara ambavyo wakati mwingine vinapendekezwa. Watu wanapunjwa, inakuwa ni matatizo, ndiyo maana wakati mwingine unaweza ukakuta kunakuwa na matatizo yanayosababisha hata migomo ya wafanyakazi. Kwa hiyo, sehemu hiyo ya ukaguzi, katika Wizara hii tuweze

kuiimarisha ili angalau tuweze kugundua hayo yanayofanyika huko ambayo siyo mazuri kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende Wizara ya Jinsia, Wanawake na Watoto, hapa pia kama wenzangu walivyotangulia kusema bajeti ni ndogo ni kweli na hii Wizara ina mambo mengi kwa sababu ndiyo inakumbatia yatima, wanawake, yaani wengi wengi, jamii kwa ujumla wake, lakini fedha daima zinakuwa ndogo. Hebu wawezeshwe basi jamani ili maendeleo hayo yaweze kuonekana makubwa zaidi katika kila eneo la jamii nchini hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukatili wa kijinsia hasa kwa watoto ni mkubwa na unakithiri na wanawake na watoto hapa naenda mpaka watoto wenye ulemavu siku hizi wana matatizo kweli kweli. Kwa upande mfano tu, kulikuwa na mtoto mwenye ulemavu Morogoro kule, akateswa akateswa baadaye akaishia kufariki maskini ya Mungu, tukamwita mtoto wa *box!* Ulemavu huu wa watoto hasa wenye ulemavu ndiyo ambao unajionesha sasa hata kwa tatizo hili la mauaji ya *albino*. Wengi mimi naona wanaouawa, kukatwa mikono ni watoto ama wanawake, akina baba si sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa tuna changamoto kubwa, hivi ni nini, ni *weakness* ya viumbe hivi kuonekana dhalili ndiyo maana wanashambuliwa? Hapa kautafiti kanahitajika, kwa nini sana wao? Hiyo ni changamoto ya nchi nzima na hapa niombe jamii jamani tunaohusika hapa, hatuwezi kuidai tu Serikali, tunawafahamu hawa, tunao hawa, kwa nini hatuwatoi hadharani tukaona tunaweza kuwafanya nini? Hapa inaingiliana na yaliyokwishafanyika kwamba, basi wakosefu kamilifu, wapate adhabu ya kutosha kabisa hata kama ni kuuawa kama wao wanayoua na kukata mikono ya wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake, Benki ya Wanawake ni mkombozi na mwanzo wake ulikuwa hivyo, lakini niungane na Kamati kwamba, ile fedha ya mitaji iliyoahidiwa, itimizwe kusudi benki hii iweze kujitanua. Sasa hivi iko katika maeneo machache na akinamama wengine wanafanya kushangaa sasa, hata wa kule vijiji ambao ndiyo wana matatizo makubwa, kwamba hii benki labda ni ya Dar es Salaam tu, lakini ni kwa nini, uwezo wa kimtaji haupo! Kwa hiyo, Serikali itimize ule wajibu kusudi benki hii ijitanue, wanawake ndiyo jeshi kubwa, wanawake ndiyo walezi, waweze kuwezesha kwa mikopo nafuu kama benki ilivyoanzishwa na dhamira yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa sababu muda wenyewe ni mdogo, naunga mkono hoja, nawatakiya heri ya kazi nzuri, pamoja na kwamba waendeleo kuvumilia, lakini kuvumilia kuna mwisho, wawezeshwe, Wizara hizi mbili zote ziwezesha, kazi ni muhimu na maendeleo ya jamii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Kigola, Mheshimiwa Riziki Omar Juma ajiandae!

MHE. MENDRAD L. KIGOLA-: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia. Hii Wizara ni muhimu sana na tunajua kabisa maendeleo ya jamii ndiyo kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia kwangu, sehemu kubwa nitaomba Wizara, ni kwa kama walivyosema wezangu, hii bajeti ni ndogo sana, lakini kwa sababu ilishafika tayari kwa Bunge, ili tuweze kuipitisha na hii bajeti tunaipitisha, lakini kwa kiasi hiki tulichopitisha, naomba kisimamiwe vizuri. Kwa mfano, kwenye Wilaya ya Mufindi tuliomba kile Chuo cha Rungemba, kile chuo ni cha miaka mingi sana na kinatoa wataalam wengi na kilianza kutoa Diploma, sasa tuliomba kiwe chuo kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye mipango ya maendeleo ya jamii, naomba hili lipitishwe, Chuo cha Rungemba kiwe chuo kikuu ili tuweze kupata wafanyakazi wazuri kutoka pale. inachukua miaka mingi bado hatujapata tamko la kuwa chuo kikuu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tunasema kwamba, mama na mtoto, hakuna mtu ambaye hamheshimu mama, mama anaheshimiwa sana, lakini bado Wizara haijamwona vizuri huyu mama. Kwa mfano, tukiangalia vijijini kule, hata kwenye Jimbo langu kule, kuna watu wanaishi kwenye vijiji vigumu sana. Kwa mfano, nikiangalia vile Vijiji vya Idete kule na vijiji vya Kwaturanga, ni vijiji vya porini, Vijiji vya Idumlavanu, ukienda kumwona mama wa kijijini unaweza ukatoa mchozi. Wizara hii bado haijasimamia kuhakikisha mama anapata haki zake na haki za mama ni za kawaida tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mama anatakiwa apate maji, sasa unaweza ukaona mama anatembea kilomita 10 anatafuta maji na Wizara ipo! Hili suala siyo kwamba lazima tuseme ni Wizara ya Maji tu, hii Wizara inasimamia haki ya mama kuhakikisha kwamba anapata vitu hivi vya msingi. Sasa akinamama vijijini bado hawajasimamiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Waziri amesema kuna mashirika makubwa ambayo yanasaidia maendeleo ya jamii. Haya mashirika nayapongeza, tunayo mashirika makubwa, kwa mfano tunataja mashirika ya UNICEF, hata kwangu kule nawapongeza, wapo watu wa UNICEF, kuna UNDP,

kuna mashirika WHO, kuna mashirika mengi sana, lakini lazima tufanye *assessment* kubwa, vitu gani wanatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa nasema siku zote kwamba, katika kusaidia, lazima wafanye vitu ambavyo tunaviona, kuna vitu ambavyo tunaviona. Kwa mfano, kule vijijini tunasema akinamama na watoto wanapata shida, hasa sehemu ya matibabu. Siku ile nilisema, kule vijiji akinamama wanatembea kilomita nyingi, mtu anatembea kilomita 40, kilomita 50 mpaka 60 anatafuta Zahanati, haya mashirika kwa nini yatusaidie, yatuletee magari kule! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la kununua tu, magari yanauzwa milioni 12 mpaka milioni 20. Unaweza ukaona pale wamesema *building capacity* wametumia milioni 200, kwa nini wasitusaidie vitu hivi vya kawaidia tu. Naomba Mashirika ya UNICEF watusaidie kama kweli wanataka kuhudumia watoto, hata ILO, kama wanahudumia watoto, ni lazima watafute vitu ambavyo kweli vinaonekana, hilo litatusaidia. Kwa sababu muda ni mfupi, niende moja kwa moja kwenye upande wa ajira. Ajira ni tatizo, kwa vijana ni tatizo kubwa mno! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali iliangalie hilo, itengeneze mikakati mizuri kwa ajili ya kutatua tatizo la vijana. Vijana wa vyuo vikuu wanamaliza wengi sana. Juzi nilikuwa pale Malangali, vijana wengi sasa hivi ajira ya kujitegemea wanasema ni bodaboda tu, lakini mbona hata bodaboda hao hatuwapi mitaji? Tuwape mitaji watu wa bodaboda ili waweze kujiendesha wenyewe, lakini sasa hivi linakuwa tatizo kubwa. Naomba Wizara hilo iliangalie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kuna masuala ya bima ya afya. Sasa hivi kuna bima ya afya na Mifuko ya Jamii, tunasema inatoa bima ya afya. Unaweza ukaona mtu kwenye bima ya afya anakatwa mara mbili! Kwenye NSSF wanasema wanamtibu, tena huku kuna bima nyingine ya afya, sasa unaweza kuona tunam-*double pay*. Tunaomba hili liangaliwe vizuri na liwekwe vizuri watu wasiweze kulalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kitu kingine nimekipata sasa hivi, wanasema mtu, kwenye fao la kujitoa. Mtu anakatwa asilimia 3.6, lakini wafanyakazi bado hawajaelewa vizuri, tusianze kuwakata bila kuwasomesha, inabidi iende elimu, mtu aelewe kwamba anakatwa kiviipi, akishaelewa vizuri, kunakuwa wala hakuna tatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara, masuala yote ambayo yanahusiana na wafanyakazi hata na masuala ya mishahara, mashirika ya umma, bado mishahara kiwango cha chini hakijawekwa vizuri. Kwa sababu, kwa mfano, mashirika ya kilimo, kwa mfano haya mashirika ya chai, kuna

mashirika makubwa na mashirika madogo, unaweza ukaona shirika kubwa na shirika dogo, kiwango cha chini cha mshahara wameweka sawa, wakati mitaji ile ni tofauti. Naomba, kwa viwanda vidogo, vitenganishwe, viwanda vikubwa vitenganishwe, siyo kiwanda kikubwa kinasema mshahara mdogo analipa laki moja na shirika kubwa laki moja, hii haileti uwiano. Naomba Wizara iangalie, Wizara ya Kazi na Ajira, hebu iangalie haya mashirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika makubwa kiwango cha mshahara kilingane na shirika hilo na mashirika madogo kiwango cha chini cha mshahara kilingane na uzalishaji mali na shirika lilivyo, lakini siyo mashirika makubwa yabebe mgongoni, mpaka sasa hivi nikiwauliza kule wanasema sisi Serikali imetupangia, imesema tulipe laki moja, wakati wenyewe wana uwezo wa kulipa hata laki tatu, laki sita mpaka laki ngapi. Tunaomba hilo Wizara ilitengeneze vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja niliongea na Waziri alijibu vizuri, alisema kuna Tume inafanya utafiti. Sasa hii Tume inafanya utafiti miaka mingapi? Naomba kama utafiti ulishakamilika, unapokuja kupanga mishahara hii, basi tusomewe vizuri, ili hata kule wafanyakazi wetu wasiwe wanatuuliza maswali. Hii itatusaidia sana sisi Wabunge, kwa sababu sasa hivi tunashindwa hata kufanya mikutano kwa wafanyakazi, maama watakuuliza swali kama hili. Wanasema yule mfanyakazi wa ndani, kiwango cha chini analipwa laki moja na nusu, mimi nafanya kiwandani, kiwango cha chini ni laki moja na nusu, Unashindwa kujibu vizuri, naomba Wizara itusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kwa sababu muda umekwisha, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Riziki atafuatiwa na Mheshimiwa Mwaiposa!

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii, lakini namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kuwa mzima hadi hii leo, pamoja na ajali ambayo imenikuta, namshukuru Mwenyezi Mungu, amenisuru mimi na mwenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishukuru Ofisi ya Spika na Katibu wa Bunge kwa msaada wao mkubwa ambao wametupa wakati wa ajali hiyo na kuweza kutufikisha tena hapa Bungeni. Mwenyezi Mungu atawapa lenye heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumtahadharisha mwenzangu Mheshimiwa Nchambi ambaye amemaliza kusema muda si mrefu, kwamba amewafananisha wenzake na firauni na paka, jambo ambalo hata Mwenyezi Mungu analikataza, usimfananishe mwenzako na kitu kibaya. Yeye

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kama ni muumini wa kweli wa dini ya Kiislam, hawezi kufananisha mwenzake na firauni, lakini sisi tunasema *Alaysallahu biahkamil hakimin*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite zaidi kwenye Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Wizara hii ni Wizara ambayo imebeba kila kitu, imetubeba sisi wote, wanawake, wanaume, watoto, wagonjwa, wazima, walemavu, kila mtu ameingia katika Wizara hiyo, lakini ukiangalia bajeti ambayo inatengewa ni ndogo, lakini licha ya kuwa imetengewa bajeti ndogo, hata kuwasilishwa hiyo bajeti yenyewe ikafikia kiwango cha mahitaji, haifikii. Hadi hivi sasa tunavyozungumza, bajeti ambayo ilitengwa katika mwaka huu ambao tunamalizia, bado hadi leo haijapatikana, sijui Wizara hii inaweza ikaendaje. Kwa hiyo, wakati mwingine tunawalaumu Mawaziri, lakini pia tunailaumu Serikali kwa jumla kwamba, wao ndiyo ambao wangewawezesha kwa kuwapa fedha ya kutosha kuweza kukidhi mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na Chuo kile cha Tengeru; chuo kile kizuri sana, kinafanya kazi nzuri, lakini ukienda ukiangalia nyumba za wafanyakazi au nyumba za Walimu, ambazo zimejengwa tangu labda mimi ndiyo kwanza nazaliwa mpaka leo bado nyumba zile ziko katika mazingira yale yale, kama zimefanyiwa ukarabati, basi ni juzi na jana. Naiomba sana Serikali kupitia Wizara, iziangalie sana zile nyumba, zina umuhimu wake mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda mbiombio kulingana na muda, naomba niende kwenye suala la mikopo ya wanawake. Wanawake wanapewa mikopo ili waweze kujikwamua katika hali ya umaskini, wanawake ni watu ambao wanalisaidia sana Taifa hili, wanawake ni wazalishaji wakubwa, wanawake ni wahangaikaji wakubwa, lakini jambo la kusititisha na la kuhuzunisha, wanawake wakishapewa mikopo, wale wajasiriamali kama mama ntilie, Askari wa Jiji wanakwenda wakiwanyanyasa, wakiwadhalilisha na kuwanyang'anya zile mali zao, wanawake wale mnategenea wafanye nini jamani! Mnawategemea waende wakajitie katika magesti wafanye ngono zembe badala ya kujituma wakapata riziki halali! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kitu kizuri hata kidogo ambacho kinafanyika, naomba sana Serikali iliangalie kwa umakini jambo hili, wanawake wale wasinyanyaswe, wale wanajitafutia riziki halali na kwa sababu wanajitafutia riziki halali, pale Serikali ingewaandalia mazingira mazuri basi ya kufanya shuguli zao, kuliko kuwaacha wakihangaika, wakidhalilishwa na Askari wa Jiji katika kutafuta riziki zao, pale Serikali na wale Askari wa Jiji wanafanya dhambi kubwa sana na Mwenyezi Mungu mara anaweza akawapiga laana. Wale wanajituma, wanahangaikia kutafuta riziki, lakini tunawanyanyasa na kuwanyang'anya mali zao, hatimaye tunawaacha katika hali ngumu, mikopo ile wanashindwa kurejesha. Si jambo zuri, ni jambo baya sana, naomba Serikali iliangalie kwa umakini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ambalo ningependa nilichangie, ni suala la unyanyasaji wa wafanyakazi wa majumbani. Jambo hili limekuwa likipigiwa kelele sana humu ndani, tunatunga sheria, lakini kuzisimamia hatuwezi, wafanyakazi wa majumbani mishahara yao ni midogo sana, stahiki zao hazipatikani, lakini licha ya hilo, wananyanyasika sana, wananyanyaswa na mama mwenye nyumba, lakini pia hata baba mwenyenyumba anawanyanyasa. Baba mwenye nyumba anamnyanyasa kijinsia, halafu anamtelekeza, anamtupa huko, hashughuliki naye tena. Kwa hiyo, lazima sheria hizi ambazo tunazitunga, tuzisimamie ili kila mtu aweze kupata haki yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema, wafanyakazi wa majumbani wanadhaliwa sana, ni lazima Serikali izingatie kwa umakini sana, kuona kwamba kila mwenye kustahili kupata haki yake, basi aweze kupata kwa njia za usalama na siyo kunyanyasika na kudhalilishwa. Wale ni binadamu kama sisi, wale ni watu ambao wanatafuta riziki na wao, kila mmoja kaumbiwa kutafuta riziki kwa njia yake. Kwa hiyo, naomba sana, Serikali izingatie sana, kuona kwamba hawa vijana ambao wanafanya kazi za majumbani, nao waangaliwe stahiki zao kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukataji wa viungo wa ndugu zetu au watoto wetu *Albino*, ni jambo linalosikitisha sana, kila siku, haichukui muda mrefu, utakuta kijana amekatwa kiungo, kijana ameuliwa, yaani vitu vya kusikitisha, vinatisha, hivi Taifa hili tunaelekea wapi? Lazima, naomba sana, Serikali ichukue hatua za haraka sana, kuhakikisha kwamba jambo hili linatokomezwa, halitokei tena katika nchi hii, ni aibu, ni fedheha! Hivi sisi tuna uwezo wa kuwalinda wanyama wetu, tembo mmoja akipotea ni balaa, lakini *albino* anakatwa viungo, *albino* anauliwa, lakini Serikali haionekani kuchukua *effort* yoyote, kuona kwamba wanakomesha jambo hili!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la kusikitisha jamani, wenzetu wanatembea hawana amani, hawawezi hata kufanya kazi katika mazingira mazuri kwa sababu ya uoga ambao umewatawala katika vichwa vyao, anatembea anahisi kana kwamba hatofika popote anaweza akauawa. Kwa hiyo, ni jambo la kusikitisha, naomba tuchukue tahadhari, ulinzi upatikane kwa ndugu zetu na watoto wetu hawa, hili kila mmoja, kila mtu linaweza likamkuta, *albino* wanazaliwa kila leo, leo wewe kesho mie, kesho mtoto wako, kesho ndugu yako, anaweza akazaa *albino*. Sasa hivi kweli, tuko tayari sisi kuwaona hawa wanaendelea kunyanyasika kwa kuuliwa hovy hovy? Kwa nini Serikali haichukui hatua za haraka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku nasikia kunafanywa uchunguzi, kunafanywa uchunguzi, hapana! Uchunguzi wa mambo ambayo yanafanywa, kweli Serikali wakitaka kufanya, wanafanya na watu wanawatia mkononi na hatua zinachukuliwa na hili jambo linaweza likakoma.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Mwaiposa!

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kuipongeza tena Serikali pamoja na watendaji wake katika Wizara zote mbili. Naomba nianze, kwa sababu muda ni mfupi, pia niwapongeze sana na kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Ukonga kwa jinsi ambavyo wamenipa ushirikiano katika kipindi chote hicho, hakika ushirikiano wao ndiyo uliokuwa unanitia nguvu na moyo kuendelea kuwatumikia kwa kiwango cha hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukurani hizo, naomba sasa nichangie kwenye Wizara ya Kazi na Ajira. Katika Wizara ya Kazi na Ajira, nipende tu pia, pamoja na pongezi hizo, kuwaambia kwamba, kwa kweli Serikali inatakiwa ianze kuangalia vyanzo vya fedha ili kuwepo na Mfuko mwingine au utaratibu mwingine wa kuwakopesha fedha vijana wanaomaliza darasa la saba na kidato cha nne ili wao waweze kwenda kusoma sasa katika Vyu vyetu vya VETA na Vyu vya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Serikali inakopesha vijana wanaosoma vyuo vikuu, lakini katika nchi hii kundi kubwa zaidi ni lile linalobaki nyuma. Tunaona sasa hivi vijana wengi wanajijiri katika maeneo ya bodaboda, lakini pamoja na kwamba huo ni ujasiriamali lakini athari zake ni kubwa. Vijana wetu wanapata matatizo makubwa licha ya kwamba kazi zao zina changamoto ya kukamatwa na Polisi barabarani kila wakati, lakini pia ajali wanazozipata ni mbaya sana ambazo zinawafanya wanakosa baadhi ya viungo vyao vya mwili. Vijana hao wengi wao wangukuwa wamepata mikopo, wangukuwa wamejiunga na Vyu vya VETA pamoja na Vyu vingine vya Maendeleo ya Jamii na kujijiri katika nyanja nyingine. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iangalie utaratibu wa kuwakopesha vijana hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo nizungumzie kwa kifupi sana Mfuko wa Pensheni kwa wazee. Wazee katika nchi hii ni rasilimali nzuri, lakini pamoja na kwamba ni asilimia 11 ya Watanzania milioni 49, wanatakiwa kupata haki yao ya msingi ya kupata pensheni kwa sababu wao wana kiwango ambacho wame-contribute katika uchumi wa nchi hii. Niiombe sana Serikali pamoja na changamoto zilizoelzwa katika kitabu kwamba, Serikali ina mambo mengi. Kusema ukweli lazima tuwatendee wazee haki kwa kuwapa pensheni na wale ambao wanapata pensheni ni lazima pensheni zao ziongezeke.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwapa wazee hawa pensheni, kwanza umri wao utakuwa ni mkubwa, asilimia 11 siyo wazee wengi, tungekuwa tunawajali sana wazee wangukuwa wamefika mpaka kwenye asilimia 20 ya Watanzania wote, lakini wazee hawa wanapoteza maisha kwa kukosa matibabu, licha ya kwamba ipo Sera ya Wazee ya Matibabu, lakini wanakosa matibabu hayo kwa sababu ya utendaji mbovu wa watendaji wetu. Kwa hiyo, niombe Serikali iangalie ni namna gani inaweza ikahakikisha wazee hawa wanapata pensheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, katika jamii ya Tanzania, wanawake ni wengi kuliko wanaume, lakini ndiyo walioonekana kujishughulisha vizuri sana na ujasiriamali na shughuli nyingi za kiuchumi katika nchi yetu. Nafikiria kwamba, hawa wanawake wangewezeshwa vizuri, wangeweza wakainua uchumi wa nchi kwa kasi iliyo kubwa zaidi. Mfuko huu wa Maendeleo ya Wanawake, unategemea asilimia zile tano. Tumeshuhudia katika Halmashauri nyingi kutokutenga zile fedha, lakini hata wale wanaotenga, basi nyingi zinaishia kwenye Mifuko ya walio wajanja, haziwafikii wale wanawake waliolengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana pia, utaratibu wa kutoa fedha hizi kwa pale ambapo zinakuwa zimetengwa, basi uangaliwe upya. Fedha hizi zikipatikana zina ukiritimba mkubwa na utaratibu wake ni mrefu sana. Mara wanawake wanaambiwa lazima wakae kwenye vikundi, saa nyingine lazima wapeleke mchanganuo benki, mara nyingine lazima uwe na *account* au biashara unayoifanya ni lazima iwe imesajiliwa, saa nyingine lazima iwe na faida kubwa na mambo yanayofana na hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo kubwa kwa hawa wajasirimali wadogo, kwa sababu ukiangalia kutengeneza mchanganuo ni kitu kinachohitaji fedha, kuwa na *account* benki, inahitaji fedha. Kwa hiyo, tukiwawekea masharti magumu hivi, tutafika mahali tutakuta kwamba wanawake wanaokopa fedha hizo, siyo wale waliolengwa, ni wanawake wenye uwezo. Kwa hiyo, naomba pale ambapo fedha hizi zinapatikana, basi Serikali iangalie ni namna gani inaweza ikafanya utaratibu ukawa mwepesi zaidi kwa wajasiriamali hawa wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, muda uliobaki, basi niongelee benki ya wanawake.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda umemalizika, nashukuru, lakini naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Ahsante sana, muda umekwisha. Wachangiaji watakoachangia mchana, wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Subira Mgalu, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati.

Sasa naomba nitishe shughuli za Bunge mpaka saa kumi jioni.

(Saa 8.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae. Waheshimiwa Wabunge, mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Subira Mgalu atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati. Mheshimiwa Mgalu!

MHE SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa dhiti kabisa kwa kunifanya niwe mchangiaji wa kwanza jioni ya leo na kwa haraka haraka nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama ndani ya Bunge lako hili Tukufu. Nawashukuru wapiga kura wanawake wa Mkoa wa Pwani kwa kuendelea kuniunga mkono katika kipindi hiki cha miaka mitano. Nimewawakilisha kadiri Mwenyezi Mungu alivyonyalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wote waliowasilisha bajeti zao leo, mama zangu wanachapa kazi vizuri na mchango wangu leo, kwa kuwa muda wenyewe hautoshi, utajielekeza kwenye Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Naomba niungane na maoni ya Kamati namna ambavyo Wizara hii, pamoja na unyeti wa majukumu yake, na upana wa mazingira wanayofanyia kazi, kuwa mpaka tarehe 30 Aprili, wamepata asilimia 22 tu ya bajeti waliyotengewa kwa kweli si jambo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu naamini viongozi wa Wizara hii tukianza na mama yetu Sophia Simba Mwenyekiti wetu wa wanawake wa nchi hii kwa umahiri wake wa kazi na kwa namna anavyozunguka katika maeneo mbalimbali kuhangaikia masuala ya maslahi ya watoto, wanawake na suala zima la jinsia, kwa kweli niombe Serikali, kwa kuwa Wizara hii ni mtambuka, ingejitahidi kadiri inavyowezekana basi angalau kiwango cha asilimia 50 ya bajeti iliyokusudiwa iweze kutengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba huu wa bajeti unaonesha katika maeneo yetu kwamba kuna shughuli zilipangwa kufanya, kwa mfano ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na katika Mkoa wetu wa Pwani tuna Chuo cha Maendeleo ya wananchi Kisarawe, tuna Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha, tuna Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Rufiji. Kwa kweli ukarabati unahitajika na haukufanyika mwaka huu mpaka sasa kutokana na uhaba huu

wa fedha. Naomba Serikali kwa kweli iangalie Wizara hii na ukiangalia viongozi wake na Naibu wake Dkt. Pindi Chana pamoja na Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya, naamini wakiwezesha wanaweza zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo lakini pia nipongeze utendaji kazi wa Benki ya Wanawake inayosimamiwa na viongozi wa Wizara hii. Pamoja na upungufu wa mtaji waliokuwa nao, ukilinganisha na mahitaji ya bilioni kumi na tano na waliyokuwa nayo bilioni nane lakini benki hii imeweza kuongeza madirisha mengi, imewafikia wanawake wengi, hata Mkoa wa Pwani wamefika, wamefika Kibaha, wamefika Bagamoyo, wamefika Rufiji, lakini pia hata idadi ya mikopo imeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza kwa dhati Mkurugenzi wa Benki hii, pamoja na changamoto hiyo naamini kabisa kama ingekuwa Serikali tunatekeleza ahadi ya kuwapatia mtaji wa bilioni mbili kila mwaka, ambapo kwa mwaka huu wa fedha mpaka sasa hivi tunavyozungumza hawajapewa hela yoyote; ni imani yangu benki hii ingefanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na pongezi hizo pia chini ya uongozi wa Awamu hii ya Nne nipende kushukuru kuanzia Mheshimiwa Rais na viongozi wa Wizara hii kwa namna ambavyo imetuwezesha wanawake. Nasimama ndani ya Bunge hili kwa ajili ya uwezeshaji huo. Wabunge wanawake tumeongezeka, Wakuu wa Wilaya wanawake tumeongezeka, Mawaziri wanawake tumeongezeka, ni wazi kabisa kazi kubwa imefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika eneo hili nipongeze kwa namna ambavyo Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, hasa Halmashauri zinazofanya vizuri kutenga asilimia tano ya mapato ya ndani na asilimia tano ya mapato ya ndani mengine kwa vijana. Kwa Wilaya zetu za Mkoa wa Pwani nawapongeza Wilaya ya Bagamoyo, Halmashauri ninayoifanyia kazi na hata kesho nafanya kikao kwa ajili ya kugawa mikopo hiyo kwa wanawake. Nawapongeza wanawake wote waliopata fursa, naipongeza Wilaya ya Kisarawe, Kibaha, Rufiji, Mafia, Mkuranga, lakini rai yangu kwa Wakurugenzi, kuhakikisha asilimia inayotengwa ni tano ya mapato ya ndani ya kilichokusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie pia kwa kushukuru Wizara ya Kazi na Ajira kupitia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Naona wenzetu hapa wamepiga piga maneno tu, lakini kazi nzuri inayofanywa na Mashirika ya Hifadhi ya Jamii inaonekana. Imetajwa miradi hapa ya *NSSF*, tunajua namna gani uwekezaji ule hasa kwenye ujenzi wa nyumba mbalimbali zilizotusaidia sisi wafanyakazi na wengine kupata makazi bora ambayo ni Sera ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mshangao wangu, hata baadhi ya viongozi hao wanakaa katika nyumba hizo, maoni yao kwamba ziwekezwe kwenye hati

fungani, ina maana hela zingekaa tu bila uwekezaji wowote, lakini zinapowekezwa kwenye maeneo haya ya *fixed assets* ambapo kila mwaka *value* yake inapanda, ni wazi kwamba ni uwekezaji ulio na tija, naomba NSSF na mashirika mengine, PSPF waendeleo. Pia kwa kuwa hakuna mtumishi hata mmoja aliyeshindwa kupata mafao yake kwa ajili ya uwekezaji huo, naamini uwekezaji huo unaendana na taratibu na sheria mbalimbali zinazoendesha mashirika hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tuna mamlaka ya udhibiti (SSRA) kazi yake kubwa kuangalia hali ya Mifuko hii, pamoja na changamoto iliyokuwepo, lakini ni imani yangu na Watanzania naomba waamini hivyo, uwekezaji una tija. Kwa watu tunaoka Kigamboni daraja lile ni ukombozi, foleni itakuwa imepungua, tutawahi makazini, tutafanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nyumba zinazojengwa maeneo mbalimbali watu ambao pengine hawana kipato cha uhakika wa kujenga nyumba haraka, watakata makazi na wataishi. Naomba tuwatie moyo viongozi wa mashirika hayo. Mama yangu Gaudensia Kabaka umesimama vizuri na naomba niipongeze Serikali kwa namna ambavyo mmeshughulikia mgogoro wa madereva, pamoja na kwamba katika msafara wa mamba na kenge wamo, lakini mlisimamia maslahi ya madereva. Madereva wanapokosa mikataba ya uhakika ya ajira zao, Serikali inapoingilia kati na kusimamia, naipongeza sana. Pia napongeza namna mlivyochukua hatua ya kufuta ada ambayo ilikuwa inapendekezwa kwa ajili ya wao kujiendeleza. Napongeza maamuzi hayo na inaonesha namna gani Serikali hii ilivyokuwa sikivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, naomba kazi iendeleo na nadhani wafanyakazi hatujasusa sherehe za Mei Mosi tunaendelea kuandamana kama kawaida. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mgalu kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Rita Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mheshimiwa Faida Bakari ajiandae!

MHE. RITA E. KABATI-: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi na kwa kweli nikushukuru kwa ushirikiano wako mkubwa ambao tumekuwa tukishirikiana kwa ajili ya maendeleo ya wanawake wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nitoe pongezi kubwa kwa Mawaziri wote wa Wizara hizi zote ambazo zimewasilisha bajeti zao hapa na watendaji wao na vile vile pia nipende sana kumpongeza mno Mheshimiwa Rais ambaye ametupatia nafasi nyingi sana wanawake kwenye vyombo mbalimbali vya maamuzi. Kwa kweli hakuna Rais aliyefanya kama Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Vile vile ameweza hata kumteua kwenye nafasi zake za

viti maalum mwenzetu Mbunge ambaye ni Mheshimiwa Mbatia. Kwa hiyo pia hata UKAWA amewaona. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nianze mchango wangu kuzungumzia Benki ya Wanawake. Wengi wamesema, hii Benki ya Wanawake ni mkombozi kwa sisi wanawake wote Tanzania nzima mpaka Visiwani. Kwa hiyo, naomba Serikali itoe kipaumbele kikubwa sana kuhakikisha benki hii inapewa mtaji wa kutosha ili mpaka kule vijiji, kwa sababu sasa hivi tukifanya ziara kwenda huko Mufindi, kwenda Kilolo, kwenda Iringa Vijijini bado wanaona kama benki hii haijafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, niwashukuru sana kwenye Mkoa wetu wa Iringa kuna kituo. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Sophia Simba na Naibu wake. Pia nimpongeze Margareth, amekuwa akifanya kazi nzuri kuhakikisha benki hii mitaji inakua japokuwa kwa kususa sua na ameweza pia kukopesha hata viwanja sasa hivi. Kwa hiyo, sasa hivi ukitaka kiwanja nenda Benki ya Wanawake utapata. Hii ni kazi nzuri sana ya Benki ya Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu sheria ya kuwalinda wafanyakazi wa majumbani. Mheshimiwa Kabaka nikushukuru kwa kazi zako nzuri unazozifanya, lakini bado hii sheria haijaletwa. Unajua mimi natokea Mkoa wa Iringa na Mkoa wa Iringa asilimia kubwa sana ya watoto wameajiriwa kufanya kazi za majumbani, lakini sheria hii ulituhadi kwamba ungeleta kabla Bunge halijakwisha, ni lini italetwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza hivi kwa sababu wafanyakazi wa ndani wamekuwa wakinyanyasika sana, wengine wanabakwa, tukienda kwenye ziara tunakuta wengine wana watoto, wamebakwa tu kwa waajiri wao, hawafanywi kitu chochote. Hawana mikataba ya ajira, hawawezi kuwa na hata likizo, hawawezi hata kujiunga kwenye Mifuko ya Jamii. Kwa kweli tunadhaliika sana, wanadhaliika sana wafanyakazi wanaofanya kazi za majumbani. Kwa hiyo, naomba leo hii tuambiwe kuhusu sharia hii na tusipoambiwa mimi naomba tu nitatoa Shilingi Mheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukatili na ubaguzi wa kijinsia. Hivi vitendo vya Ukatili dhidi ya mwanamke hata wewe umekuwa ukisaidia sana pale Iringa na umefungua kituo, lakini bado bado kabisa wanawake wananyanyasika. Tumekuwa na kesi nyingi sana pale Iringa. Watoto wengi wanabakwam kesi haziishi pamoja na kuwa kuna vidhibiti kabisa. Kuna wanawake ambao wamezaa watoto wenye ulemavu, wanaachwa na waume zao ndoa zinavunjika kwa sababu tu mwanamke amezaa mtoto mwenye ulemavu, hata wenye ulemavu wa ngozi. Pia tumeona kuna baadhi ya wanaume ambao sasa hivi wanafanya mpango wa kuhakikisha kwamba wanauza viungo vya watoto wao wenye ulemavu wa ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sheria kali ije na adhabu kali itolewe ili hawa wanaume hata ikiwezekana wanyongwe au wafungwe hata miaka 18 kwa sababu hiki kitu wanaume hawatutendei haki na wamekuwa wakifanya ukatili wa wazi kabisa ambao sisi wanawake kwa kweli tunaona kama tunanyanyapaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili mlizingatie kabisa kwa sababu wanawake tuna kesi nyingi sana pale Iringa. Watoto wanabakwa, wanabakwa kila siku na tumekuwa tukilalamika lakini kesi hizi zinachukua muda mrefu. Bado kwenye Magereza watoto wanachanganywa na watoto wadogo. Sasa hii tunamfundisha mtoto au tunafanya nini. Kuna watoto wengine, nimekwenda, kuna wanawake wawili wamefungwa na watoto pale gerezeni. Sasa je tunafanyaje, naomba hili liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu madeni kwenye Mifuko ya Jamii. Kwa kweli niwapongeze sana hawa wenzetu wa Mifuko ya Jamii, wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana hawa *NSSF, PPF, GEPF, LAPF* na kadhalika, wamekuwa wakiisaidia Serikali yetu kutukopesha. Utaona Chuo cha *UDOM* kile kimejengwa kwa kutokana na hii Mifuko. Vile vile kuna barabara nyingi, miradi ya barabara kama daraja lile la Kigamboni, nyumba za Polisi hata nyumba tunazoishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, naomba Serikali yetu leo ituambie, kwa nini wamekuwa hawalipwi kwa wakati kwa sababu hii Mifuko wanachangia wafanyakazi. Sasa wafanyakazi wanakuwa hawaelewi kama Mifuko hii inachelewa muda mrefu kulipwa na najua kama ingelipwa miradi mingi sana ya maendeleo ingeweza kufanywa kwa ajili ya hii Mifuko. Sasa naomba Serikali yetu leo ituambie sasa kwenye hizi bajeti inatenga kiasi gani ili tuweze kulipia haya madeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vyetu vya Iringa, kuna Rungemba na kile cha pale Ruaha, bado havitengewi fedha za kutosha. Kuna mwenzangu alizungumza asubuhi Mheshimiwa Kigola kwamba kile Chuo cha Rungemba kilitakiwa kiwe chuo kikuu, sasa nami niulize tena ni lini na vile vile pesa inatengwa kidogo sana. Kama kile cha Ruaha kilichopo Iringa Mjini bado kina miundombinu siyo mizuri, wafanyakazi wanafanya kwenye mazingira magumu sana. Naomba mnapotoa hizi bajeti, basi tuangalieni na pale Iringa kwa sababu vyuo vyetu vinatakiwa viangaliwe ili watoto waweze kusoma zaidi, wasiendelee kuajiriwa kenye hizi ajira ambazo bado hazijawa na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu ile asilimia tano kwa ajili ya vijana na akinamama. Sheria ilishapitishwa hapa Bungeni kwamba lazima

Halmashauri zote zitenge asilimia tano kwa ajili ya mikopo ya vijana na akinamama, lakini bado kabisa. Kuna baadhi ya Halmashauri bado hazijaweza kutekeleza agizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashangaa tunaamua hapa Bungeni lakini bado mambo hayafanyiki. Vile vile katika Halmashauri nyingine bado vijana na akinamama hawajaweza kupata elimu ya kuweza kuifikia hiyo Mifuko. Pale Iringa tuna vijana wetu wengi sana ambao wamekuwa wakijishughulisha na kazi ndogo ndogo, lakini bado mitaji yao hawana uhakika nayo kwa sababu hawajaweza kupatiwa hii mikopo na hawajui wataifikia vipi. Kwa hiyo, naomba Serikali yetu leo hii hebu iweke wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alituelezea kwamba, adhabu kali itatolewa kwa Halmashauri ambazo hazitengi hii Mifuko, lakini bado utekelezaji wake siyo mzuri sana kwa sababu na sisi tuko kwenye Halmashauri hizo. Kwa hiyo, naomba Serikali itueleze ni hatua zipi zitafanyika ili kuhakikisha kwamba Mifuko hii inapata fedha na naomba iongezewe kwa sababu ile asilimia tano kuna ongezeko kubwa sana la vikundi vya akinamama na vijana, bado ni ndogo sana. Hata ule Mfuko unaotoka Wizarani bado ni mdogo, naona unafika kwa shida, nishukuru Iringa tulipata kiasi, lakini mikoa mingi wamekuwa hawapati. Kwa hiyo, naomba Serikali yetu leo hii itoe pesa ya kutosha kuhakikisha kwamba Wizara hii inapatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja. Nashukuru.
(Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ritta Kabati. Sasa namwita Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Faida Bakari, Mheshimiwa Zainab Vullu ajiandae!

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nitangulie kwa kusema kwamba, nashangazwa sana na jinsi watu walivyo-panic humu ndani na sisi UKAWA kuungana na kufanya kazi pamoja kwa nia positive ya kuiokomboa hii nchi Oktoba. Hata hivyo, nashangaa kwamba kwa nini wao Chama cha Mapinduzi wana *affiliation* wanashirikiana na vyama vingi tu vya Upinzani lakini sisi hatuwaingilii, wakiwemo ACT, wanashirikiana nao, lakini sisi hatuwaingilii lakini wao wamekuwa *all over* UKAWA, UKAWA, UKAWA. Watuache na watuache tuendeleo na mipango yetu ya kuikomboa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda niwapongeze wana Mbeya na wananchi wote wa Tanzania ambao wako kwenye mchakato wa kujiandikisha sasa hivi. Nawapongeza kwa kuvumilia foleni kwa sababu foleni zimekuwa

kubwa sana. Niwatie moyo tu kwamba wakomae, wakomae wahakikishe kila mtu anajiandikisha na siku saba tunasisitiza kwamba hazitoshi.

Sisi Mbeya tumeshakubaliana na wengine mtuige, kwamba kama Waziri wa Vijana pia nasisitiza kwa vijana wote nchi nzima wasiruhusu mashine itolewe katika kituo chochote ikiwa nje kutakuwa na mamia ya watu wanasubiri kujiandikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasikubali mashine zitolewe kutoka kwenye vituo kama nje bado kutakuwa na makundi makubwa ya mamia ya watu wanasubiri kujiandikisha, maana mchakato huu umegeuka kuwa adhabu sasa, badala ya kuwa mchakato wa maendeleo umegeuka kuwa adhabu. Mbeya watu wandala vituoni, watu wanasonga ugali kwenye foleni, lakini kwangu mimi si kitu kibaya kwa sababu hii ni ishara kwamba, namna gani wananchi wamechoka na namna ninyi ambavyo mmechoka, yaani mlivyochooka, mmewachosha wananchi na wananchi wako tayari sasa kuwatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye ajenda iliyopo mezani, nitaanza na Vyama vya Wafanyakazi na Mzee wangu Nicholas Mgaya najua yuko hapa. Kuna tatizo moja la Vyama vya Wafanyakazi kwenda kuwashawishi wafanyakazi hasa katika sehemu ndogo ndogo, kama viwanda vidogo vidogo, kuwashawishi wajunge na vyama vile, lakini wakijunga wanapata madhara ya kufukuzwa kazi. Wanafukuzwa kazi kwa kujiunga na Vyama vya Wafanyakazi halafu kwa bahati mbaya sasa vyama hivi vya wafanyakazi vinashindwa kuwatetea wale watu ambao wamepata madhara hayo na mifano hii imetokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano Mbeya kuna kijana mmoja katika eneo langu kwenye kiwanda cha vifaa vya ujenzi, kutengeneza matofali, sijui kujenga *concrete*, amekwenda pale kiongozi wa Vyama vya Wafanyakazi, amewashawishi vijana wajunge, vijana wale wamejiunga kesho yake tu wakafukuzwa kazi. Wamefukuzwa kazi wamekwenda CMA. CMA nako ni shida tupu, hii Tume ya Upatanishi wa Wafanyakazi, nako kumekuwa shida tupu, wafanyakazi wanaopeleka kesi zao wanahangaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuwalaumu sana kwa sababu nilijaribu kufuatilia pale CMA Mbeya kuangalia, kwa kweli hali za wale vijana pale ambao wanafanya kazi za upatanishi ukiwaangalia tu wamechoka. Kwa hiyo kuchoka kule kwa hali ile kunasababisha vijana wale sasa nao wachukue rushwa.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta mfanyakazi ana kesi, yule mfanyakazi mwenye kesi anaambiwa hukumu yake tayari, lakini hakuna karatasi, yaani CMA wanamwambia hatuna karatasi za A4 kwa ajili ya kuandika hukumu ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vitu kama hivi ni sababu nyingine, kwamba mnaunda vitu vizuri, lakini vile vitu vizuri mnashindwa kuvisimamia na hiyo ni ishara nyingine kwamba mmechoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasihi sana wafanyakazi wote ambao mmegombana nao; mmegombana na wafanyakazi, mmegombana na madereva wafanyakazi, mmegombana na wafanyabiashara, hawa wote wakomae wajandikishe ili twende tukawang'oe Oktoba. Mnagombana mpaka na madereva na Maaskofu! Hivi mnavyokaa hapa na kuwaponda UKAWA kwamba, UKAWA hivi na vile mnatarajia ni nani atawachagua kama ikiwa makundi yote hayo ya Watanzania mmeshagombana nayo kabisa. Kwa kweli, sijui mikoa mingine lakini kule Mbeya hawataki hata kuwaona na cha moto mtakiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunawaambia, tutafanya nini, kwa sababu tumesema hatuombi tena, muda wa kurekebisha hamna, mishahara midogo na ajira hamna. Sisi UKAWA tutakachofanya tutaimarisha *small businesses* ambazo zinaajiri watu watano, kumi, wengi wa kutosha. Wafanyabiashara wanapotaka kuzungumzia masuala ya kodi hatutawapeleka Polisi kama mlivyompeleka Minja. Hatutawapeleka polisi au gerezani, badala yake tutakaa nao tutawajengea mazingira rafiki ya kodi ambayo yatawasaidia kukua kibiashara. Tukiwasaidia kukua kibiashara, tutakuwa tumefanikisha suala zima la kusimamia *small businesses* ambapo wakikua sasa wanakuwa na uwezo wa kuajiri watu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana ninyi mmekaa kusema tu tutaongeza ajira, ajira zipo tatizo hamjaziboresha. Mngeweza kusimamia na kuboresha ajira hata za kwenye baa na hoteli, haina tatizo. Wapunguzie kodi wale wenye baa, wape mazingira mazuri ya kukua kibiashara, watakapopata faida zaidi watakuwa na uwezo sasa wa kuajiri hata wale *barmails or barmen* na kuwalipa vizuri. Nchi kama Marekani au Ulaya kazi za baa zinafanywa na watoto wa chuo kikuu, siyo kazi za aibu na wala hakuna mambo ya kushikwashikwa kama hapa. Unakuta wanafunzi wa vyuo vikuu wakiwa likizo ndiyo wanakuwa wamejazana katika maeneo yale na kufanya kazi kwenye baa na hoteli na kwa sababu mishahara ni mizuri *automatically* zile kazi zinakuwa na hadhi na vijana wale wanafanya bila kudhalilika wakati wakiwa chuo kikuu na wakitoka pale wanaenda kufanya mambo yao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninyi mmekaa tu hapa, kazi kila mtu akisimama, sijui Nchambi amesimama anasema UKAWA, UKAWA, UKAWA, yule

akisimama UKAWA, UKAWA! Nye kaeni muwe mnapiga kelele ya UKAWA, UKAWA wako nje huko, Mzee Lipumba sijui yuko Lindi, Dkt. Slaa sijui jana alikuwa Kawe, sijui nani yuko wapi, watu wanapiga jaramba wanafanya kazi tayari kwa Oktoba kwenda kulikomboa hili taifa litoke katika mikono yenu dhalimu. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana muda umeisha. Sasa namuita Mheshimiwa Faida Bakari, atafuatiwa na Mheshimiwa Zaynab Vullu.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie hoja hizi za Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza Serikali yangu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna inavyotenda mambo ya maendeleo katika nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napingana na Mheshimiwa Mbilinyi, a.k.a Sugu kwa kusema kwamba, Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi imechoka. Mimi ninamwambia hivi Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi haijachoka na watakiona 2015 ni kesho kutwa, Oktoba. Vilivyochooka ni vyama vya upinzani ndiyo maana havikuweza kujiendesha kimoja kimoja wakaungana na kujita UKAWA. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kuchangia na nianze na Mifuko ya Jamii. Napenda kuipongeza Serikali, mifuko hii ya *NSSF*, *PPF*, *PSPF* na kadhalika kwa kazi zao kubwa wanazozifanya katika kuendeleza jamii yetu ya kitanzania. Mifuko hii inafanya kazi kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Kambi ya Upinzani nashangaa wamesema kwamba, Mkurugenzi wa *NSSF* awajibishwe, awajibishwe kwa kitu gani? Hivi kuna mtu anafanya kazi katika nchi hii kama Dkt. Dau? Yuko mwingine? Hakuna! Ni mfano bora. Kwa hiyo, nafikiri ninyi mmepeleza tu dira, nakuambieni Wapinzani mmechoka sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mkurugenzi huyu. Pia napenda kumpongeza Mkurugenzi wa *PPF* na Mkurugenzi wa *PSPF* kwa kazi kubwa wanazozifanya. Hivi jamani mwenye macho haambiwi tazama. Tunaona ni jinsi gani mifuko hii inavyoisaidia jamii yetu ya Kitanzania, wakiwemo ninyi wapinzani. Wapinzani wengine wanakaa kwenye nyumba za *NSSF*, nyumba za Serikali hii ya Tanzania ambayo inaongozwa na Chama cha Mapinduzi...

MBUNGE FULANI: UDOM

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Wamebakia kuandamana kwenye barabara tu.

MWENYEKITI: Utulivu!

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Sasa nataka hawa wapinzani wanipe utulivu nataka kuwapasha hapa. Nashangaa wao wenyewe ndiyo wanakaa kwenye hizo nyumba, zimejengwa na nani, *NSSF!* Mkurugenzi ni nani, Dkt. Dau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka vyuo mifuko hii imejenga mfano Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*), Chuo Kikuu cha Nelson Mandela, Daraja la Kigamboni, nyumba za kuishi wananchi zimeenea. Nategemea na kule Zanzibar, Pemba na Unguja zitafika. *CCM Oyeeee! (Makofi/Kicheko)*

WABUNGE FULANI: Oyeeee!

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake Tanzania. Mama Sofia nakupongeza sana kwani unaweza. Pindi Chana, ndugu yangu nakupongeza unaweza. Ninyi ndiyo wanawake wazalendo wa nchi hii. Ninyi ndiyo mnawaongoza wanawake wa Tanzania na jamii yote ya Kitanzania. Benki ya Wanawake Tanzania imewakomboa wanawake na wanaume wa Tanzania wakiwemo wapinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kuipongeza Serikali lakini kuna neno moja ambalo kila siku nalifuatilia hapa Bungeni kuhusu Zanzibar. Mama Sofia naomba sana hii Benki ya Wanawake ifike katika Visiwa vya Zanzibar kwa sababu na kule nako kuna wanawake wengi ambao wana miradi mbalimbali ya biashara ili waweze kujikomboa. Naishukuru sana Serikali kwa kazi hiyo na naamini kwamba, Serikali hii ni sikivu, benki hii itafika Zanzibar ikawakomboa wanawake na waanume wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukatili wa kijinsia. Sisi ni mashahidi wa mambo yanayofanywa hapa Tanzania kwa baadhi ya watu ambao *memory* zao nafikiri ni finyu. Wanaona kama wazee wetu, wanawake na wanaume, vikongwe wakishakuwa na macho mekundu tu, vijana fulani fulani, nafikiri hawa wanakuwa wanatumia bangi na ndiyo maana wanafanya mambo kama haya wangukuwa na maadili mazuri wasingekuwa wanafanya mambo kama haya, kwa hiyo, wanawaua wazee. Wengine wanawaua wazee vikongwe na wakati mwingine wanawafukia wakiwa hai. Hivi kweli hii ni haki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ifuatilie janga hili lililopo katika nchi yetu ili vijana wanaofanya ukatili waweze kuwachukulia hatua kama huu kwa wazee wetu vikongwe. Pia wale albino wengi wanauawa kutokana na

ngozi zao. Vilevile watoto wananyanyasika, mzazi akifariki anayenyanyasika pale ni mtoto. Naomba Wizara hii ifuatilie mambo kama haya kwani ni mabaya sana katika nchi yetu na yanaondosha maadili ya nchi yetu na siyo sera zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo kwa watu wenye ulemavu. Kila siku nikisimama hapa huwa naongea sana na hata Bunge lililopita nilileta swali hapa Bungeni kuhusiana na mikopo hii ya watu wenye ulemavu. Nashukuru Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi inatoa mikopo sana kwa wananchi wake ili kuwasaidia lakini mimi niko hapa kwa walemavu, nahisi kama (haya ni mawazo yangu) kwamba watu wenye ulemavu bado hawajaonekana kwa kiasi kikubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri wawape upendeleo watu wenye ulemavu kwa sababu na wao pia ni binadamu kama wengine. Sisi pia hatujijui huko mbele tutakuwaje, Mwenyezi *inshallah* atusitiri, lakini nawatetea hawa watu wenye ulemavu kwa sababu wakati mwingine kujitetea wenyewe wanakuwa hawawezi kujitetea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, nimemaliza hapo. Ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Faida. Mchangiaji wetu anayefuata ni Mheshimiwa Zaynab Vullu na wa mwisho atakuwa ni Lolesia Bukwimba.

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyeniwezesha kufika jioni hii na kusimama ndani ya jengo hili na kuweza kuongea. Pia niwashukuru wanawake wa Mkoa wa Pwani pamoja na wananchi wote kwa ujumla kwa kunipa imani, nguvu na ari ya kuweza kuja kuwakilisha humu ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze sasa kwa kuwapongeza Mawaziri wa Wizara zote na Manaibu wao pamoja Makatibu Wakuu wakiongozwa na Watendaji wengine kwa mawasilisho mazuri ya bajeti zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, maana yake tunaangalia ni vipi wanawake hawa, wanaume hawakuandikwa pale lakini ukishasema jinsia maana yake na wanaume wamo mle ndani na watoto wataendeleza vipi maisha katika nchi hii ya Tanzania, nchi yenye amani, upendo na utulivu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha kushangaza ni kwamba, bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni ndogo sana. Ombi langu kwa Serikali iingalie bajeti hii na ikiwezekana basi mwisho wa mjadala huu wa bajeti waongezewe ili tuone tunakwenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Naweza kusema yeye ndiye miongoni mwa waanzilishi wa Benki ya Wanawake wa Tanzania na ukizingatia kwamba yeye ndiye Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania chini ya Chama cha Mapinduzi, kwa maana ya Jumuiya ya UWT. Hongera sana Mheshimiwa Mwenyekiti wetu, pigania maendeleo ya wanawake, pigania sisi wanawake tuliomo humu ndani umetuwezesha pamoja na Serikali yako lakini tunaomba benki hii iingaliwe kwa jicho la huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna fedha ambazo Serikali iliahidi itaipatia benki hiyo lakini mpaka leo benki hiyo haijaweza kufikia kiwango ambacho imeahidiwa. Niiombe Serikali iingalie hiyo benki ili iweze kufika kwenye mikoa, wilaya na hata kata zetu na iwezeshe wanawake. Benki ile imepewa jina la wanawake tu lakini hata wanaume na vijana wa kiume wakienda wanapewa mikopo. Kwa hiyo, itakuwa ni sehemu ya ukombozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda ni mchache niende kwenyue Wizara ya Kazi na Ajira.

MBUNGE FULANI: *NSSF.*

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Itasemwa wala usikonde Kaka yangu, powa tu. *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Zungumza na mimi, zungumza na Kiti, usimjibu wewe endelea.

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wizara ya Kazi na Ajira inafanya kazi nzuri na nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake kwa kusimamia mgomo, lakini endeleeni kutafuta suluhu ili tusiendeele kupata migomo ya namna ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira imekuwa ni tatizo katika nchi yetu lakini kuna fani nyingine naiomba Wizara na ije inipe majibu, sijui kama imefanyia kazi vya kutosha. Kuna wasomi wanaosoma kwenye vyo vyetu wa fani mbalimbali, kuna wale wanaochukua *engineering* na mambo mengine mengi tu lakini kuna wale wanaochukua fani ya Kiswahili kama somo. Hii ni ajira moja kubwa sana. Ukiangalia Taifa letu la Tanzania, ndiyo tunaajulikana kwamba Kiswahili ndiyo lugha yetu. Ukiangalia katika nchi za jirani wanatumia Kiswahili lakini sisi wenyewe hatujakipa nafasi ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara iangalie na itafute utaratibu wa kutafuta ajira kwa wale wanaomaliza Shahada za Kiswahili ili waweze kupata kazi mbalimbali nchini. Jana nilikuwa napitia mtandao mmoja, nikakuta kuna gazeti moja la Zimbabwe limeonesha kuna kongamano ambalo wananchi wa Zimbabwe wanaweza kutumia lugha ya Kiswahili kufanyia kazi, iweje sisi ambao kwetu ndiyo Kiswahili kimezaliwa tunashindwa kukienzi. Niiombe Wizara ya Kazi iangalie utaratibu wa kutoa ajira za Kiswahili kwenye nchi yetu. Kwa kufanya hivyo, tutatoa nafasi nyingi za kazi kwa sababu watu wengi nchini wanapenda kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wana hamu niizungumzie NSSF. Bila ajizi, naomba niwaambie hivi, Waswahili wana misemo yao, “hoja ya mja kunena, muungwana ni vitendo”. Sasa mtu anapofanya vitendo vizuri na vya maana halafu usimsifie una matatizo gani? Basi usiposhukuru kidogo, hata Mwenyezi Mungu akikupa kikubwa utashindwa kushukuru. Wewe umepata Ubunge kwa bahati mbaya, leo usipomshukuru Mwenyezi Mungu kwa Ubunge huo ulioupata kwa bahati mbaya, Mheshimiwa wangu basi wewe utakuwa ni mchache wa kushukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme watu wanaibezwa NSSF lakini hakuna asiyejua kazi ambayo inaifanya. Chini ya uongozi wa Dkt. Ramadhan Kitwana Dau, yeye ndiye Mkurugenzi, amesimamia miradi mingi, ndani ya jengo hili tulilokaa ni usimamizi wa NSSF, Chuo cha UDOM kimesimamiwa na mashirika ya hifadhi ya jamii, NSSF -Dkt. Dau, watu wana hamu na hii NSSF jamani, PPF - Ndugu yangu Erio na PSPF - Ndugu yangu Adam. Hawa watu wanafanya kazi kwa kujituma na kwa kujitolea, lakini kujitolea kwa sababu uzalendo umewakolea ndani ya damu yao na ndiyo maana wanaleta maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona UDOM, Chuo cha Nelson Mandela, kuna miradi kadhaa inakuja ikiwemo ya Hospitali ya Apolo, ujenzi wa barabara ya Chalinze – Morogoro...

(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Ya kwanza hiyo?

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa hiyo ni kengele ya pili.

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nawapongeza Wakurugenzi wote wa mashirika ya hifadhi ya jamii. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa namkaribisha msemaji wa mwisho, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba.

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika hoja zilizoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote ambao kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana kwa ajili ya kujenga Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalie hii bajeti katika Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwanza, nianze kwa kusema kwamba, hii ni Wizara muhimu sana kwa Taifa letu na kwamba, kwa bajeti hii ambayo inatengewa kila mwaka ni ndogo sana kuweza kufanya kazi zake vizuri inavyotakiwa. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kuiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuiwezesha Wizara hii kwa sababu inashughulikia ustawi wa wanachi wote; watoto, akina mama na akina baba, ni watu wa aina zote. Ili tuweze kupata maendeleo endelevu kwa jamii ya Kitanzania, Serikali iangalie uwezekano mkubwa wa kuiwezesha Wizara ili iweze kufanya kazi zake vizuri kwa ajili ya ustawi wa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nikiangalie kitabu cha bajeti katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, nimeona kipengele muhimu kabisa katika bajeti hiyo ambacho ni muhimu nikizungumzie. Kwanza kabisa, ni upungufu wa watumishi wa kada ya maendeleo ya jamii katika kata zetu. Tumeona jinsi ambavyo katika nchi ya Tanzania tuna upungufu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii 2029, ni watu wengi sana na ni changamoto kubwa katika Taifa letu kwani wananchi watawezaje kuchochea maendeleo yao wasipowezeshwa na hawa watendaji wetu ambao kazi yao ni kutuwezesha sisi wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza bajeti kwa ajili ya kuweza kuajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii katika kata hizi ikizingatiwa kwamba, ni watu muhimu sana kwa sababu bila maendeleo endelevu ambayo yanatokana na sisi wenyewe wananchi. Mimi sina uhakika kama kweli tutaweza kufikia malengo ya *millennium* ambayo yanatutaka kupunguza umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia tu katika Mkoa wangu wa Geita, kati ya kata 97 ni 23 tu ndiyo zina Maafisa Maendeleo ya Jamii. Kwa hiyo, upungufu huu ni mkubwa sana. Naiomba Serikali iweke mkazo katika kuona umuhimu wa kuwa na hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika kata zetu ili waweze kufanya kazi nzuri ya kuelimisha wananchi kwa sababu bila ya hawa haiwezekani kutatua changamoto za kimaendeleo ambazo zipo katika jamii ya Watanzania. *(Makofi)*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya jamii ni pamoja na watoto wetu, hasa katika masuala ya afya. Tukiangalia katika hospitali zetu, zahanati na vituo vya afya, tunaona kuna upungufu mkubwa wa dawa kwa ajili ya watoto. Sera ya Taifa inasema watoto chini ya miaka mitano wanatakiwa kutibiwa bure lakini pia hata akina mama wajawazito wanatakiwa kupewa huduma bure, lakini ni kinyume kwani mara nyingi wanapokwenda hospitali hawapati huduma hizi bure, hii ikiwa ni pamoja na wazee. Kwa hiyo, hii ni changamoto kubwa sana vijijini, wazee wengi wanateseka hawapati huduma bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali katika kuboresha maendeleo ya jamii yetu iangalie sekta ya afya, iboreshe na ihakikishe dawa zinapatikana katika zahanati na hospitali. Kwa mfano, katika Hospitali ya Geita changamoto ni kubwa sana, juzi kuna mtu mmoja aliniandikia meseji kwamba mke wake alikwenda kujifungua kwa *operation* akaambiwa alipe Sh.200,000/= jambo ambalo kwa kweli ni hatari kubwa ndiyo maana inasababisha vifo vingi vya akina mama wajawazito. Kwa hiyo, naiomba Serikali iwekeze zaidi katika kuboresha huduma kwa ajili ya watoto, akina mama na wazee ili wafanye kazi vizuri na kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeza Serikali kwa kukusudia kuanzisha vyuo vya VETA. Kwa mfano, katika mikoa mipya imekusudia kujenga vyuo vya maendeleo. Kwa hiyo, naiomba Serikali ihakikishe katika mwaka huu wa fedha inawezesha vyuo vya VETA ili ujenzi uanze mara moja kwa sababu katika mikoa mingine hakuna chuo chochote cha maendeleo ya jamii. Kwa hiyo, naiomba Serikali iwekeze katika hili ikikumbuka katika Mkoa wetu wa Geita tuna changamoto hiyo, mkoa mzima hatuna chuo hata kimoja. Naiomba Serikali iwekeze hasa Katoro, Rwamgasa na sehemu nyingine ili watu wapate huduma hii kwa ukaribu, nina hakika kwamba watafanya kazi vizuri katika shughuli mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nikiangalia suala la kuwezesha vijana, Serikali imeweka mipango mizuri sana katika bajeti ya mwaka huu, naomba iangalie kwa mfano sekta za madini, kuna vijana wengi sana wanahitaji kuwezesha katika elimu, mitaji na vifaa kwa ajili ya kufanya kazi za uchimbaji wa madini. Tukifanya hivyo tutaongeza ajira nyingi zaidi hasa kwa Watanzania ambao wengi wao hawana ajira. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie uwezekano huo hasa katika sekta muhimu kuwawezesha vijana kwa kuwapa elimu na mitaji ili kuongeza ajira zaidi na wananchi walio wengi waweze kufanya shughuli zao mbalimbali kwa ajili ya ufanisi na maendeleo ya taifa letu.

(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Lolesia.

MHE. LOLESIA M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema kwamba naunga mkono hoja nikiamini Serikali itayafanyia kazi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa kuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

MICHANGO YA MAANDISHI

MICHANGO YA MAANDISHI KWA WIZARA YA KAZI NA AJIRA

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka (Mb) na Bibi yangu mpendwa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dokta Makongoro Mahanga (Mb), Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti wakiwemo Wakurugenzi Wakuu wa Mifuko ya Hifadhi, nao ni Mkurugenzi Mkuu wa PPF - Ndugu Erio, Mkurugenzi Mkuu wa PSPF - Ndugu David na Mkurugenzi Mkuu wa NSSF - Alhaj Dokta Ramadhani Dau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, madeni ya Mifuko ya Jamii. Mifuko ya Jamii imefanya kazi kubwa sana ya kuleta maendeleo ya nchi hii kwa kutoa misaada ya kijamii kwa Watanzania wanaojitahidi kuondokana na umaskini kwa kujenga Chuo Kikuu cha UDOM, Daraja la Kigamboni, majengo mengi ya makazi na kadhalika. Majengo haya mengi na daraja la Kigamboni imekuwa ni ukombozi kwa Watanzania walio wengi. Hoja yangu ni kuiomba Serikali ilipe madeni haya kwa Mifuko yetu ya Hifadhi kwani fedha hizo ni za wafanyakazi kwa maana ya wanachama. Madeni haya yakilipwa tutaipa moyo Mifuko hii kuendelea kuikopesha Serikali kwa maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Mifuko ya Jamii kuwekeza mikoani. Naiomba hii kuwekeza mikoani kwa kufungua matawi ya ofisi zao pamoja na kujenga nyumba za kuuza na kupangisha Watanzania hususan wafanyakazi ambao hawana nyumba za kuishi hata nyumba za kudumu. Napenda kujua Singida mifuko hii itaanzisha ofisi lini na kujenga nyumba za kuuza na kupangisha? Nasubiri majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kima cha chini cha mishahara ya wafanyakazi. Naipongeza Serikali kwa vile imekuwa ikiongeza kiwango cha kima cha chini cha mishahara ya wafanyakazi, bali kiwango kinachotolewa bado hakijatoshleza kulingana na hali halisi ya maisha. Ni lini Serikali itaongeza kiwango cha mishahara ili kilingane na hali halisi ya maisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, pamoja na kurudisha posho ya kufundishia kwa asilimia 50 naomba kionekane, kisiunganishwe na mshahara kwani tunaona kama viini macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, ajira ya watumishi wa ddani. Napenda kueleza Serikali kuwa mikoa inayotoa wasichana wa ndani ni Singida, Iringa na kadhalika. Naiomba Serikali kusimamia utekelezaji wake kwani bado watumishi hawa wa majumbani wanadhulumika, hawalipwi kiwango kilichowekwa na Serikali. Vilevile elimu itolewe kwa njia ya televisheni, redio na magazeti ili wajue kwani wengi wao hawajui. Naomba majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, wanawake kupoteza haki wanapoachika, Kufiwa na kuzalishwa nje ya ndoa. Ni ukweli usiofichika bado kuna kudhulimiwa sana kwa wanawake wengi wanapofiwa, kuachika au kuzaa nje ya ndoa. Naiomba Serikali kuunda chombo cha kisheria cha kuwasaidia wanawake wenye uelewa mdogo wa kisheria, naomba majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumaliza kwa kurudia kutoa pongezi pamoja na kuunga mkono hoja nikitegemea Singida na wao watapatiwa gari kama walivyopewa jirani zao wa Tabora.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumpongeza Waziri, Naibu na Watendaji wa Wizara nashauri yafuatayo:-

(i) Kima cha chini cha mshahara wa sekta binafsi kipangwe na Serikali haraka.

(ii) Usalama sehemu za kazi ni mdogo hakuna vifaa vya kuzima moto, usafi wa mazingira ni hafifu hasa Idara ya Mahakama. Wafanyakazi wa Idara hii wanafanya kazi sehemu yalipohifadhiwa mafaili yaliyojaa vumbi. Wafanyakazi hao wataugua ugonjwa wa kifua kikuu (TB) mfano ni Mahakama Kuu - Arusha na Mahakama ya Mkoa wa Arusha.

(iii) Ukuzaji ajira, Serikali imeshindwa kusababisha uongezekaji wa ajira kwani kama hakuna kiwanda hapa nchini kazi zitakuwa hamna. Kilimo cha mkono siyo ajira (*subsistence agriculture*)

(iv) Mwisho kabisa nashauri Serikali iwatafutie wasomi wake kazi nchi za nje, kuna wataalam wengi hawana kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikichangia mara nyingi kuhusu tatizo la ajira nchini. Katika mwaka 2014/2015, Wizara hii ilipangiwa shilingi bilioni 2.925 kwa ajili ya programu ya ajira kwa vijana hadi kufikia mwanzo wa mwezi huu wa Mei hata shilingi moja haijawekwa katika kifungu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia Wizara ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha iliahidi kukiwekea kifungu hiki fedha kwa ajili ya mikopo kwa vijana yenye riba nafuu. Napenda kujua ni kiasi gani cha fedha kimewekwa katika kifungu hiki na kama zimewekwa, je, fedha hizo zimeshapelekwa kwa vijana? Nitazuia shilingi ikiwa sikupata majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wengi wa mahotelini hasa lodge na mabaa wanalipwa malipo madogo sana. Baadhi yao wanalipwa kutokana na chupa za bia wanazouza kama hawakuuza basi hawana malipo kwa siku ile. Wafanyakazi hawa ambao wengi wao ni wanawake inabidi wafanye kazi za ziada zisizokuwa za heshima ili waweze kuendesha maisha yao. Namuomba Waziri alipe kipaumbele tatizo hili kwa kutumia sheria zilizopo ili wafanyakazi hawa wapewe malipo yanayostahiki na kuwa na mazingira mazuri ya kufanyia kazi.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni kuhusu Mfuko wa Pensheni wa NSSF. Mfuko huu umekuwa ukisaidia nchi yetu katika shughuli mbalimbali za maendeleo hususan ujenzi wa vyuo, barabara, madaraja na kadhalika na kwa kweli umesaidia katika kuinua hali ya uchumi na nchi yetu. Kwa kuwa Mfuko huu hutumia fedha za wanachama wake katika kukamilisha shughuli zote hizo za maendeleo, ni matumaini yangu kwamba wanachama ambao ndiyo wadau wakubwa (Na.1) wana haki ya kufurahia matunda ya jasho lao kwa 100% kuliko mtu mwingine yeyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, natambua jitihada za Mfuko katika kuwawezesha wanachama wake kujikwamua katika hali duni za uchumi kwa kuwajengea mazingira ya kujiunga katika SACCOS na kuweza kukopa huko. Jitihada hizi ni nzuri lakini nataka kujua Serikali/NSSF imejipangaje au inakusudia vipi kuhakikisha kwamba mwanachama mmoja mmoja ananufaika na mikopo yeye binafsi ili aanze kujiandaa mapema na maisha baada ya kustaafu kuliko kulazimishwa kujiunga kwenye SACCOS?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, natambua kuna sheria inayozuia fedha za mwanachama kuwa dhamana ya mkopo lakini sheria si msahafu. Ni lini sheria hii italetwa ili kubadilishwa ili wadau wa Mfuko huu wafaidike na fao la kukopa wao wenyewe kama ambavyo Mifuko mingine inafanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ni lini NSSF itaanza kutoa mikopo ya ujenzi wa nyumba kama inavyofanya Mifuko mingine kuliko utaratibu huu wa kukopesha nyumba ilizojenga kwa bei kubwa sana ambazo mtumishi wa kawaida hatamudu kuzilipia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuongelea kuhusu kaguzi za kazi zinazohusu zaidi afya na usalama mahali pa kazi, hivyo zinahusu zaidi rasilimali watu. Rasilimali watu ndiyo msingi mkuu katika shughuli za miradi yote ya maendeleo sambamba na rasilimali fedha, vifaa na kadhalika. Kama Taifa tumekuwa tunaamini kwamba ili tuendeele tunahitaji watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa rasilimali watu ni dhahiri, hivyo napendekeza na kushauri yafuatayo:-

(i) Kaguzi za kazi zisiishie usalama wa afya pekee yake bali utoshelezi wa wafanyakazi kwa idadi, ujuzi na uzoefu katika kazi mbalimbali. Maboresho yataongeza tija.

(ii) Taarifa za kaguzi za kazi iwasilishwe na kufanyiwa kazi kama zile za CAG ambazo kwa kiasi kikubwa zinahusu rasilimali fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni ajira kwa wageni. Kufuatia Sheria za Ajira kwa Wageni ya mwaka 2014 inayoipa Wizara mamlaka ya kuwa msimamizi wa utoaji vibali vya ajira kwa wageni, nashauri katika utekelezaji wa jukumu hili ishirikiane na vyombo vingine vya Serikali ambavyo tayari vinafanya shughuli kama hizo kwa mujibu wa sheria na kwa kadri itakavyoonekana inafaa. Mfano, madaktari, wahandisi, manesi, wahasibu na kadhalika wanazo bodi na taasisi nyingine na licha ya kuwezesha kisheria tayari wanazo kanzidata ya wataalam kulingana na mahitaji kitaifa ambao wanatekeleza jukumu hilo. Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012- 2015/2016) umeainisha mahitaji ya wataalam katika kila sekta na katika kila kipaumbele. Ni vema sasa kama Taifa tukaianzisha, kuiboresha na kuifanya kuwa hai wakati wote kanzidata ya wataalam kulingana na mahitaji ya kitaifa.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kuwapongeza Mawaziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kuleta bajeti ili tuweze kujiadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ambayo ningependa kuyachangia na kupatiwa ufafanuzi kutoka Serikalini.

(i) Madeni kwenye Mifuko ya Jamii. Nianze kwa kutoa pongezi kubwa sana kwa Mifuko hii ya Jamii, *NSSF, LAPF, PPF, GEPF* kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakifanya hasa kuikopesha Serikali kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo kama ujenzi wa Chuo Kikuu Dodoma, nyumba za Polisi, barabara, madaraja na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini inasikitisha mpaka sasa hivi Serikali haitengi bajeti ya kutosha ya kuhakikisha madeni haya yanalipwa kwa wakati na Mifuko hii iendeleo kujijendesha kibiashara ili wanachama waweze kufaidika. Ningependa kujua mkakati wa Serikali kuhakikisha madeni haya yanalipwa kwa sababu mengine ni ya muda mrefu sana.

(ii) Sheria ya wafanyakazi wa majumbani. Naomba kujua sheria ya kuwalinda wafanyakazi wa majumbani italetwa lini sababu pamoja na Serikali kuleta Muswada wa Kimataifa ili uridhiwe humu Bungeni bado kumekuwa na unyanyasaji mkubwa sana kwa wafanyakazi hao ikiwemo kutokuwa na mikataba ya kazi, kutokupatiwa likizo ya mwaka na kutojiunga katika Mifuko ya Jamii. Naomba Serikali itoe majibu ya uhakika kuhusiana na sheria hiyo ili haki itendeke.

(iii) Pensheni ya wazee. Niwapongeze wenzetu wa Baraza la Wawakilishi Serikali ya Zanzibar kwa kupitisha sheria ya kuhakikisha wazee wote wanapatiwa pensheni. Pamoja na kuwa tumekuwa tukilalamika kila linapokuwa Bunge la bajeti na kwa maswali mbalimbali, lakini bado Serikali haijaweza kusimamia utekelezaji kwa kuhakikisha haki ya wazee inatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee wengine bado hawajaweza kupata bima ya afya, wazee bado wanafanyiwa ukatili na hasa kuuwawa. Serikali ilijenga nyumba kwa baadhi ya mikoa lakini wazee hao hawatengewi bajeti yoyote na kusababisha wazee wetu kuwa ombaomba na kudhalilika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itupatie majibu ya uhakika ina mkakati gani wa kuhakikisha wazee wanapata haki zao.

(iv) Ajira kwa vijana. Kwa mujibu wa takwimu hizi inaonesha wazi kuwa bado Serikali haijaweza kuwa na mikakati madhubuti ya kusaidia vijana. Kuna vijana milioni 15 ambao hawana ajira za uhakika. Serikali iliagiza kila

Halmashauri itenge eneo kwa ajili ya kujenga eneo la biashara kwa ajili ya vijana lakini sijajua Wizara hii imesimamia vipi agizo hili. Vijana wengi wamekuwa wakinyanyasika kutokana na kufanya biashara ndogondogo inayotambulika kama wamachinga kwa kunyang'anywa bidhaa zao, kupigwa na kutopewa mitaji ya biashara. Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhusiana na suala hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Wizara hii. Wizara hii ni muhimu sana na ina uhusiano wa moja kwa moja na maendeleo ya jamii lakini pia na vijana. Vijana ni zaidi ya asilimia 50 ya Watanzania lakini pia ni vijana ambao ndiyo waathirika wa ukosefu wa ajira. Ni katika Wizara hii ndiyo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ipo ambayo inaweza kuwa na mchango mkubwa katika utatuzi wa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina ardhi kubwa sana yenye rutuba ambayo bado iko wazi. Tanzania ina maji mengi, mito, maziwa na ya visima virefu. Ni kwa nini Serikali isitumie Mifuko hii kuanzisha mashamba kwa kuandaa ardhi na kutoa pembejeo kwa vijana wengi kwa njia ya mikopo, mikopo inaweza kulipwa baada ya mavuno. Ni vigumu vijana kuanzisha mashamba bila msaada lakini iwapo utaratibu huu utawezekana, vijana wengi wanaweza kujiunga na *scheme* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi wasomi sasa wamekubali kuwa maendeleo yao na ya nchi yako kwenye kilimo lakini wengi wao hawana uwezo wa kuanzisha mashamba yao wenyewe. Kuna ushahidi na mfano hai wa vijana watano waliomaliza elimu ya chuo kikuu walioamua kuingia kwenye kilimo na kupata mafanikio. Hii itasaidia vijana wengi kujijiri lakini pia kukuza makusanyo ya Mifuko ya Jamii na kuongeza uzalishaji na pato la jamii husika na Taifa kiujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko ya Jamii imehusika na maendeleo makubwa ya nchi hii. Napongeza kwa ujenzi mbalimbali wa miundombinu na taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na vyuo vikuu mbalimbali. Shirika la NSSF limejenga Daraja la Kigamboni na linasaidia sana wakazi wa Dar es Salaam. Kuna tatizo kubwa upande wa Kigamboni kuhusiana na barabara inayounganisha daraja la Kigamboni. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu ambapo tuliomba NSSF ichukue jukumu la kujenga barabara hiyo duni ili daraja liweze kutumika na Wizara ya Ujenzi ilikubali. Sasa napenda kujua ni hatua gani sasa iliyofikiwa kati ya Serikali na NSSF kuhusiana na ujenzi wa barabara hiyo. Waziri atakubaliana nami kuwa bila barabara hiyo daraja litakuwa ni mapambo na kwa ajili ya kuvusha waenda kwa miguu tu. Fedha za ujenzi wa daraja ni za wananchi.

MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga kwa hotuba yao nzuri na kwa moyo wao wa uzalendo wa Taifa na kwa Watanzania wenzao. Nawapongeza pia Watendaji Wakuu na wataalam wa Wizara hii na taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua katika kutekeleza dira ya Wizara hii, ni vijana wangapi hapa nchini ikiwezekana Kimkoa wamenufaika katika shughuli mbalimbali za kiuchumi. Kwa maneno mengine naomba kujua Wizara imetengeneza ajira kiasi gani katika kipindi cha miaka mitano (2010-2015).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara imekiri kupitia hotuba yake kwamba kuna changamoto nyingi zinazowapelekea vijana kukosa ajira. Je, Wizara ina mkakati gani ambao utapelekea kuondoshwa au kupunguza changamoto hizo ili kuwezesha vijana kupata ajira salama zisizohatarisha afya na maisha yao? Tumejionea watu katika mataifa ya nje wakijiingiza kwenye soko la ajira la Tanzania, mbaya zaidi watu hao hufanya kazi ambazo Watanzania wana uwezo nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi nyingi za kifedha hasa zenye kutoa mikopo hazina mazingira rafiki kwa vijana kuweza kukopa na hivyo kuweza kujijiri. Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi utakaolazimisha mabenki kushusha riba katika mikopo, kuzisaidia NGOs na taasisi nyingine zisizo za Serikali kutoa mafunzo yatakayowajengea uwezo vijana waweze kujijiri na kuanza kuwa wabunifu wa miradi mbalimbali itakayowasaidia kuondokana na umaskini kati yao kama Dira ya Taifa inavyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na takwimu zinazoonesha ajira zilizozalishwa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, bado hali ya ajira kwa vijana hapa nchini ni mbaya sana. Vijana wengi wanaishi maisha ya kubahatisha. Serikali inapaswa kuja na mpango wa dharura ili kuokoa vijana na ombwe hili la ukosefu wa ajira hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni inayodaiwa Serikali na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ni lini itayalipa ili iweze kuhudumia wanachama wake vizuri zaidi? Niiombe Serikali iwaambie Watanzania kiasi cha fedha inachodaiwa na Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya waajiri hapa nchini hawazingatii masuala ya afya na usalama mahali pa kazi. Napenda kujua ni waajiri wangapi wamewajibishwa na Serikali? Ni faini kiasi gani walitozwa ili iwe ni fundisho kwao na kwa waajiri wengine wasiozingatia matakwa ya kisheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali kwamba SSRA itumie nguvu iliyonayo kisheria kuhakikisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hapa nchini haihujumiani kwa lengo la kutafuta wanachama huku ikidhoofishana kwa upande mwingine. Sambamba na hili, nashauri SSRA ihakikishe inasimamia utekelezaji wa miongozo na kanuni mbalimbali inayotoa mara kwa mara ili kuwe na uendeshaji bora wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iandae programu ambayo itasaidia kuwatambua wazee wote hapa nchini na hivyo kuweza kuandaa malipo ya pensheni kwa wazee hawa. Hii ni muhimu sana. Watumishi waliotumikia Taifa hili lazima kupitia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wawekewe hatma njema baada ya utumishi wao uliotukuka.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi sana kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu na Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushukuru sana Shirika la NSSF kwa ushirikiano na wananchi wa Mbinga.

Msimu uliopita NSSF walikopesha AMCOS nne jumla ya shilingi bilioni mbili. Fedha hizi ziliwezesha ukusanyaji wa kahawa na kuiza. AMCOS zilipata faida ya zaidi ya shilingi bilioni 1.7 ambazo ziliwezesha malipo ya pili kwa wakulima kufanyika. Faida hii zamani ilikuwa inakwenda kwa makampuni binafsi lakini kwa mkopo huo, fedha hizi zilienda kwa wakulima. Msimu huu pia AMCOS hizi zimeidhinishwa kiasi cha mkopo wa kiasi hicho hicho. Maombi ya AMCOS karibu 10 yamefanyiwa kazi na NSSF. Hongera sana Dkt. Dau, hongera sana NSSF, hongera sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, endeleeni kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na kumpongeza Waziri wa Wizara hii, Naibu Waziri na hata Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji wengine wa Wizara hii kwa uchapaji wao wa kazi uliotukuka. Naomba kuchangia hoja hii kwa kuuliza maswali yafuatayo:-

(i) NSSF ilikuwa na mpango wa kujenga *commercial complex* katika Halmashauri ya Mji wa Tarime. Eneo lilitengwa nafikiri hata michoro iliandaliwa. Je, mpango huo umefikia wapi? Ni lini ujenzi huo utaanza na kwa nini umechelewa?

(ii) Suala la kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ni muhimu sana kwa maendeleo yoyote ya jamii. Watanzania walio wengi kwa sasa hivi hawana ari

na moyo wa kujituma kufanya kazi kwa juhudi na maarifa. Kwa nini hali hii imetokea kwa Watanzania? Je, Wizara imefanya utafiti wowote kuhusiana na hali hii? Kama ndiy, imegundua nini? Kama siyo inasubiri nini kufanya utafiti? Kauli kama vile Kazi ni Uhai, Kazi ni Utu, Kazi ni Msingi wa Kujitegemea na kadhalika kwa nini hazitumiki siku hizi kuhamasisha watu kufanya kazi?

(iii) Ujasiriamali ni dhana pana sana ambayo ikitumika vizuri na jamii ikaiielewa vizuri itasaidia sana kupunguza pengo la ajira hapa nchini. Je, Wizara ina mkakati gani mahsusi kuhakikisha kuwa dhana hii inamfikia kila Mtanzania?

(iv) Ni kwa nini Wizara hii haishirikiani na Wizara ya Chakula, Kilimo na Ushirika ili kuanzisha makambi ya kilimo kwa kila Mkoa ili kuwajiri vijana wetu katika sekta hii ya kilimo?

(v) Wizara ina mkakati gani madhubuti wa kuwafanya wasomi wengi wa Tanzania wapende kujijiri kuliko kusubiri ajira rasmi toka Serikalini?

(vi) Kuna tetesi nyingi kuwa Watanzania walio wengi hubaguliwa katika ajira hasa katika migodi, viwanda vya watu wenye asili ya Asia (Waarabu na Wahindi) na kadhalika au hata wakibahatika kufanya kazi au kupata ajira hunyanyasika sana. Je, Serikali inasema nini juu ya hali hii?

(vii) Baadhi ya wanasiasa hutoa matamko ambayo huwafanya vijana waache kujijiri kwa matumaini kuwa ajira iko Serikalini tu. Mathalani wanasema Serikali iajiri vijana wote wanaohitimu vyuo vikuu au ajira kwa vijana ni bomu linalosubiri kulipuka na kadhalika. Je, Serikali inawashauri nini wanasiasa hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MICHANGO KWA MAANDISHI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO

MHE. DKT. HAJI H. MPONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti iliyotengwa kwa Wizara hii ni ndogo sana kulingana na majukumu ya Wizara. Aidha, hata fedha zilizotengwa mwaka 2014/2015 bado zimekuwa zikicheleweshwa hivyo kuiathiri Wizara kutekeleza majukumu yake. Naiomba Serikali kuongeza bajeti iliyotengwa kwa Wizara hii ili na fedha hizi zipelekwe katika wakati mwafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kufanya ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi – Sofi. Naomba ukarabati huu umalizie majengo na miundombinu mingine iliyobaki. Chuo hiki cha Sofi kipo katika

maeneo pembezoni na mbali sana na Makao Makuu ya Wilaya ya Ulanga. Kutokana na mazingira yalivyo chuoni hapo, chuo kinahitaji sana usafiri wa angalau gari moja ili kiweze kutimiza kwa ufanisi majukumu yake. Hivyo, naomba Serikali kupita Wizara kukipatia chuo gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii iliyoletwa na Waziri. Ninampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii wakiwemo Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata na Wilaya, kwa kazi nzuri wanazozifanya katika mazingira magumu na yenye ufinyu mkubwa wa bajeti.

Benki ya Wanawake ilianzishwa ili kuwa mkombozi wa wanawake na jamii kwa ujumla na iweze kuwafikia wanawake wengi vijijini na vijijini. Serikali iliahidi kutoa shilingi bilioni mbili kwa miaka mitano mfululizo. Ninashauri pesa hizo zitolewe ili mikopo iweze kuwafikia wanawake wengi mikoani.

Fedha za benki zilipwe kwa wakati. Ninampongeza Mkurugenzi Mkuu wa Benki hii Mama Margreth Chacha, kwa umahiri wake yeye na watumishi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki za watoto zimeendelea kuvunjwa na tumeshuhudia watoto wengi wakipata shida, pamoja na juhudi zinazofanywa na Serikali tunashuhudia vitendo vya ukatili kwa watoto vikiendelea. Nitaoa ushauri kuwa, Serikali iendeleo kutoa elimu kwa jamii kutekeleza majukumu yake. Ninapongeza hatua kubwa zinazochukuliwa kuhakikisha haki za watoto zinaingizwa katika Katiba Pendekezwa.

Wananchi tuipegie kura Katiba hii wakati ukifika ili kuhakikisha kwamba, Haki za Watoto, Wanawake na Jamii kwa ujumla zipate kutekelezwa kama haki za Kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Janga la UKIMWI limeendelea kuwa tatizo kubwa miongoni mwa wanawake na wasichana. Pamoja na juhudi kubwa zinazofanyika katika Mikoa ya Njombe na Iringa, kumeendelea kuwa na maambukizi makubwa. Elimu ya ukatili wa kijinsia haikuwafikia wanawake wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Waziri aje akutane na Viongozi Wanawake pamoja na Wadau wa Maendeleo, kuona mikakati ya dharura ifanyike katika Mikoa hii miwili. Tukiweza kupunguza maambukizi mapya katika Mikoa hii miwili, tutakuwa tumeshusha maambuki kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia kwa kuwashukuru Wanawake wote wa Mkoa wa Iringa, kwa imani yao kubwa kwangu. Ninaomba niwahakikishie kwamba, nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote.

Ninaomba wajiandikishe kwa wingi katika Daftari la Wapiga Kura ili kukipigia kura Chama cha Mapinduzi (CCM) ili kiendelee kudumisha amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mashirika yasiyo ya Kiserikali; Mheshimiwa Waziri akiwasilisha hotuba yake kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya 2014/2015 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Mheshimiwa Esther N. Matiko alitaka Serikali kutoa maelezo ya kina, ni kwa nini Serikali imekusudia kuzifutia usajili wake NGOs zaidi ya 1000 katika kipindi hiki tunapoelekea Uchaguzii Mkuu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitoa sababu zifuatazo:-

(a) Kwamba NGOs nyingi zimejikita mjini badala ya vijijini na hivyo kukiuka masharti ya usajili;

(b) NGOs nyingi zinapokea fedha kutoka nje ya nchi;

(c) NGOs hizi hazijatoa taarifa za uendeshaji wake toka mwaka 2005 kwa miaka 10 sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata maelezo ya kina, kwa sababu hizo zilizotolewa na Serikali: Je, kwa NGO kujikita mijini ni kosa la NGOs au la Serikali kushindwa kuweka mazingira mazuri ya kuziwezesha kufanya kazi vijijini? Je, ni jitihada zipi zimefanywa na Serikali kuhakikisha kwamba maeneo ya vijijini yanakuwa ni rafiki kwa NGOs hizi?

Pili, kwa kusema kwamba NGOs hizi zinapokea fedha toka nje hata kwa masuala madogo madogo hata yale ya ujenzi wa vyoo vya shule: Je, fedha hizi zinawanufaisha hawa wenye NGO au Watanzania kwa ujumla wake? Nataka maelezo ya kina, ni kwa namna gani fedha za nje zinaweza kuhatarisha usalama wa nchi kama zinapatikana kwa kufuata masharti na utaratibu uliowekwa na nchi?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Tatu, kwa kusema kwamba NGO hizi hazijatoa taarifa zake toka mwaka 2005 mpaka sasa, nani ni mzembe? NGOs au Serikali ambayo ndiyo msajili wa NGOs hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Baraza la Taifa la NGOs halikuhakikisha kwamba NGOs zote zinatoa taarifa zake kila mwaka kama ambavyo sheria zinataka? Serikali kwa kukiuka Sheria ya Ukaguzi wa NGOs, imechukuliwa hatua gani? Nani amewajibishwa kwa hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nataka kujua kama WAMA nayo itafutiwa usajili wake kwa sababu nayo ilikiuka masharti ya uanzishwaji wake kwa kumjumuisha Waziri mwenye dhamana ya kusimamia NGOs kuwa mjumbe wa Bodi hiyo. Vinginevyo hatutatenda haki kwa kuzifutia NGOs usajili wakati kazi zake zinaonekana na zimefanya kazi kubwa ya kufichua maovu, uchafu na ufisadi wa Serikali. Hivyo, tuziunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina vyo vingi vya maendeleo ya jamii pamoja na vile vya ustawi wa jamii. Vyo hivi vinazalisha Maafisa Maendeleo ya Jamii ambao kama wangetumika vizuri wangeweza kusaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa matatizo yanayokususu ustawi wa jami. Mfano, watoto wa mitaani, wazazi kutelekeza watoto, unyanyasaji wa kijinsia na ukatili wa wanawake, watoto na wanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitaka Serikali ituambie imejipanga vipi kimkakati kuhakikisha kwamba inatoa ajira kwa wahitimu wa vyo hivi ili waweze kufanya kazi zao walizosomea kuliko ilivyo sasa? Maana wengi wamehitimu na wanazurura mitaani bila ajira ya maana. Wengine wanaamua kutafuta vibarua mahali ambapo hata hawawezi kutumia elimu yao waliyoipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa kuwa na vituo vingi hasa vijijini kwa Benki ya Wanawake ni kubwa maana itasaidia wanawake wengi kupata mikopo ya riba nafuu, hivyo kujiendeleza wao wenyewe na kujitegemea hususan kwenye shughuli za ujasiriamali. Je, kwa mwaka huu wa fedha Serikali itatimiza ahadi yake iliyoitoa hapa Bungeni ya kuanzisha kituo cha benki hii katika Mkoa wa Singida? Ahadi hii ilitolewa na Mheshimiwa Pindi Chana, Naibu Waziri akijibu swali langu nililomwuliza: ni kwa nini mpaka sasa hakuna kituo Singida? Kwa kuwa ilikuwa ni ahadi ya Serikali kwamba mwaka huu wa fedha itatekeleza, naomba kujua mchakato wake uko katika hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa pongezi nyingi kwa Waheshimiwa Waziri na Manaibu Waziri wawili na Katibu Mkuu na Wizara nzima. Mnajitahidi sana.

Nampongeza pia mtendaji Mkuu wa TWB; tunaomba tawi moja lifunguliwe Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba fedha ya kujenga majengo mawili ikiwemo nyumba ya kuishi kwa ajili ya Mwalimu/Wataalam wanaokuja kujitolea kufanya kazi Mbinga. Tumeanzisha kozi ya kuongeza thamani madini kwa kushirikiana na Chuo cha Maestu cha nchini Korea Kusini. Tayari tunaye Mwalimu mtaalam wa mambo hayo mwenye *PhD. (Jewelry and Gemstone School)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni shule muhimu sana kwa Watanzania ukizingatia utajiri wa madini tulionao kwa sasa hivi, vijana hawa wanauza na kutengeneza mikufu ya shaba, hereni, pete za harusi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana *support* za Wizara kwa ufanisi zaidi. Tunaomba pia fedha zaidi kwa ajili ya wanawake na vijana.

Naunga mkono hoja hii. Nawasilisha.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nizungumzie upungufu wa wafanyakazi wa Maendeleo ya Jamii. Umuhimu wa Maendeleo ya Jamii, umefafanuliwa vizuri katika ukurasa wa tisa aya ya 15 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Upungufu wa wataalam katika sekta hii Kitaifa ambao ni asilimia 61 (ukurasa wa 65) ni mkubwa sana. Naishauri Serikali kuongeza nguvu ya kibajeti na kimkakati ili kuondoa tatizo hili.

Kwa kuwa, upungufu huo ni mkubwa zaidi katika Wilaya ya Tunduru (Kikata asilimia 86) kupita ule wa Kitaifa kwa mbali, naomba mkakati wa kuondoa tatizo hili uipe kipaumbele Wilaya ya Tunduru

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunashukuru kupewa gari na tutalitumia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni uvamizi na matumizi kinyume cha taratibu katika maeneo ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Nandembo, ufuatiliwe na Serikali na kurudisha maeneo hayo kwa matumizi ya chuo.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya kuokoa muda mchango wangu nauorodhesha (*bullet points*) nao ni:

(1) Serikali ifanye juhudi zaidi kuwaondoa watoto wa mtaani, hii ni *time bomb*.

(2) Ukatili wa wanawake, Serikali isimamie fika Sheria ya Ndoa. Polisi wachukue hatua za sheria kwa wanaume wanaowapiga wake zao, hakuna sheria inayoruhusu wanawake kupigwa.

Ndoa za utotoni, Sheria ya Ndoa ibadilishwe umri wa kuoa uanzie miaka 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa juhudi zake za kutoa elimu ya haki za wanawake na watoto kwa redio, lakini juhudi zinaelekea kukwamishwa na uhaba wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono bajeti kwa sababu ni ndogo sana shilingi bilioni 31 zitafanya nini?

Samahani, nilisahau uboreshaji wa Vyuho vya Jamii hasa Chuo cha TANGO Mbulu ambayo inatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii haijapewa umuhimu na Serikali mbali na kwamba inahusu suala zito la Maendeleo ya Jamii nzima ya Watanzania. Fedha iliyotengwa ni ndogo sana kiasi unauliza ni maendeleo gani fedha hii inaweza kufanya. Pia fedha za maendeleo – mikopo inayotolewa kwenye Manispaa, Wizara haina uwezo nazo kwa hiyo, ni vigumu sana kuratibu. Ni kwa nini fedha hizi zisiwe chini ya Ofisi za Maendeleo ya Mikoa husika ili basi ofisi hizo ziweze kuratibu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya ina Ustawi wa Jamii chini yake, lakini kwenye idara hii ina kambi za wazee, watoto ambao kwa kiwango kikubwa hawapatii huduma inayostahili kwa sababu Wizara ya Afya ina jukumu kubwa la kuangalia afya ya Watanzania. Serikali haioni iko haja ya kulirudisha suala la ustawi wa jamii kwenye Wizara ya Maendeleo ili kuondoa adha na hali mbaya ya kambi hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa muda mrefu imefanya kazi kubwa juu ya kuzuia ukatili wa watoto na wanawake, lakini bado kuna kesi nyingi sana za unyanyasaji wa watoto. Je, Serikali haioni iko haja ya kuwa na kitengo maalum cha kushughulikia kesi hizi za unyanyasaji wa watoto na wanawake na

hukumu kutangazwa ili zijulikane na jamii? Hii inaweza kutoa elimu na fundisho, lakini pia itakuwa chachu kwa wale ambao wanaona haya kuripoti unyanyasaji anaopata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuanzisha Benki ya Wanawake. Serikali iliahidi kutoa mtaji wa ziada kila mwaka, lakini fedha hizi bado hazitolewi. Je, Benki hii sasa hivi ina mtaji na shilingi ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki hii ilichukuliwa kuwa mkombozi wa mitaji kwa wanawake, lakini bila Serikali kuisaidia haiwezi kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitoa fedha, mikopo, malipo mbalimbali kupitia benki tofauti. Ni kwa nini mikopo hiyo tofauti isipitie pia benki hii ili kupitia *commission* iweze kusaidia kukuza mtaji wa benki hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali na hata wanaharakati wamekuwa mstari wa mbele kupiga vita mimba za utotoni, lakini elimu kwa wazazi hasa vijijini bado na hivyo wazazi kuhusika na ongezeko la mimba za utotoni. Wizara ina mpango gani kupambana na suala hilo?

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Sophia Simba kwa hotuba nzuri na kwa kazi nzuri unayoifanya. Aidha, ninampongeza sana Naibu Waziri Dkt. Pindi H. Chana kwa kazi nzuri ambayo anaifanya kwa kushirikiana na wewe. Ninampongeza Katibu Mkuu, watendaji wote wa Wizara yake kwa kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichangie yafuatayo:- Naungana na Wizara kuitaka Serikali iongeze bajeti kwa Wizara hii. Tumekuwa tukilalamika mwaka hadi mwaka bila mafanikio lakini mwaka huu lazima tupate mabadiliko. Ninashauri Waziri akutane na Kamati ya Bajeti wakati wanajadili bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ni tatizo; kwa mfano, Wilaya ya Kilindi hawana usafiri wa aina yoyote, hivyo hata zile kazi wanazostahili kufanya ni ngumu sana hasa ukizingatoa Halmashauri yenyewe haina magari ya kutosha. Naomba angalau tupate hata pikipiki, kwani kuna changamoto nyingi sana kwa upande wa mimba za utotoni, ukatili wa kijinsia na malezi ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wa mitaani ambao wanazungumziwa mara nyingi ni wa mjini. Naomba niwakumbushe na huko vijijini kuna watoto wenye mazingira magumu, labda tuweke mikakati ya jinsi ya kuwatambua watoto hao na namna ya kuwasaidia Maafisa Maendeleo ya Jamii, wakipanga vizuri mikakati yao wanaweza kupeleka maombi yao kwenye Mfuko wa Jimbo na mapato yenyewe ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Maafisa Maeneleo ya Jamii ni amana kubwa huko vijijini, naomba mjitahidi kuwatembelea na kuwapatia *refresher courses* na kadhalika. Aidha hata wale wastaafu wanaweza kutumika kwani bado wana uwezo, watafutwe na wapewe kazi za mikataba, endapo wataonekana bado wana uwezo.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Sophia Simba, Naibu Waziri, watendaji wote wa Wizara kwa kuleta bajeti yao ili tuweze kujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti finyu: Wizara hii ni nyeti sana na inashughulikia mambo muhimu ya watoto na wanawake ambao ndio msingi wa maendeleo yetu, lakini bado haijaweza kupewa kipaumbele. Tunaona kila mwaka inapatiwa pesa kidogo sana na haifiki kwa muda muafaka na kusababisha miradi ya maendeleo kutopewa kipaumbele kabisa. Hii inaathiri sana ustawi wa shughuli za kijamii zinazosimamiwa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa makundi mbalimbali ya watoto na wanawake: Ukisoma ukurasa wa 5 na 6 wa kitabu cha hotuba ya Waziri, pamoja na Serikali kuleta sheria kwa kila Halmashauri kutenga 5% ya mapato kwa ajili ya kukopesha makundi ya akina mama na vijana, utekelezaji umekuwa ukisuasua na bado makundi mengi ya vijana hayana uelewa wa kutosha wa kuweza kuifikia mikopo hiyo. Pia, bado pesa hiyo ni kidogo sana ukilinganisha na idadi ya vikundi vingi na hamasa iliyopo kwa ajili ya mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeomba Serikali itueleze mpango gani umewekwa kwa zile Halmashauri ambazo bado hazitekelezi agizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuvo vya Maendeleo ya Jamii: Vyuvo vingi vya maendeleo vimekuwa vikikabiliwa na changamoto nyingi sana ikiwemo migogoro ya mipaka kama kile cha Lungemba kilichopo Iringa. Napenda kujua migogoro umefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake: Nimpongeze Waziri na Mkurugenzi wa Benki hii kwa kuendelea kusaidia kuwakopesha wanawake nchini na kuweza kufungua kituo cha Benki hii katika Mkoa wetu wa Iringa na pia kutoa hata mikopo ya viwanja. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, pamoja na kazi nzuri hii bado Serikali haijaweza kutoa mtaji wa kutosha kama iliyoahidi. Naomba kujua mkakati wake wa kuhakikisha mikopo hii inawafikia wanawake wote walio mpaka vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukatili na ubaguzi wa kijinsia: Ukurasa wa 17 wa kitabu cha hotuba unazungumzia ukatili na ubaguzi wa kijinsia, lakini bado, vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika jamii unaendelea kwa kasi kubwa. Mkoa wetu wa Iringa unakabiliwa na kesi nyingi sana za ubakaji wa watoto wadogo, lakini pamoja na kesi nyingine kuwa na vidhibiti, lakini zimekuwa zikichukua muda mrefu sana na kesi hizi kwa kiasi kikubwa zimekuwa zikiathiri kisaikolojia watoto hao na wazazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wadogo kuchanganywa na wakubwa katika magereza: Ukienda katika mahabusu za magereza yetu, bado watoto wadogo wanachanganywa na watu wazima. Hii inasababisha badala ya kuwasaidia watoto hawa, tunazidi kuwaathiri kwa kufanyiwa vitendo vibaya vya ubakaji katika magereza zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua je, Wizara hii ina mchango gani wa kuhakikisha haki inatendeka kwa watoto hawa? Pia, kuna watoto wanaozaliwa Magarezani Serikali inawasaidiaje watoto hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la watoto mitaani: Bado sijaona mkakati mahsusi uliowekwa na Wizara kuhakikisha wazazi na walezi wanapata adhabu ya kutosha ili kutoa fundisho. Mfano halisi ni wale wazazi walio katika Mkoa wa Dar es Salaam. Tunaomba kupewa mkakati wa kuhakikisha tatizo hilo linakuwa fundisho kwa watoto wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Sasa namwita mtoa hoja, Naibu Waziri wa Kazi na Ajira, dakika kumi.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua kwanza nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hoja ya Waziri wa Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunjalia afya njema. Vilevile nakushukuru na kukupongeza wewe na Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wenzako kwa kazi nzuri mnayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana wapiga kura, wananchi wa Jimbo la Segerea ambao wameendelea kuniunga mkono na kushirikiana na mimi katika kuleta maendeleo makubwa sana katika Jimbo la Segerea ambalo ni mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge kwenye hoja hii ya Waziri wa Kazi na

Ajira na kutokana na muda nitakwenda kwenye hoja chache tu na Mheshimiwa Waziri atakamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Nassib Omar, Mbunge wa Mfenesini kuhusu wafanyakazi kwenye hoteli na baa kulipwa malipo kidogo sana. Kama jambo hilo linafanyika basi ni ukiukwaji wa sheria kwa sababu sheria yetu ya kazi na ajira pamoja na Tangazo la Serikali la kima cha chini ambalo limeweka kima cha chini cha mshahara wa sekta ya huduma za majumbani na hotelini ambapo kama kikikiukwa ni makosa na tunapenda tupate taarifa inapotokea hali ya namna hiyo ya wafanyakazi kupunjwa. Vilevile tunaendelea na kaguzi ambazo zinatwezesha tukipata hali ya namna hiyo tuweze kuchukua hatua. Natoa wito kwamba ni marufuku mfanyakazi yeyote hata akiwa mfanyakazi wa ndani au hoteli kulipwa kiwango ambacho kipo chini ya kima cha chini kilichotangazwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine alizungumzia vitendo vya ubaguzi katika maeneo ya uwekezaji. Kwa kweli suala hili haliruhusiwi na jambo lolote la ubaguzi kwa wafanyakazi iwe ni vitendo vya ubaguzi au sera ambayo imewekwa na wawekezaji ni makosa kisheria. Kwa maana hiyo, sisi tutaendelea kufuata Sheria Na. 6 ya mwaka 2004 kufanya kaguzi na kuhakikisha kwamba vitendo hivi havitokei na kama vikitokea basi hatua zinachukuliwa. Waheshimiwa Wabunge na wananchi inapoonekana kwamba kuna hali kama hii basi taarifa zitolewe kwenye Ofisi za Kazi zilizo karibu na maeneo husika na hatua zitachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mustapha Akunaay alizungumzia kima cha chini cha mshahara kwa ujumla katika sekta binafsi. Serikali imejitahidi sana kuongeza kima cha chini ingawaje tunasema bado hakitoshi na hata Serikali inakubaliana na hilo. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita kima cha chini cha mishahara kwenye sekta binafsi kimeongezwa mara mbili, mwaka 2013 vilirekebishwa kati ya 21% - 65% na mwaka 2010 vilevile tulifanya marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea mwaka ujao wa fedha kima cha chini cha mshahara katika sekta binafsi kitaangaliwa kwa mara nyingine tena. Kwa kweli Serikali inathamini sana mchango wa wafanyakazi hawa kwenye sekta binafsi kwa manufaa ya waajiri wao kama makampuni binafsi lakini vilevile kwa maslahi ya nchi na maslahi yao wenyewe kama wafanyakazi. Kwa hiyo, itaendelea kwa kutegemea uwezo wa uchumi vilevile uwezo wa kuzalisha wa kampuni au sekta husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Eng. Ramo Makani alizungumzia suala la kaguzi za afya na usalama mahali pa kazi. Ametoa ushauri mzuri na sisi

tunaupokea na tunamhakikishia kwamba suala hili ni matakwa ya sheria. Kwa hiyo, tutaendelea kulishughulikia kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Eng. Ramo vilevile alizungumzia Sheria mpya ya Ajira kwa Wageni ya mwaka 2014 ambayo tumeipitisha hasa kuhusu wataalamu. Sisi tumekubaliana na kwa kweli tutaendelea kushirikiana na vyombo vya wataalam vinavyoundwa kwa mujibu wa taratibu za kisheria ili kuona namna gani tunaweza kukubaliana kuhusu vipengele vya kuwaruhusu wataalam kuingia ndani na kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ritta Kabati na wengine wengi wamezungumzia suala la kuridhia mikataba ya *ILO* na sisi tunasema kwa upande wa sharia, hawa wafanyakazi wa ndani wanalindwa na sharia lakini mkataba wa *ILO* upo katika hatua ya mwisho na mimi nadhani Bunge linalofuata tutaauridhia. Namwomba Mheshimiwa Ritta asije akatoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi walizungumzia masuala ya hifadhi ya jamii ikiwepo Kambi ya Upinzani na hasa kuhusu suala la pensheni. Suala hili Serikali inaendelea nalo na hivi karibuni nimechungulia nimeona na Mwenyekiti anayetengeneza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na ambacho ndiyo chama kitakachoingia madarakani tena mwezi Oktoba, amenieleza kwamba hili suala wanaliweka kwenye Ilani ya Uchaguzi kwamba katika miaka mitano inayokuja, pensheni ya wazee itaanza kutolewa kwa utaratibu ambao tutaona unafaa na tutaangalia ni miaka mingapi na watu gani. Suala hili sasa linaingia kabisa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu maandalizi tutakuwa tumeyakamilisha itakuwa ni utaratibu tu wa namna gani tuanze kulipa katika kipindi kisichozidi miaka miwili ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani Bungeni wamezungumzia masuala ya Hifadhi ya Jamii na hasa kuhusu suala la kuunganisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Suala hili linaendelea kuangaliwa na *SSRA* ikishirikiana na *ILO* wameleta Mtaalam Mwelekezi na suala hili tutaendelea kuliangalia. Katika mambo machache yaliyobaki ambayo *SSRA* wamekuwa wakifanya ni pamoja na kuangalia suala hili itakuwaje kama tukiamua kuunganisha Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii. Suala hili limezungumzwa sana, tutaendelea kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la uwekezaji wa mifuko hii nje ya miongozo. Nadhani kwa sababu *SSRA* wapo pale, suala hili linaangaliwa vizuri sana ili Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ifuate miongozi iliyowekwa na *SSRA* pamoja na Benki Kuu katika kufanya uwekezaji. Mimi nina hakika kwamba uwekezaji mpaka sasa haujakwenda kinyume cha miongozo ambayo imewekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Sylvester Mabumba alizungumzia kuhusu kuhujumiana katika mifuko hii wakati wa kuandikisha. Suala

hili litaendelea kufanyiwa kazi na SSRA na hasa kutoa elimu kwa sababu sasa hivi hii ni sekta ya ushindani. Kwa hiyo, kitakachofanyika ni kutoa elimu ili sasa katika ushindani wa kupata wanachama kusiwe na aina yoyote ya hujuma au upendeleo. Mimi nadhani suala hili litaendelea kushughulikiwa kama ilivyo kwenye kifungu cha 30 cha Sheria Na.8 ya SSRA ya mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madeni kwamba Mifuko hii inaidai Serikali kiasi kikubwa cha fedha, niseme tu suala hili ni kweli lakini tayari Serikali imeridhia kutoa hati fungani ya shilingi trilioni 1.2 kwa ajili ya kulipia miradi mbalimbali iliyotekelezwa na Mifuko ya Hifadhi za Jamii lakini vilevile pamoja na michango ya nyuma ya Mfuko wa PSPF ambayo imekuwa ikipigiwa kelele mara nyingi kwamba haijalipwa. Vilevile, tayari fedha zimetengwa kwenye bajeti ijayo shilingi bilioni 44.5 ambazo zitakuwa zinalipwa kila mwezi kwa ajili ya malipo ya mafao ya wastaafu wa PSPF, utekelezaji utanza mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa hoja ya Mheshimiwa Kigola ambaye alisema kwamba wafanyakazi wandalipwa ...

(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa naomba nimwite Waziri, Mheshimiwa Gaudencia Kabaka, Mwalimu wangu.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nikushukuru sana baada ya kukupongeza pia kwa kazi nzuri uliyoionyesha mpaka sasa hivi, kwa kweli unaonekana kama vile umekuwa kwenye hicho kiti siku nyingi. Unakimudu na naomba uendelee kukimudu na ni kwa sababu ulifundishwa na Mwalimu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana ukiangalia na muda uliokuwepo. *Of course* wengine walikuwa wanachangia maeneo yote mawili lakini kwa ujumla wachangiaji wetu wamekuwa 19 ukimuongezea na Mheshimiwa Naibu Waziri ni 20, waliochangia kwa kuandika ni tisa na waliochangia kwa kuongea ni 11. Naomba niwashukuru sana wote kwa michango yenu na kwa ajili ya muda naomba nisiwataje majina lakini wote tumewachukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ndiyo bajeti ya mwisho naomba niseme kwamba Wizara ya Kazi na Ajira ni Wizara ambayo zaidi inashughulika na masuala ya sera na sheria. Kwa hiyo, ni Wizara iliyojaa takwimu, *facts*, ukweli na uhakika siyo Wizara ya blablabla na ya maneno. Kwa hali hiyo, kwa muda

ambao tumekaa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwenye Wizara hii kwanza tulianza na Mheshimiwa Mbiliyi na baadaye Mheshimiwa Cecilia, nilifikiri atakuwa amesha-*catch up* katika mwenendo mzima wa ku-*report* kuhusu Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kusoma hiki kitabu kutoka ukurasa wa 1-45, najua umeniandikia *note* kwamba unanisaidia, lakini kitabu hiki hakiwezi kumsaidia mtu yeyote ambaye anataka kujua unasema nini hasa mbadala kuhusiana na haya ambayo tumeyafanya katika Wizara hii ukiacha mambo ya ajira, masuala ya wafanyakazi na hifadhi ya jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri hotuba yangu imekuja wakati muafaka ambapo tumekuja na taarifa au matokeo ya utafiti wa hali ya nguvukazi nchini kwa kipindi cha mwaka 2006 - 2014. Hii taarifa nilitoa jana kwa vyombo vya habari, imejaa takwimu za ajira, hali ya soko la ajira lilivyo, watu ambao wameajiriwa, wameajiriwa maeneo gani, sekta binafsi, sekta ya umma, sekta rasmi au sekta isiyo rasmi. Kwa hiyo, mtu ambaye anataka kukusaidia katika hili ungependa ajaribu kuoanisha yale ambayo mmesema au mmeyafanya, mngefanya nini zaidi ili kusudi muweze kuongezea kwa sababu hii nchi ni yetu sote. Mimi nachoshangaa kwa kweli kama Mwalimu ni kuangalia kitabu kimeandika mambo tunayosema ni *sweeping statements* kwa sababu ni manung'uniko, ni kukandia na kutoridhika. Sasa huwezi kumsaidia mtu kwa kutoridhika, kwa kukandia na kwa *sweeping statements*, naomba niseme hivyo.

MHE. ESTHER N. MATIKO: (*Hakutumia kipaza sauti*)

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Naomba usinjibu Esther! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapotoa taarifa sisi tunanyamaza kama waungwana, naomba na mimi napoongea nisijibiwe na mtu mpaka atakapopewa ruhusa na Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, endelea!

MHE. ESTHER N. MATIKO: (*Hakutumia kipaza sauti*)

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *I can not concentrate* wakati anaongea.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri endelea, ongea na kiti!

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tuwe waungwana kwa sababu hili ni Bunge, siyo mahali pa porojo wala siyo sokoni. Kwa hiyo, naomba ...

MHE. ESTHER N. MATIKO: (*Hakutumia kipaza sauti*).

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Matiko, naomba tafadhali!

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na hili neno la falsafa ya *self-reliance*. Falsafa ya *self-reliance* katika nchi yetu ni hai, haijafa, itaendelea kuwepo chini ya Chama cha Mapinduzi. Nikijaribu kuelezea maana ya neno falsafa, kwa Kingereza wanasema ni *principles of reality, knowledge or values based on reasoning*. Ukiangalia falsafa ya elimu, unaposema unataka kutoa falsafa ya aina fulani unazungumzia madhumuni ya elimu, majukumu ya mwalimu katika darasa yatakuwa ni yapi, pia, unazungumzia ni nini kifundishwe kwa maana ya mtaala. Kwa hiyo *philosophy* yote inakuwa *carried* na mtaala lakini pia unazungumzia njia za kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipopata uhuru tulianza na *philosophy* ya kujitegemea kwa sababu tulitaka tujenge Watanzania wanaokuja kwamba sisi hatutaendelea kuwa tegemezi, kuna mahali tunatakiwa tusimame sisi wenyewe. Kwa hiyo, tuli-define maudhui, aina ya Walimu na namna ya kufundisha kwa maana ya njia zilizokuwa zinaendana na wakati ule kuonyesha vijana wetu kwamba tunataka vijana wawe wakakamavu na wajitegemee, kwa hiyo, utaona mitaala ilikuwa na mambo ya kulima mashamba madogomadogo. Sasa anapoeleza Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba tumeachana nayo nafikiri ana-base zaidi katika mashamba yaliyokuwa yanalimwa wakati wa vipindi kwa maana ya *methodology of teaching*. Nasema hivi bado *philosophy* ya kujitegemea ipo, tuliambia hivyo na tuliwaandaa Watanzania hivyo na wale ambao wamesoma enzi hizo wanaelewa kwamba bado tunaendelea na elimu ya kujitegemea na ndiyo maana tulipoendelea kubadilisha mitaala tulikuja na kitu kinaitwa stadi za kazi kwa maana ya kuwaandaa vijana kujitegemea baada ya kumaliza shule ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana mitaala iliendelea kubadilika siku hadi siku sasa hivi tume-introduce masuala ya ujasiliamali na nimeambiwa na Wizara ya Elimu kwamba masomo haya yataanza kuanzia darasa la kwanza kwa maana ya *primary school, secondary school* na kuendelea na vyuo vikuu sasa hivi vinafundisha ujasiliamali. Hii yote ni *philosophy* ya elimu ya kujitegemea (*education for Self reliance*). Mwanafalsafa wetu Mtanzania Mwalimu Nyerere aliiweka hii vizuri, ukitaka kujua falsafa hii haijafa msome Mwalimu vizuri. Kwa wale ambao wamesoma vyuo vya ualimu au vyuo vikuu wanamjua Mwanafalsafa Maria Montessori ambaye anasema mtoto lazima umpe nafasi ya kuonyesha anachojua, wewe usimuonyeshe kwamba hajui kitu. Tunao akina John Dewey, tuna Paul Freire ambaye anasema *a child is not an empty tin* na mambo kama hayo. Haya yote tumeyafundisha katika mtaala wetu kuonyesha

kwamba mwanafunzi au mtoto anapoanza shule siyo *empty tin*, siyo *empty* kabisa ni kwamba unamuandaa yeye mwenyewe ajitegemee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme hivi, tunapokuwa tunatoa taarifa hapa twende *deeper* kuliko kuangalia *superficial*. Nimesoma sana hii taarifa, ukiangalia taarifa za ajira kwa mfano, kwenye kitabu cha hotuba yangu utaona kwamba utafiti wa nguvu kazi tuliufanya umejaribu kugusa maeneo yote ambayo Serikali kama mtengeneza fursa au mbuni fursa lakini kwa maana ya kutumia Sera ya Ajira ambayo ni shirikishi kwamba wadau wote washiriki katika kutengeneza ajira kwa sababu ajira haitengenezwi ndani ya Wizara ya Kazi Ajira inatengenezwa na wadau mbalimbali tukiwemo sisi Waheshimiwa Wabunge. Utaona kwa mfano mwaka jana tulipopata fedha za *development* shilingi bilioni tatu, kuna Wabunge wengi sana ambao walikuwa na uchungu wa kusaidia vijana wao kutengeneza ajira. Walikuja ofisini kuulizia ni lini tutawasaidia kuunda vikundi, kwa kweli nisema kwamba Wabunge wengi wa CCM, siwezi kuwataja hapa walikuja kujaribu kuona jinsi wanavyoweza kusaidia kutengeneza fursa za ajira, licha ya kushirikiana na mashirika mengine mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunao wadau kama *ILO*, wametusaidia sana kwenye masuala ya kurasimisha sekta hii isiyo rasmi. Sasa hivi sekta hii isiyo rasmi inachangia sana katika pato la Taifa. Tunataka sasa tuirasimishe kusudi iweze kuchangia vizuri zaidi lakini pia iweze kulipa kodi. Tunao wajasilimali ambao wanajitegemea lakini hatujawafahamu, hatujawasajili na hawawezi kukopesheka kama hawajarasimishwa. Kwa hiyo, kazi tunayofanya sasa hivi ndiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie hili suala la mahusiano kati ya wafanyakazi na Serikali. Kuna kurasa hapa zimeongelea sana kwamba Serikali inawanyanyasa wafanyakazi. Mimi nafikiri kurasa hizi zingezungumzia suala la wafanyakazi ndani ya Serikali lakini unapozungumzia wafanyakazi ndani ya sekta binafsi naomba uelewe kwamba Serikali ni mdau kwa sababu katika Wizara ya Kazi na Ajira tunathamini udau kwa maana ya utatu. Tunayo Serikali kama *coordinator* lakini tunao wafanyakazi na tunao waajiri. Tunachofanya katika mahusiano yao, tunahakikisha kwamba sheria zinawalinda wafanyakazi na waajiri. Pale ambapo wanakosana, kuna vyombo ambavyo vimewekwa kisheria kimojawapo ni *CMA*, tuna Ofisi zetu za Kazi, tunao *OSHA* ambao wanaangalia maeneo ya kazi na kuhakikisha kwamba vifaa wanavyotumia katika kazi yao vinaendana na taratibu zilizowekwa lakini mahali ambapo inashindikana, nimesema katika hotuba yangu hatua stahiki zinachukuliwa ikiwemo kuwapeleka Mahakamani, wanalipa faini na wengine wanapewa *compliance order*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kujua kati ya nchi ambazo zinaheshimiana na kuwa na mahusiano mazuri na wafanyakazi ni katika mikutano ya ILO. Mheshimiwa Sugu alihudhuria moja ya mikutano hii, Tanzania haijawahi kukemewa kwa unyanyasaji wa wafanyakazi na ndiyo maana hata Ofisi ya Kanda ya Mashariki na Rwanda ya ILO imejengwa Dar es Salaama. Ukiangalia katika kitabu changu kwa nyuma utaona *Director General* alipoteuliwa kwa mara ya kwanza nchi ya kwanza aliyoitembelea Afrika ni Tanzania. Kwa hiyo, hii yote inaonyesha kwamba tuna mahusiano mazuri sana kati ya wafanyakazi na tunapokwenda kwenye vikao vyetu tunaenda kama Tanzania, wafanyakazi, Shirikisho la Waajiri na Serikali tunaenda na Tamko la Serikali. Nchi ambazo zina mahusiano yasiyokuwa mazuri kati ya Serikali na waajiri, Serikali na wafanyakazi kila mtu anakwenda na hotuba yake lakini siyo Tanzania. Kwa hiyo, niseme mahusiano yetu ni mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi wasiwasi wangu mkubwa ni wenzetu upande wa pili kwa sababu wanapenda sana kuchochea mahusiano haya yasiwe mazuri, wanapenda sana kuongeza chumvi ili mahusiano haya yasiwe mazuri na nina mifano wa mgomo wa madereva. Huu mgomo wa madereva nina taarifa rasmi kuna Wabunge wawili wa upande huu wamejaribu sana kuchochea mgomo huu uendelee na nilitaka kuwanasa nirekodi yale mazungumzo bahati yao machale yaliwacheza.

Kwa hiyo, mimi naomba na nina uhakika na mkiendelea kusema nitawataja, nina uhakika kwamba mnapenda migogoro iendelee kwa sababu mnafikiri ndiyo itawapa *political mileage which is not true*. Mtanzania yeyote ungependa kuwe na amani, ungependa kuwe na utulivu, ungependa kuwe na upendo, ushirikiano kati ya wafanyakazi na Serikali au Vyama vya Siasa, mbona sisi tunapenda huo umoja tukiwa na mikutano yetu tunawaalika lakini nyie hamtualiki sijui kwa nini, hampendi tushirikiane. Ukiangalia sasa hivi hotuba zote ni kampeni tu. Mimi naomba TAKUKURU waanze kuchukua hatua *this is campaigning* na muda wa *campaign* bado. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tangu mwaka 1992 wakati upinzani umeingia Tanzania mngeweza kuzungumza haya mnayozungumza sasa hivi mngefanya nini, siyo mwaka huu wa mwisho mnaanza kusema UKAWA ikishika nchi itafanya hivi, hakuna Mtanzania mjinga anaweza kuamini vitu hivi kwa sababu hamna hata *statistics* humu kwenye kitabu chenu za kuonyesha mtakachofanya. Ndiyo maana Mheshimiwa Turkey juzi alisema hamu huondosha fahamu, mna hamu ya kutawala ndiyo maana hata fahamu inaondoka kwa sababu mnashindwa kuandika vitu ambavyo ni *relevant*.
(Hapa baadhi ya Wabunge wa Upinzani walikuwa wakiongea bila kipaza sauti)

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mmemaliza niendelee?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naongelea hilo la ajira lakini pia mahusiano kati ya Serikali na wafanyakazi.

Mheshimiwa Cecilia nimesahau hili lakini umesema, niliwahi kusema kwamba Serikali haiwezi kuajiri vijana wetu wote na wewe leo umesema kwamba, niliposema kwamba vijana wanapomaliza vyo vikiu au wanapomaliza elimu wasifikirie tu kuajiriwa Serikalini na makampuni, wafikirie tu kujijiri, *this is a trend*.

Sasa hivi tunazungumzia *unemployment rate* ya Tanzania imeshuka imekuwa n 10.3 na wala siyo 11.7 na najua itaendelea kushuka chini ya uongozi wa Chama cha Mapinduzi lakini pamoja na hilo huwezi kuajiri vijana wote wanaomaliza vyo vya elimu ya juu na hii ni *fact* mnayoifahamu. Hii ni *fact* inayofahamika hakuna nchi ambayo 100%, hata Amerika yenye uchumi mzuri ina *unemployment rate* ambayo labda haijafika kwenye makumi lakini hawawezi kuajiri 100% na ndiyo maana inashuka kwa sababu tunajaribu kutoa fursa nzuri kwa wawekezaji ambapo kwa kweli sekta binafsi ndiyo inatusaidia kuajiri zaidi. Kwa sababu kuajiri kila anayemaliza chuo kikuu na sasa hivi wanamaliza zaidi laki mbili *it is not an easy thing* na hata kama ungechukua nchi ukiwa juu ya anga huwezi kufanya kitu kama hicho.

Kwa hiyo, msiwapumbaze Watanzania, muwaambie ukweli, ukasema nifute kauli yangu, mimi naomba wewe ndiyo ufute kwa sababu umesema watoto wa vigogo peke yao ndiyo wenye haki ya kupata ajira Serikalini na watoto wa kimasikini hawana ndiyo wajijiri, siyo kweli! Ungeweza kunihakikisha ningesema kweli lakini kwa kuwa huna uhakika naomba ufute huo usemi wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NSSF*, naposema kwamba Ndugu zetu hawa sasa wanaona moto wa kuotea mbali wanaanza kutapatapa, hivi ni nani anaweza kubeza kazi zinazofanywa na *NSSF*? Ni nani kati ya wapinzani anaweza kubeza ujenzi wa jengo hili la Bunge, Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*), Chuo Kikuu cha Mandela, nyumba za jeshi, nyumba za polisi, daraja la Kigamboni, naomba mtembee pia, ujenzi wa nyumba zaidi ya 7400 kule *Dege Eco-Village*, ujenzi wa nyumba za bei nafuu Kinyerezi, Mtoni Kijichi, ujenzi ambao unatarajiwa wa ofisi za Wabunge Majimboni na ujenzi wa hospitali ya kisasa ameitaja Mheshimiwa Vullu ya Apolo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna Waheshimiwa Wabunge wakio Apolo hebu *imagine* kama ile *service*, wale Madaktari sasa wanakuwa Dar es Salaam halafu unaibeza *NSSF*? Sasa wanataka kuwekeza kwenye *megawatt* 1000 za umeme Mkuranga na ujenzi wa barabara ya kwenda haraka ya Chalinze - Dar es Salaam. Mimi nafikiri ni kwa sababu mnaona hivi vitu vyote sasa vinawaondolea sababau ya kusema CCM haijafanya kitu. Naomba msemi hilo kwamba sababu kubwa ndiyo hiyo lakini kwa mtu anayeona na

mambo mengine mengi yanayofanywa siyo na NSSF peke yake kwa sababu baadhi ya hii miradi wameshirikiana na Mifuko mingine ya Hifadhi ya Jamii na bado mnaibezwa. Mmeshambiwa hapa mara nyingi na wengi mpo kwenye Kamati yetu mnasikia kwamba uwekezaji wa Mifuko hii unaendana na miongozo ya BOT kama hamuiamini BOT msem lakini pia na Mdhibiti na Mdamini ambaye ni SSRA. Mimi nafikiri mna sababu nyingine na nafikiri mmeshachelewa kwa sababu mambo yaliyofanyika katika nchi hii siyo kupitia tu Mifuko lakini na juhudi zingine za Chama cha Mapinduzi na Serikali yake, kwa kweli *you are late*, sasa mtafute wimbo mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wastaafu wetu kwa kweli hasa NSSF wamekuwa wakiboreshewa maslahi yao na wanafanyiwa kitu kinaitwa *indexation*, kila baada ya tathmini ya Mfuko kufanyika wanaongezewa mafao. Kwa mfano, mwaka 2010 NSSF iliongeza 52% na ndiyo maana inatoa mafao bora sasa nikisema kuliko Mifuko mingine, katika jangwa la Sahara *its true* kuwa NSSF inatoa mafao bora. Siyo kweli kuwa Watendaji wa NSSF wamekuwa wakipokea rushwa au kutoa tenda za ujenzi kwa makampuni yao binafsi. Anayesema kitu kama hiki kwa nini asituletee taarifa, ni kwa nini asubiri siku hii ndiyo aje azungumze kama siyo kuchonganisha Serikali, wananchi na kazi nzuri inayofanywa na Mifuko hii ikiwemo NSSF.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba tenda za ujenzi hutangazwa kwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi na washindi wa tenda hii ni wale ambao wamezingatia vigezo vyote. Kama kuna shirika ambalo wanazitumia vizuri *financial regulations* ni Shirika la NSSF na mashirika yote, kwa sababu yanakaguliwa na yanaonekana hayana matatizo, hayajawahi kupata hati chafu. Sasa *from no where* unaanza kusema Mkurugenzi Mkuu hatimize vigezo, nafikiri jamani kwa kweli tuwe tumwogope Mungu tusiwe tunasema vitu ambavyo havipo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya utafiti yanaonyesha, maana kulikuwa na utafiti unaonyesha kwamba NSSF ndiyo Taasisi ambayo haina rushwa. Sasa unaposema leo ina rushwa ni kwa sababu mnajua mna kinga humu ndani ya Bunge *otherwise* hii ilikuwa ina *call for* kuwachukulia hatua. Nafikiri kuhusiana na suala la NSSF limeeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Nyambari Nyangwine ameuliza NSSF imefikia wapi katika utekelezaji wa mradi wa kujenga *Tarime Commercial Complex* ambapo ndiyo eneo lipo na mchoro inasemekana upo tayari. Mheshimiwa Nyambari utekelezaji wa mradi wa *Tarime Commercial Complex* upo katika hatua ya uteuzi wa *consultant*, michoro inategemewa kukamilika mwezi Septemba 2015 na utekelezaji wa mradi utanza kabla ya mwezi Desemba. Mimi nina-*declare interest* kwamba mradi huu ukijengwa kwa kweli utakuwa umetusadia hasa wafanyabiashara wa Tarime watapata mahali

pa kupanga biashara zao, ofisi na pia *NSSF* wenyewe watapata ofisi palepale maana ofisi waliyomo sasa hivi haina hadhi ya shirika letu. Kwa hiyo, nawashauri *NSSF* kwa kweli wajenge haraka ofisi hii pale Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Gaudence Kayombo anasema pongezi kwa Dkt. Dau, ahsante sana Mheshimiwa Gaudence. Vilevile anashukuru kwa *NSSF* kutoa mikopo ya *two billion shillings* kwa *AMCOS* za Mbinga kwa ajili ya kununua kahawa. Anaomba maombi ya *AMCOS* nyingine kumi yamaliziwe. Jibu ni kwamba pongezi zinapokelewa na mimi nimezipokea na juhudi zinafanyika ili maombi ya *AMCOS* nyingine kumi yakamilike na mikopo itoke. Pia *NSSF* inatoa pongezi kwa *AMCOS* nne za Mbinga kulipa mikopo yao ya shilingi bilioni mbili kabla ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Christowaja anatoa pongezi wa *NSSF*, afadhali Mheshimiwa Christowaja umetupongeza, tunakushukuru sana na pongezi hizo zimepokelewa. Hawa ni kati ya watu wachache ambao wanajua faida ya *NSSF* na unakaribishwa kuhakikisha kuwa *SACCOS* yako kama unayo Mheshimiwa Christowaja inapata mikopo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sheria ya kutumia 50% ya akiba ya wanachama kama dhamana itaanza kufanya kazi? Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta za Hifadhi za Jamii (*SSRA*) pamoja na mambo mengine imeingia mkataba na Shirika la Kazi Duniani ili kuandaa miongozo ya utekelezaji kipengele cha dhamana ya mikopo ya nyumba. Mwalimu nategemea uwe mfano mzuri sana unapokaa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mbunge wa Viti Maalum ametoa pongezi kwa *NSSF*, nashukuru sana Mheshimiwa Madabida na jibu ni kwamba pongezi zimepokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani kuhakikisha barabara unganishi la kutoka mwisho wa mradi wa *NSSF* wa daraja la Kigamboni inajengwa bila hivyo daraja halitakuwa na faida inayotarajiwa. Maana yake ni kwamba pale ambapo daraja linapoishia barabara inayokwenda kule mbele haina hadhi. Jibu ni kwamba tayari Serikali na *NSSF* zimekubaliana kujenga kilomita mbili kuunganisha mradi wa daraja na barabara ya Kibada kwa utaratibu wa ubia kati ya Serikali na *NSSF*. Mchakato wa kuwateua washauri na wakandarasi waliopo kumaliza barabara hiyo umeshaanza. Ujenzi wa barabara hiyo utakamilika mwezi Oktoba mwaka huu wakati ambapo na daraja lile litakamilika. Kwa kuwa limeanza chini ya utawala wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete wa Awamu ya Nne, kati ya mambo mazuri yaliyofanyika na hayo pia mnashindwa kupongeza, nawashangaa sana, lakini mwezi Oktoba Mheshimiwa Rais atazindua wanasema *soft opening* ya lile daraja na kuacha waendeleo kulimazia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira na vibali vya ajira, maswali yameulizwa na Waheshimiwa Wabunge wengi wakiwemo Mheshimiwa Agness Hokororo, Mheshimiwa Cecilia Paresso. Suala la ukuzaji ajira linahusika na wadau wote, hili nimeshaeleza. Pia suala la ajira ya vijana nimeshazungumzia lakini sasa hivi vibali hivi vya kudhibiti ajira za wageni tunasubiri tukamilishe kanuni kusudi sasa tuanze kufanya kazi kwa kutumia mamlaka moja tu ambayo itakuwa inatoa vibali hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwashukuru wote na kama sikukujibu tutawajibu baadaye kwa kutumia bango kitita kwa sababu mambo ni yaleyale, lakini naendelea kuwaomba wenzetu hawa kwamba kwa kweli waanze sasa kuzungumza vitu ambavyo ni vya kweli. Kwa sababu Watanzania siyo kwamba ni watu ambao hawana akili, wanaelewa, hawa wanapiga porojo, hawa wanazungumza na hawa wanatoa takwimu, hawa hawana takwimu. Ni vizuri muanze kuonyesha kwamba mnaweza kuichukua nchi sio kwa porojo, kwa kudanganya, kwa kuingilia migogoro ya wafanyakazi, kuhamasisha migogoro ya madereva na ingekuwa mgogoro ule wa madereva au mgomo usingekuwepo hata hotuba nyingine zisingeandikwa maana zilikuwa zimejaa tu migogoro ya madereva. Najua wengi wenu ni wasomi mnaweza mkatumia taalamu yenu mkaandika vitu *very constructive* na mkasaidia Serikali kusonga mbele kwa sababu hii ni Serikali yetu wote na ndiyo hiyo kwa kweli inawaneemesha na Watanzania wanawategemea kwa jinsi mlivyoelimishwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache sitaki kupigiwa kengele lakini naendelea kuwaomba kwakweli muwe na uvumilivu wenzenu wanapoongea. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nami naipongeza *NSSF* kwa kazi nzuri, wamejenga nyumba lringa mpaka tunapanga. Mimi na Mheshimiwa Msigwa ni wapangaji *NSSF*. Sasa hivi ametoka lakini alikuwa mpangaji kwenye nyumba za *NSSF*. Kwa hiyo, *NSSF* mimi naipongeza kwa kazi nzuri. (Makofi)

Katibu.

KAMATI YA MATUMIZI

KITABU CHA PILI

MATUMIZI YA KAWAIDA

FUNGU 15 -WIZARA YA KAZI NA AJIRA

Kif. 1001 - Administration and HR Mgt.....Sh.4,097,054,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Najielekeza pale kwenye *item 221400, Hospitality Supplies and Services*. Nina hoja moja tu hapa na ningeomba Serikali itupe maelezo ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tumeona kumekuwa na *trend* baadhi ya Wizara na tuli-*appreciate* hapa majuzi, Wizara ya Katiba na Sheria walau walipunguza hizi pesa za vitafunwa. Hapa tunakuja kuona kwamba hizi pesa za vitafunwa, pesa za matumizi ya kawaida zimeongezeka kutoka shilingi 163.752 za mwaka jana, mwaka juzi ilikuwa ni shilingi milioni ishirini. Hili jambo mwaka jana pia kuna Wabunge walihoji mahali hapa. Mwaka huu tena inatoka shilingi milioni 163 inakuja shilingi milioni 219, pesa za utafunaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri ajaribu kuwa mzalendo kwa nchi yake na kwa watu wengine, ni sababu gani ambazo zimeifanya Wizara iongeze pesa za kutafunwa wakati huo tunalia kama Taifa hatuna fedha za kuzi-*commit* kwenye miradi ya maendeleo. Ni kwa nini msipunguze hizi pesa kama ambavyo tumeona Wizara ya Katiba na Sheria wamefanya na tukawa-*appreciate* mahali hapa. Ninyi kuna kitu gani hapa? Tunaomba ufafanuzi na kauli ya Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, ufafanuzi, kwenye Tume ya Usuluhishi.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tujue kwamba bajeti ya Serikali imeongezeka, kwa hiyo si ajabu vifungu vya fedha kuongezeka. Kubwa zaidi niseme tu kwamba hii Tume sasa imekuwa na shughuli nyingi, itakuwa na bodi mpya, ilikuwa haina bodi. Kwa hiyo, kutakuwa na mambo mengi ambapo imeonekana kwamba inafaa hizo fedha ziongezeke kutoka hiyo shilingi 163 mpaka shilingi 269. Kwa hiyo, nadhani ni suala la kawaida tu la ongezeko la shughuli za Tume.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

FUNGU 65 - WIZARA YA KAZI NA AJIRA

Kif. 1001 - Administration and HR Mgt.....Sh.3,616,846,074/=

MWENYEKITI: Majina yalishaletwa hapa, kwa hiyo, kila mtu akae nitamuita. Mheshimiwa Jafo!

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Suala langu ni katika utaratibu wa kustaafu, sasa hivi umri wa kustaafu ni miaka 55 ule wa hiari na miaka 60 wa lazima. Tunajua kwamba mtoto anaanza na umri wa miaka saba mpaka darasa la saba anakuwa na miaka kumi na nne, atasoma miaka minne, halafu miaka miwili, *then* ataenda chuo kikuu ambapo kozi ndefu zaidi *maximum* miaka mitano ambayo itamfikisha umri wa miaka 25. Jumlisha miaka mitatu kwa ajili ya kutafuta ajira ambayo unaipata ataipata akiwa na umri wa miaka 28. Huyo mtu hata akifanya kazi kwa miaka kumi na mitano unaona bado hajafika katika ule umri wa kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni nini? Sasa hivi mwajiri mkubwa sana ni *private sector* ambayo inaonekana mtu akiingia kule ni mtu ambaye anaaminika na anaweza kufanya kazi za kutosha. Bahati mbaya sana katika sekta zingine binafsi watu wakienda kufanya kazi huko, baada ya muda wanakuwa wamechoka kutokana na mazingira ya kazi, kwa hiyo, ina maana wengine inabidi wache au wakome kufanya kazi kabla ya ule muda wa miaka 55 au 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya msingi ni kwamba, je, Waziri na Ofisi yake wana mkakati gani wa kurekebisha umri wa kustaafu hasa tukizingatia *life expectancy* ya Mtanzania sasa hivi. Katika *private sector* au kwa vyovyote Serikali itakavyoona inafaa umri wa kustaafu uwe miaka 50 kwa hiari au miaka 55 kwa lazima ili mradi kuwa-*accommodate* watu wengine ambao wanafanya kazi katika *private sector* ambao katika hali moja au nyingine, ndani ya miaka hiyo atakuwa ameweza kutimiza ule utaratibu wa michango 180 kwa mujibu wa sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, swala la kustaafu ni la kisera. Hoja yake yeye anasema miaka ipunguzwe lakini ipo hoja wengine wanasema iongezwe kwa sababu *life expectancy* imeongezeka. Sasa hivi kuna maombi mahsusi kwa Maprofesa waongezewe muda wa kustaafu.

Kwa hiyo, anaposema kushuka basi vijana wastaafu watakuwa wengi sana nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nadhani ni hoja yake Mheshimiwa lakini vilevile ukija kwenye taratibu zetu, sera zote za kustaafu, za pensheni tumeshafikiria na imepigwa hesabu kwamba watu watastaafu wakiwa na umri wa miaka 55 na 60. Ukianza kurudisha ghafla utaleta matatizo makubwa sana kwenye mipangilio ya fedha na kutoa pensheni kwa mfano.

Kwa hiyo, mimi nadhani hiyo kama ni hoja ambayo ni nzito labda tu iletwe kwa utaratibu wake ili lijadiliwe kwa upana zaidi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafo.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sina nia ya kutoa shilingi isipokuwa ni kwa ajili ya kuishauri Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafo, unatoa shilingi au unaendelea tu?

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana! Sina nia ya kutoa shilingi isipokuwa naishauri Serikali.

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukipita kwa wadau mbalimbali katika sekta binafsi, ambapo sekta nyingine zinachosha sana mfano wale wanaofanya kazi katika mashamba ya maua, madini na sekta zingine mbalimbali katika *private sector*. Japokuwa kuna Maprofesa katika sekta zingine wanapata unafuu lakini kuna sekta zingine zina changamoto zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali ikiwezekana ifanye *research* ya kutosha kuwashirikisha wafanyakazi wa kada mbalimbali. Kwa sababu kuna wengine wana hicho kilio kwamba kama ikiwezekana mje katika mpango mkakati mpana wa kiseru, tuangalie ni jinsi gani tutafanya, lengo kubwa ni kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo ushauri wangu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ritta Kabati!

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba kupata ufafanuzi kuhusu ule mkataba wa Kimataifa wa ILO Na. 139, kuhusu wafanyakazi wa majumbani maana wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha hoja yake alisema kwamba anadhani ungeweza kuja

kwenye Bunge lijalo. Inaonyesha bado alikuwa hajaji-*commit*, alikuwa anadhani, hana uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *commitment* ya Serikali kuhusiana na jambo hili ili angalau tuweze kuweka kwenye *record* ili wale watakaorudi au mimi mwenyewe nitarudi kwenye Bunge lijalo kwamba *commitment* ilikuwepo toka kwenye Bunge hili. Kwa sababu kwa kweli Tanzania ilikuwa nchi zile za mwanzo mwanzo kabisa kwenye kusaini huu mkataba na karibu miaka minne sasa toka umesainiwa ule mkataba wa kimataifa na wanajua kwamba hii ajira watu wanateseka sana, wamekuwa wakipata mateso makubwa sana wafanyakazi wa majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *commitment* ya Serikali. Sitatoa shilingi kama nilivyosema lakini *atleast* nipate *commitment* ya Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *commitment* ipo na isingekuwepo tusingekuwa tunaendelea na mjadala sasa hivi wa wadau mbalimbali kwenye suala hili. Kama unavyojua mikataba hii tunakuwa tumeisaini lakini inatakiwa sasa iridhiwe na Bunge lakini kabla ya kuridhia wadau mbalimbali lazima waangalie mle ndani kwa sababu zinakuwa ni *general* lakini unaangalia kwa mazingira ya Tanzania, vipengele gani havijakaa vizuri Kitanzania kulingana na *culture* na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, hili linaendelea na halitakwamisha, tutafika mahali tutakubaliana na kama nilivyosema bila shaka kwenye Bunge lijalo inaweza ikawa tumekamilisha mjadala hiyo na wadau mbalimbali na mkataba huo utaletwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa. Kwa hiyo, *commitment* ipo.

MWENYEKITI: Ahsante. Ni moja moja tu kwa sababu hukudhamiria kutoa shilingi. Mheshimiwa Cecilia Paresso.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabla sijatoa hoja yangu niseme maneno yafuatayo:-

Kwa kweli nimemshangaa sana mama yangu Kabaka wakati anajibu hapa, ni mama kwangu mimi. Nilifikiri angejibu hoja zilizomo humu. Tumeongelea masuala mengi kuhusu Wakala Binafsi wa Ajira, masuala ya ukosefu wa ajira nchini, mishahara isiyo na staha kwa wafanyakazi, madeni ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, masuala ya OSHA, masuala ya PAYEE kwa wafanyakazi, halafu anadiriki kusema hii ni *sweeping statement*? Naamini Watanzania ambao wameisikiliza na ambao watakuwa na hotuba hizi, watakuwa wanajua yapi katika haya niliyoyasema na yapi ambayo ameyasema Mheshimiwa Waziri ni *sweeping statements*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukiwa ndani ya Bunge kama Kambi ya Upinzani Bungeni tumeshauri miaka yote masuala mengi sana. Hata siku moja hawajawahi kuchukua ushauri wetu na kuufanyia kazi lakini leo wanadiriki kusema efi hatushauri, ni hotuba ya manung'uniko, hotuba ya malalamiko wananchi wataamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu na nitatoa shilingi, katika ukurasa wa 41, tumesema Kambi Rasmi ya Upinzani siyo kama inapinga uwekezaji unaofanywa na NSSF, haipingi uwekezaji unaofanywa na NSSF, baadhi ya Wabunge wamepotosha, Mheshimiwa Waziri naye amesema kwamba tunapinga, hatupingi. Ila tunasema uwekezaji huo unaofanywa na NSSF, je, unazingatia miradi hiyo italeta faida ya uwekezaji huo? Ndiyo hoja yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, NSSF miradi waliyoifanya na kuwekeza tunaitambua na tumeonyesha kwenye hotuba yetu. Tunachosema wanafuata utaratibu na huo uwekezaji una faida? Tukatoa mfano, NSSF wamejenga jengo Kigoma wametumia gharama ya shilingi bilioni saba, mpaka leo jengo hilo halijapata mwekezaji, miaka miwili sasa. Zile fedha za NSSF siyo za mtu yeyote ni za wafanyakazi wanaokatwa kama akiba yao. Hizi fedha zisipotumika na kufanya marejesho maana yake ni fedha za wafanyakazi zinatumika isivyo. Ndiyo hoja yangu, tunaomba majibu na tusipopata majibu natoa shilingi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kuendelea kubishana na Mheshimiwa Cecilia, inawezekana kweli mengine hatukuyajibu na muda anavyoona ulikuwa ni mdogo, ningekuwa na saa nzima ningeweza kujibu yote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la uwekezaji ambao unafanywa na NSSF kama unazingatia faida, nasema faida ipo! Sikulijibu lakini jibu ninalo, faida au *returns on investment* ni moja ya vigezo vinavyozingatiwa katika kufanya uwekezaji na uwekezaji unaofanywa na NSSF unazingatia vigezo hivyo. Kwa kuthibitisha hilo, Benki Kuu na SSRA wameweka kigezo kwa *ROI (Return On Investment)* cha *one percent*, sawa, katika uwekezaji wote unaofanywa na Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii ikiwemo cha NSSF.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nimueleze katika kipindi chote tokea kigezo hiki kimewekwa faida iliyopatikana kutoka uwekezaji wa NSSF imepita kiwango hicho kilichowekwa. Mfano mwaka 2013/2014 badala ya *one percent* ambayo ndiyo kigezo cha mwisho, NSSF ilipata 2.1 percent. Mwaka 2012/2013, NSSF ilipata 3.0, kwa hiyo faida ipo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Paresso.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi hoja yangu ilikuwa ni kuhusu jengo la Kigoma ambalo limejengwa kwa thamani...

MWENYEKITI: Mheshimiwa, hiyo hoja ya Kigoma ni hoja nyingine, ulidhamiria kutoa shilingi, ndiyo ilikuwa hoja, kwa hiyo naomba uendelee. Naomba useme jibu alilokupa, umelikubali au unaendelea na kutoa shilingi?

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi, sijaridhika na majibu kwa sababu hoja yetu ya msingi ilikuwa ni uwekezaji na uwekezaji upo mwingi mno, ameeleza hapo kiasi.

Hata hivyo, hoja yangu ya mwanzo ambayo nilieleza, pamoja na uwekezaji wa miradi mingi nikatoa *specific* ya Kigoma, nikasema mradi wa Kigoma umewekezwa kwa gharama ya shilingi bilioni saba lakini mpaka leo ni miaka miwili hajapatikana hata mpangaji, maana yake hata faida ya uwekezaji haijaanza kurejeshwa. Hoja yangu ni kwa nini wanawekeza kwenye vitu kama hivi ukiwemo mfano huu wa Kigoma kwenye miradi ambayo haileti faida kwa haraka, maana yake uwekezaji ni wa bure hauleti faida ya haraka, ndiyo hoja hoja yangu, kwa hiyo, natoa shilingi.

MWENYEKITI: Hoja yako haijaungwa mkono, imeungwa mkono na mtu mmoja tu, ni lazima iungwe mkono na zaidi ya mtu mmoja.

MHE. ALLY K. MOHAMMED: Kaa chini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali endelea kuchangia, hiyo hoja haikuungwa mkono, ni mtu mmoja tu, haya tuendelee Mheshimiwa Machali.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelea na hoja hii au nyingine?

MBUNGE FULANI: Hiyo hiyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali endelea na hoja yako.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Madam, ni hiyohiyo!

MWENYEKITI: Hapana! Siyo hiyohiyo, hata kuunga mkono kwenyewe walikuwa wamekaa tu, tuendelee Mheshimiwa Machali na hoja yako.

MHE. MOSES J. MACHALI: Amekataa basi acheni fujo! Tulia basi, amekataa.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Siyo, hata Kanuni haziruhusu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Paresso haikuungwa mkono walikuwa wamekaa tu, tuendelee na hoja nyingine.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kidogo tu niseme kwamba suala la kuunga mkono hoja hizi siyo watu kumi tunapokuwa kipindi cha Bunge kukaa kama Kamati.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali ulikuwa umekaa tu mpaka tulipoanza kukumbusha, endelea na hoja yako.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ngoja niendelee na hoja yangu.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Achana nao.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa nikiwa nina jambo moja ambalo nimekuwa nalia nalo mara kwa mara kuhusiana na *issue* ya fao la kujitoa. Nimefanya *study* kutoka kwenye maeneo tofauti, fao la kujitoa lipo kwenye maeneo tofauti, tofauti na ambavyo imepata kuelezwa hapa kwamba wamefanya *study* duniani mpaka Kamati ya Maendeleo ya Jamii iliwahi kutoa taarifa ya uwongo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri amekuwa ni mtetezi wa kuwaminywa wafanyakazi wanaofanya kazi za mikataba, mathalani labda mtu ana mkataba wa kufanya kazi miaka miwili, anachangia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, anafanya kazi miaka mitatu anachangia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, wakati sheria ya mafao inatuambia kwamba ili mtu aweze kuwa *pensionable* ni sharti afanye kazi kwa miaka 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikiuliza hapa na leo nauliza tena na kama sikupata majibu ya kutosha nakusudia kutoa shilingi.

Mheshimiwa Waziri naomba atuambie anapata kigugumizi gani kupitia Wizara yake ambayo ndiyo inasimamia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kukubali hilo fao kwa watu ambao pengine wanafanya kazi kwa muda mfupi halafu wanataka kuchukua fedha zao hata kama ni sehemu siyo lazima iwe yote. Kwa sababu kama mtu pengine amefanya kazi miaka mitatu amemaliza halafu hana mpango wa kuchangia, hizo pesa zao mnasema kwamba ni kwa ajili ya pensheni baadaye uzeeni atakuwaje *pensionable* wakati hakuchangia miaka 15 mbona mnaji-*contradict* ni kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kama mara ya nne nauliza swali hili, napata mashaka inawezekana baadhi ya Mawaziri mnaweza kuwa mmewekwa mfukoni. Naomba mnijibu mtu amefanya kazi miaka mitatu, sheria inasema kwamba atakuwa *pensionable* kwa kuchangia miaka 15, mtamlipa pensheni kutoka kwenye pesa gani wakati hajakidhi kigezo cha kisheria cha miaka 15? Pesa zake mnapeleka wapi kama siyo wizi? Naomba kauli ya Serikali kwa sababu hatujui kwamba hizo pesa zinapelekwa wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba leo ajibu atuambie, watu walifanya kazi kwenye migodi na mashirika mengine kwa mfano kule kwetu watu wanafanya kazi na mashirika ya wakimbizi, mnawasaidiaje wananchi wa namna hii na wengine walio kwenye makampuni, mikataba ni miaka miwili wakati pensheni ni miaka 15. Naomba kauli ya Serikali na maelezo ya kina leo hii kuhusiana na suala hili, kama sikuridhika nitatoa shilingi. Nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakubali, kwanza nijibu lile la Mheshimiwa Cecilia la Kigoma, kwa kweli nyumba ya Kigoma imepangwa na *ICAP* - mita za mraba 221 na *THPS* - mita za mraba 70. Wapangaji wafuatao mikataba yao inasainiwa wiki hii, *World Line Foundation* - mita za mraba 70, *High Court* - mita za mraba 442, Kampuni ya Sigara - mita za mraba 221. Kati ya mita za mraba 1,325, upangaji ni mita za mraba 954 ambayo ni asilimia 70 ya eneo, hilo nimemaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye swali la Mheshimiwa Machali. Mheshimiwa Machali mimi nashangaa kwa kweli wewe ni mbishi sana.

MBUNGE FULANI: Ndiyo profession yake.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Ni mbishi halafu umesema tumewekwa kwenye mfuko, halafu ni wezi, mimi naomba kwanza afute hizo kauli kwa sababu siwezi kuendelea kumjibu mtu ambaye ananifikiria ni mwizi.

MHE. MOSES J. MACHALI: *(Aliongea bila ya kipaza sauti)*

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema ni mbishi kwa sababu nimeshawahi kueleza hapa mara nyingi Mheshimiwa Machali, mbona wenzako wameelewa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali, subiri upewe majibu, Mheshimiwa Waziri naomba utoe majibu.

MHE. ALLY K. MOHAMMED: Ampe vidonge vyake huyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri usijibishane huko, ongea na Kiti hapa.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la fao la kujitoa *actually* linafanyiwa kazi na Serikali kwa maana kwamba SSRA na Wizara yangu tunataka kufanya kitu ambacho hata mtu kama anajittoa, kile kipindi ambacho bado anatafuta ajira aweze kuhimili maisha kwa maana ya kupata pato ambalo linastahili. Hili fao la kujitoa sasa hivi linatolewa na Mifuko mingi, wanachama wa mifuko hii wanajittoa na karibu mifuko yote tumeruhusu wanajittoa, migodini wanajittoa. Tunachotaka kufanya ni kwamba anapojittoa kwa mfano anajittoa kwa sababu hana ajira, tuendeleo kum-*contain* kwa sababu tunajua huyu lazima tu atahitaji mafao mengine ya ile mifuko. Kwa mfano, matibabu akijittoa maana yake anajittoa katika mafao mengine yoyote yale ambayo mifuko ile inatoa, yeye asiseme tu ni ile kuchukua zile hela lakini tumewaruhusu wanajittoa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwalimu Machali.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo hapa, bahati mbaya wanafunzi wangu wengine hawapo, nashukuru. Mimi ni Mwalimu wa Walimu pia nina-*declare interest*. (Kicheko)

MWENYEKITI: Tuendeleo.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba wanaruhusiwa kujittoa, sina tatizo na hilo ndilo nililokuwa nataka kulisikia kwa sababu nimefanya *study* Kenya wanaruhusu jambo hili kupitia Mifuko yao ya Hifadhi za Jamii. Nilikuwa nakuwa *worried* kuona *always* Waziri amekuwa *rigid*. Sasa leo kwa *statement* hiyo, sioni sababu ya kuendelea. Nimeridhika na majibu ya Serikali mathalani amewaruhusu watu.

MWENYEKITI: Nilijua Walimu mtaelewana tu. Sasa namuita Mheshimiwa Masoud, huyo ni Mwalimu wangu.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi napenda kupata maelezo kwa Mheshimiwa Waziri juu ya sera ya kuwalinda walemavu kupatiwa ajira ama walemavu wa ngozi (albino), walemavu wa masikio, walemavu wa viungo kwani watu hawa kwa maumbile waliyojaliwa na Mwenyezi Mungu, mara nyingi huwa hawapati elimu inayostahili. Serikali inapotoa matangazo ya ajira haizingatii watu hawa ambao wamekosa elimu ama kutokana na afya zao au kutokana na kutopata fedha. Sera ni ipi kwa nchi yetu ya Tanzania juu ya kupatiwa ajira hawa wenzetu wenye walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilifikiria kwamba, pale Serikali inapotoa matangazo yake, wakasema ajira fulani inahitajika lakini awe mtu ambaye ana digrii moja isipokuwa walemavu wa aina fulani, kwa sababu haya ni majaliwa ya Mwenyezi Mungu, sera ni ipi? Kama sikupata majibu yanayostahili juu ya kupata ajira kwa kundi hili ambalo nimelitaja basi natoa shilingi. Nashukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Ajira ya Watu Wenye Ulemavu ipo na sera hiyo inasema kwamba angalau asilimia tatu ya wafanyakazi wawe ni walemavu lakini nikiri tu kwamba hiyo asilimia haijafikiwa...

MWENYEKITI: Wawe ni watu wenye ulemavu.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wawe ni watu wenye ulemavu lakini hatujafikia na tupo kwenye asilimia moja. Siyo kwa sababu wanazuiwa kuajiriwa inatokea hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kupunguza sifa nadhani itakuwa ngumu kwa sababu sera hiyo haisemi kwamba wapate ajira kwa kupunguza sifa za ajira. Kwa sababu kama kazi fulani inahitaji elimu fulani ukaweka mtu tu ambaye ana elimu ya chini ya hapo, kazi ile inaweza isitekelezwe labda kwa sababu tu ni mtu mwenye ulemavu ukamweka pale lakini hana sifa unaweza ukaharibu kazi. Kwa ujumla hiyo sera ipo kwa maana tu waweze kuajiriwa. Tungependa kusikia pale ambapo kwa kweli hawa watu wenye ulemavu wana sifa na hawakuajiriwa Serikali inaweza ikachukua hatua.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Naibu Waziri, rafiki yangu muafaka na naona hajaweka muafaka unaostahili. Amesema imefikiwa asilimia mia moja tu, lengo ni asilimia tatu. Pamoja na maelezo yake aliyosema kwamba hawezi kupunguza kiwango cha elimu kwa watu hawa lakini bado mimi naomba nisisitize, hamjafikia asilimia tatu mpo asilimia moja, mnasema hamuwezi mkapunguza kiwango kile cha elimu kwa sababu ya walemavu, kila binadamu ni mlemavu mtarajiwa.

Mimi nilisema tu kwamba hata kama mnataka watu wa digrii moja lakini mkisema kwamba mtu mlemavu aliye na *Advanced Diploma* basi hilo ni suala la kufikiwa, lakini ukiniambia huwezi ukafanya hivyo mimi sikuelewi kwa sababu kila mtu ni mlemavu mtarajiwa. Ulivyokuwa mwaka 2005 wewe jiangalie na leo tunakokwenda.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naendelea kusema kwamba kama sikupata jibu la ziada naondoa shilingi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, rafiki yangu muafaka, labda nisisitize tu kwamba kwanza hiyo aliyosema *Advanced Diploma ni equivalent to degree*, kwa hiyo hapo wala sidhani kama kunaweza kuwepo na tatizo lolote. Kwa hiyo, mimi nadhani hii sera tukubali, tutoe tu wito kwa waajiri waizingatie kwamba ikiwezekana asilimia tatu wawe ni watu wenye ulemavu. Pale wanaposhindwa kuwapata hao watu utawalazimishaje kwamba sasa waende kuwatafuta wapi na mtu hajajitokeza? Sera hiyo kwa kweli ndivyo ilivyo na hatuwezi kufanya jambo lolote zaidi ya kumdhirisha Mheshimiwa Masoud hapa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa manufaa ya Watanzania, nafikiri somo limeeleweka, nafikiri niliache Serikali ilitafakari ione ni nini cha kufanya zaidi. Sitaki kuendelea kubishana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Masoud.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - Finance and Accounts.....Sh.502,187,966/=
Kif. 1003 - Policy and Planning.....Sh.538,848,941/=
Kif. 1004 - Internal Audit Unit.....Sh.187,336,802/=
Kif. 1005 - Procurement Management Unit...Sh.203,344,647/=
Kif. 1006 - Government Comm. Unit.....Sh.194,136,963/=
Kif. 1007 - Information&Comm. Tech Unit.....Sh.84,422,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1008 - Legal Service Unit.....Sh.31,470,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali, Mwalimu alifikiri yupo darasani. (Kicheko)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 - Labour.....Sh.8,540,530,832/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Msibeze taaluma ya ualimu, ualimu ni taaluma na niko fresh.

MWENYEKITI: Mimi mwenyewe ni mwalimu.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, wala sijifichi mimi ni Mwalimu wa Walimu. Najielekeza pale kwenye *item 221300, Educational Material, Supplies and Services*. Naona hakuna pesa yoyote ambayo imetengwa kwa ajili ya vitu hivi ambavyo vingeweza kutumika kuwaelimisha watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifanya utafiti utabaini kwamba yapo mambo mengi ambayo watu wengi pengine hawayaelewi kuhusiana na masuala haya ya wafanyakazi. Naomba kupata sababu ni kwa nini Wizara haijaona umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili kuwawezesha kukutana na wafanyakazi na kuwaelimisha juu ya masuala mbalimbali ambayo yanawahusu. Kuna sifuri ambayo imetengwa hapo, ni kwa sababu gani, naomba Serikali pengine iweze kufafanua juu ya suala hili, kwa nini ni zero?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu, lakini sijabeza taaluma ya ualimu ndiyo maana nilimtambua Mwalimu wangu kabla sijaanza.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho kimepewa bajeti ya Sh.800,000 katika Idara ya Utawala, kwa hiyo ikaonekana hakuna sababu ya kuweka kwenye kifungu hiki.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2002 - Employment Division.....Sh.3,371,623,808/=

Kif. 2003 - Registrar of Trade Union.....Sh.144,487,967/=

Kif. 2004 - Arusha Regional Labour Office.....Sh.61,587,000/=

Kif. 2005 - Dodoma Regional Labour Office.....Sh.36,952,000/=

Kif. 2006 - Geita Regional Labour Office.....Sh.18,902,000/=

Kif. 2007 - Iringa Regional Labour Office.....Sh.39,057,000/=

Kif. 2008 - Kagera Regional Labour Office.....Sh.38,842,000/=

Kif. 2009 - Kigoma Regional Labour Office.....Sh.39,203,000/=

Kif. 2010 - Kilimanjaro Regional Labour Office..Sh.45,846,000/=

Kif. 2011 - Lindi Regional Labour Office.....Sh.40,451,000/=

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kif. 2012 - Manyara Regional Labour Office....Sh.30,660,000/=

Kif. 2013 - Mara Regional Labour OfficeSh.39,139,000/=

Kif. 2014 - Mbeya Regional Labour Office.....Sh.48,726,000/=

Kif. 2015 - Morogoro Regional Labour Office...Sh.55,177,000/=

Kif. 2016 - Mtwara Regional Labour Office.....Sh.47,960,000/=

Kif. 2017 - Mwanza Regional Labour Office.....Sh.63,488,000/=

Kif. 2018 - Njombe Regional Labour Office.....Sh.42,346,000/=

Kif. 2019 - Pwani Regional Labour Office.....Sh.40,596,000/=

Kif. 2020 - Rukwa Regional Labour Office.....Sh.40,888,000/=

Kif. 2021 - Katavi Regional Labour Office.....Sh.40,750,000/=

Kif. 2022 - Ruvuma Regional Labour Office.....Sh.40,487,000/=

Kif. 2023 - Shinyanga Regional Labour Office...Sh.40,014,000/=

Kif. 2024 - Simiyu Regional Labour Office.....Sh.23,856,000/=

Kif. 2025 - Singida Regional Labour Office.....Sh.40,014,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2026 – Tabora Regional Labour OfficeShs.42,893,000/=

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mwaka jana nilipochangia kifungu hiki cha 2026 na nimepitia hapa vifungu vyote vidogo sioni *Oil and Lubricant!* Kwa maana nyingine naomba Waziri tu anipe majibu, je, ombi tulilomba kupatiwa gari Ofisi ya Mkoa, safari hii anakusudia kutupatia?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu, Mkoa wa Tabora waliomba gari mwaka jana hawalioni hapo, wanataka majibu.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nia iko palepale, pesa ikipatikana Tabora mtapata gari.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2027 – Tanga Regional Labour OfficeShs.55,696,000/=

Kif. 2028 – Temeke Regional Labour OfficeShs 33,242,000/=

Kif. 2029 – Kinondoni Regional Labour Office ..Sh.31,500,000/=

Kif. 2030 – Ilala Regional Labour OfficeShs.29,079,000/=

Kif. 2031 – Social Security DivisionShs.360,442,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

WABUNGE FULANI: Bado maendeleo.

MWENYEKITI: Katibu alishazoea haoni kama mna maendeleo. Kwa hiyo, tunaendelea Waheshimiwa na maendeleo.

KITABU CHA IV

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 65 - WIZARA YA KAZI NA AJIRA

Kif. 2002 – *Employment Division*.....Shs.20,000,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira.

TAARIFA

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kuwa Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Kazi na Ajira ya Mwaka 2015/2016, Kifungu kwa Kifungu na kuyapitisha bila Mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa na iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka 2015/2016 yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Watendaji wote wa Wizara hii pamoja na taasisi zake kwa kazi nzuri. Nina uhakika mwaka huu fedha zilizoombwa basi, zitatolewa ili kuweza kutekeleza majukumu ambayo yamepangwa. Ahsante sana. Katibu.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Matiko?

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba Mwongozo wako, wakati wa Kamati ya Matumizi Mheshimiwa Paresso aliazimia kushika shilingi kitu ambacho ulimruhusu; akaongea, Mheshimiwa Waziri akajibu, akaazimia kushika shilingi, akatoa maelezo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida huwa siyo lazima aungwe mkono na watu sijui kumi, anaweza akakosa mtu wa kumuunga mkono lakini bado Waziri anawajibika kumjibu. Akipata mtu mmoja, bado ilikuwa anatakiwa Waziri amjibu halafu yeye ahitimishe, kitu ambacho hakikwenda hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mwongozo wako isije ikajitokeza tena kwenye Wizara ambayo tunaenda, ilikuwa ni kupitiwa tu au imebadilika? Tunaomba utueleze ili tujue kabisa.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Esther. Alitoa hoja, mtu wa kumuunga mkono hakusimama mpaka baada ya muda. Ndiyo, hakusimama na wewe ulikuwa umekaanaye hapo, ulikuwa na haki ya kusimama! Kwa hiyo, hayo ndio majibu ya mwongozo wangu. *(Makofi)*

Kama ni jibu, baada ya hapo jibu alipewa na Waziri kama alivyokuwa ameomba. Kwa hiyo, wakati ule alitakiwa asimame, hakusimama mpaka mimi ndiyo nikawa namuona amekaa tu hapo. Kwa hiyo, macho ya Mwenyekiti, hayakumuona mtu aliyesimama. Hayo ndiyo majibu ya mwongozo wangu. Katibu. *(Makofi)*

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Naona Katibu ana haraka. Sasa hivi anayelitwa ni Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii ili ajibu hoja. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tulitakiwa tuhitimishe Wizara zote mbili, lakini kwa sababu maalum kwamba Waziri wa Kazi ana jukumu lingine, imebidi tufanye Wizara moja ndiyo maana unaona Makatibu wanapata tabu kidogo hapa. Kwa hiyo, tumemaliza Wizara moja, sasa tunaingia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Naomba nimuite Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, dakika 10, Mheshimiwa Dokta Pindi Chana.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nianze kwa kumshukuru Mungu.

MWENYEKITI: Dakika 15 halafu Mheshimiwa Waziri atakuwa na dakika 35.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nianze kwa kumshukuru Mungu kwa ulinzi na neema tela. Vilevile naomba kuishukuru sana familia yangu kwa kipindi cha miaka mitano imeweza kunivumilia kwa kazi nyingi. Nawashukuru sana watoto wangu, mume wangu na familia nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete. Naomba pia kumpongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dokta Mohamed Gharib Bilal, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda bila kumsahau Waziri wangu, Mama Sophia Simba, kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya kwa ajili ya Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Kambi ya Upinzani wamenukuu sana maneno ya Mwalimu, Baba wa Taifa na mimi kwa heshima kubwa naomba ninukuu maneno ya Mwalimu wakati anang'atuka alisema, *"Nchi yetu bila CCM itayumba."* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naomba kuishukuru Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Vilevile, naomba kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Njombe kwa kuniwezesha kuwa Mbunge na kuendelea kunishawishi na mimi naomba niwaambie nimeshawishika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa nichangie Hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto aliyowasilisha leo asubuhi hapa Bungeni kwa kujibu baadhi ya hoja za Wabunge kama ifuatavyo; kulikuwa na hoja nyingi na michango yote ni michango ambayo ina afya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja inayohusu migogoro ya ardhi katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Hoja hii ilitolewa na Wabunge mbalimbali. Kuhusu migogoro, Wizara imevianisha vyuo vyote vyenye migogoro ya ardhi na mwaka 2015/2016 imejipanga kupima na kuvipa hati vyuo 10 vya Ifakara, Ikwiriri, Misingi, Mwamva, Musoma, Anatougrou, Chilala, Kilwa Masoko, Chisalu na Kisarawe. Vyuo vitatu vya Maendeleo ya Jamii ambavyo ni Rungemba, Ruaha, Mbugai, vimeshapimwa vinasubiri kupatiwa hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hiyo, kulikuwa na hoja inayohusiana na suala zima la uchakavu wa majengo na miundombinu katika

Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Kwa kweli, Wizara imekuwa ikikarabati majengo na miundombinu ya vyuo kwa awamu kufuatana na upatikanaji wa fedha. Mwaka 2014/2015, vyuo saba vya Tarime, Mwananhala, Kilwa Masoko, Mputa, Msaginya, Nandembo na Mto wa Mbu vilikarabatiwa. Wizara imepanga kukarabati Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vinane kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja pia kuhusu ombi la fedha za kujenga jengo la mtaalam wa kujitolea kutoka Korea, wanaofanya kazi Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mbinga na kuanza kozi ya kuongeza thamani ya madini kwa kushirikiana na chuo na nchi ya Korea. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Gaudence Kayombo. Jibu lake ni kwamba, Wizara tuna mkakati wa ushirikiano na Korea kupitia KOIKA na vyuo vyetu. Chuo Cha Maendeleo ya Wananchi Mbinga kimeshaanza kozi ya kuchakata madini. Aidha, Wizara ipo tayari kuwezesha chuo ili kiweze kufanikisha lengo lake la kushirikiana na chuo hicho cha Korea Kusini na pia kuona uwezekano wa kujenga nyumba ambazo wageni wa chuo watatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna shukrani ambazo zimetolewa kwa kupewa gari la shule. Shukrani hizi zilitolewa na Injinia Ramo Makani na sisi tunasema tumezipokea shukrani hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja kwamba, uvamizi maeneo ya chuo na matumizi yasiyofuata utaratibu nayo ni changamoto. Tunasema kwamba, Wizara imeshaainisha vyuo vyote vyenye migogoro ya ardhi na imetenga fedha kwa ajili ya kupima na kuvipatia hati vyuo 10 kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi mabaya ya ardhi, tunashukuru kwa taarifa, tutafuatilia na kuchukua hatua stahiki pale tutakapogundua matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja kuhusiana na ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Sofi na ombi la kumaliza majengo na miundombinu iliyobaki baada ya ukarabati na kuwapatia gari kwa ajili ya chuo. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Dokta Haji Mponda. Tunaendelea kusema kwamba, tunazipokea pongezi za Mheshimiwa Mbunge na tunamuahidi kuwa, lengo la Wizara kukarabati majengo na miundombinu ya vyuo liko palepale. Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Sofi, kitaendelea kukarabatiwa kwa jinsi fedha zitakavyopatikana. Sofi kama chuo kilichopo pembezoni tunakiangalia kwa umakini mkubwa na katika kukipatia chombo cha usafiri mara tu fedha au gari litakapopatikana chuo hiki kitapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine ambayo inasema Serikali ina utaratibu gani wa kuwakopesha vijana wanaomaliza darasa la saba na *form four* ili waweze kusoma katika vyuo vya VETA na Vyuo vya Maendeleo

ya Wananchi? Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Bukwimba na Mheshimiwa Mwaiposa. Serikali haina utaratibu wa mikopo kwa vijana wanaosoma VETA, ufundi, wanaomaliza darasa la saba na sekondari. Hata hivyo, tunapokea kama ushauri, tutaufanyia kazi lakini pia, ada za vyuo hivi kwa kweli ni ndogo ukilinganisha na vyuo vya binafsi. Kwa hiyo, lengo la Serikali la kuviboresha vyuo hivi liko palepale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni Sheria ya Ndoa. Polisi wachukue hatua za kisheria kwa wanaume wanaopiga wake zao, masuala ya ukatili, alitwambia Mheshimiwa Akunaay. Kwa kweli, kupiga ni kosa la jinai. Wizara imekuwa ikitoa elimu kwa jamii kuhusu kuheshimu haki za binadamu na kufuata sheria kwa kupitia vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana sasa masuala ya ukatili yote yanakuwa *reported* tofauti na zamani. Zamani masuala ya ukatili yakifanyika kwenye jamii, watu hata namna ya kuripoti walikuwa hawajui. Sasa hivi uelewa umeongezeka, watu wanafahamu, kwanza watajua hili jambo ni ukatili lakini pia wananchi wanaenda kuripoti haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja inahusu kusudio la Serikali kufuta NGOs. Hii iliulizwa na Mheshimiwa Christowaja Mtinda. Ufafanuzi ni kwamba, si kweli kwamba Serikali inakusudia kuyafutia usajili mashirika 1,000 kwa sababu ya kujikita mijini na kupokea fedha kutoka nje ya nchi. Hiyo, siyo sababu ya msingi kwamba ya NGOs kufitiwa usajili. Hata hivyo, ieleweke kwamba, kusudio la Serikali kuzifutia usajili NGOs hizo halina uhusiano na masuala ya kisiasa, bali linatokana na ukiukwaji wa Sheria ya NGOs kwa kutowasilisha taarifa zao kama zinavyotakiwa na sharia. Kila mwaka NGOs zinapaswa kuwasilisha taarifa kwa hiyo, zisipowasilisha maana yake hazijakidhi matakwa yale kwa hiyo, zinaweza zikafutiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwe macho na baadhi ya NGOs zisizo na dhamira njema ya ujenzi wa nchi kwa kufanya vitendo vya uchochezi vinavyosababisha uvunjifu wa amani. Hoja hiyo, ilitolewa na Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi.

Serikali imekuwa ikifuatilia utendaji wa NGOs na pale inapobainika zinaendeshwa kinyume cha sheria, ilkiwemo uvunjifu wa amani, hatua stahiki huchukuliwa kwa mujibu wa sheria, ikiwa ni pamoja na kufutiwa usajili na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria. Kuna sababu mbalimbali, maana kuna NGOs moja yenyewe ilikuwa inahubiri mambo ambayo ni kinyume na Katiba ya Jamhuri, kwa mfano, masuala haya ya ndoa za jinsia moja na kadhalika, kwa hiyo, unapokiuka sheria za nchi ndipo unapoweza kufutiwa usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii kufafanua baadhi ya maeneo na baadhi ya maeneo atafafanua Waziri wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nashukuru kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Asante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa naomba nimuite Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto!

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja niliyowasilisha leo tarehe 25/05/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kwa kuisimamia Wizara yangu kwa umakini mkubwa.

Naishukuru Kamati kwa jitihada zao za kuiwezesha Wizara kuongeza bajeti ya Serikali, ingawa bado kuna ufinyu wa bajeti ikilinganishwa na majukumu ya Wizara.

Pia tumeipokea Hotuba ya Kambi ya Upinzani na naahidi Wizara yangu itajibu hoja zote na kuufanyia kazi ushauri mzuri waliotupa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa upande wake, inachua hatua mbalimbali za kupambana na ufinyu wa bajeti. Moja ya hatua hizo ni kuandika maandiko ya miradi na kuwasilisha Serikalini na kwa wabia wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii sasa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia hoja yangu niliyowasilisha leo hii, kwa michango mizuri, yenye kutia moyo na yenye kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 25 walichangia hoja yangu, kati yao 14 wamechangia kwa kuongea na 11 wamechangia kwa maandishi. Katika michango iliyotolewa, iko inayotoa ushauri na mingine ni maswali ambayo nitajitahidi kwa uwezo wangu kuweza kujibu na kwa muda kama utaniruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inaithamini sana michango yote iliyotolewa na ninalithibitishia Bunge lako tukufu kuwa tutaifanyia kazi. Kutokana na ufinyu wa muda sitoweza kujibu maswali au hoja zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, lakini naahidi kwamba Wizara yangu itajibu hoja zote na kuziwasilisha Ofisi ya Bunge.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inalaani vitendo vyote vya ukatili kwa wanawake, watoto, wanaume na mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi (albino) vinavyoendelea katika sehemu mbalimbali nchini hususani Kanda ya Ziwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu hoja naomba kufanya marekebisho kidogo katika hotuba yangu, kulikuwa na makosa ya kimaandishi tu. Ukurasa wa 39 wa hotuba yangu *para* 60, Maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani huadhimishwa kila mwaka tarehe 15 Mei na siyo tarehe 16 Juni.

Pili, ukurasa 39 huo huo *para* ya mwisho, mpaka ukurasa wa 40, Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika kila mwaka Huadhimishwa tarehe 16 Juni na siyo tarehe 15 Mei. Nawashukuru sana kwa uvumilivu wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa nijibu baadhi ya hoja zilizotolewa kama ifuatavyo:- Lakini kabla sijaanza kujibu hoja kama zilivyoletwa, naomba nianze kwa kusema machache hapa kwamba Mheshimiwa Mbilinyi (Sugu), alisimama hapa na kusema kwamba tumechoka. Sisi hatujachoka, Serikali yetu haijachoka na Chama chetu hakijachoka, tuko imara, hajachoka mtu hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu amesema tuna mahusiano mazuri na ACT. Sisi hatuna shida ya kuunganishwa na mtu mwingine yeyote. Wao ndiyo waliopata tabu wakaungana ili wapate nguvu, lakini sisi hatuna shida hiyo, kwa hiyo, asitutilie maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameitaja kama vile UKAWA tunawafuata fuata! Hivi UKAWA ni nini, ni kitu ambacho hata hakijakuwa *registered!* Sisi hatu-*deal* na kitu ambacho hata hatukifahamu kimaandishi, mmeji-*register* wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa "Sugu", ameendelea kuzungumzia uandikishwaji. Amenipa nafasi nzuri ya kusemea uandikishwaji kwa sababu kuna fujo zinafanyika huko za uandikishwaji, kuwatishia wazee wasitoke kwenda kujiandikisha. Na mimi nawambia nikiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, jamii ijitokeze iende ikajiandikishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hapa Bai kuna chama fulani kilienda kikaanza kuwasimamisha wananchi na kuwaambia hapana, leo wanachama wa CCM hawaandikishwi kaeni. Hizo hila hizo haziwafikishi mahali popote. Kwa hiyo, hawaandikishi chama wanaandikisha wananchi, nendeni mkajiandikishe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, wengi wameonyesha *concern* au kusikitishwa na ufinyu wa bajeti ya Wizara

yetu. Mimi nawashukuru sana, lakini Serikali imesikia na itaangalia katika vipaumbele vyake kuhakikisha kwamba Wizara yetu, Wizara ambayo ni mtambuka inapata bajeti, inaongezewa bajeti. Aidha, tunawashukuru kwa kutupongeza kwa kazi nzuri tunayoifanya pamoja na ufinyu wa bajeti lakini tumekuwa tukifanya kazi kwa hali hiyo hiyo ambayo tupo nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie kidogo hoja za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii. Nawashukuru sana kwa jinsi wanavyoendelea kutushauri. Imezungumzia kwamba tutafute vyanzo vingine vya mapato; kama nilivyosema katika hotuba yetu tumeandika aandiko la awamu ya pili ya programu ya vyuo vya maendeleo ya wananchi, programu za kuwawezesha wanawake na wasichana na programu ya maelezi, makuzi ya maendeleo ya awali ya mtoto kwa ajili ya kutafuta fedha za utekelezaji kutoka vyanzo mbalimbali vikiwemo vyanzo vya wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wamezungumzia hatimiliki katika vyuo vyetu; hili linaendelea kufanywa, Wizara tayari imeishaainisha na kuvitambua vyuo vyote vyenye migogoro ya ardhi na imepanga kupima na kuvipatia hati vyuo kumi vya Ifakara, Ikwiriri, Msingi, Mwava, Musoma, Chilala, Kilwa Masoko, Arnaoutonglou na vinginevyo ambavyo nimevitaja katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumzia pia kuhusu ajira kwa wahitimu ya vyuo vya maendeleo ya jamii; Wizara inaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kibali kitolewe kwa mamlaka husika kuwezesha wataalam wa maendeleo ya jamii waweze kuajiriwa moja kwa moja kutoka vyuoni. *(Makofi)*

Aidha, wamezungumzia pia kwamba Serikali itoe fedha zote zilizoombwa mwaka 2015/2016 za Benki ya Wanawake Tanzania ili kutimiza ahadi ya Rais. Katika mwaka wa Fedha 2015/2016 Serikali imeishatenga jumla ya shilingi bilioni tatu ili kukamilisha ahadi yake ya kutoa shilingi bilioni 10. Katika bilioni 10 alizoahidi Rais alipoingia madarakani, ameishatoa kiasi kikubwa, bado bilioni tatu ambazo ameahidi kuzitoa kabla ya kuachia kijiti na kumwachia mwenzie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani nayo pia imezungumzia suala la kuajiri wataalam wa maendeleo ya jamii ambapo jibu lake ni sawa na huko kwamba mazungumzo yanaendelea kuomba kwamba waajiriwe moja kwa moja.

Kambi ya Upinzani pia imezungumzia uwezekano wa kukarabati miundombinu ya majengo ya vyuo vya wananchi na vya maendeleo ya jamii ili kurudisha majengo haya katika hadhi yake na kutoa elimu inayostahili. Wizara imekuwa ikikarabati majengo na miundombinu ya vyuo kwa awamu kufuatana na upatikanaji wa bajeti. Vyuo saba vilikarabatiwa katika mwaka 2015/2016 na

hivyo vinane vinatarajiwa kukarabatiwa. Naomba mkumbuke vyuo vingi hivi siyo kama vya enzi za Mwalimu, vyuo vingi hivi toka enzi za ukoloni, kwa hiyo ukaratabati wake una kazi kubwa sana; hizi nyingine ndiyo zile zilikuwa *middle schools* ambazo wengine hamziji. Kwa hiyo, ni majengo makuukuu sana, hata hivyo tunajitahidi kuweka mazingira yawe mazuri na vijana wetu bado wanafaidika kwa kutumia majengo hayo kwa kupata ujuzi wa stadi mbalimbali za maisha.

Wamezungumzia pia Serikali itoe elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike ili kuweza kutoa fursa kwa wanawake kupata nafasi za juu za maamuzi. Serikali kwa kushirikishikana na wadau mbalimbali imeendelea kufanya kazi hiyo na mnaona matokeo yake wengi mko humu, wengi watoto wa kike sasa hivi na wa kiume wote wako shuleni sawa kwa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwepo kwa ongezeko la viongozi wanawake katika ngazi za juu, anasema mchango gani katika kuwakomboa wanawake wanaofanyiwa vitendo vya ukatili. Viongozi wanawake wamekuwa mstari wa mbele katika kupiga vita ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa kuhamasisha jamii na kuhakikisha kuwa kunawepo na mipango madhubuti ya kupinga ukatili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani imezungumzia tena kuhusu Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 na Sheria ya Mirathi ya mwaka 1865. Serikali inayo nia ya kurekebisha Sheria ya Ndoa na Sheria ya Mirathi kwa kuwa zimepitwa na wakati; zimo kwenye *process* ya kufanya hivyo. Tulitegemea sana Katiba ingepita hii ingekuwa rahisi zaidi kwa sababu Sheria ya Ndoa ina kipengele kimoja kigumu ambacho kwa sababu Katiba tuliishazungumza kwenye Katiba umri wa mtoto ni miaka 18, kile kipengele kingetoka kule na hilo ndilo tatizo kubwa la Sheria ya Ndoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani pia inasema Benki ya Wanawake ina mikakati gani kuwafikia wanawake na wanaume wengi zaidi. Kwa kutambua changamoto ya kuwafikia Watanzania wengi, Benki ya Wanawake imedhamiria kutoa mfumo wa uwakala wa benki (*agency banking*) utakaowezesha benki kufikia mikoa yote. Kama nilivyosema, kujenga au kuweka *branch* ya benki inahitaji pesa nyingi kwa hiyo tunafanya *agency banking* kwa vituo mbalimbali. Wanawake pia wataendelea kupatiwa mikopo kupitia vyanzo mbalimbali ikiwepo mifuko ya *Self*, *VICOBA*, *SACCOS* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasema kwamba Serikali imeshindwa kufuatilia utendaji wa mashirika yasiyo ya kiserikali kama yanavyotakiwa kisheria. Hapana, sio kweli kwamba Serikali imeshindwa

kufuatilia utendaji wa NGOs, bali imekuwa ikifuatilia utendaji wa mashirika hayo na matokeo ya ufuatiliaji huo yanadhibitika kwa kuimarika kwa michango ya NGOs na hatua zinachukuliwa kwa yale yanayoenda kinyume na sheria na ndiyo maana kuna manung'uniko mengi. Hatuwezi kuvumilia kuona NGOs zinafanya shughuli ambazo hazikuwa-registered kufanya. Kwa hiyo, mimi nadhani ni wakati umefika kuipongeza Serikali kwa sera yake ya NGOs. (Makofi)

Serikali kuyafutia mashirika yasiyo ya kiserikali kwa mashinikizo ya CCM! Mmh! Hizi ni ndoto sio kweli kwamba Serikali imekuwa ikiyafutia usajili mashirika yasiyo ya kiserikali kwa shinikizo la CCM. Wanafuatiwa NGOs kutokana na kukiuka Sheria ya NGOs, Sheria ya Na. 24 ya Mwaka 2002 kama ilivyorekebisha mwaka 2005 na Bunge hili Tukufu; tumetunga wenyewe sheria. Aidha, Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa NGOs kufichua maovu, kuongeza uwazi na uwajibikaji, lazima wafanye kazi kwa uwazi na wawajibike.

Kambi ya Upinzani inasema Serikali ina mkakati gani wa kulinda watoto wenye ulemavu ikiwemo ulemavu wa ngozi! Serikali inaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo zikiwemo Halmashauri, Asasi za Kiraia na wengine wote. Lakini pia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeendelea kuhamasisha uanzishwaji wa timu za ulinzi wa mtoto katika wilaya ili kuzuia ukatili dhidi ya watoto, mpaka sasa timu hizo zipo katika wilaya 31 hapa nchini. Wizara kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi imehamasisha uanzishwaji wa madawati ya jinsia na watoto katika vituo 417 vya polisi ili kushughulikia vitendo vya ukatili dhidi ya watoto wasichana na vishawishi vinavyosababisha mimba katika umri mdogo. Aidha, wadau wa maendeleo wamekuwa wanaunga mkono Serikali katika ujenzi wa mabweni maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niwajibu Waheshimiwa Wabunge mmoja mmoja na wale ambao wameleta michango yao kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mendrad Kigola, hoja yake Wizara isimamie haki za wanawake katika kupata maji na matibabu kirahisi. Wizara imekuwa ikielimisha na kuhamasisha wadau mbalimbali kuzingatia masuala ya jinsia katika sera. Mkumbuke sera zote zinazoandaliwa zinaweka suala la jinsia ndani yake na mikakati ya maji, afya, *environment* na mengine yote yanaweka masuala ya jinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya ukatili yamezungumzwa sana, yamezungumzwa na Waheshimiwa wengi akiwemo Mheshimiwa Madabida, Mheshimiwa Riziki, Mheshimiwa Agness Mkanga, Mheshimiwa Agness Hokororo, Mheshimiwa Subira, karibu kinamama wote wameonyeshwa kuchukizwa na ukatili. Waheshimiwa Wabunge Wanawake na Waheshimiwa Wabunge Wanaume wamechukizwa sana. Ningependa kusema najisikia vizuri sana ninapoona wananchi nao sasa wanachukizwa na vitendo vya ukatili. Serikali

imefanya kazi kubwa kuhamasisha wananchi, wanapoona ukatili unafanywa wanaenda wenyewe polisi kuripoti na ndiyo maana ripoti zimekuwa nyingi kuliko huko.

Mheshimiwa Zarina Madabida alitaka kujua kwa nini ukatili wa jinsia bado unaendelea pamoja na juhudi kubwa za kuzuia. Jibu letu ni kwamba bado kuna baadhi ya mila na desturi zipo zinawakandamiza wanawake, umaskini miongoni mwa jamii na pia kutokuwepo uelewa wa kutosha wa haki na sheria miongoni mwa jamii.

Mheshimiwa Riziki alitaka kujua ukataji wa viungo vya binadamu, Serikali ichukue hatua za haraka kukomesha ukatili huu. Pamoja na juhudi za kuhamasisha na kuelimisha jamii, Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani kuhakikisha kuwa vitendo vya ukatili vinatokomezwa ikiwa ni pamoja na kuchukuliwa hatua kali wale ambao wamefanya maovu hayo.

Aidha, Mheshimiwa Angness Margreth Mkanga, alitoa hoja kwamba ukatili wa jinsia kwa watoto umekithiri hasa kwa wenye ulemavu wa ngozi (albino); je, ni udhaifu wa ulemavu wao ndiyo unaopelekea ukatili ufanyike? Akaomba ufanyike utafiti ili kuona nini cha kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukatili wa jinsia kwa watoto, hasa kwa watu wenye ulemavu kwa sehemu kubwa unatokana kwa fikra potovu za kupata utajiri wa haraka. Serikali inaendelea kutoa elimu pamoja na kuhamasisha jamii juu ya athari za kuwepo kwa ukatili huo. Aidha, itaendelea kufanya utafiti juu ya ukatili wa kijinsia na watoto kwa lengo la kuchukua hatua stahiki. Tunaendelea, tumeishafanya utafiti wa kwanza, mambo yakizidi tutafanya tafiti nyingine na nyingine, sisi hatuchoki na zile tafiti tunapeleka kwa maafisa maendeleo ya jamii ambao wako karibu na jamii na maafisa ustawi wa jamii ambao wanafuatilia mambo haya katika halmashauri zenu huko mnakotoka. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, mkiwa kama Madiwani tunaomba hizi tafiti mzijue matokeo yake ni nini ili nanyi msaidie kuelimisha jamii kuhusu madhara ya ukatili.

Mheshimiwa Agness Hokororo wa Mtwara, anasema vitendo vingi vya ukatili wa kijinsia, jamii ishiriki kutokomeza vitendo vya ukatili. Ni kweli, jamii inaposhiriki masuala ya ukatili yatakuwa historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mdogo wangu Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na Mheshimiwa Zarina Madabida wanazungumzia ongezeko la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani. Jibu ni kweli, taarifa za ongezeko la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani ni changamoto kubwa nchini kwetu. Wizara yangu imeweka mikakati ifuatayo:-

Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeanda mpango kazi, *in fact* inatekeleza mpango kazi wa kudhibiti tatizo la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani. Mpango huo ni wa kutoka 2014 mpaka 2019. Mpango kazi huo unatekelezwa na Wizara, Halmashauri na Asasi za Kiraia zinazoshughulikia masuala ya watoto. Mpango kazi huu unawezeshwa kutolewa kwa elimu kwa jamii, huduma mbalimbali kama vile za lishe, malezi, afya pamoja na kuwatenganisha watoto na familia zao. Mpango kazi huu pia unatoa fursa kwa wazazi na walezi kujifunza na kuendesha miradi ya ujasiriamali ambayo itasaidia kukuza kipato cha familia. Na hapa TASAF inafanya kazi kubwa sana kuhakikisha familia hizi zinakuwa na uwezo na hivyo kuweza kulea watoto wao. Naishukuru sana TASAF kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa watoto walio nje ya shule watapata elimu ya ufundi stadi ambayo itawezesha kujijiri wao wenyewe badala ya kwenda mitaani na kufanya kazi zisizokuwa na tija. Hapa kubwa ni kwamba watoto wale kukubali kuondoka mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Maulidah Komu, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Akunay, Mheshimiwa Sylvester Mabumba, nao walizungumzia pia kuhusu ukatili dhidi ya watoto nchini. Majibu ndiyo kama hayo mnayaona tunaendelea, kazi inaendelea, kila siku wanabuni mipango mingine na sisi tunaendelea kuwafuatilia, lakini mkumbuke jukumu la kwanza watoto hawa ni wazazi.

Mheshimiwa Riziki na Mheshimiwa Agnes Mkanga tena wamezungumzia ulemavu wa ngozi. Kama nilivyosema hapo mwanzo, kubwa ni kuwaelimisha familia za watoto wenye ulemavu wa ngozi, kuwapa mbinu za kuwalinda, kuimarisha mfumo wa ulinzi wa watoto katika ngazi ya jamii ikiwemo timu za ulinzi wa mtoto, dawati la jinsia, watoto katika vituo vya polisi. Waheshimiwa Wabunge ni vizuri kama tukielewa kama hivi vyombo viko huko vimeundwa vinafanya kazi kujenga uwezo wa kamati ya watoto walio katika mazingira hatarishi, wale watoto wajue kujihami, wanapoona mtu ambaye hawamfahamu wakimbie mara moja, hakuna rafiki kwa mtu ambaye mtoto hamfahamu.

Watoto wadogo kuchanganywa na wakubwa kwenye magereza, limeulizwa na Mheshimiwa Rita Kabati. Wizara yangu imeanza kutembelea magereza ya Kigamboni mkoani Pwani, Isanga mkoani Dodoma, na Mkuza mkoani Morogoro ili kuandaa orodha ya wanawake wenye watoto magerezani. Baada ya zoezi hili kukamilika taarifa hii itawasilishwa katika kikao cha Kamati ya Kushughulikia Masuala ya Ukatili Dhidi ya Watoto ambayo inahusisha wadau wote wanashughulikia masuala ya ulinzi wa mtoto ili kupata suluhisho la pamoja kuhusu hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watoto magerezani tumekuwa tukilizungumza siku zote na tunaendelea kulifuatilia na sehemu ambapo tunakuta watoto hawapati huduma sahihi tunaingilia kati na hatua stahiki zinachukuliwa na ndiyo maana tumeenda huko na tunajitahidi kurekebisha hali mbaya iliyokuwepo pale.

Mheshimiwa Amina Makilagi, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Subira Mgallu, wote wamezungumzia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Wizara imekuwa ikihimiza Wizara ya Fedha kuongeza fedha za Mfuko wa Halmashauri kuchangia asilimia tano ya mapato yake katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Halmashauri zinatambua vikundi, aidha Wizara ya Mambo ya Ndani inaviandikisha. Wizara inaendelea kuhimiza Wizara ya Fedha kutoa fedha kama zinavyotengwa. Aidha, tunawaomba Madiwani waendeleo kushughulikia suala hili kwa kuhimiza kurudisha mikopo kwa wale ambao wamepata bahati ya kupata mikopo hii ili zile fedha zizunguke wanawake wengi waweze kufaidika na mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Zaynabu Vullu, Mheshimiwa Mwaiposa, nao pia wanasema utaratibu wa kuunda vikundi na taratibu nyingine zinawakataza wanawake kupata mikopo ya Mfuko wa Wanawake. Wizara inahamasisha wanawake kuunda vikundi ili kupata mikopo kwa kuwa vikundi ndiyo dhamana ya mikopo, haiwezekani kuwapa mikopo halafu hatuji wanaenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *Tanzania Women Bank*, (Benki ya Wanawake Tanzania) limezungumzwa karibu na Wabunge wote wakiwemo Mheshimiwa Kayombo, yeye anaulizia ni lini atapa tawi kule Mbinga. Kutokana na ufinyu wa bajeti kwa sasa hatuna mpango huo, lakini tutahakikisha tunapeleka vituo vya kukopeshea. Mheshimiwa Diana Chilolo anazungumzia pia kuongeza matawi ya Benki hii, lakini hali ya kuongeza matawi ya Benki hii ni ngumu na tumeamua kuanzisha vituo vya *Tanzania Women Bank* ili kuweza kuwafikia wanawake wengi zaidi na kwa maeneo mengi tuliyoyafikia wanawake wameitikia vizuri sana.

Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Zaynabu Vullu, Mheshimiwa Faida Bakari, wote wanazungumzia suala la Benki. Lakini, nasema kwamba kwa sasa Benki ina mtaji wa shilingi 8,746,053,000/= na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo mmiliki mwenye hisa nyingi ikiwa na hisa 98. Hisa mbili tu ndiyo zinatoka kwa wananchi, lakini hivi karibuni tutaanza kuuza hisa nadhani hali hii itabadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wengine wamechangia kwa maandishi na wao pia wanazungumzia wangependa Benki hii kuwafikia. Hii hapa inazungumzia Singida, lakini Mheshimiwa Mabumba na Mheshimiwa Faida Bakari wao bado wana hamu sana kuona Benki hii inafika Zanzibar. Benki itakapopata mtaji wa kutosha itaanza mchakato wa kuanzisha matawi katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar. Tulianza, lakini kulikuwa na matatizo tukarudi nyuma, kwa hiyo ikabidi twende kwingine. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itajadiliana na Serikali ya Mapinduzi kuangalia ni namna gani Benki ya Wanawake itaweza kufanya kazi Zanzibar kwa sababu ya taratibu mbalimbali za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe Mheshimiwa Mng'ong'o uliuliza Benki ya Wanawake ilianzishwa ili iweze kumkomboa mwanamke, unashauri fedha zile fedha bilioni mbili za kila mwaka zitolewe ili mikopo iwafikie wanawake katika mikoa mbalimbali. Kama nilivyosema awali, kwa kipindi hiki cha 2015/2016 Serikali imetuahidi kwamba itatupatia shilingi bilioni tatu kabla ya mwisho wa mwaka huu. Wizara itaendelea kuhimiza wenzetu wa Wizara ya Fedha watoe pesa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maswali yaliyoletwa kuhusu masuala ya maendeleo ya jamii hasa maafisa maendeleo ya jamii kuajiriwa moja kwa moja. Kama nilivyojibu pale mwanzo, mazungumzo yanaendelea baina yetu na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kibali kitolewe waweze kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kulikuwa na swali la Chuo cha Rugemba ili kiwe Chuo Kikuu. Hili limeulizwa na Mheshimiwa Kigola, lakini pia Mheshimiwa Ritta ameulizia. Napenda kuwajibu kwamba, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba kitaanza kutoa mafunzo kwanza kwa kujiunga (*affiliate*) na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Wizara inaendelea kuboresha rasilimali watu na miondombinu ili kiweze kufikia vigezo vya kutoa shahada, baada ya hapo ndipo utaratibu wa kukipandisha hadhi utaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Riziki Omar Juma amezungumzia uchakavu wa nyumba za wafanyakazi wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Jibu ni kwamba, nyumba za wafanyakazi wa taasisi pamoja na miundombinu mingine kama kumbi za mihadhara mabweni na ofisi hazijafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu kutokana na ufinyu wa bajeti. Hata hivyo, juhudi zinafanywa kupitia vyanzo vingine vya fedha ili kuweza kufanya ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ritta Kabati, nimeishajibu swali lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (Makofi)

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Lakini Mheshimiwa Mwenyekiti wangu hujanijibu swali langu, nafikiri labda utanijibu wakati utakapokuwa unachangia vifungu. Nakupongeza sana. Hoja imeishatolewa na imeungwa mkono. Katibu!

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

FUNGU 53 – WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO

Kif. 1001 – Administration and HR
Management.....Tshs.1,622,466, 000/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa, majina ya Waheshimiwa wote ninayo, sasa tunaanza na Mheshimiwa Esther Matiko!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa nipate ufafanuzi wa kina maana kumekuwa na *statements* zinajichanganya; nisiporidhika nitatoa shilingi. Kuhusiana na suala zima la mashirika yasiyo ya kiserikali, kupitia Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Serikali alitoa orodha ya Mashirika zaidi ya 1000 ambayo yamefutiwa na hata Bodi iliyokaa Geita ilieleza hayo na hata wakati tumewasilisha bajeti ya uratibu na mahusiano tulieleza wakati Waziri anajibu alisema ni shirika moja tu la Sisi kwa Sisi. Lakini leo kwenye kitabu chao wamesema ni mashirika 24 na kati ya mashirika 24 hayo, mashirika 10 yaliomba yenyewe kujitoa kwa maana ni mashirika 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitaka kujua, huu mkanganyiko, Msajili anasema haya mashirika yamekosa sifa kwa sababu hayajawasilisha taarifa zao za mwaka, lakini hayo mashirika ni kati 2005 na 2007. Sasa yamesajiliwa 2005 - 2007 na kwa mujibu wa Sheria Namba 24 ya mwaka 2002 ambayo imefanyiwa marekebisho mwaka 2005. Walikuwa wanasubiri nini kama kweli ana makosa hayo, kuyafuta au kuyaondoa hayo mashirika kati ya 2007 mpaka leo tunazungumza ni 2015? Ni kwa nini tusiamini kwamba, yanafutwa kwa sababu

yanasema yale ambayo Serikali ya Chama Cha Mapinduzi hamtaki kuyasikia?
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi wakati Waziri anaongea hapa alisema changamoto mojawapo mashirika yanaomba hela kutoka nje, lakini kingine akasema mashirika yamejikita mjini zaidi na akasema ndiyo maana inapelekea kuwa sifa mojawapo ya kuondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nijue, na mnijibu kwanza mkanganyiko; ni kwa nini Msajili anasema mashirika takribani 1000 yanafutwa, siku ile Waziri alisema ni shirika moja la Sisi kwa Sisi linajishirikisha sijui na mashoga na nini huko. Leo kwenye kitabu chenu mnasema ni mashirika 24, 10 yamejiondoa yamebaki 14. Naomba kwanza mkanganyiko huo na mtueleze bayana ni sababu zipi ambazo zinapelekea hayo mashirika kufutwa. Kwa sababu kama ni kutopeleka taarifa za mwaka kati ya 2007 na 2014, na watendaji wawajibishwe na ninyi wenyewe muwajibike kwa sababu kwa nini hamkuweza kuyafuta haya mashirika kama yalienda kinyume na sheria tuliyotunga sisi wenyewe Bungeni. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufafanuzi!

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kwa nini analing'ang'ania suala hili la NGO! NGOs hizi zimefutwa kwa kukiuka kanuni na taratibu na Sheria Namba 24 ya NGO ya mwaka 2002. Kama NGO yoyote inaona kwamba imefutwa kinyume na utaratibu, haiwezi kuja ku-*appeal* humu Bungeni, kuna vyombo vyake vya kwenda kua-*appeal*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jibu langu nililompa hapa Bungeni bado linabaki vilevile. Kwanza, Sheria ya NGO kama hukutimiza yale masharti, unajifuta wewe mwenyewe. Ikumbukwe kwamba Sheria ya NGO imeanza baada ya Sera ya NGO ya 2001, halafu 2002 ikatungwa sheria. Huko nyuma kulikuwa hakuna Sheria ya NGO, kwa hiyo kwa vile kulikuwa hakuna Sheria ya NGO, NGOs zilikuwa zikisajiliwa BRELA, zikisajiliwa RITA, zikisajiliwa Home Affairs (Wizara ya Mambo ya Ndani). Kwa hiyo, sheria hii ilipokuja, wale wote ambao wamejisajili kule, sasa wanatakiwa wajisajili hapa. Lakini kwa bahati mbaya sheria zile tatu kule ambazo zilikuwa zina-*register* hizi NGOs hazijarekebishwa ili wasiwe wana-*register* NGOs.

Kwa hiyo, kwenye sheria tukaweka kipengele kinachosema wale wote waliokuwa *registered* kwenye hizo sheria waje kwenye Sheria ya NGO wapate *Certificate of Compliance* ya ukabilifu. Wengine wamefanya, wengine hawakufanya. Kwa hiyo, tukatangaza kwenye gazeti tukawapa muda wa mwaka mzima waje wapate *Certificate of Compliance* kama inavyotaka sheria

ili tutekeleze matakwa ya sheria. Sasa sijui unapingana na sheria au unataka vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hilo jambo la kwamba CCM, CCM, sisi wala hatuna shida na NGOs. Hapa nilichosema changamoto wanazozipata NGOs hizi ni changamoto kwamba wanategemea zaidi wafadhali, fedha za nje. Ni kitu kigumu, huwezi ukaanzisha NGO yako ya watoto yatima halafu utegemee upewe pesa kutoka nje, lazima utafute njia ya kutengeneza pesa uweze kulea hawa watoto, kutegemea fedha za wafadhili, siku moja itakubidi ufunge kile kituo chako, matokeo yake wale watoto watahangaika. Hicho ndiyo ninachosema. Sikutaja zile fedha zinazokuja pengine zinawafikia, aha aha, hizo wala sijazigusa, nilisema kwa ujumla changamoto ambazo NGOs zote wanapata. Kuna watu wanafungua NGO kwa kutegemea pengine kuna pesa kutoka nje, mimi huwa wanafika ofisi kwangu, Mheshimiwa tutafutie wafadhili kwa NGO yangu, hiyo hamna, hiyo ni changamoto. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (Makofi)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kiuhalisia Waziri hajajibu kabisa swali langu, kwa hiyo natoa shilingi na naomba kama kuna Wabunge wata-support hoja yangu watachangia baadae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeuliza mantinki nzima, Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali alisema yanafutwa mashirika zaidi ya 1000, na hayo mashirika asitupe story za 2001 sijui sera ikaja ikaenda ikarudi, yamesajiliwa kati ya 2005 na 2007 na sababu mliyotoa; hayajatoa taarifa ya mwaka. Nikataka nijue kitabu chenu kinasema ni mashirika 24, Msajili wa Mashirika anasema ni Mashirika 1000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, sababu ya kutokupeleka taarifa; siku ile Waziri wakati unajibu hapa ukasema ni shirika moja tu la Sisi kwa Sisi ambalo linajishirikisha na mashoga. Kwanza, nikawa najiuliza, siku ile nilikuwa nimechelewa kufika na kifungu changu kikapita; kama shirika linajishirikisha na mashoga, ni nani hapa aulizwe? Ni wale ambao wameruhusu lisajiliwe au ni wale...? Yaani ninyi wenyewe mnalisajili, maana lazima wanaleta katiba yao, mnaona wanataka wajishughulisha na nini, leo mnakuja mnafuta, mna- *justify* hapa, hiyo moja.

Pili, kwa kusema kwamba hajatimiza vigezo, kwamba yanaomba hela sijui kutoka nje, yanajikita mjini zaidi. Mimi nikawa najiuliza zaidi, mashirika mengi zaidi na mengine wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri ni *Board Member*, kwa WAMA, fedha nyingi za kuindesha inatoa nje, nyingi, asilimia zaidi ya 80 wanapata kutoka kwa wafadhili wa nje. Nataka nijue, unijibu swali langu la msingi, bado hujalijibu, usipige siasa nyingi mama yangu, nijibu swali la msingi, ni

mashirika 1000 au ni mashirika hayo 24 ambayo umeyataja leo kwenye hiki kitabu na ni sababu zipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshika shilingi, kwa hiyo, naomba na Wabunge wengine wachangie, mnipe majibu ya kina, aidha NGOs mnazosisajili mnasajili ili ziweze kuwasaidia Watanzania na zinatuelimisha sisi wote ikiwepo ninyi Serikali. Msije mkaleta enzi zile za Mkapa Haki Elimu imeongea, imeongea ikafungiwa, yaani mkiona zinawasema mnazipiga chini. Toa majibu ya msingi, ni NGOs hizo 1000 za Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Umma au ni NGOs hizo 24 ambazo umezitaja leo au ni ile NGO moja ya Sisi kwa Sisi! Maana unaji-*contradict* kati ya juzi, leo na jana. Nashukuru naomba mniunge mkono.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, siji-*contradict*, nalielewa hili somo vizuri sana. Sheria ya NGO ina kanuni zake, ukikiuka tu huo utaratibu, kwanza aidha umejifuta mwenyewe, unajifuta *automatically* hatukutambui. Kwa hiyo, hiyo mambo ya NGO zako 1000 ulizozikazania ulikozitoa na takwimu zako, nipe hiyo *source of information* yako! Mimi nafuata mambo yanayofanyika ofisini kwangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi NGOs zimesajiliwa kwenye taasisi nne tofauti, usiniambie niwajibie na Wizara ya Mambo ya Ndani. Mimi kwangu nimekuambia mashirika 24 ambayo 10 wenyewe wameamua...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ongea na mimi usizungumze...

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ili wenye NGOs wajue, kuna kanuni zake, ni lazima kila mwaka ulete taarifa ya kazi, kila mwaka ulete taarifa ya fedha ambazo zimekuwa *audited* na kampuni inayotambulika, umelipa ada. Sasa, wanapoleta zile taarifa ndiyo tunajua, wengine ni *briefcase* kabisa. Kwa hiyo, lingine alilozungumzia kwanza nakataa, namwambia hayo 1000 anayajua yeye, mimi yangu ninayojua ni haya kutoka Bodi ya NGO ambayo iko chini yangu. Hizo nyingine ambazo unazijua kama una *interest* nazo, zilete!

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo tumezungumza toka *last week*, leo ungekuja na hiyo *list* hapa halafu nikwambie, hii nime-*register* katika Sheria ya NGO au hii imekuwa *registered* wapi, au *BRELA*, ningekwambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine hili la mashoga, kwa nini tumewafutia, wamekuja wakionyesha madhumuni yao ni tofauti. Tulipokuja kugundua

kwamba wanafanya madhumuni mengine, ile Sisi kwa Sisi kumbe badaye ikawa masuala ya ushoga, jina ni jina, na wanakuandikia tutaelimisha jamii, tutafanya nini, ikabidi tulifunge. Sasa nini hii mambo ya mashoga unayozungumza saa zote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, au huyu Mheshimiwa ana tatizo, hili la mashoga linampa tabu vipi? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie hapa, halafu achukue hiyo shilingi yake, nimalizie kwa kusema hivi, hivi ni kitu gani, kila mkiongea lazima mtaje WAMA, *where is the problem?*

WABUNGE FULANI: NGO!

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO: NGO ndiyo! NGO ya WAMA...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ongea na mimi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, inatekeleza, ina kanuni zote, inaenda kwa mujibu wa sheria, WAMA ni *organization* kubwa, sasa inawawasha nini hii WAMA?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechoka kujibu masuala ya WAMA kila siku, mimi ni mkurugenzi katika WAMA na ninajitolea, sina *monetary benefit* pale, ndiyo maana siku-*declare interest*. Kwa hiyo, mkumbuke kwamba, wake wa Marais duniani kote wana *organization* yao. Ndiyo, na kila mke wa Rais anakuwa na NGO yake. Mama Bush ana NGO yake, mama Clinton ana NGO yake na mama Salma ana NGO... (Makofi/Vigelegele)

MWENYEKITI: Tusikilizane, tusikilizane! Mheshimiwa Waziri maliza! Waheshimiwa Wabunge, naomba make, wote mliosimama naomba make. Naomba wote mliosimama make! Mheshimiwa Gekul, naomba ukae, naomba wote mkae.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Kuwashwa ndiyo nini?

MWENYEKITI: Naomba make! Naomba wote make. Sasa, naomba niwaeleze hivi, kwanza hata mimi nashangaa, Waheshimiwa Wabunge! Ngoja, ngoja! Ninashangaa kama Waheshimiwa Wabunge hamjui kwamba NGO zinasajjiwa hata kwenye ngazi ya Wilaya! Ndiyo, nataka niwaambie.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kutumia kipaza sauti)

MWENYEKITI: Tusikilizane, sasa, naomba tusikilizane! Waheshimiwa tusikilizane! Kwanza, watu wanawasgangaa, mnapiga kelele!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Naomba, Waziri ameishamaliza, anayechangia achangie. Mheshimiwa!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Naomba Mheshimiwa Waziri amalize kuchangia, akimaliza ndipo anayetaka kuchangia hiyo hoja achangie.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, taarifa kidogo.

MWENYEKITI: Nasema hivi, atakayetaka taarifa ataitoa wakati anachangia.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Waheshimiwa naomba mkae.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, afute kauli yake!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul kaa!

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, anakuwaje Mwenyekiti wa Wanawake anaongea lugha chafu hivyo!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul, naomba ukae, wala sijakuruhusu kusema. Sijakuruhusu kusema, naomba mkae! Sikilizeni hoja zikitolewa, mna muda wa kuchangia mtachangia. Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, yale yale niliyosema. Sasa taarifa nilizozipata sasa hivi kutoka kwa wataalam wangu ni kwamba, NGOs 1000 ilikuwa ni tangazo la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, hilo unalolisema hilo, lakini sisi bado tuko pale pale kwenye 24. *(Makofi)*

Sasa, suala hili, kama unataka shilingi chukua, lakini...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, naomba uongee na mimi, ongea na Kiti, usiongee na... wewe ongea na Kiti.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Gekul! Kuwashwa, unawashwa kichwani, unawashwa wapi, kwani ni kitu gani, ni Kiswahili cha kawaida!

MWENYEKITI: Mheshimiwa, naomba umjibu Mheshimiwa Esther, usimjibu Mheshimiwa Gekul, mjibu Mheshimiwa Esther usiwajibu wale!

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kutumia kipaza sauti)

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichosema ni kwamba, masuala ya WAMA mbona yanawawashawasha? Inamuuma nini!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namalizia kwa kusema, mtoa hoja nimemjibu, zile NGOs zake 1000 anazosema ni za Mambo ya Ndani ya Nchi, NGOs 24 ni zetu!

MWENYEKITI: Sasa tuchangie, Mheshimiwa Mbarouk!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kidogo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Jafo! Jirani yangu nyumbani, hapa tuko Bungeni. *(Kicheko)*
Naomba nimuite Mheshimiwa Mbarouk.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru...

MWENYEKITI: Kabla sijakuita, naomba...

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, uliishaniita.

MWENYEKITI: Naomba kwanza nimpe nafasi Mheshimiwa AG! Atatoa mwishoni, haya Mheshimiwa endelea, atatoa mwishoni.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza nakushukuru. Lakini la pili, namuunga mkono Mheshimiwa Matiko kutokana na hoja yake kwamba, bado haikupata majibu, majibu ambayo alikuwa anayahitaji ni kuhusu ile namba ambayo wanapishana na Waziri, lakini vilevile kutokupelekwa kwa taarifa kamili zile za mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, Meshimiwa Waziri anasema kwamba CCM haina shida ya NGO na anasema kwamba hii WAMA inatuwashawasha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sheria za NGOs, ni NGO kutojihusisha na masuala ya kisiasa. Pale NGO itakapokuwa inajihusisha na masuala ya kisiasa, NGO inahitaji kufutwa! WAMA inajishughulisha kisiasa, Board Members wote wa WAMA ni maCCM! Mwenyekiti wa Bodi, Zakia Megji, Wajumbe mke wa Mheshimiwa Lowassa, mke wa Waziri... (Makofi)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Wewe kaa chini na wewe, kaa chini!

MBUNGE FULANI: Sikai!

MHE. ALLY K. MOHAMED: Kaa chini, weka sura wewe muha wewe! umechanganyikiwa nini wewe! Tutakufunga kamba humu Bungeni, watakufunga kamba wakupeleke uha!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, board members wote ni wana CCM watupu, wanaishikilia kwa ajili ya siasa, na hii WAMA hawawezi kuifuta, kwa sababu Waziri mwenyewe ambaye anasimamia hii sheria, yeye ni board member, atawezaje kuifuta WAMA? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa hayo mafupi tu mimi namuunga mkono Mheshimiwa na kusema kwamba sisi WAMA haituwashiwashi, ila tunasema kwamba WAMA iko zaidi ya kisiasa, na imekiuka hata hii sheria ambayo imeunda NGO.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Silinde!

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mwingine sisi kama Bunge tunatakiwa tuwe tunaangalia hoja kwamba, mantiki ya hoja ni nini. Ukimsikiliza Mheshimiwa Esther Matiko, alichokuwa anakihitaji hapa tangu awali, alikuwa anataka atueleze, kwa nini panakuwa na contradiction ndani ya Serikali moja kwamba, Wizara inasema kuna NGOs 24...

MBUNGE FULANI: Changia!

MHE. DAVID E. SILINDE: Ndiyo hoja ya kuchangia, sawa! Wizara inasema kuna NGOs 24, wakati ukija kwenye usajili ziko zaidi ya 1000.

Sasa Waziri anapokuja na majibu mawili yanayokuwa yana-contradict panakuwa na tatizo kubwa. Kwa hiyo, hapa tunachohitaji ufafanuzi, na katika hizo NGOs ambazo zimefutwa, tunataka sababu, usiwe unataja tu NGO moja

kwa nini imefutwa na NGOs zingine zimeshindwa kufutwa. Kwa hiyo, hicho ndicho tulichokuwa tunahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la WAMA limekuwa na malalamiko mengi siyo tu ndani ya Bunge peke yake, yaani hata Taifa zima wanajua nini kinachoendelea, na hii siyo kweli kwamba eti kila mke wa Rais ni lazima awe na NGO, huu utaratibu umekuja sasa hivi, Mama Maria Nyerere hakuwa na NGO katika hili Taifa. Wake wa Marais wa sasa wamekuwa wakitumia NGO kuiba, uwizi tu huu ndiyo umekuja ukifanyika kwenye hizi NGOs. Sasa hatuwezi kuendelea na huu utaratibu, eti ukishakuwa mke wa Rais...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Silinde, muda wako umekwisha. Naomba nimuite Mheshimiwa Jafo.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tukiwa kama viongozi, tunalingoza tafa letu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuatilia mijadala nadhani lilikuwa suala zima la *contradiction* ya *statement*, lakini bahati nzuri Mheshimiwa Waziri ameishatoa *clarification* kwamba zile NGOs 1000 ni katika Wizara ya Mambo ya Ndani na katika Wizara yake ni NGOs 24, kwa hiyo, hakuna tatizo hapo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilitaka niwasihi sana viongozi, vyombo vya habari siku tatu zilizopita, tulisikia nchi ya kule *Ireland*, wenzetu wamepitia sheria katika suala zima la ushoga. Kwa hiyo, katika hili kuna hatari sana kwa nchi zetu zinazoendelea. Kwa hiyo, hili linatupa angalizo katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwamba lazima wawe wakali. Lazima wasimamie NGOs ambazo zitavunja utaratibu kwa kuliangamiza Taifa letu, lazima zifutwe. Kwa hiyo, mjadala wa kwamba NGOs zingine zinafutwa inaonekana kwamba zinaenda kuiangamiza nchi yetu ni jambo la msingi ndugu Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nahisi, naomba nikusihi, Mheshimiwa Matiko, hoja yako ya msingi ndiyo maana nasema naunga mkono kwa sababu kulikuwa na *contradiction*, Waziri ameishatoa *clarification*. Lakini kama viongozi wa Taifa, lazima tujue kwa sababu kuna janga kubwa la hatari linaedelea, kuna mataifa ambayo yamepitisha sheria ambazo kwa utamaduni wa nchi zetu hizi hatuwezi kukubaliana nazo. Kwa hiyo, ni wajibu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kusimamia utaratibu kwamba zile NGOs zote zitakazovunja utaratibu ni kwa mujibu wa utaratibu na sheria lazima zifutwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Sasa, kabla sijamuita AG na mtoa hoja, naomba niweke vizuri haya mambo. Kwanza, mimi naomba ku-*declare interest* kwamba niko kwenye NGO sekta muda mrefu. Naomba niseme kabla sijaanza kusema ninalotaka kusema. Napenda niwaambie ili Watanzania wote msikie, kwamba, wake wa Marais duniani kote, wanafanya kazi za jamii na wanafanya hizi kazi kupitia kwenye mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, badala ya kupokea hizo fedha wao wenyewe, yanayopokea ni mashirika yasiyokuwa ya kiserikali! Hapana, imepotoshwa, Mheshimiwa Silinde amesema siyo kweli kwamba wake wa Marais...

MHE. DAVID E. SILINDE: (Hakusikika vyema)

MWENYEKITI: Naomba usinijibu, naomba niseme, wewe ulipokuwa unasema tulinyamamza, naomba niseme ili Watanzania waelewe, tusidanganye umma. Kamati yangu imetoka Kenya, imetoka Uganda, tumeona shughuli zinazofanywa na mke wa Rais, naomba niyaseme kabisa haya, mnataka kupotosha umma. Tumeona masuala yanayofanywa na mke wa Rais wa Kenya, tumeona masuala yanayofanywa na mke wa Rais wa Uganda. (Makofi)

Tumeona Marais wote duniani, wake wa Marais, naomba hilo niliweke vizuri ili Watanzania wasifikiri kwamba ni WAMA.

La pili, kila mwananchi duniani hapa, anayo haki ya kujiunga na shirika lisilokuwa la kiserikali mahali popote, ni haki yake, na unapokwenda kujiunga na shirika la kiserikali hupeleki kadi yako, unakwenda wewe mwenyewe. *Civil Society* hiyo inatoa fedha nyingi kwenye mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, bila kujali vyama vyao.

Naomba niliweke vizuri, tusipotoshe umma, nilitaka tu niliweke vizuri, maana yake tunataka kwenda ambako siyo. Hata Mama Maria Nyerere anafanya kazi kwa uwezo wake, na naomba tusitumie jina la Mama Maria Nyerere kufanya tubadilishe mambo hapa. Naomba nimuite AG! AG! Ukweli ndiyo huo hata kama hamuukubali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa ya Bunge ni kutunga sheria, na sisi Wabunge wajibu wetu ni kuzitetea sheria zilizotungwa. Mojawapo ya sheria muhimu sana zilizotungwa na Bunge hili ni Sheria ya Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali (*The Non-Governmental Organization Act, 2002*). Sheria hii ilirekebisha mwaka 2005 na Sheria Na. 6 ya mwaka 2005 na zinaweka masharti. Moja, inaweka masharti ya kusajili hizi NGOs na sifa zake.

Sasa, tunajua kwamba imekuwepo mifumo kabla ya sheria hii. Usajili wa hizi taasisi ulikuwa uko katika Wizara mbalimbali au taasisi nyingine tofauti. Kwa hiyo, katika Sera ya 2001 ilisema kwamba:- “...to put in place registration procedures which are transparent, decentralized and which will facilitate beter coordination of non-governmental organizations where safeguarding the freedom of association.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kutokana na sera hii, ndiyo ilitungwa hiyo sheria ya mwaka 2002 ya *Non-Governmental Organizations* na ikarekebishwa mwaka 2005. Iliporekebishwa mwaka 2005, iliweka sharti kwamba, *non-governmental organizations* ambazo zimesajiliwa katika mamlaka mengine tofauti na haya yaliyoko kwa Msajili ya hizi NGOs, Wizara ya Maedeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, basi wataomba *certificate of compliance*, kwa hiyo, mashirika haya yanatakiwa yaombe *certificate of compliance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sababu nyingine, mbali na ile iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri, kwamba kushindwa kutekeleza masharti ya usajili wa hizi, kwa mfano, kutoa ripoti za mwaka za kifedha, ni kwamba wametakiwa, watoe taarifa, waombe hizi, wamepewa *notice* ya kuomba hii *certificate of compliance*, hawaendi kusajiliwa, wakishapewa *certificate*, basi inatosheleza kwamba sasa wanachukuliwa kwamba wamesajiliwa pale, lakini unatekeleza sharti la kiseria na ni sharti la kisheria, na katika kuomba kule, kwa mujibu wa sheria hii, hawatozwi ada yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoomba kushauri, ni kwamba, sisi Wabunge tunaotunga sheria hizi kwa kweli lazima tujenge tabia ya kuziheshimu, na ndiyo maana kwanza, kazi ya Serikali ni kusimamia utekelezaji wa sheria na ndiyo maana kuna kitu kinaitwa utawala wa sheria, shughuli zote za umma zinatawaliwa na kuongozwa na sheria na hii ndiyo inazaa kitu kinachoitwa utawala wa sheria. Na Mwalimu Nyerere alisema hivi, Serikali ni sheria, hakuna kitu kinaitwa Serikali bila sheria na sheria zikishatungwa lazima zifuatwe, na ndicho tunachokifanya kapa Serikali, kwamba, haya mashirika yasiyokuwa ya kiserikali haya, nayo sasa yafanye kazi zake kwa kuzingatia sheria, na ndiyo hizo hatua zimechukuliwa. Waziri amesema ziko 24 na tena nyingine 1000, haijalishi, lakini suala hapa tunachotaka tu ni kwamba, haya mashirika yasiyokuwa ya kiserikali yafanye kazi zake kwa mujibu wa sheria. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni hili la wake wa Marais kuwa na hizi NGOs, hii inatokana na *Geneva Convention on the Laws of First Ladies*. Na wana mchango mkubwa na wana vyama vyao wanakutana kila mwaka. Juzi wamemchagua mke wa Rais mteule wa Nigeria kuwa Kiongozi wa *First Ladies*. Kwa hiyo, hiki kitu haiwezi kuwa ni *issue*, *issue* ingekuwa ni kwamba wanakiuka masharti yao ya usajili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kushauri kwamba, Waheshimiwa Wabunge hili suala halipati kutupa shida na sisi tunapaswa tuwe wa kwanza kulinda maadili ya Watanzania, tunapaswa tuwe wa kwanza kuhakisha kwamba sheria tunazozitunga zinasimamiwa na kutekelezwa ipasavyo na Serikali na ndiyo jukumu la Bunge la kuisimamia na kuishauri Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake. Sasa Serikali inaposimamia nayo inakuwa ni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba Wabunge kwa hili, tumeelewana, mmruhusu tu Mheshimiwa Waziri na mimi naomba sana Waheshimiwa Wabunge nashauri, nashauri sana, tumruhusu. Kwa sababu Waziri sasa anatekeleza majukumu yake kwa ajili ya mamlaka aliyopewa! Sasa kama hamtaki hata hizi taasisi hizi zilizochukuliwa hatua za kinidhamu, watu watawashangaa, sisi tunavunja sheria.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea
bila kutumia kipaza sauti)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa, naomba uongee na Kiti. Mheshimiwa, ongea na Kiti.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, WAMA inaweza tu ikachukuliwa hatua za kisheria kama nayo imevunja taratibu za usajili wake!

MWENYEKITI: Mheshimiwa AG naomba umalizie, uongee na Kiti usiongee na hao Wabunge, wewe ongea na kiti huku.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii, kwa sababu muda umeenda, lakini mimi ningeweza kuwafafanulia, labda waisome sheria hii kama tafasili yake ilivyotolewa kwenye mabadiliko ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri Kiti kwamba, Waheshimiwa Wabunge wamwelewe Waziri tu na ili mambo yaende kama ambavyo Serikali imependekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niliomba mbona ulinikatalia!

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo hakuomba wakati ule, utende haki, nilisimama, hokusimama, yule hokusimama.

MWENYEKITI: Naomba mkae.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukae unaendesha unavyotaka, tufuate sheria basi! Tufuate sheria, tulisimama wakati wa hoja, hokusimama!

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Msigwa, naomba uzime hiyo mic.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba hukunipa, sasa mbona unapendelea na yule kawasha, kawasha na yule.

MWENYEKITI: Mheshimiwa, naomba usikilize! Kanuni inaturuhusu, ikishatolewa hoja, tunatoa watu watatu kuchangia. Nimeishampa Mheshimiwa Mbarouk, Mheshimiwa Silinde! Naomba usikilize, naomba usikilize. Kama viongozi jifunzeni kusikiliza. Kiongozi yeyote ambaye hana sifa ya kusikiliza ana kasoro, jifunzeni kusikiliza. Tumetoa kanuni, tunafuata kanuni. Wachangiaji watakuwa watatu, Serikali inajibu. AG ni Serikali.

(Hapa Wabunge fulani waliongea bila kutumia vipaza sauti)

MWENYEKITI: Naomba, nimesema hiyo ni Serikali inatakiwa kujibu, kwa sababu mmesema ufafanuzi. Mheshimiwa Ghasia, dakika mbili.

MBUNGE FULANI: Huo sio utaratibu!

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wanaunga mkono hoja...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Anasemaje Waziri? AG kajibu, Waziri anasema nini?

MBUNGE MWINGINE: Haiwezekani!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: AG ndiye mwenye ushauri hapa, Waziri anakwenda kusema nini! Hili Bunge gani sasa hili? AG kasema halafu Waziri anakwenda kusema nini tena!

MBUNGE FULANI: Sio utaratibu huo!

MWENYEKITI: Naomba wote make! Wote naombeni tukae. Mheshimiwa Waziri kama huna la kuongeza tupige kura. Kama hayo maelezo aliyokwishatoa mtoa hoja, ndiyo kama huna la kuongeza...

(Hapa Wabunge waliendelea kupiga kelele)

MWENYEKITI: Tunajua bado. Yote hayo tunayajua. Watanzania wote wanawaona lakini!

MBUNGE FULANI: Na wewe wanakuona!

MWENYEKITI: Ndiyo, mimi wananiona, lakini na ninyi wanawaona, kelele za nini?

MBUNGE FULANI: Acha watuone na wewe wanakuona Watanzania!

MWENYEKITI: Endelea Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nifafanue masuala ambayo wameyazungumza ambayo hawana uhakika nayo.

MWENYEKITI: Kwa ufupi, ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi sana. Kwa mfano, Mheshimiwa Mbarouk nimesikitika sana kwa uwezo wako mkubwa leo unasema kwamba WAMA imekiuka kipengele, kipengele gani? WAMA inafanya kazi kubwa hapa nchini. Inaelimisha, ina shule...

MWENYEKITI: Ongea na meza, ongea na meza.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, imejikita katika elimu, inaelimisha watoto yatima kuanzia *standard seven* mpaka wanafika *form six* kutoka mazingira magumu, na watoto hawa si kama wanakuwa *hand picked*, wanaombwa, TAMISEMI ndiyo inawatafuta inawapelekea WAMA. Hawa watoto shule mbili ninazozijua sasa hivi zinahudumia watoto hawa. Isitoshe WAMA imekuwa iki-supply, ikipeleka hospitalini vifaa vya afya. Hapa Wabunge wengi katika vituo vyao kuna vifaa hivyo. Vifaa vile...

MHE. ALLY K. MOHAMED: Hata Kirando imepeleka kontena la vifaa, Kirando...

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO: Ile sio siasa. Hivi kweli unahudumia wagonjwa hospitali unaita siasa! Jamani, fanyeni haki, semeni yale ambayo yako kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo wamelisema; msimtaje Mama Maria Nyerere hapa. Wakati wa enzi za Mama Maria Nyerere hii *convention* aliyoitaja AG ilikuwa bado, na wakati ule hata NGO zenyewe zilikuwa bado. Kwa hiyo, pengine kwa umri ndiyo maana mnadhani toka miaka ya 1960 NGOs zilikuwepo, hapana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakushukuru sana, lakini nawaomba wenzetu wasitete NGO ambazo wanajua kweli hazitekelezi yale majukumu ambayo yamesajiliwa kuyafanya kama masuala ya ushoga. Msiwatete watu kama hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MHE. ESTHER N. MATIKO Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianza na hiyo ya ushoga. Nafikiri mtakumbuka wakati Waziri Kivuli wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Wenje, alikemea hapa mambo ya ushoga. Nafikiri baada ya ninyi kuwa mmesajili mkaona tumekemea huku ndipo mkaenda kuifuta, kwa hiyo ninyi ndio mnatetea ushoga na sio sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nirudi kwenye hoja ya msingi. Msajili huyu aliyesema amefuta mashirika 1,000 yuko chini ya Wizara yako, amehandika kabisa Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Kwa hiyo jibu langu bado hujalijibu, unapiga dana dana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hii ya WAMA kwa nini tunaisema, hatukatai, kama wake wa Marais wameamua sasa kuanzia awamu hiyo ya Mkapa sijui ya Kikwete, lakini tunajua Mama Mwinyi na wengine hawakuwa nayo. Na hata mkitoa *reference* ya dunia yote wanawake wanashiriki wana hizi NGO, hawazitumii kisiasa. Leo hii WAMA ikienda hata kutoa misaada huko mnavaa magwanda ya CCM, mnataka msemi hii WAMA ni...

MHE. ALLY K. MOHAMED: Uongo huo ni uongo...

MHE. ESTHER N. MATIKO: Ya kisiasa hii, zaidi hayo mashule...

MHE. ALLY K. MOHAMED: Uongo.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Haya mashule ambayo unayataja yamesajiliwa kwa jina la Salma Kikwete...

MHE. ALLY K. MOHAMED: Muongo! Muongo! Muongo mkuwa, huyo muongo.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mnasema nini, yamesajiliwa, hayajasajiliwa kwa WAMA, *is not it?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, kingine, mnapokwenda kutoa *release* za fedha hamtuambii, mbona haiko hata *open* tujue. Kwa hiyo, tunapoongea WAMA tunaona inakiuka, mkienda kutoa zawadi, jezi, *board members* wote ni CCM, mnakwenda kutoa zawadi jezi za CCM. Hatujawahi kuona...

MBUNGE FULANI: Kweli! Kweli ! Kweli! Kweli!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Na zaidi imejikita Pwani zaidi...

MHE. ALLY K. MOHAMED: Uongo! Uongo! Uongo!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Kwa nini isisambae Tanzania kote, ije na kule Mara tuione, iende sijui wapi tuione, amejikita kisiasa kwenye jimbo...

MHE. ALLY K. MOHAMED: Uongo! Uongo! Uongo! Uongo! Kaa chini uongo!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mwisho, Mama yangu, ulisema mimi sijui tumewashwa na WAMA, hatujawashwa, zaidi tunaipenda Tanzania, tunataka haki zitendeke kote. Hakuna shirika hata moja litasimama hapa liseme mimi naitetea kwa nini, nataka haki itendeke isije ikawa...

MHE. ALLY K. MOHAMED: Uongo! Uongo! Uongo! Uongo! Uongo! Uongo!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Yanakuja yale ya Haki Elimu ya kufutiwa mashirika kwa sababu yanasema Serikali. Nachukua Shilingi yangu, najua mtasema ndiyo lakini Watanzania watasikia huko waliko. *(Makofi)*

MHE. ALLY K. MOHAMED: Uongo! Uongo!

MWENYEKITI: Ahsante! Lakini, sio kweli kwamba WAMA imejikita mkoa mmoja, sio kweli.

(Hapa Wabunge kadhaa walipiga kelele)

MWENYEKITI: Sasa naomba niwahoji! Naomba niwahoji, naomba niwahoji!

MWENYEKITI: Umeshatoa hoja yako! Mheshimiwa Matiko, umeishatoa hoja yako. Naomba mnyamaze, umeishatoa hoja. Umeishatoa hoja.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Nasema hivi... Mheshimiwa Mgalu naomba ukae! Naomba tuwahoji.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kukataliwa)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selemani Jafo bado una hoja.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba kwanza niipongeze Wizara, japokuwa ina *resources* chache, lakini imefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na mapendekezo tu; sasa hivi nchi yetu ina NGOs ambazo nyingine zinafanya kazi kwa umakini wa hali ya juu. Nikifanya *reference* ya hizo NGOs nyingine zinafanya kazi katika sekta ya afya, nyingine kuwahudumia watoto, nyingine akina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja yangu ya msingi nilikuwa naiomba Wizara, Waziri aangalie uwezekano wa kwamba kuwena *NGO coordination unit* ambayo hiyo kazi yake itakuwa kila mwaka inaratibu vizuri kujua kazi za NGO zinafanyaje nchini Tanzania. Kwa mfano nikifanya *reference* Siku ya Watoto, tunaona NGO mbalimbali zime-*invest* pesa yake kwa kuisaidia Tanzania. Kwa mfano, nikifanya *reference* ya *Plan International*, *UNICEF* na nyinginezo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri, kama ikiwezekana tuwe na kitango maalum ambacho hicho kila mwaka kitakuwa kina-*recognize* vizuri kazi za NGOs ilimradi kwamba kuweza kuwapa moyo kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, juzi juzi kuna taasisi moja inaitwa *The Nurain Foundation*, ilisaidia kufanya *coordination* na taasisi moja kule Uingereza, tulipata madaktari, na wakawafanyia *operation* vijana wetu, watoto wadogo karibuni 51, ni kazi kubwa sana imefanyika. Sasa nimuombe Mheshimiwa Waziri ikiwezekana tuwe na kile kitengo ambacho kwa kila muda kinafanya *coordination* vizuri na kutoa ripoti ilimradi hata zile NGOs ambazo zinafanya kazi

kwa uzuri zaidi angalau na wao waweze ku-appreciate kwamba kweli wanakuwa-recognized vizuri katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni huo tu.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Jafo kwamba, *concern* yake kwamba kuwepo na kitengo maalum cha NGO, kipo, na sio tu kitengo, lakini tunalo hata baraza maalum, bodi inayoshughulika na masuala ya NGOs. Kitengo hiki kinafanya majukumu mengi, ikiwa ni pamoja na masuala ya ukaguzi, kwa sababu kuna baadhi ya NGOs wanafanya kazi chini ya *standard*. Kwa mfano, NGOs zinazosema labda zinalea watoto, kwa hiyo, kitengo hiki huwa kinakagua, wale wanaolea watoto je, wanayo miundombinu stahiki! Kwa hiyo tunashukuru sana kwa ushauri wake, na kitengo hicho kipo, na kama tulivyosema kwenye taarifa yetu ukurasa wa nane, pia kimefanya ukaguzi wa NGOs mbalimbali. Naomba arejee ukurasa wa 8 wa hotuba yetu, na maboresho zaidi yanaendelea kufanyika, tunashukuru kwa ushauri.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hoja yangu ni kwamba, tunapozungumza mara nyingi tunasema wanawake na maendeleo, na maendeleo hayawezi kupatikana bila kujituma. Lakini wanawake wengi katika nchi hii wanajituma sana kwa kufanya shughuli mbalimbali kama vile mama ntilie au sijui tunawaita mama lishe, wanafanya ujasiriamali mbalimbali; na wanafanya shughuli hizo kutokana na fedha za mkopo pengine, lakini badala ya kupata faida wanapata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi askari wa Jiji wanakuwa wakiwatesa wanawake hawa, wakiwanyanyasa sana na kuwadhalilisha kwa kuwafurusha, kuwapiga na kuwanyang'anya mali zao ambazo tegemeo lao ni kuuza wapate faida ili waweze kurejesha mikopo. Naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi, wanawake hawa ambao wananyanyasika kila siku kutokana na askari wa Jiji, mikopo yao watawezaje kurejesha katika mazingira kama hayo na kwa vile kwamba badala yake wanakwenda pengine wanauziwa mali zao, wanauziwa vibanda vyao ili waweze kurejesha mikopo hiyo kutokana na unyanyasaji huu ambao unaendelea!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, kama mwanamke; bahati nzuri Mawaziri wote hawa ni wanawake; hawawaonei huruma wanawake wenzao wanawaachia askari wa Jiji wanawanyanyasa namna hii? Wana mkakati gani wa kuhakikisha unyanyasaji huu na udhalilishaji huu unakoma kwa wanawake hawa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMI JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali lake zuri. Ni kweli sote tunasikitika tunapooni akina mama wanabomolewa, wanaondolewa ondolewa hapa na pale. Lakini, kila mji, miji, zinakwenda kwa taratibu na sheria zake. Kwa hiyo, sisi tunapowapa mikopo wanatuonyesha eneo gani wanapofanyia kazi. Katika kuhangaika unamuona huyu mama amepewa mkopo akiwa eneo zuri la kufanyia kazi, lakini anakwenda sehemu nyingine, ndipo yanawakuta hayo. Kwa kupitia Bunge lako Tukufu mimi nawaomba sana akina mama, wajitahidi wafanye shughuli zao kwenye maeneo yaliyotengwa. Unapooni kwamba umechukua mkopo fanya shughuli zako kwenye eneo lililotengwa. Kama Dar es Salaam kuna maeneo mbalimbali ambayo yametengwa ambayo unaweza ukafanyia biashara vizuri. Usikope uende barabarani, utamwagiwa ndizo zako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio vizuri kuona vinamwagwa, lakini sheria za kiafya nazo pia zinawafunga, ni lazima tufuate kanuni na taratibu ili wakati unafanya biashara usimkere yule mwingine ukaleta madhara. Kwa hiyo, ni vyema kina mama tufuate sheria na taratibu ili tusipatikane na matatizo haya.

Ni kweli inauma sana kumuona mwanamke amemwagiwa chakula chake, wakati mwingine chakula kile kikibaki ndicho wanachokitegemea watoto nyumbani kwa usiku ule, lakini ndiyo kimemwagwa, tunasikitika sana. Lakini pia nawaomba na wale pia huko wanaohusika, mgambo, kwenye Halmashauri zetu, ninyi nyote ni Madiwani, tuwaombe, wawaondoe, wawaambie ondokeni na vitu vyenu, sio unawaondoa unawanyang'anya chakula, unawanyang'anya sufuria. Ukimchukulia chakula chake na sufuria na vifaa vyake maana yake yule mama ndio amekwisha kabisa, kwa sababu mfanya biashara ndogo ndogo *capital* yake ni lile sufuria lake kubwa, chupa zake za chai na kile chakula kilichokuwepo mle.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba sana wenzetu kwenye Halmashauri na sisi tukiwa kama Madiwani, tuepukane na vitendo vya kuwachukulia vifaa vyao. Leo wasogee hapa, ondoka na vitu vyako. Akina mama ni watu wazuri sana, ukiwaambia ondoka, wanaondoka jamani, sio wakorofi. Lakini ukiwaendea na tingatinga na kuvunja masufuria na chupa za chai, kwa kweli sio tendo jema kwa akina mama zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana kwa swali hilo zuri, limenisaidia na mimi kuongea na Madiwani nchi nzima, kuwaomba waweke utaratibu mzuri wanapovunja vunja. Ahsante. *(Makofi)*

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba *feelings* zake zimeonekana, na naomba tu nimwambie kwamba ajitahidi sana kuona kwamba wanawake hawa

ikiwezekana basi wapewe ushauri zaidi, wapewe elimu zaidi ili waweze kufanya kazi zao vizuri na kwa umakini. Sitoi Shilingi ya Mheshimiwa Waziri. Nashukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante! Mheshimiwa Machali.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naamini na Serikali naamini itakuwa inaamini kama ninavyoamini kwamba, inakuwa ni utaratibu mbaya sana au mbovu pale tunapoona kunakuwa kuna matumizi mabaya ya fedha za Serikali au matumizi yasiyokuwa ya lazima. Sio sera ya Serikali kuwa na matumizi ambayo ni *unnecessary*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake, Jinsia na Watoto. Kwa sababu hawa wanashughulikia maendeleo, tena ya jamii, Wizara inaitwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Lakini nilikuwa najaribu, nimefanya *analysis* hapa kwenye kitabu chake Mheshimiwa Waziri, nimekuta bado *trend* ya matumizi ya pesa za vitafunwa, pesa zile za kutafunwa zile, (*hospitalities*) bado ziko nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu ni moja, na Mheshimiwa Waziri naomba mnijibu kwa kweli kwa majibu ambayo ni sahihi, kama hamkujibu nitatoa Shilingi, tena mimi nitaondoka nayo kabisa nikimbie nayo nje ili kusudi mkwame hapa, utaratibu huo nafikiri unaruhusu kwa mujibu wa Kanuni, nikiondoka hapa mtasimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waniambie ni kwa nini Wizara yako isijaribu kuweza kupunguza matumizi ya *hospitalities* kwa kiwango kikubwa ili mkapeleka kwenye Halmashauri mbalimbali. Leo ukiangalia, hizi *Folk Development Colleges* (Vyuo vya Maendeleo) vina hali mbaya. Kwenye kona mbalimbali za nchi yetu, mwenyewe umekuwa unasema kwamba bajeti ni ndogo, tena mwaka huu wamekupunguzia, una bilioni 17 hapa tumeona. Sasa, naomba kauli ya Serikali, kauli ya Wizara yako; ni kwa nini msianzishe utaratibu mzuri wa kupunguza pesa zenu za *hospitalities* ili kusudi mzi-*commit* kwenye maendeleo ili hivi vyuo tuvione basi vinang'aa, ili tuone vijana kule kwenye *Council* wakikopeshwa? Wanawake na vijana suala la asilimia tano umekuwa ni mgogoro, vijana hawakopeshwi vilivyo, wanawake hawakopeshwi vilivyo, lakini bado pesa za utafunaji kwenye Wizara yenu pia bado tunalikuta kama ilivyo kwenye Wizara nyingine. Naomba msimamo wenu, hizi pesa kwa nini msizichukue mkazipeleka sehemu nyingine? Kwa nini mnapenda tu kufyonza tu, kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hawakutoa maelekezo, natangaza nakusudia kuweza kuondoa Shilingi kwa nini wasizipunguze!

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kimsingi hicho anachokisema Mheshimiwa Machali ndiyo *spirit* ya Wizara, maeneo mengi safari hii tumepunguza. Lakini amekuwa *too general without showing exactly* ni kifungu gani. Naomba nichukue mfano, kwa mfano, *sub vote 221400* inasema *hospitality supplies and services*. Mwaka 2013/2014 ilikuwa milioni 12, mwaka 2014/2015 milioni 47, sasa hivi ni milioni 26; tumekwenda *50 percent less*, ndiyo *spirit* ya maeneo yote ya Serikali. Sasa sijaelewa hicho anachokizungumza na tuko fungu hili ni *where exactly*, twende na *statistics* na kadhalika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali, lakini nakualifu kwamba huruhusiwi kwenda na Shilingi nje kwa sababu kanuni haituruhusu, tutapiga kura, kwa hiyo hakuna kanuni inayosema Shilingi utaondoka nayo. Shilingi inabaki humu humu, uamuzi utafanyikia humu humu ndani. Endelea.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ungeniruhusu nikaondoka nayo ili kusudi waende wakajifunze.

MWENYEKITI: Haya, endelea.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba, ni kweli katika baadhi ya maeneo mmepunguza, sina tatizo na hilo. Lakini, nasema kwamba bado kiwango ambacho mmepunguza, na maeneo mengine hamjapunguza mmeongeza pia, mmeongeza maeneo mengine. Kwa hiyo, usiseme kwa kuangalia tu kwamba upande mmoja mmepunguza, sehemu nyingine mmeongeza. Kwa hiyo, ungesema na hapo mlipoongeza ungelikuwa uko *balanced*. Bado sehemu nyingine unakuta mmepunguza pengine 5%.

Sasa kwa sababu tu Mheshimiwa Naibu Waziri, umekiri, naomba niwasamehe, ila mwakani punguzeni hizi fedha na hii *spirit* tuone kwenye Wizara nyingine. (Kicheko)

MBUNGE FULANI: Mwakani UKAWA bwana!

MHE. MOSES J. MACHALI: Ninyi mkicheza, sisi tunaingia madarakani, mmesikia? Mmelewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana na hawatacheza! Ndiyo mwisho!

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi na Marekebisho yake)

Kif. 1002 Finance and Accounts...Tshs. 530,166,800/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud!

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipo katika *sub vote 1002, item 220800 - Training Domestic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hizi ni gharama za mafunzo ndani ya nchi; mwaka 2014/2015 gharama za mafunzo ndani ya nchi ilipangiwa Shilingi 16,500,000/=, mwaka huu gharama hizi za mafunzo ndani ya nchi imewekwa Shilingi 27,000,000/=, ongelezo la Shilingi 11,500,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua, bajeti yenyewe ni ndogo, Wizara yenyewe haina fedha za kutosha, sasa ni gharama za aina gani ndani ya nchi mara hii zimepangiwa mpaka itokee ongezeko la zaidi ya 50% Shilingi 11,500,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi wa kina juu ya ongezeko la gharama za mafunzo ndani ya nchi, ni ya aina gani? Ni sehemu gani? Na mahali gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kabla ya ufafanuzi, naomba kuongeza muda wa nusu saa kwa mujibu wa kanuni. Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi!

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ongezeko hili ni kutokana na kujumuishwa kwa bajeti ya mafunzo ya muda mfupi ambapo awali haikuwepo. Kwanza, tuna-*encourage* wasome ndani, lakini watumishi wanaokwenda kusoma wameongezeka, mkumbuke Wizara ina vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi, lakini pia ina vyuo vingine vya Maendeleo ya Jamii. Kwa hiyo, hawa lazima wawe wanakwenda kusoma mara nyingi ili wanaowafundishwa wapate uelewa mzuri zaidi na mambo yanayokuja ya kisasa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul, ulikuwa hujasimama toka mwanzo.

MHE. PAULIN P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, majibu ya Waziri yamenifanya nisimame.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul, kaa kwanza! Hukusimama mwanzo umesimama sasa hivi.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu yamenifanya nisimame!

MWENYEKITI: Mheshimiwa hatuendi hivyo, kanuni unazijua kwa hiyo nahoji hiki kifungu.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)

Kif. 1003 – *Policy and Planning*.....Tshs. 702,809,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Matiko!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Sub vote 1003, kasma ndogo ya 230400 - routine maintenance and repair of vehicles and transportation equipment.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mwaka 2013/2014 walitenga Shilingi 1,999,500/=, lakini mwaka 2014/2015 walitenga Shilingi 15,343,000/=. Mwaka huu imeongezeka takribani Shilingi 12,000,000/= yaani wametenga Shilingi 27,000,000/=. Kwa hiyo, nataka nijue hizi *routine maintenances and repair vehicles*, magari yameongezeka ama lah? Maana kule kwetu Tarime kile chuo hata bili ya umeme hakijalipiwa na kiko hoi, kama hizi fedha hazieleweki mzi-*allocate* ili ziende kule.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi!

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko limetokana na tengeo la deni la matengezo ya magari kwa mwaka 2014/2015 na makisio ya kupanda kwa gharama ya vifaa na gharama ya ufundi wa matengenezo ya magari kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na magari haya makuukuu, yaliyopo Wizarani, matengenezo nayo yanakuwa makubwa. Sisi sote tuna magari, kutengeneza magari ni gharama kubwa na hapa tulikuwa na madeni ya nyuma, inabidi tulipe ili mwaka huu magari yaweze kuingia kwenye gereji kubwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbarouk!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Na mimi pia niko katika *sub vote* hiyo hiyo 1003, katika *item 210100 – basic salaries*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya kulalamika kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusiana na bajeti na kupunguzwa kwa bajeti, lakini inaonekana katika Idara ya Sera na Mipango, mishahara imezidi kwa zaidi ya 50%, imeongezeka kwa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Shilingi 157,000,000/=. Wakati huohuo na posho nazo zimeongezeka kwa zaidi ya 50%. Naomba maelezo ya Waziri, ni kwa nini katika Idara hii ya Sera na Mipango kuna ongezeko kubwa la mishahara namna hii pamoja na posho?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufafanuzi kwa kifupi!

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Kimsingi kuna sababu kadhaa katika eneo hili, kwanza, tumekuwa tukiomba vibali mara nyingi sana vya wafanyakazi, huko nyuma vilikuwa havijapatikana, lakini sasa kuna kuongeza wafanyakazi. Pamoja na kuongeza wafanyakazi, kuna wale ambao vyeo vinapanda kwa hiyo, kunakuwa na mabadiliko ya mishahara. Kwa hiyo, ni nyongeza ya mishahara kwa vifungu hivyo pamoja na ajira mpya.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)

Kif. 1004 – *Internal Audit Unit*.....Tshs. 181,892,000/=

Kif. 1005 – *Government Communication Unit*...Tshs. 299,659,000/=
(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1006 – *Procurement Management Unit*.....Tshs. 241,791,900/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)

Kif. 1007 – *Information, Comm. and Technology*Tshs. 204,264,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul!

MHE. PAULIN P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba ufafanuzi katika kasma ndogo ya 229900 – *other operating expenses*. Miaka iliyopita ilikuwa 00, lakini mwaka huu ni shilingi 40,300,000/=. Mimi naomba Mheshimiwa Waziri anijibu vizuri, asije akanijibu kama alivyomjibu Mheshimiwa Masoud, alikuwa anahoji mafunzo gani ndani ya idara yeye anajibu mafunzo ya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahoji hilo nikitegemea kwamba randama ambazo tunawekewa hapo mbele ni *current*, ni randama ambazo zimeshapitiwa na zimeisharekebishwa. Nimechukua randama ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 86 inaeleza hizo gharama, tena kwanza zimetofautiana kwani kwenye randama ni Shilingi 30,300,000/=, lakini kwenye kitabu ambacho Wabunge tunapitisha ni Shilingi 40,300,000/=, maana yake kuna *increment* ya Shilingi 10,000,000/= ambayo ipo hewani hewani na kwenye randama haijaelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye randama Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba Shilingi 30,000,000/= ni kwa ajili ya gharama za mtaalamu mwelekezi. Sasa kama waliishapitia mpaka Kamati imepitia, mkapitisha na hii randama kwa Shilingi 30,300,000/=, ni kwa nini sasa hapa mnatupiga changa la macho zaidi ya Shilingi 10,000,000/= mmeongeza, umesema Shilingi 40,000,000/= Nielezwe hizo Shilingi 10,000,000/= unazipeleka wapi? Naomba majibu!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul, Serikali imeishaleta marekebisho haya hapa, sijui kama unayo! Unayo hii karatarasi? Hiyo karatasi ndiyo yenye marekebisho au majibu.

Mheshimiwa Waziri una majibu?

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Tayari!

MWENYEKITI: Jibu ndiyo hili hili, lipo humu ndani. Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Waziri mjibu!

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza jibu la tofauti la hiyo Shilingi 10,000,000/= ameishalipata. Lakini anauliza huko nyuma zilikuwa hazipo! Sasa hivi tunaanzisha Benki ya Takwimu ya Wizara, kwa hiyo, ndiyo maana huko nyuma ilikuwa haipo, kwa hiyo ipo haja ya kupata mtaalamu mwelekezi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Silinde!

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipate ufafanuzi mdogo kwenye *sub vote 1007, 22100*. Mwaka uliopita ilikuwa Shilingi 1,520,000/=, sasa hivi tumeingia karibu kwenye Shilingi 31,600,000/=. Sasa, tunahitaji tujue maana hiki ni kitengo kidogo ndani ya Wizara nzima, fedha hizi zinakwenda kufanya shughuli gani, lengo hasa ni nini? Kwa sababu isije ikawa ndiyo haja tulikuwa tunanayajadili kwamba inapofika nyakati za uchaguzi, mambo mengi yanaingizwa kwa lengo la kusaidia Chama Cha Mapinduzi.

Kwa hiyo, sisi tunachotaka, maana tunachozungumza, kwa sababu tutakapokuwa tunakaa mwezi wa Novemba kama Mawaziri tunataka tujue namna gani tutakavyoisimamia bajeti hii. Kwa hiyo, tunatengeneza bajeti mbadala kwa ajili ya UKAWA, kwa hiyo, tunahitaji ufafanuzi kutoka kwa Waziri! (Kicheko/Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi! Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana pesa ilikuwa ndogo kutokana na ufinyu wa bajeti, lakini sasa hivi kifungu hiki kimetengwa hivi kwa sababu Idara hii ya *Information, Communication and Technology* pia inapaswa kufanya shughuli fulani fulani katika vyuo vyetu vya maendeleo. Kwa hiyo, wanatakiwa kwenda katika vyuo vyetu hivi vya maendeleo na tuna vyuo 55 nchini na vyuo tisa, kwa hiyo kuna baadhi ya mambo yanafanyika katika vyuo hivi, kwa hiyo *traveling in the country*.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizipamoja na marekebisho yake)

Kif. 1008 – *Legal Service Unit*.....Tshs.145,749,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haroub!

MHE. HAROUB MOHAMMED SHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipo katika *sub vote 108* lakini katika kifungu kidogo cha 221000 - *Traveling in the country*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana zilipangwa katika kifungu hiki Shilingi 7,900,000/=, lakini mwaka huu zimepangwa Shilingi 29,000,000/= ambalo ni ongezeko la 400%. Kwa nini zimepangwa fedha nyingi namna hii wakati mwaka huu gharama ya mafuta imepungua na gharama za usafiri zimekuwa chini? Kuna nini hasa hata fedha zote hizi 400% zikaongezwa katika kifungu hiki?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, ufafanuzi!

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hiki ni kifungu kinachohusiana na masuala ya sheria. Katika kuchangia hapa, Wabunge wengi wamesema kuna migogoro ya ardhi, yaani vile Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi lazima vipate hati na lazima ardhi yake ipimwe. Kwa hiyo, Idara ya sheria lazima itembelee kwenye vyuo ili kuhakikisha kwamba hati zinapatikana na mipaka inajulikana ili kupunguza migogoro na majirani, kwa ajili ya ku-clear. Kwa hiyo, ndiyo maana hii idara inatakiwa *i-travel in the country*.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 – *Training and Folk Development Colleges.....Tshs. 8,486,399,000/=*

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba *no sweat no sweet*, hawa ni Waingereza wanasema. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri usikasirike sana kwani tunafanya kazi yetu hapa, tunakushukuru pia. Tuvumiliane tu ili tuhoji na utusaidie majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza kwenye *item number 221400 - hospitality supplies and services*. Ukiangalia *trend* kati ya mwaka wa fedha 2013/2014 ilikuwa ni Shilingi milioni 430 *plus*, mwaka uliofuata ilikuwa Shilingi milioni 906. Mwaka huu naona wametenga Shilingi 7,400,000/= jambo ambalo ni jema, *spirit* ya kupunguza matumizi. Lakini, nina swali moja mahali hapa, naomba Waziri atusaidie ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sababu gani ambazo zimepelekea mwaka jana mlitenga fedha nyingi sana, halafu mwaka huu mmezunguza mnaacha Shilingi 7,400,000/=. Ni *spirit* nzuri kwanza kwa upande mmoja, *na-appreciate* hilo. Mwaka jana kulitokea nini mpaka mkatenga kiasi hiki kikubwa cha fedha na sasa hivi kutoka Shilingi 900,000,000/= mpaka Shilingi 7,000,000/=. tunaomba ufafanuzi wa kina hasa kwa mwaka jana, kulikuwa na shughuli gani mpaka mwaka huu mmeamua kushusha!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante!

Kifungu hiki mwaka 2014 kilijumuisha Shilingi 896,940,000/= za chakula cha wanafunzi, ambapo kwa mwaka 2015/2016 zimetengwa katika kifungu kidogo cha 221700 hapo chini. Na hii ilikuwa ni kutokana na ushauri, kwenye Kamati walitushauri na tumefanya haya mabadiliko.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi ya pamoja na marekebisho yake)

Kif. 2002 – *Community Development..... Tshs. 6,893,412,000*

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata ufafanuzi katika kifungu kidogo cha 270300- *Current Grant to Non-Financial Public Units Academic Institutions*. Miaka miwili iliyopita ilikuwa Shilingi milioni 987, ikawa Shilingi 1,700,000,000/= na sasa hivi ni Shilingi 4,769,000,000/=. Napenda kufahamu, nini kimeongezeka, vyuo hivi vimeongezeka au ni kitu gani kwa sababu ni *increment* ya hali ya juu sana zaidi ya mara tatu! Naomba ufafanuzi!

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili ni kutokana na kuongezeka kwa makusanyo ya maduhuri katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii pamoja na nyongeza ya mishahara kwa watumishi 59 wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali!

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mimi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, amesema ni makusanyo, lakini hayo ni matumizi, sasa sijui...

MWENYEKITI: Jamani taratibu taratibu, taratibu!

MHE. PAULINE P. GEKUL! Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba...

MWENYEKITI: Uko kwenye kifungu hicho hicho?

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Waziri anasema ni makusanyo, lakini hiki kitabu *volume II* ni cha matumizi.

MWENYEKITI: Anasema ni cha matumizi!

MHE. PAULINE P. GEKUL: Yes, makusanyo yange-reflect kwenye kitabu *volume I*, kama sikosei ni *volume I*, yasinge-reflect kwenye *Volume II* ya matumizi. Kama ni makusanyo, hayatakiwi kuwa hapa, sasa atupe majibu yanayoeleweka.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya taasisi zinaruhusiwa kukusanya na kutumia wenyewe, kwa hiyo, ni lazima waziweke kwenye bajeti kwamba watazitungia. Kwa hiyo, hakuna mahali ambapo utaona inaonyesha kwamba watazitungia kwenye hivi vitabu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali!

MHE. MOSES J. MACHALI: Wewe unayesema subiri tuongoze, kweli tunaingia...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali, aongea na Kiti, huyo hakuhusu, wewe ongea na Kiti.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naanza kwa kutoa taarifa kwamba tutaingia Oktoba, kaeni vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza kwenye *item number 229900 - Other Operating Expenses*. Nina swali moja tu. Wakati nazungumzia kwamba kuna pesa nyingi zinatumiwa kwenye maeneo tofauti, zinapelekwa kwenye utafunaji na kadhalika na nikasema kwamba Mheshimiwa Waziri angelikuwa *focused, angelikuwa objective, angesema pia maeneo mengine wameongeza sana*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa unaona kwa mwaka jana ilikuwa Shilingi 2,000,000/=, imetoka Shilingi 2,000,000/= imekuja Shilingi 20,000,000/=. Naomba ufafanuzi, ongezeko hili ambalo pengine ni zaidi ya 900% linatokana na nini?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana kulikuwa na madeni kutokana na ile Shilingi milioni mbili, fedha haikutosha, bajeti haikutosha. Kwa hiyo, hii Shilingi milioni 20 kwanza tunalipa madeni ya mwaka jana na matumizi ya kipindi hiki cha sasa, ndiyo maana ya *other operating expenses*. (Makofi)

(Kifungu kilichotajwa kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 3001 – Gender Development.....Tsh. 432, 311,300/=

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ningependa ufafanuzi kwenye kipengele 220600 – *clothing, bedding, footwear and services* ambacho mwaka wa fedha wa 2014/15 zilitengwa Shilingi milioni nane na mwaka 2015/16 zimetengwa Shilingi milioni 200. Ningependa kujua ni maafisa gani katika Wizara hii ambao wako *entitled* kupewa *bedding, footwear and services*, wakati kuna vyyo ambavyo havina fedha za kutosha kufanya tafiti mbalimbali kama vile Tengeru na vingine vya Maendeleo ya Jamii.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilidhani angeanza kwa kutupongeza kwamba imetoka milioni nane imeenda milioni mbili. Mpendwa wangu amesahau kutupongeza. Lakini hawa ni maafisa ambao ni kwa mujibu wa Sheria na Kanunui za Utumishi ambayo inasema kwamba, kuna baadhi ya wakurugenzi na maafisa wanayo haki ya kupata *clothing, bedding, footwear and services*.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine, unajua haya mambo ya MTEF yako so *technical*, sasa yale maneno *clothing, bedding, footwear and services*, yasitupe wasiwasi. Inakuwa ni kama *other utilities*, lakini ni wale maafisa ambao ni kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi kwa mujibu wa sheria za nchi. Ahsante.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mpaka madereva wanapewa.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Sub vote 3001 ni gender development, lakini kasma ndogo ya 222100 – *travel out of country*. Mwaka jana ilikuwa ni Shilingi 152, 160,000 mwaka huu ni Shilingi 8,580,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hiki kitengo cha *gender development* ni muhimu sana, sasa najiuliza hizi Shilingi milioni nane *travel in country*, kwa sababu sidhani hata kama hizi zitawawezesha kwenda nje ya Dar es Salaam. Wanategemea kwenda Tanzania pote au ni kwa nini wameamua kutenga hii Shilingi milioni nane tu kutoka milioni 152 za mwaka jana au mmeisharidhika na *situation* nzima inayohusiana na hiki kitengo kwa nchi yetu?

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ni kwamba, mwaka jana tuliadhimisha Siku ya Mwanamke Duniani. Kwa kawaida katika kipindi cha miaka mitano, kila mwaka siku ya Wanawake Duniani inaadhimishwa kimkoa, baada ya miaka mitano inaadhimishwa kitaifa. Kwa hiyo, mara moja kila baada ya miaka mitano inaadhimishwa kimkoa na ndiyo maana inaonekana hapa kwamba, mwaka jana *expenses* zimekuwa kubwa zaidi.

(Kifungu kilichotajwa kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 3002 - *Children Development*....Tsh. 512, 713,000/=

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa nakushukuru. Kwanza, ningeomba Mheshimiwa Waziri ajielekeze kwenye majibu yaliyo sahihi kwani pale sikuridhika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme sasa kwamba, tunakwenda kwenye maendeleo ya watoto, *sub vote 3002 item 221000* - safari za ndani...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud, rudia, hawajakipata vizuri.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub vote 3002 item 221000 – travel in country*. Mmeipata hiyo! Ninaona tayari, mpo makini sasa. Mwaka jana katika maendeleo haya ya watoto kulikuwa na Shilingi 38,500,000, na mara hii kuna ongezeko kubwa ambalo limepelekea Shilingi 74, 190,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maendeleo ya watoto ambayo tunayahitaji, sasa ningepata kupata ufafanuzi, safari hizi za ndani, je, ongezeko hili ambalo wameliweka linahusisha jambo gani zaidi? Maana tunaelekea kwenye mwaka wa uchaguzi, sasa tunapata wasiwasi kweli sasa kwamba, mnaongeza vipengele vya hapa napale, isije ikawa fedha zinaenda upande mwingine. Nashukuru na naomba ufafanuzi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tunaadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika, inafanana na ile Siku ya Wanawake. Kitaifa siku ya Wanawake tunafanya maadhimisho mara moja baada ya miaka mitano. Hivyo hivyo, Siku ya Mtoto wa Afrika tunafanya maadhimisho mara moja baada ya miaka, kwa sababu ukifanya kila mwaka ni gharama. Lazima mikoa ifanye maadhimisho kutafuta mtoto gani amepata *award*, ana vipaji maalum na kadhalika, na tunakuwa jukumu la kuwaleta watoto na kuwapa elimu ya ulinzi, Mabaraza ya Watoto. Sasa mwaka huu kimsingi ndiyo tunaadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa shahidi, itakapofika, kama Bunge litakuwa linaendelea, tutaomba tumualike "Mheshimiwa Waziri" ili aje ashuhudie. *(Kicheko)*

(Kifungu kilichotajwa kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 4001 – *Non-Government Organization*.....Tsh. 309, 588,000/=

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nianze kwa ku-*declare interest* kwamba, mimi ni Mjumbe wa Bodi ya Taifa ya Uratibu wa NGOs. *(Makofi)*

Katika *Sub vote 4001, item 210100*, nimeona jinsi ambavyo bajeti imeendelea kupungua sana mwaka huu. Mwaka jana walipitishiwa Shilingi 103,750,000, lakini mwaka huu ni Shilingi milioni 75 tu, jambo ambalo naona kwa kazi ambazo zinafanyia kwa kweli zinahitaji fedha nyingi ili kuweza kufanya kazi kwa ubora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua kwa kupunguza fedha huku, hii *Coordination Board* watawezaje kufanya kazi ili kuimarisha utendaji kazi wa NGOs katika taifa hili!

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza uniruhusu nimpongeze Mheshimiwa Lolesia kwa kazi nzuri anayoifanya kutokana na jukumu ambalo analo la ku-coordinate masuala mbalimbali ya NGOs.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lolesia, asiwe na wasiwasi, watumishi waliokuwa wanalipwa katika kifungu 4001 wamehamishiwa katika kifungu 1008 kinachohusu huduma za sheria. Zamani wanasheria walikuwa wanalipwa kutoka katika kifungu hiki, sasa wametolewa pale na ndiyo maana inaonekana ni pungufu. Fedha hizo zinaonekana katika kifungu kingine. *(Makofi)*

(Kifungu kilichotajwa kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

KITABU CHA NNE

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 53 – WIZARA YA MAENDELEO JAMII, JINSIA NA WATOTO

Kif. 1001 – *Administration HR Management*.....Tsh. 50,000,000/=

Kif. 1003 – *Policy and Planning*.....Tsh.141,180,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 – *Training and Folk Development*.....Tsh. 2,361,050,000/=

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Najielekeza pale kwenye *item 6229 - Rehabilitation of Folk Development Colleges (FDCs)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kwamba kwa mwaka wa fedha ambao utaishia Juni walitenga Shilingi bilioni moja, ni jambo jema kwamba, kwa mwaka ujao wa fedha wametenga Shilingi bilioni mbili. Lakini, bado nina *concern* moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipita kwenye hivi vyuo ya maendeleo ya wananchi, vingi vina hali mbaya. Utengaji wa fedha kwa ajili ya kuvifanyia *rehabilitation, terminology* ambayo wameitumia wenyewe. *Trend* hii ya kutenga Shilingi bilioni moja mwaka jana, mwaka juzi ilikuwa Shilingi bilioni 1.3 na kwa mwaka ujao wa fedha Shilingi bilioni mbili, bado fedha hizi ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali inisaidie, tunapokwenda kwenye ofisi zao za Wizara tunafurahi kwamba, wana jengo zuri ambalo wamejenga kwa bilioni kadhaa za fedha, lakini maeneo ambayo tunatakiwa tu-*commit* fedha ambazo zitakuwa na matokeo makubwa na tena yenye faida kwa watu wengi, tumekuwa na mwenendo wa kutenga fedha ambazo ni kidogo, matokeo yake vijana na hata watu wazima...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali, nakuomba, swali lako uliekeze kwamba ni nini hasa unataka kujua ili wapate jibu zuri la kukujibu, maana umeenda mbali. Jielekeze kweye hicho kifungu.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko hapo kwenye kifungu, ninachofanya ni *comparative analysis* ya fedha ambazo zinatengwa hapa na nyingine ambazo zimetengwa, jambo ambalo ni la kawaida. Kwa hiyo, wasikimbie kwanza, hebu tulieni, mbona mnakuwa na wasiwasi!

MWENYEKITI: Hakuna ambaye amekimbia, Mheshimiwa Machali unaongea na mimi, wala hawajakuzungumzisha.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Wewe ongea na mimi tu, wala wale hawajaongea na wewe.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa hiyo, watulize watulie ili wasikilize swali langu vizuri, nina hoja nzuri. Nasema kwamba wanatenga fedha nyingi kwenye maeneo mengine, mfano, kujenga majengo ambayo Waziri na Katibu Mkuu wanakaa, ni jambo jema. Lakini huku kwingine ambako ndio watoto wa wakulima wanahitaji kwenda kupata *skills*, zinatengwa fedha kidogo. Hata ukija pake Kasulu Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, hali ni mbaya, mabweni ni ya hovyoy, na ndio hizi fedha za *rehabilitation* shilingi bilioni mbili...

MWENYEKITI: Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba,...

MWENYEKITI: Muda umeisha.

MHE. MOSES J. MACHALI: Naomba wanieleze ni kwa nini wanatenga fedha kidogo wakati wanajitengea fedha nyingi!

MWENYEKITI: Muda umeisha ulikuwa haujauliza swali. Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kutokana na uwezo ambao tunao kwa sasa hivi. Tuna Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 55. Mpaka sasa tumefanyia ukarabati vyuo vingi kwa kutumia ule Mfuko wa *Education Sector Development Programme* ambao umefanya karibu nusu ya vyuo hivi vinatoa mafunzo ya VETA. Ili kufanya kutekeleza hilo tumevifanyia ukarabati mkubwa. Kwa hiyo, tunaenda awamu kwa awamu. Roma haikujengwa kwa siku moja. Hata hilo jengo la Waziri unaloliona, unaona jingo la Utumishi. Wewe kabla hujaja Dar es Salaam, Waziri wa Utumishi na Waziri wa Maendeleo ya Jamii tulikuwa kwenye yale mabanda unayoyaona pale. Wizara ilikuwa pale mabandani, sasa tunakwenda kidogo kidogo na kwenye hii *programme* yetu tutafikia huko Kasulu na mahali pengine.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho cha *2001 - Training and Folk Development, kipengele cha 4312 - Education Sector Development Programme*, ingawa mwanzoni nilikuwa nime-target hicho cha Mheshimiwa Machali kwa ajili ya FDC ya Tarime, iko hoi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo kwenye *education sector development programme* wametenga Shilingi milioni 361 tu. Nilitembelea Chuo cha Wananchi pale Tarime na ilikuwa ni muda mfupi tu baada ya Mheshimiwa Waziri kuwa umetoka pale. Hizi fedha ulizotenga ni kidogo sana, tulipoenda kule tulikuta hawana vitabu, maana hapa umesema ni *education sector programmes*.

Nataka nijue, ni *programmes* zipi, ni hizo za vitabu, za vitendea kazi au ni *programme* zipi za *Folk Development Colleges* Shilingi milioni 361, naona ni ndogo sana. Kwa hiyo, naomba kujua zinaenda ku-cover nini kwenye hiyo *education sector development programme*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther, wewe ni Mwenyekiti wa CHADEMA wa Mkoa wa Mara, mbona unazungumzia FDC ya Tarime peke yake badala ya kuzungumzia na FDC ya Bweri, Musoma wakati wewe ni Mwenyekiti wa Mkoa? (Makofi)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, FDC ya Tarime ndiyo niliyoitembelea, ndiyo naijua.

MJUMBE FULANI: Anagombea!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, na pia nagombea pale, nimetangaza nia. Umezata jibu! *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ndiyo! Ungetueleza hilo. Kwa hiyo, wa Musoma wanasikia hao. *(Kicheko)*

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Eeh! Kwa hiyo, tunatafuta na kura hapa! Haya tuendele. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ndizo tulizopanga. Kubwa ni kwamba, bajeti ni finyu, tufanye kazi ya kuhakikisha makusanyo yanakuwa makubwa. Tuache kuwaambia wafanyabiashara wasitumie mashine za EFD ili makusanyo yawe mengi, tutaleta fedha nyingi kule. Kama kodi hailipwi vizuri, kule nako muwambie, siyo mnawaambia watu wagome tu hapo.

(Kifungu kilichotajwa kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 2002 – *Community Development*.....Tsh. 1,370,000,000/=

MHE. DAVID E. SILINDE: Nani anakiafiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko kwenye hicho kifungu 2002, kifungu kidogo cha 6229 - CDTI Tengeru ambacho kimetengewa Shilingi bilioni moja ambazo ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri anajibu kwenye Kitabu cha Matumizi, alisema moja ya vyo ambavyo vimeongeza mapato ni Tengeru mpaka kufikia Shilingi bilioni 4.7. Sasa hizi *local* ni fedha za ruzuku na ukienda kuangalia mbele kuna watu watatoa hoja yao, utakuta wanawake wametengewa fedha kidogo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niseme kwamba, ameeleza kwenye fedha za makusanyo ziko kwenye matumizi, katika yale makusanyo hoja yetu ilikuwa ni kwamba, kwa nini hao waliozidi hicho kiwango kwa mara tatu wasingepoleka hata moja ya tatu ya zile fedha zilizoziidi kwenye maendeleo ya vyo vyao, halafu fedha hizo ambazo ni ruzuku ya Serikali zisiende katika mifuko ya akina mama kwa ajili ya kuwawezesha.

Ni kwa nini Serikali inakuwa kama vile haijielewi kwamba, makusanyo kwenye matumizi na ruzuku kwenye *development*?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nifahamu ni kwa nini mambo kama haya yanakuwa yanajitokeza?

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Tengeru sasa hivi ni chuo kikuu na fedha zao zinabaki kule kama *retention*. Hizi fedha tunazopeleka za maendeleo ni kuboresha kile chuo. Sasa hivi kuna *library* ambayo hawajamaliza kuitengeneza, kwa hiyo, ni lazima tuendeele kukijali kile chuo. Zile fedha anazozisema ni za *retention* zimebaki kule kutokana na makusanyo yao.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafo umepata majibu ya kukuridhisha au?

MHE. SELEMAN SAID JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naenda katika kifungu cha 6330 ambacho tumesogea na kufikia shilingi milioni 370, niishukuru Wizara katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kwa lengo la kuweka angalizo kwamba, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kama Wabunge tunaona kwamba, wanataka kufanya kazi lakini *resources* zake ni *limited*. Kwa hiyo, nimuombe tu Mheshimiwa Waziri, baadae wakati tunapitisha bajeti huko kwenye mafungu, tutaomba Wizara hii iongezewe fedha kwa kadri itakavyoweze kana ilimradi vyuo viweze kupata nguvu kubwa na Wizara iweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi, vyuo vya Ilula navyo vina matatizo hayo hayo.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea ushauri wake. Ahsante. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kif. 3001 – Gender Development...Tsh. 5,224,297,000/=

(*Hapa Wabunge wengi walisimama*)

MWENYEKITI: Wako wengi, tunaenda kwenye *guillotine*. Waheshimiwa wote kaeni. Waheshimiwa, tukae!

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *guillotine* muda si bado?

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Bado, mimi ndiye naangalia saa, nyinyi hamuangalii saa. Walioomba kuchangia wako wengi, hatuwezi kumaliza, kwani bado dakika 10 kwa hiyo, tunaenda kwenye guillotine. *(Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni muhimu sana.

MBUNGE MWINGINE: *This is very important!*

Kif. 3002 – Children Development...Tsh.1,756893,000/=

(Kifungu kilichotajwa kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tukae. Mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. *(Makofi)*

TAARIFA

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limepitia Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka 2015/2016 kifungu kwa kifungu na kuipitisha pamoja mabadiliko yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naafiki!

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Makadirio ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, bajeti yake imepitishwa. Napenda niwashukuru sana Mheshimiwa Waziri (Mwenyekiti wangu) kwa umahiri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii.

Pia, napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Ni matumaini yangu kwamba, fedha zitatolewa na yale yaliyopangwa kutekelezwa na Wizara yatatekelezwa. Nawaomba siku nyingine Waheshimiwa Wabunge,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

muombe hata NGOs zipewe fedha na Serikali badala ya kuuliza tu kwa nini zinafutwa, mziombee fedha ili ziongezewe.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika! Mwongozo wa Spika! Mwongozo wa Spika!

MWENYEKITI: Naomba niliahirishe Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2:24 siku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumanne,
Tarehe 26 Mei, 2015 Saa Tatu Asubuhi)*